Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TAZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Ishirini na Tisa – Tarehe 22 Julai, 2008

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mheshimiwa Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hazi zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:

Taarifa ya Mwaka na Hesabu Zilizokaguliwa za Shirika la Makumbusho ya Taifa la Tanzania kwa Mwaka 2005/2006 *(The Annual Report and Audited Accounts of The National Museum of Tanzania for the year 2005/2006).*

Taarifa ya Mwaka na Hesabu Zilizokaguliwa za Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania kwa Mwaka 2006/2007 *(The Annual Report and Audited Accounts of Tanzania Wildlife Research Institute for the year 2006/2007).*

Taarifa ya Mwaka na Hesabu Zilizokaguliwa za Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania kwa mwaka 2004/2005 na 2005/2006 *(The Annual Report and Audited Accounts of Tanzania Forestry Research Institute for the year 2004/2005 and 2005/2006).*

Taarifa ya Mwaka na Hesabu Zilizokaguliwa za Shirika la Hifadhi za Taifa kwa mwaka 2006/2007 *(The Annual Report and Audited Accounts of the Tanzania National Parks for the year 2006/2007).*

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

MHESHIMIWA JUMA S. NKUMBA (K.N.Y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):

Taarifa ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa Mwaka wa Fedha Uliopita pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2008/2009.

MHESHIMIWA JUMA SAID OMAR (K.N.Y. MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA):

Taarifa ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa Mwaka wa Fedha uliopita pamoja na Maoni ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2008/2009.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 257

Mradi wa Utunzaji Mazingira Ziwa Tanganyika

MHESHIMIWA SAID A. ARFI (K.N.Y. MHESHIMIWA MHONGA S. RUHWANYA) aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 2006 ulianzishwa Mradi wa Utunzanji wa Mazingira wa Ziwa Tanganyika chini ya udhamini wa *African Development Bank (ADB)*:-

(a) Je, mpaka sasa mradi huo umefikia wapi?

(b) Je, elimu itatolewa kwa wananchi waishio katika Mwambao wa Ziwa hilo wanufaike na mradi huo?

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.N.Y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Utekelezaji wa Mpango wa Usimamizi Endelevu wa Mazingira ya Ziwa Tanganyika unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)*, Benki ya Uwekezaji ya *Nordic*, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa na Mfuko wa Dunia wa Mazingira umefikia katika hatua nzuri. Nchi zote nne zinazozunguka Ziwa hilo zimeridhia Mkataba wa kuanzisha Mamlaka ya Ziwa Tanganyika. Kila nchi imekubali kuchangia kiasi cha Dola za Marekani 303,900 kwa mwaka kwa ajili ya uendeshaji wa Mamlaka ya Ziwa Tanganyika yenye Makao Makuu yake Bujumbura, Burundi.

Kwa upande wa Tanzania, tayari Kamati ya Usimamizi wa Mradi imeundwa, ofisi zimepatikana Mjini Kigoma na Mratibu wa Mamlaka ameajiriwa. Nafasi zaidi za ajira zimetangazwa kwa ajili ya miradi inayofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP)*. Tunategemea shughuli zote kuanza rasmi kabla ya Desemba, 2008. Miradi ambayo itaanza ni ile ya Usimamizi wa Hifadhi ya Mazingira ya Bonde la Ziwa Tanganyika na Mradi wa Uvuvi Endelevu.

(b) Elimu imeanza kutolewa na itaendelea kutolewa kwa wananchi waishio katika Bonde la Ziwa Tanganyika ili waweze kunufaika na miradi itakayotekelezwa. Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* inashirikiana na Mkoa wa Kigoma na Mkoa wa Rukwa katika kutekeleza Programu ya Elimu kwa Umma.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Usimamizi Endelevu wa Mazingira ya Ziwa Tanganyika ni sehemu muhimu katika utekelezaji wa Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji na mkakati wa kuhifadhi mazingira ya Bahari, Maziwa, Mabwawa na Mito. Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Mikoa ya Kigoma na Rukwa na Halmashauri zake itasimamia kwa karibu utekelezaji wa mpango huu unaoshirikisha pia Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Zambia.

MHESHIMIWA SAID A. ARFI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, tayari ofisi zimeshapatikana mjini Kigoma na tayari mradi huu unaweza kuanza wakati wowote ifikapo Desemba, 2008; ninapenda tu anihakikishie, ni vijiji vingapi katika Mkoa wa Kigoma na Mkoa wa Rukwa ambavyo vimewekwa katika mpango wa awali wa uetekelezaji wa mradi huu?

SPIKA: Naona ni swali la takwimu hivi, sijui!

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.N.Y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA): Mheshimiwa Spika, mradi au miradi niliyoitaja, utekelezaji wake unahusu Wilaya zifuatazo:- Wilaya ya Kasulu,

Wilaya ya Kigoma Vijijjini, Wilaya ya Kigoma Mjini, Wilaya ya Mpanda, Wilaya ya Nkasi na Wilaya ya Sumbawanga.

MHESHIMIWA PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majawabu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, mradi huu umechukua muda mrefu sana na kila wakati tumekuwa tunaambiwa sasa utaanza mwaka huu, naona leo tunaambiwa utaanza Desemba: Katika mradi huo kulikuwepo na kipengele kwa ajili ya mradi wa maji katika Manispaa ya Kigoma, Ujiji.

Lakini, naona kipaumbele imewekwa kwenye miradi hiyo miwili ambayo Waziri ameisema ambayo itaanza; nataka kuuliza: Je, mradi huu wa maji nao umeondolewa au wenyewe utaanza lini?

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.N.Y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA): Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna mradi katika mpango huu unaohusu uondoaji wa maji taka katika Manispaa ya Kigoma, Ujiji. Mradi huu ni ule ambao unafadhiliwa na *Global Environment Facility* kwa Dola 300,000 na vile vile unafadhiliwa na *Nordic Bank* kwa *Euro* 6,000,000. Mradi huu utatekelezwa pamoja na mpango wa maji wa Mji wa Kigoma ambao unasimamiwa na Wizara yangu.

Hivi sasa, tunafanya maandalizi ya kumpata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya Mradi Mkubwa wa Kigoma wa muda mrefu. Sasa, maji taka yanapatikana kutokana na uchafuzi wa maji safi. Kwa hiyo, mradi wa kwanza utakuwa ni mradi wa maji safi ambao utafadhiliwa na *EU Facility* na unafuata au sambamba na huo utakuwa ni utekelzaji wa mradi huu ambao uko katika programu hii ya maendeleo endelevu ya Ziwa Tanganyika.

Na. 258

Sheria ya Kuadhibu Uhalifu wa Mazingira

MHESHIMIWA DK. CHRISANT M. MZINDAKAYA aliuliza:-

Kwa kuwa uharibifu mkubwa wa mazingira unatokana na uchomaji moto na ukataji miti ovyo ikiwa ni pamoja na kulima kwenye vyanzo vya maji:-

Je, Serikali italeta lini sheria ambayo itatoa adhabu kali zaidi kama vile kifungo cha miaka mitatu mpaka saba kwa makosa hayo?

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.N.Y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, Mbunge wa Kwela na kaka yangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na uharibifu wa mazingira, sheria ya misitu Na.14 ya mwaka 2002, Sheria ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 na Sheria ya Makosa ya Jinai *(penal code)* kifungu Na. 321 zinatoa adhabu mbalimbali dhidi ya makosa niliyoyataja. Adhabu hizo ni kali kwani kuna kifungo cha mwaka mmoja mpaka miaka 14 jela na vile vile faini kuanzia Sh. 50,000/= hadi shilingi milioni 50.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, sheria ya misitu kifungu 91(2) inatoa adhabu kwa mtu yeyote atakayepatikana na hatia ya kuchoma moto msitu wa hifadhi, mashamba ya misitu au mbuga kwa makusudi, kutumikia kifungo cha miaka 14 jela kulingana na adhabu ya makosa ya jinai *(penal code)* kifungu Na. 321. Kuhusu kulima kwenye vyanzo vya maji, Sheria ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 inatoa adhabu ya faini kuanzia Sh. 50,000/= mpaka shilingi milioni 50 au kifungo cha miezi mitatu mpaka miaka saba jela au vyote viwili.

Mheshimiwa Spika, katika kesi iliyofunguliwa na Jamhuri katika Mahakama ya Mwanzo ya Matai mwaka 2007, mwananchi mmoja aitwaye Kanchure Siuluta kutoka kijiji cha Katete, Sumbawanga Vijijini, alihukumiwa kifungo cha miaka mitano kwa kosa la kuchoma moto nyika kwa makusudi. Naamini hii itakuwa ni fundisho kwa wengine wa aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hii, tatizo siyo sheria, bali elimu kwa jamii na zaidi usimamizi wa sheria zilizopo. Ofisi ya Makamu wa Rais ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha kanuni za kuwezesha kuwa na Wakaguzi wa Mazingira na kukasimisha shughuli hizi katika ngazi za Mikoa na Wilaya ili kuimarisha usimamizi na udhibiti wa uharibifu wa mazingira. Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* na wadau wengine itaendelea kutoa elimu juu ya umuhimu wa kuhifadhi na kulinda mazingira kwa faida ya kizazi hiki na vizazi vijavyo. Wananchi wanaombwa kuzingatia umuhimu wa kulinda na kuhifadhi mazingira ikiwa ni pamoja na kuzingatia sheria ya mazingira na sheria zinaoendana na sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuuliza swali hili, inadhihirisha kwamba Mheshimiwa Mzindakaya ni Mwana-Mazingira! *(Makofi)*

SPIKA: Na bado anataka kuuliza swali la nyongeza! *(Kicheko)*

MHESHIMIWA DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA: Mheshimiwa Spika, nimeridhika kwamba sheria ipo. Lakini Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba, inavyoonekana hasa ukizingatia uchomaji moto ulivyo mkubwa katika nchi hii, inavyoonekana, usimamizi ni hafifu kuhusu sheria hii?

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.N.Y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA): Mheshimiwa Spika, kwa kifupi, nakubaliana naye! Lakini, kwa ziada niseme tu kwamba moja ya Mikoa iliyoathirika sana na uchomaji moto na uharibifu wa mazingira ni Mkoa wa Rukwa. Lakini, vile vile Mkoa wa Rukwa kwa juhudi za uongozi wa Mkoa pamoja na Wabunge wa Mkoa wa Rukwa wamefanya mambo makubwa. Kwa mfano; mwaka 2008 kwa Mkoa wa Rukwa ni Mwaka wa Mazingira kwa madhumuni ya kudhibiti kilimo kwenye miinuko, kudhibiti mioto vichaa, kutunza na kulinda vyanzo vya maji na kuboresha sheria ndogo za mazingira.

Mheshimiwa Spika, kama unavyojua, mioto huanza mwezi wa nane na naomba Mikoa izingatie kusisitiza na kudhibiti mioto hiyo mwaka huu. Tatizo lililojitokeza Rukwa ni tatizo linaloweza kutokea nchi nzima. Mwaka 2006 kulikuwa na kampeni kubwa ya kuzuia uchomaji moto Rukwa, lakini mwaka 2007 matukio yakazidi, ilikuwa ni kupimana nguvu. Lakini, naamini mwaka huu tutafanikiwa. Ahsante.

Na. 259

Barabara ya Soni – Old Korogwe

MHESHIMIWA WILLIAM H. SHELLUKINDO aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya kuunghanisha Wiulaya ya Lushoto na Tanga Makao Makuu ni ile itokayo Mji wa Lushoto kwenda Mombo yenye urefu wa kilomita 30 za lami; na kwa kuwa barabara hiyo haiwezi kuongezwa upana wake kwa sababu ya milima na miamba:-

Je, sio vyema Serikali ikaendeleza mawazo ya Wajerumani wakati wa Ukoloni ya kufungua barabara ya Soni – Bumbuli – Kwa Shemshi hadi *Old Korogwe* na kuifanya barabara mbadala ya uchumi na yenye uhakika kuliko ile ya Lushoto – Mombo ambayo inafaa zaidi kwa aili ya utalii wa kuzunguka Mlima kwa magari?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara zote mbili zilizotajwa na Mheshimiwa Mbunge ni barabar za Mkoa na zinahudumiwa na Wizara ya Miundombinu kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* Tanga. Barabara ya Soni – Bumbuli – Dindira – *Old* Korogwe ina urefu wa kilomita 80, ni ya changarawe kwa sehemu kubwa na sehemu ndogo ni ya udongo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilishauona umuhimu wa kuifungua barabara ya Soni – Bumbuli – Dindira – *Old* Korogwe tangu mwaka wa fedha wa 2004/2005. Upembuzi yakinifu *(feasibility study)* ulifanywa na matokeo yake ni kuwa kipande cha Soni – Bumbuli – Dindira (Km. 47) kilikidhi vigezo vya kiuchumi vya kujengwa kwa kiwango cha changarawe. Hivyo, sehemu hiyo inafanyiwa ukarabati kwa kiwango cha changarawe kwa kutumia fedha za Mfuko wa Fedha wa *STABEX*. Gharama za ukarabati huo ni shilingi bilioni 1.76.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilisha ukarabati wa sehemu ya barabara kutoka Soni – Dindira (Km. 47), kilomita 33 zilizobaki kati ya Dindira na *Old* Korogwe, zinaendelea kutafutiwa fedha ili zikarabatiwe kutoka kwa wahisani na fedha za ndani.

MHESHIMIWA WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa kuwa upembuzi yakinifu uliokwishafanyika umeonyesha waziwazi kwamba barabara hii itakapofika mwaka 2010 itastahili kutengenezwa kwa kiwango cha lami; Je, maandalizi yamekwishaanza? Swali la pili; kwa kuwa mkandarasi aliyepewa barabara

hiyo aitwaye *BECCO* amechelewesha ukarabati wa eneo lile la kilomita 47 kwa karibu miaka miwili; Serikali inachukua hatua gani?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, kuhusu upembuzi yakinifu; upembuzi huo yakinifu kama nilivyojibu katika swali la msingi, ni kwamba umekamilika na kiwango ambacho kimepangwa ni ujenzi kwa kiwango cha changarawe na siyo kwa kiwango cha lami.

Kwa hiyo, Serikali sasa hivi inajitahidi kuhakikisha kwamba barabara hiyo inafunguliwa kwa kiwango cha changarawe ili iweze kupitika kwa wakati wote. Pili; kuhusu mkandarasi *BECCO*, *BECCO* ambao wanajenga barabara hii, barabara hii wanaijenga kwa *package* mbili:- Moja ya kutoka Soni – Bumbuli na *package* namba mbili ni Bumbuli – Dindira. Soni – Bumbuli imekamilisha *survey* kwa asilimia 70 na Bumbuli – Dindira kwa asilimia 60. Kwa bahati mbaya *BECCO* anasuasua kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema, lakini kwa vile wametiliana saini *BECCO* na Hazina, mradi huu umechelewa, ulitakiwa umalizike mwezi Juni, Hazina sasa iko katika taratibu ya kusitisha mkataba huo ili aweze kupatikana mkandarasi mwingine ambaye atafanya kazi hiyo kwa ubora zaidi.

Na. 260

Idara ya Utabiri wa Hali ya Hewa

MHESHIMIWA JACKSON M. MAKWETTA aliuliza:-

Kwa kuwa miezi ya kati ya Novemba na Mei ni miezi ya mvua nyingi na ni miezi ya shughuli za kilimo; ili wakulima wafaidike na elimu ya Utabiri wa Hali ya Hewa itolewayo mara kwa mara:-

(a) Je, kwa nini Idara ya Hali ya Hewa isiongeze vipimo vya kupima mvua, upepo na joto Mikoani na kutangaza mara nyingi kuhusu hali ya hewa nchini hasa wakati huu wa kilimo?

(b) Je, kwa nini Idara hiyo isifungue Kituo cha Hali ya Hewa eneo la Igeri (Uwemba) ili kusaidia kutoa matangazo ya hali ya hewa mara kwa mara kuwasaidia wakulima kujua wakati wa kupanda viazi mviringo, matunda, miti na mahindi kwa sababu wanafanya kazi mwaka mzima?

(c) Kutokana na kukua kwa teknolojia katika masuala ya utabiri wa hali ya hewa: Je, Idara yetu ya Utabiri wa Hali ya Hewa imeweza kutabiri kwa usahihi kuwa ni siku ngapi mbele ya siku inapotoa matangazo?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jackson Muvangila makwetta, Mbunge wa Njombe Kaskazini lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wakala una vituo mbalimbali vya kupima hali ya hewa ambavyo vimesambazwa nchi nzima kama ifuatavyo:-

- Uchunguzi wa hali ya hewa katika vituo Vituo Vikuu 26 nchini kote hufanywa kwa muda wa saa kati ya 15 hadi 24 kila siku na vipimo hivi hufanywa kila baada ya saa moja;

- Vituo 11 vinavyotoa taarifa ya hali ya hewa na kilimo;

- Vituo 80 vya kupimia mvua na joto; na

- Vituo 1,600 vya kupimia mvua peke yake.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Hali ya Hewa Tanzania ina mpango wa kuongeza vituo vya kupimia hali ya hewa nchini ili kufikia lengo la kitaifa na kimataifa ambalo ni kuwa na kituo kikuu kila baada ya umbali wa kilomita 112.

Hadi sasa asilimia 35 ya lengo hilo limefikiwa. Hata hivyo, mpango wa muda mrefu wa Wakala ni kuongeza vituo vikuu 70, vituo vya hali ya hewa na kilimo 35, vituo vya kupima joto na mvua 250, vituo vya mvua 2,800 na vituo vinavyojiendesha vyenyewe kufikia 80.

Wakala wa Hali ya Hewa hutoa utabiri wa taarifa nyingine za hali ya hewa za kila siku na zile za msimu kupitia redio, televisheni, magazeti, ofisi za hali ya hewa mikoani, ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya ili ziweze kuwafikia wakulima. Aidha, Wakala inaandaa utaratibu ili vituo vyake huko Mikoani viweze kutoa taarifa hizo pamoja na elimu kwa umma pale inapohitajika.

(b) Mheshimiwa Spika, Wakala wa Hali ya Hewa ina kituo kinachopima taarifa za hali ya hewa na kilimo katika kituo kidogo cha utafiti cha Igeri, Wilayani Njombe. Kituo hicho kinapima taarifa za hali ya hewa na kilimo na kuchambuliwa na kutolewa utabiri na huduma za hali ya hewa katika maeneo ya Mkoa wa Iringa na sehemu nyingine hapa nchini. Pamoja na kuimarisha kituo hiki, Wakala ina mpango wa kujenga kituo kikuu Mjini Njombe ili kuimarisha huduma kwa wananchi wa Wilaya hiyo.

(c) Mheshimiwa Spika, Wakala wa Hali ya Hewa inatumia mbinu za kisasa katika kuchambua na kutoa utabiri wa hali ya hewa. Mbinu hizo ni kama vile kutumia utaalam wa kutabiri mahesabu kwa kutumia kompyuta *(Numerical Weather Prediction)* ambapo utabiri hutolewa kulinga na mahitaji ya watumiaji wa utabiri huo huweza kuwa kwa siku moja, siku kumi, mwezi au kwa msimu. Kimsingi, kadri muda wa utabiri unavyokuwa mfupi, usahihi wake ndivyo unavyoongezeka.

MHESHIMIWA JACKSON M. MAKWETTA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Kutokana na ongezeko la

joto duniani linalosababisha utabiri wa hali ya hewa kuwa mgumu kuutabiri: Je, Wizara au Wakala ana mikakati gani ya kuboresha kazi hii ili utabiri wa hali ya hewa angalau ufikie asilimia 90 ya usahihi?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, kama nilivyoongea katika jibu la swali la msingi kwamba mahitaji ya vituo vya hali ya hewa kukidhi mahitaji ya viwango vya kimataifa ni kuwa na vituo vikuu walau kimoja baada ya umbali wa kilomita 112. Bado hatujafikia hapo, Serikali kupitia Wakala wa Hali ya Hewa Tanzania tuko katika juhudi ya kuhakikisha tunafikia hapo. Sasa hivi tumefikia aslimia 35 ya lengo na tumeitengea Wakala fedha mwaka huu wa fedha na tutaendelea kutenga mafungu ya fedha kiasi kikubwa iwezekanavyo ili Wakala iweze kukidhi mahitaji ya kuweza kutoa utabiri ambao utasaidia wakulima na wafanyakazi wote nchini Tanzania.

MHESHIMIWA JAMES P. MUSALIKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Taasisi ya Utabiri wa Hali ya Hewa ina uwezo wa kutabiri kipindi hata cha msimu mzima; na kwa kuwa taarifa zake Mheshimiwa Waziri amesema zinapelekwa kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, lakini mimi nina ushahidi kwamba taarifa hizi haziwafikii wakulima, huwa wakati mwingine taarifa za Januari zinafika mwezi Julai, taarifa za Novemba zinafika mwezi Mei, msimu umeshapita: Je, Serikali inaonaje sasa kuzielekeza Halmashauri na ziwekewe kanuni kwamba, kabla ya msimu zitafute taarifa hizo na ziwaambie Madiwani au kwenye mtandao wa Serikali za Mitaa ili wananchi watangaziwe ili wajue kama wanalima kwenye mabonde yanayojaa maji au vinginevyo kufuatana na hali itakavyokuwa msimu huo?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, tumepokea ushauri wa Mheshimiwa Musalika, tutauzingatia na tutajitahidi kufanya hivyo ili tuweze kuboresha kilimo nchini Tanzania kwa kufikisha taarifa mapema iwezekanavyo.

Na. 261

Utalii wa Watanzania kwenye mbuga za Wanyama

MHESHIMIWA DORA H. MUSHI aliuza:-

Kwa kuwa, nchi yetu ina mbuga nyingi na nzuri zinazosifiwa duniani; na kwa kuwa wageni kutoka sehemu mbalimbali huja kutembelea na kuona wanyama wetu tena kwa gharama kubwa sana:-

Je, kwa nini Watanzania wasiwe na utamaduni wa kutembelea mbuga zao na kuwaona wanyama hai badala ya kuamini kuwa vivutio hivyo ni kwa ajili ya watalii tu?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dora Heriel Mushi Mbunge wa Viti maalumu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, shughuli za utalii wa kutazama wanyama hufanyika katika hifadhi za Taifa *(National Parks*) na baadhi ya mapori ya akiba hususani Seleous na Hifadhi ya mamlaka ya Ngorongoro. Utalii wa aina hii hupendelewa na watalii wa ndani na nje. Katika kipindi cha kati ya mwaka 2004/2005 na 2006/2007, jumla ya watalii 1,872,195 walitembelea hifadhi za Taifa ambao kati yao wageni walikuwa ni 1,130,886 na Watanzania 741,309 ambao ni asilimia 40 ya wageni wote waliotembelea hifadhi za Taifa katika kipindi hicho. Kulingana na takwimu hizi ni kweli kuwa idadi ya Watanzania wanaotembelea vivutio hivyo ni ndogo ukilinganisha na wageni.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na taasisi zake, katika jitihada ya kusaidia kuwajengea Watanzania utamaduni wa kutembelea mbuga zetu hatua za makusudi zimechukuliwa zikiwemo ifuatavyo:-

(i) Kushiriki katika maonyesho ya Saba Saba na Nane Nane yanayofanyika kila mwaka;

(ii) Kuandaa safari *(Promotion Tours)* kutembelea mbuga ya mikumi wakati wa maonyesho ya Saba Saba kwa kiasi cha Sh. 10,000 kwa mtu mmoja. Katika maonyesho ya mwaka huu Watanzania 777 wametembelea hifadhi ya Mikumi;

(iii) Kuchapishwa vipeperushi kwa lugha ya Kiswahili kwa lengo la kuwaelimisha wananchi;

(iv) Kuweka utaratibu wa wanafunzi na watoto kuingia bure katika mbuga zetu. Vilevile *hostel* zilizojengwa kwenye hifadhi hutoa huduma ya malazi bure kwa wanafunzi. Aidha, Watanzania hulipa kiasi cha Sh. 5,000/= kwenye mabanda *(tourist bandas)* wakati wageni hilipa *USD* 20 kwa siku;

(v) Kuhamasisha na kusaidia wanafunzi wa shule za sekondari na vyuo kuandika *writer up* au *projects* zao za shule kuhusu sekta ya utalii ambapo kwa mwaka 2006/2007 jumla ya wanafunzi 290 walisaidiwa;

(vi) Kuhamasisha wamiliki wa shule za msingi na sekondari kuandaa safari za kuwapeleka wanafunzi kutembelea maeneo ya vivutio vya utalii;

(vii) Viwango vya ada vinavyotozwa Watanzania wanaotembelea hifadhi zetu ni wastani wa Sh. 1,500/= kwa Mtanzania wa umri wa miaka 16 na zaidi na Sh. 500/= kwa umri wa miaka 5 hadi 16.

Kiwango kinachotozwa kwa wageni katika hifadhi hizo ni wastani wa dola za kimarekani 10 hadi 60 sawa na takribani Sh. 60,000/=.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kuwahamasisha Waheshimiwa Wabunge kutembelea maeneo yetu ya utalii ili waweze kutusaidia kuhamasisha zaidi

wananchi, hivyo kukuza uelewa wa hazina tuliyonayo na kuwa na utamaduni vivutio vya utalii zikiwemo mbuga za wanyama

MHESHIMIWA DORA H. MUSHI: Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, naomba kuuliza maswali mazuri ya nyongeza:-

(a) Kwa kuwa, Mbuga nyingi za wanyama ziko mbali na Mijini na kwa kuwa watu wengi wanapenda kutembelea kule lakini kupata usafiri ni kazi ngumu, aidha, labda kukodisha yale magari ya utalii: Je, Wizara sasa haiwezi kuona umuhimu wa kutenga mabasi ambayo yanaweza kupatikana angalau kila mwezi mara moja ili wananchi wengi wavutiwe kwenda kuona mbuga zao wenyewe?

(b) Kwa kuwa Wabunge wengi hatujawahi kwenda kutembelea Mbuga za wanyama: Je, Wizara haiwezi kuwapa Wabunge *offer* ili baada ya kipindi hiki cha bajeti waweze kutembelea Mbuga za wanyama hasa Mbuga ya Serengeti ambayo ina wanyama wengi ili nao pia waweze kuja kuhamasisha wananchi waweze kupenda kutembelea mbuga zao?

SPIKA: Kwa swali moja dogo la pili, Ofisi ya Bunge inahusika. Kwa hiyo, hakuna haja ya kutafuta *offer* kwa Maliasili, tutatengeneza utaratibu ili muweze kufika lakini itabidi mjiorodheshe. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii na utalii, kwanza naomba nikushukuru sana kwa kujibu au kufafanua swali la pili la Mheshimiwa Dora Mushi.

Naomba kujibu swali lake la kwanza kwa kifupi kwamba kwa muda mrefu wa nyuma, Wizara yangu imekuwa ikilenga zaidi katika kushirikisha sekta binafsi kwa sababu sekta ya utalii haiwezi ikakua kwa nguvu za Serikali peke yake, kwa hiyo, huduma nyingi zinazotolewa katika sekta hii zikiwemo mahoteli, usafiri pamoja na *Tour Guiding Services* zimekuwa zikitolewa na sekta binafsi.

Lakini kutokana na shinikizo au *interest* kubwa ya wananchi kujengeka ya kutaka kushiriki zaidi katika eneo hili, tumepokea wazo lake tutashirikiana na wenzetu wa *TTB* kuona ni jinsi gani tunaweza tukaweka utaratibu huo. Utaratibu utakuwa ni wa kulipia lakini angalau kwa na *rates* ambazo siyo za faida kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunashukuru Mheshimiwa Mbunge wazo lako tutalifanyia kazi.

Na. 262

Kutimiza lengo la Ajira Milioni Moja, 2010

MHESHIMIWA ANASTAZIA JAMES WAMBURA aliuliza:-

Kwa kuwa, lengo la Serikali ni kuona kuwa ajira mpya zaidi ya milioni moja zinapatikana ifikapo mwaka 2010 na kwa kuwa eneo la kuajiri ndiyo lenye nafasi nyingi za ajira kwenye nchi yetu:-

Je, mpaka sasa Serikali imewezesha wananchi wangapi hasa vijana na wanawake kujiajiri vijijini na mijini?

WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalumu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu za utafiti wa nguvu kazi za mwaka 2006, na taarifa za kiutawala *(Administrative Routine Data)* kutoka Wizara Halmashauri za Jiji, Manispaa, Miji, Wilaya na Taasisi za Serikali zinazoonyesha kuwa kuanzia kipindi cha Januari, 2006 hadi Juni, 2008, jumla ya ajira mpya zinazojumuisha vijana na wanawake ni 474,849 kama ifuatavyo:- Sekta ya umma 96,043, sekta binafsi rasmi 183,789 na sekta binafsi isiyo rasmi na kilimo 195,017.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu inafanya uchambuzi wa taarifa ya utafiti wa mapato na matumizi ya kaya binafsi *(Household Budget survey)* ya mwaka 2007, ambayo matokeo yake yatakapotolewa rasmi yatatoa hali halisi ya ajira nchini ikiainisha mchanganuo wa sekta za umma, binafsi zilizo rasmi na zisizo rasmi, pia ajira za vijijini na mjini na pia idadi ya vijana na wanawake waliopo katika ajira

MHESHIMIWA ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Namshukuru pia Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini pamoja na majibu yake mazuri ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa, katika kuwawezesha wananchi kujiajiri Serikali imekuwa ikiweka kipaumbele kwa wale ambayo ni wajasiriamali wadogo na vikundi vya *SACCOS*, lakini kwa hali halisi wapo wananchi wengi tu ambao siyo wajasiriamali na vilevile hawana uwezo wa kujiunga na *SACCOS*. Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati wa kupanga mkakati maalumu kwa ajili ya makundi haya?

(ii) Kwa kuwa, *TASAF* hasa katika Mkoa wa Mtwara imeonyesha mfano mzuri sana kwa kuwawezesha wanawake kujiajiri wale ambao wanaishi na virusi vya UKIMWI kupitia mradi wa maziwa na baadhi ya kundi la vijana ambao walikuwa

wanajihusisha na uhalifu imewawezesha kujiajiri kwa mradi wa matofali: Je, ni kwa nini Serikali isitumie *TASAF* ili kusudi iweze kuviwezesha vikundi vingi vya aina hii?

WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Anastazia Wambura kama ifuatavyo:-

(i) Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anasema wananchi wengi sio wajasiriamali na hawana uwezo wa kujiunga na *SACCOS*, mimi sidhani kama kauli hiyo ni sahihi. Kama kuna mwananchi ambaye hatamani kutengeneza kipato atakuwa ni mwananchi wa ajabu. Wananchi wote wana matumaini ya kutengeneza kipato, tatizo ni namna ya kutoka hapo kwenye mipango yao mpaka kufikia hayo malengo yao, ndiyo maana Serikali ina mipango ya aina mbalimbali. Kama nilivyozungumza jana, tunao mpango wa kukuza ajira nchini, lakini vilevile hata hawa ambao wanakaa kijijini kabisa tuna mpango kabambe wa sekta ya kilimo ambayo Mheshimiwa Waziri ataufafanua leo vizuri zaidi ili kuhakikisha nao wanaingizwa katika mchakato mzima wa kuingia katika uzalishaji mali ili kuboresha maisha yao.

(ii) Mheshimiwa Spika, wanawake wa Mtwara wenye virusi vya UKIMWI jinsi ambavyo wamesaidiwa na *TASAF* na vilevile na vijana ambao walijiingiza katika magenge ya wizi lakini sasa hivi baada ya *TASAF* kuja mahali pale hali yao imekuwa nafuu; nataka nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba hili ndilo lilikuwa lengo hasa la kuanzisha Mfuko wa *TASAF* na Serikali ili iweze kutoa ajira vijijini na kama Mtwara tumefanikiwa, mimi nina hakika na sehemu nyingine tutakapochukua takwimu tutaona mafanikio makubwa ya *TASAF*.

Ndiyo maana tunasema watu wanapobuni mradi wa *TASAF*, kwanza kuna uwiano kati ya wanawake katika Kamati ile kuhakikisha hata jinsia inazingatiwa, lakini vilevile tunahakikisha kwamba asilimia 40 ya mradi ule nguvu kazi yake itoke katika kijiji husika. Kwa hiyo, mimi nashukuru sana kupata taarifa hii.

MHESHIMIWA LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kumekuwepo na malalamiko mengi ya muda mrefu kwa vijana wa hapa Tanzania ambao wamekuwa wakikosa nafasi katika taasisi za kimataifa ikiwemo umoja wa Mataifa ambapo tatizo kubwa limekuwa ni kwamba wana vigezo kwa maana ya kwamba elimu nzuri wanayo, lakini suala la lugha nyingi imekuwa ni tatizo ambalo limekuwa likisababisha watu wa mataifa ambayo yanazungumza lugha ya Kifaransa na lugha nyingine kuchukuliwa kuliko sisi ambao tunazungumza Kiingereza na Kiswahili: Je, kwa nini Wizara hii haioni ni busara sasa kuwasiliana na Wizara ya Elimu kuongeza lugha za kufundishia mashuleni badala ya kukazania Kiingereza tu peke yake na Kiswahili na vilevile kuwashawishi viongozi kutokuendelea na masuala ya mkakati wa kuboresha Kiswahili zaidi badala ya kuongeza lugha nyingine za Kimataifa?

WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lucy Mayenga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tuna tatizo la lugha kwa vijana wetu na ndiyo maana inasikitisha sana inapofika mahali kwamba hata baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanadhani kwamba njia sahihi ni kufuta hata kile Kiingereza kidogo kinachofundishwa katika shule zetu, mimi nilipokuwa Waziri wa Elimu nilikataa hoja hii ya kufuta Kiingereza kwamba sasa watoto wetu wafundishwe moja kwa moja kwa Kiswahili mpaka *University*. Bahati nzuri akaja Mheshimiwa Mungai akakataa, akaja Mheshimiwa Magreth Sitta akakataa, leo Mheshimiwa Maghembe kwa bahati nzuri nilikuwa nasikiliza alikuwa akizungumza nadhani Mtwara au Mafia sikumbuki vyema lakini kuna sehemu moja yupo anatembelea hivi sasa, ameanzisha programu maalum ya kuhakikisha kwamba lugha sasa inafundishwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuondokana na tatizo kwa kulikimbia tatizo. Kama tumegundua kwamba tuna udhaifu wa kuzungumza Kiingereza, kama tumegundua kwamba tuna udhaifu wa kuzungumza Kifaransa ni kutafuta dawa kwa nini Kiingereza kimeporomoka na kwa nini hatusomi Kifaransa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo hilo sio tu kazi za Kimataifa, hata katika hoteli zetu za nyota tano, tunayo matatizo ya Watanzania walio wengi wanashindwa kupata ajira kwa sababu wameshindwa kumudu lugha za mawasiliano pale. Kwa hiyo natoa wito kwa vijana wetu katika nchi ya Tanzania sasa hivi ni wakati muafaka wa kuchangamkia lugha zaidi ya Kiswahili, watu wazungumze Kifaransa na Kiingereza vizuri, Kiswahili tunakuwa nacho upende usipende Kiswahili utakijua tu. *(Makofi)*

Na. 263

Miradi ya Kupeleka Umeme Vijini

MHESHIMIWA DR. FESTUS B. LIMBU K.N.Y (MHESHIMIWA DR. RAPHAEL M. CHEGENI) aliuliza:-

Kwa kuwa, ahadi ya Serikali ya kupeleka umeme katika vijiji vya Kalemera, Nyamikoma, Kabita, Nyakaboja hadi Nyashimo na kutoka Lamadi kwenda Hospitali ya Mkula, Malili hadi Ngasamo imekuwa ikitolewa kila mara hapa Bungeni:-

Je, utekelezaji wa miradi hiyo umefikia wapi hadi sasa? Kama bado, kwa nini?

WAZIRI NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Raphael Masunga Chegeni -Mbunge wa Busega kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika Mkutano wa Nane - Kikao cha Saba cha Bunge kilichofanyika tarehe 21 Juni 2007 wakati wa kujibu swali Na. 65 la Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni lililohusu utekelezaji wa mradi wa umeme Busega, Serikali iliahidi kuwa ingevipatia umeme vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge chini ya mradi ujulikanao kama *Spanish Phase III C for Rural Electrification* uliokuwa chini ya ufadhili wa Serikali ya Ufalme wa Hispania na kupitia bajeti ya ndani ya *TANESCO*. Kwa bahati mbaya mradi huu haukupata fedha kutoka kwa mfadhili wala *TANESCO*, hivyo kuathiri utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa vijiji vya Nyamikoma, Mkula, Malili na Ngasamo pamoja na Ngasamo *ginnery* na Hospitali ya Mkula vinapatiwa umeme chini ya mradi wa *electricity V* kwa kutumia fedha za mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*). Kiasi kilichotengwa kwa ajili ya mradi wa *electricity V* wa kupeleka umeme katika Mikoa ya Mwanza na Shinyanga (Magu-Bariadi) ni dola za marekani 5,495,626.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizopangwa kuetekelezwa kwa mwaka 2008/09 ni pamoja na ujenzi wa njia kubwa ya umeme yenye urefu wa kilomita 104 na njia ndogo ya umeme yenye urefu wa kilomita 121 pamoja na *substation* 32, kama miundombinu ya usafirishaji na usambazaji umeme katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba utekelezaji wa azma hii unaendelea vizuri kwa vile utekelezaji wa mradi unaanza mwisho wa mwezi huu wa Julai, 2008 kama tulivyoeleza kwenye bajeti yetu wakati tunawasilisha.

MHESHIMIWA FESTUS B. LIMBU: Mheshimiwa Spika, napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri na nimpongeze kwa jitihada kubwa anayofanya na uwezo mkubwa aliodhihirisha katika Wizara hii ya Nishati na Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Magu hususani katika vijiji ambavyo vimetajwa vya Kalemela, Nyamikoma, Kabita, Nyakaboja, Nyashimo, Lamali na Hospitali Kuu ya Mkula kwa muda mrefu sana wamekuwa wakiona umeme unapita juu kwenye nyaya,

kama swali lilivyoulizwa, Serikali imekuwa ikitoa ahadi muda mrefu kwamba umeme utapelekwa.

Pia, Serikali imeahidi kwamba itapeleka umeme kutoka Magu kwenda Lumeji, Ng'aya, Kabila pamoja na Mahaha. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema mradi huu unaanza kutekelezwa mwezi huu Julai:

Je, tayari makandarasi wako *site*, kwenye maeneo na kwamba tutakapomaliza kikao cha Bunge tayari wananchi wataona juhudi zinafanyika?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, namshukuru kama nilivyoelezwa wakati nawasilisha bajeti yetu ni kwamba utekelezaji wa miradi yote ambayo inafadhiliwa na *African Development Bank* ikiwemo Wilaya za Magu na Bariadi na Mkoa wa Arusha kwamba utekelezaji unaanza mwezi wa saba.

Tunaposema hatua ya kwanza kabisa ni kuwapata wakandarasi na tulieleza kwenye kitabu chetu cha mawasilisho ya bajeti, uanzaji tunaosema ni pamoja na hatua ya awali kabisa ya kuwapata wakandarasi.

Kwa hiyo, ndiyo hatua ambayo tunaanza nayo na inaanza hasa mwishoni mwa mwezi huu.

Na. 264

Vyeti vya Wahitimu Elimu ya Msingi 1990

MHESHIMIWA GOSBERT B. BLANDES K.N.Y(MHESHIMIWA DIANA M. CHILOLO) aliuliza:-

Kwa kuwa wanafunzi waliomaliza elimu ya msingi mwaka 1990 nchi nzima hawakupata vyeti: Je, Serikali inasema nini juu ya tatizo hilo?

MHESHIMIWA GAUDENSIA M. KABAKA-NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kumbukumbu zilizopo zinaonyesha kuwa, mwaka 1990 hapakuwepo na matatizo ya upatikanaji wa vyeti vya kuhitimu elimu ya msingi nchini. Upungufu mkubwa wa vyeti ulikuwepo katika mwaka 1993 na 2002 uliotokana na ucheleweshaji uliofanywa na mchapaji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa vyeti hivyo, Serikali ilichukua hatua za makusudi za kulimaliza tatizo hilo kwa kuchapisha vyeti vya kutosha na kuvisambaza katika Halmashauri zote. Hata hivyo, endapo kulitokea matatizo ya

upatikanaji wa vyeti kwa baadhi ya maeneo, tunaomba tupate taarifa kupitia Halmashauri husika ambako ndiko vinakogawiwa vyeti hivyo ili kuona namna ya kushughulikia.

MHESHIMIWA JUMA S. N'HUNGA: Mheshimiwa Spika nakushukuru. Kwa kuwa mwuliza swali ameulizia kuhusu vyeti vya darasa la saba na kulingana na dunia ya hivi sasa, darasa la saba imekuwa ni elimu ndogo sana: Je, Wizara itakubaliana nami sasa kwamba elimu ya lazima iwe mpaka darasa la kumi na mbili?

MHESHIMIWA GAUDENSIA M. KABAKA-NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, hadi sasa philosophia ya elimu yetu haijabadilika. Kwa hiyo, elimu ya lazima au *compulsory education* hadi sasa ni darasa la saba, isipokuwa elimu ya sekondari badala ya kuwa asilimia ndogo, asilimia inaongezeka mwaka hadi mwaka. Sasa hivi tumeshafikia zaidi ya asilimia 90 ya wanaomaliza darasa la saba.

Kwa hiyo, tunaweza tukaita bado elimu ya msingi ndiyo *compulsory education*.

Na. 265

Uwezeshaji wa Wananchi

MHESHIMIWA DEVOTA M. LIKOKOLA aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ina nia kubwa ya kuwezesha kiuchumi wananchi nchini kote:-

(a) Je, Serikali ipo tayari kuanzisha vituo na mabaraza ya kuwawezesha wananchi katika Mikoa yote nchini?

(b) Je, lengo la Serikali ni kuwawesha wananchi wangapi ifikapo 2010?

MHESHIMIWA OMAR YUSSUF MZEE - NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, kwanza napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Devota kwa kuwa karibu na wananchi wa Mkoa wa Ruvuma hasa katika suala la uwezeshaji. Baada ya pongezi hizo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Devota Likokola - Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, baada ya kuanzisha Mfuko wa Uwezeshaji Wababchi kiuchumi na kuongeza ajira kwa kutoa mikopo yenye masharti nafuu, Serikali ilianzisha mfumo wa kusimamia na kutuatilia utekelezaji wa mfuko huo kwa kuunda Kamati katika ngazi mbalimbali utendaji wa mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vituo na Mabaraza ya uwezeshaji ngazi ya Mkoa yanapendekezwa na Mheshimiwa Mbunge vinaelekea kuwa na mtazamo nyongeza (*extra dimension*), pendekezo la Mheshimiwa Likokola ni chachu kwa Wizara yangu, napenda

kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana pamoja na TAMISEMI tutalifanyia kazi baada ya kupata maelezoya ziada au uzoefu wa nchi nyingine ili kuona kama linaweza kuingizwa kwenye mfumo ulioko sasa.

(b) Mheshimiwa Spika, kupitia Mfuko wa Uwezeshaji wananchi Kiuchumi na kuongeza ajira, hadi ifikapo mwaka 2010, Serikali imepanga kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu wananchi wapatao 200,000.

MHESHIMIWA DEVOTA M. LIKOKOLA: Mheshimiwa Spika ahsante, nashukuru sana kwa majibu mazuri ambayo Mheshimiwa Waziri ameyatoa. Nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Mheshimiwa Rais alitamka kwamba kuna Mikoa sita Tanzania iko nyuma kimaendeleo, nayo ni Ruvuma, Rukwa, Kigoma, Tabora, Lindi na Mtwara: Je, Serikali iko tayari kuanza kwanza kuwawezesha wananchi wa Mikoa hii kwa haraka ili kuleta uwiano wa maendeleo Tanzania?

(b) Kwa kuwa Serikali ilitumia fedha na gharama kubwa kuwapeleka wataalam wa vikoba kwenda kujifunza namna ya uwezeshaji wa wananchi Bangladesh:

Je, Mheshimiwa Waziri kwa kuwa amesema atashirikiana na Waziri wa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Ajira na TAMISEMI yupo tayari pia kushirikiana na mimi kwa karibu zaidi ili tuende tukaone uwezeshaji wa wananchi katika nchi za nje?

MHESHIMIWA OMAR YUSSUF MZEE-NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Devota kama ifuatavyo:-

Kwanza, nataka niseme kwamba, Serikali ilitoa bilioni moja kwa kila Mkoa. Hadi hivi sasa bado hatujafanya tathmini kuona hali halisi ikoje.

Nadhani ushauri wa Mheshimiwa Mbunge ni mzuri, lakini atuachie kwanza tufanye tathmini tuone kwamba hii Mikoa ambayo iko nyuma tumekwendaje na ile mikopo na baadaye tunawezaje tukalitekeleza lile ombi lake.

Mheshimiwa Spika, swali la pili nakubaliana naye kusafiri naye kwenda kuangalia vikoba Bangladesh. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Majibu ya maswali mengine haya naona yanapojibiwa yanakuwa na maslahi ndani yake. *(Kicheko)*

Na. 266

Mfumko wa Bei

MHESHIMIWA JUMA ABDALLAH NJWAYO aliuliza:-

Kwa kuwa changamoto kubwa iliyopo sasa nchini na hasa katika Jimbo la Tandahimba ni tatizo la mfumko wa bei *(inflation)* kwa bidhaa za ujenzi kama vile bati, saruji na hata vyakula:-

Je, Serikali inachukua hatua gani za dharura kukabiliana na hali hiyo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHESHIMIWA OMAR Y. MZEE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo - Mbunge wa Jimbo la Tandahimba, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Njwayo kuwa Serikali na wananchi kwa ujumla tunakabiliwa na changamoto kubwa ya tatizo la mfumko wa bei hasa za bidhaa muhimu kama vile vyakula na vifaa vya ujenzi. Mfumko wa bei kwa ujumla uliongezeka kutoka asilimia 5.9 mwezi Juni, 2006 hadi kufikia asilimia 9.7 Aprili, 2008. Hali nii ilichangiwa zaidi na uzalishaji mdogo wa mazao ya chakula hapa nchini na duniani kwa ujumla hasa kwa mazao ya nafaka.

Aidha, kupanda kwa bei ya mafuta katika Soko la Dunia pamoja na kuongezeka kwa bei ya umeme hapa nchini kwa sehemu kubwa kumechangia mfumko wa bei za bidhaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na vifaa vya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Njwayo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kukabiliana na mfumko wa bei. Hatua zilizochukuliwa na zinazoendelea kuchukuliwa ni kama zifuatavyo:-

(a) Kuzuia kuuza mazao ya chakula nje ya nchi hasa mahindi na mchele;
(b) Kuruhusu kwa muda kuingiza mahindi na mchele bila ya ushuru;

(c) Kuimarisha kilimo hasa mazao ya chakula kwa kuongeza kiwango cha ruzuku ya pembejeo;

(d) Kuendelea kuboresha miundombinu ili kurahisisha usambazaji wa pembejeo kwa lengo la kupunguza gharama za usafirishaji;

(e) Kuzihamasisha Halmashauri kuangalia maeneo yao ya kilimo na kuhakikisha kuwa yanalimwa ipasavyo;

(f) Mnamo mwezi Januari 2008, Serikali ilitoa msaada wa tani 625 za chakula kwa wasio na uwezo, tani 5,000 za mahindi kuuzwa kwa Tsh. 50 kwa kilo (ruzuku) na tani 32,000 za mahindi kusambazwa na kuuzwa katika soko la ndani;

(g) Kusitisha uuzaji wa saruji nje ya nchi kwa lengo la kukidhi mahitaji ya ndani;

(h) Kuendeleza mazungumzo na wawekezaji kwa lengo la kuwekeza kiwanda cha saruji katika Mkoa wa Mtwara.

(i) Kutungwa kwa Sheria ya Petroli ambayo imetoa fursa ya kuagiza mafuta kwa jumla *(bulk procurement*), ambayo itasaidia kupunguza kupanda mara kwa mara bei ya mafuta; na

(j) kuhamasisha sekta binafsi kuzalisha nishati mbadala pamoja na kuihamasisha jamii kutumia gesi na makaa ya mawe.

Mheshimiwa Spika, kutokana na juhudi za Serikali, pamoja na wananchi na juhudi zinazochukuliwa na nchi nyingine, kuna matarajio makubwa kwa bei za bidhaa muhimu hasa chakula kupungua na hivyo kuufanya mfumko wa bei kushuka.

MHESHIMIWA JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

La kwanza, kwa kuwa, katika majibu yake ya msingi ameeleza pamoja na mambo mengine kukubali kuwa mfumko wa bei unachangiwa sana na uzalishaji mdogo wa mazao; na kwa kuwa kilimo ndiyo kinachoajiri Watanzania wengi; na kwa kuwa vijana wengi hukimbia vijijini kwenda Mjini ambako ndiko kuna ajira: Je, Serikali inafanya nini ili kuleta miundombinu ya kilimo ya kutosha kule vijijini ili wananchi waweze kuzalisha mazao ya kilimo kwa usahihi?

La pili, kwa kuwa, aliyekuwa Katibu Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Masasi katikati ya miaka ya 80 ambaye sasa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kushirikiana na aliyekuwa na Mkuu wa Wilaya Ndugu yangu Jack Mwambe ambaye ni Balozi wetu Urusi walitengeneza mkakati mzuri wa kuhakikisha wananchi wa Wilaya ile ya Masasi wanakuwa na mazao ya kutosha; Mpango uliokuwa unajulikana kwa jina la Hojama: Je, kwa nini sasa Serikali isijaribu kuurudisha mpango ule Tanzania nzima ili kuhakikisha kila kaya inakuwa na angalau ekari moja ya mazao ya chakula ili tuondokane na tatizo hili lililoko sasa? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHESHIMIWA OMAR Y. MZEE): Mheshimiwa Spika, kwanza, suala la miundombinu ya kilimo vijijini, hili ni suala ambalo Serikali hivi sasa inaliangalia kwa undani zaidi ili kuweza kuimarisha suala zima la mazao ya kilimo. Kwa upande wa barabara, Serikali inaangalia barabara zinazokwenda vijijini. Kwa upande wa miundombinu, kama umwagiliaji vile vile Serikalil inaliangalia hili na kwa maelezo zaidi, Wizara ya Maji na Umwagiliaji itakapowasilisha hotuba yake italitolea ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, la pili, suala la mpango ambao ameuelezea nakubaliana naye. Katika mapinduzi ya kilimo, mipango yote ambayo italeta tija ni muhimu kuifuata na hili litakuja kuelezwa kwa vizuri zaidi na Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika atakapowasilisha hotuba yake leo hii.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda hautoshi, leo tuna mambo mengi kidogo mniwie radhi. Maswali yamekwisha na muda wa maswali umepita. Kwa hiyo, kama ilivyo desturi yetu, basi ni matangazo mafupi.

Kwanza ni wageni, nafurahi kutangaza kuwepo kwa Mama Florence Wasira, mke wa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, yule pale upande wa kushoto. Ahsante na karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, ni Bwana Peniel M. Lyimo - Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, yule pale karibuni sana. Bibi Sophia Kaduma - Naibu Katibu Mkuu yule pale, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nafurahi pia kuwatambulisha Wakurugenzi mbalimbali na Wakuu wa Idara na Vitengo wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Bwana Emmanuel Achayo, naomba asimame Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Dr. Jeremiah Haki - Mkurugenzi wa Utafiti na Mafunzo, Dr. Nicodemus Shirima - Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mazao, Bibi Lilian Mafa - Mkurugenzi wa Utawala na Utumishi, Bwana John Mgondo - Kaimu Mkurugenzi Usalama wa Chakula, ndiye anatuhakikishia tunashiba huyu, Bwana P. Tarimo - Mkurugenzi wa Matumizi ya Ardhi, yule pale, Dr. A. Kashurinza - Mkurugenzi wa Ushirika, yule pale na Bwana J.J. David - Mkaguzi Mkuu wa Ndani, yule pale. Karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia Wenyeviti wa Bodi za Mazao na Taasisi yupo Mzee Ernest Mulokozi - Mwenyekiti wa Bodi ya Kahawa Tanzania yule pale. Nashukuru Bwana Mulokozi kukuona upo imara kabisa. Bwana E. Moyo - Mwenyekiti wa *TASO* Taifa. Ahsante sana. Waliobaki ni Watendaji mbalimbali wa Wizara. Karibuni sana kwa kumsaidia Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwenye hotuba yake muhimu ya leo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wengine ni wageni wa Mheshimiwa *Engineer* Christopher Chiza - Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, ni Bwana Damian David Ruhinda - Mbunge wa kwanza wa Jimbo la Buyungu mwaka 1965 hadi 1970 karibu sana miaka 43 iliyopita. Ahsante sana Ndugu Ruhinda. Sasa hivi ndugu Ruhinda ni

Mwenyekiti wa Bodi ya Mkonge, pia *Sisal Association of* Tanzania. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wa Dr. James Msekela - Mbunge wa Tabora Kaskazini na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, yupo Bibi N. Msekela ambaye ni mkewe yupo upande huu wa kulia, ahsante na karibu sana. Pamoja na vijana wake ndugu Debora na James, naona huyu atakuwa James *junior* huyu! Ahsanteni sana na karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wa Mheshimiwa Ameir Ali Ameir ambao ni kutoka Jimbo lake la Fuoni. Wa kwanza ni Bwana Yussuf Hassan - Muweka Hazina Jimbo la Fuoni, yule pale karibu sana na wengine ni Bi. Mariam Maleo, Bi. Tatu Maligumu, Bwana Constantine Thobias, Bwana Ali Philip na Bwana Razamu Paschal. Karibuni sana wageni wetu kutoka Zanzibar na tunafurahi sana kuwaona hapa Bungeni Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia Mheshimiwa *Commissioner* Abdulkarim Hassan Shah ana mgeni wake ambaye ni Bwana Warihi Ali Aboud Mzee naona hili ni jina la Zanzibar, lakini inawezekana likawa la Mafia pia. Karibu sana, kama ni Mafia au Zanzibar, karibu sana hapa Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mwisho tunao wanafunzi 50 kutoka Shule ya Sekondari ya Kikuyu, nadhani ndiyo wapo mkono wa kulia pale. Ahsante sana vijana wetu. Tunawatakia mafanikio katika masomo, nchi yetu inawahitajini sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, leo tutakuwa na tukio maalum la kumpokea Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Dr. Asha-Rose Migiro.

Taarifa niliyonayo ni kwamba Naibu Spika, amekwishakwenda kumpokea na atafika katika maeneo ya Bunge saa 5.25, ataonana na Mheshimiwa Waziri Mkuu, baada ya hapo saa 6.10 tutampokea hapa ndani ya Ukumbi na atatuhutubia. Baada ya hapo, basi ratiba yake itaendelea. Saa 9.00 mchana tutahamia Ukumbi wa Pius Msekwa ili tuwe na kipindi cha kubadilishana naye mawazo, kitu ambacho tusingeweza kwa utaratibu kukifanya humu ndani ya Ukumbi. Itakuwa saa 9.00 hadi saa 10.00, lakini hapo hapo katika Ukumbi wa Pius Msekwa ambapo tunawaomba Waheshimiwa Wabunge wote tujitahidi kuwepo na kwa muda maana yake ni saa moja tu.

Basi pale Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Bunge pamoja na Ma-*commissioner* wa Tume wataweka saini ile azma yetu ya Kupambana na Ukatili Dhidi ya Wanawake kama lilivyo Azimio la Umoja wa Mataifa.

Kwa hiyo, tunawaomba Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge na wana-Tume ili tuokoe muda, tafadhali wawe na kalamu zao. Wataweka saini na baada ya kuweka saini, basi tutamshirikisha mgeni wetu rasmi Dr. Asha-Rose Migiro aweze kukabidhi hivyo vyeti tutakavyotia saini kuonyesha nia yetu na azma yetu ya kuendeleza Mapambano Kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Katibu amefanya utaratibu Makamishna wa Tume na Wenyeviti wakae ile mistari ya mbele itarahisisha zaidi pale sasa kutoka na kukabidhiwa na kurejea na Mheshimiwa Waziri Mkuu tutamshirikisha kwenye hilo kwa sababu yeye ndiye Kiongozi wetu, basi aweze naye kuweka saini.

Sasa kwa madhumuni hayo basi, ili mgeni huyo aweze kuingia humu Ukumbini, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi nadhani ndiye anayesimama kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Masuala ya Bunge asimame kutoa Hoja ya Kutengua Kanuni kupitia Kanuni ya 150 azijumuishe Kanuni ya 69 na Kanuni ya 140 ili tuweze kumruhusu mgeni huyo kuingia Ukumbini. Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

HOJA YA KUTENGUA KANUNI

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, kwa kutumia kanuni ya 150 napenda kutoa hoja kwamba tutengue muda ukifika, kanuni Na. 140 kifungu (f) inayozuia wageni wasiingie ndani ya Ukumbi, sasa Bunge likubali Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa aingie ndani ya Ukumbi na ahutubie Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Bunge lilipitisha utenguzi wa kanuni Na. 140 (f) ili kumruhusu Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (Mheshimiwa Asha-Rose Migiro aingie ndani ya Ukumbi na Kulihutubia Bunge)

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

(Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2008
(The Finance Bill, 2008)

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

(Muswada Uliotajwa hapo juu ulisomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa ufafanuzi tu Muswada wa Fedha, *(Finance Bill 2008)* tangu umegawiwa sasa ndiyo umetimiza siku 21 ndiyo unasomwa kwa mara ya kwanza. Mlikwishagawiwa lakini ulikuwa bado haujatimia siku zile 21 za Sheria zinavyohitaji. Kwa hiyo, sasa ndiyo umesomwa kwa mara ya kwanza.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 – Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo Mifugo na Maji inayohusu Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika, sasa lijadili na kukubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika kwa mwaka wa Fedha wa 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nitumie fursa hii kuungana na Watanzania wenzangu, kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika. Kuchaguliwa kwake na mchango wake alioutoa tangu kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa Umoja huo umelijengea Taifa letu heshima kubwa katika medani ya kimataifa.

Aidha, uongozi wake na juhudi zake za kupambana na maovu katika jamii yetu, licha ya kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi wa Mwaka 2005 ni kielelezo dhahiri kuwa ni kiongozi anayejali haki na maendeleo ya nchi yetu. Juhudi zake hizo zimedhihirisha uwezo wake mkubwa wa kuongoza na utumishi wake uliotukuka aliouonyesha katika nyadhifa mbalimbali alizowahi kushika katika Serikali na Chama cha Mapinduzi. Wananchi wanaendelea kuwa na imani na matumaini makubwa kwa uwezo wake katika kuliongoza Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (MB) kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Uteuzi huo, unadhihirisha imani kubwa aliyonayo Rais kwa utendaji wake aliouonyesha katika kutenda na kusimamia kazi katika nyadhifa alizowahi kushika. *(Makofi)*

Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa, Mheshimiwa Jenista Mhagama - Mbunge wa Peramiho na Mheshimiwa Zuberi Ali Maulid - Mbunge wa Kwamtipura, kwa kuchaguliwa kuwa wenyeviti wa Bunge. Katika kipindi hiki kifupi wameonyesha uwezo mkubwa katika kuliongoza Bunge vizuri.

Aidha, nampongeza Mheshimiwa Profesa Feetham Philipo Banyikwa kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapema mwezi Mei, 2008, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya mabadiliko madogo katika Baraza la Mawaziri. Katika mabadiliko hayo, Rais aliniteua kwa mara nyingine kuwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. Napenda kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa imani yake kwangu na kuahidi kwa mara nyingine kuwa imani hiyo ya Rais, nitaitumia kuitumikia nchi yetu kwa uaminifu, juhudi na maarifa. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Cellina Kombani (MB) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi *OWM* - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Mheshimiwa Profesa Peter Msolla (MB) kuwa Waziri wa Mawasiliano Sayansi na Teknolojia na Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa (MB) kuwa Waziri wa Miundombinu.

Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Aggrey Mwanri (MB) kuwa Naibu Waziri OWM - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Mheshimiwa Hezekia Chibulunje (MB) kuwa Naibu Waziri wa Miundombinu na Dr. Milton Mahanga (MB) kuwa Naibu Waziri wa Kazi Ajira na Maendeleo ya Vijana. Nawatakia wote mafanikio katika nyadhifa zao mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia Waheshimiwa Dr. Christine Ishengoma (MB) na Mheshimiwa Mchungaji Getrude P. Rwakatare kwa kuteuliwa kuwa Wabunge Viti Maalum, Mheshimiwa Ole Nangoro (MB), kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Kiteto na Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Bunge lako Tukufu lilipata msiba wa aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto - Marehemu Salome Mbatia na aliyekuwa Mbunge wa Kiteto - Marehemu Benedict Losurutia. Nachukua fursa hii kuwapa pole ndugu, jamaa na marafiki wa familia za Marehemu hao. Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu hao mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru viongozi wetu wa ngazi za juu wa Serikali ya Awamu ya Nne kwa kukipa kilimo msukumo unaostahili. Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, amekuwa akisisitiza mara kwa mara kuhusu umuhimu wa kilimo, hususan utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo nchini *(Agricultural Sector Development Programme - ASDP)* na Programu ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika *(Cooperative Reform and Modernization Programme-CRMP)*. Katika ziara zake, Mheshimiwa Rais amekuwa akitoa maelekezo ya namna kilimo kinavyotakiwa kuendelezwa ambapo amekuwa akisisitiza umuhimu wa kuwa na Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(District Agricultural Development Plans – DADPs)* iliyoandaliwa kwa umakini na kwa kuwashirikisha wakulima, wafugaji na wanaushirika. Kwa mfano, katika hotuba yake kwenye siku ya kilele cha Sherehe za Nane Nane tarehe 8 Agosti, 2007, Rais aliagiza maeneo ya kuzingatiwa ili kilimo kikue kwa kasi itakayotoa mchango mkubwa zaidi katika maendeleo ya Taifa.

Maeneo hayo ni pamoja na kuhakikisha kuwa kila Wilaya inaandaa na kusimamia utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya. Namshukuru sana kwa

kuwa maelekezo na maagizo yake yameendelea kutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya sekta ya kilimo na katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, katika ziara ambazo amekuwa akifanya Mikoani, amekuwa akitenga muda kuona shughuli za kilimo na kutoa maagizo mbalimbali kuhusu kilimo endelevu na kinachozingatia utunzaji wa mazingira. Maagizo na maelekezo hayo yanazingatiwa katika utekelezaji wa *ASDP* ili uzalishaji katika kilimo uwe endelevu na unaozingatia utunzaji wa mazingira. Aidha, Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (MB), kwa kipindi kifupi tangu awe Waziri Mkuu amekuwa akizungumza na wananchi na viongozi wa sehemu alizotembelea kuhusu namna ya kuendeleza kilimo na kukabiliana na upungufu wa chakula nchini.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani na pongezi za pekee kwa wananchi wa Jimbo la Bunda, kwa ushirikiano wanaonipa na kwa juhudi wanazofanya katika kujiletea maendeleo. Naendelea kuwaahidi kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa moyo wangu wote na kutoa mchango wangu katika kupambana na matatizo yanayotukabili.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa kuipokea na kuifanyia uchambuzi wa kina taarifa ya utekelezaji ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika ya mwaka 2007/2008 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2008/2009 katika kikao chake kilichofanyika Dar es Salaam tarehe 3 - 4 Juni, 2008. Ushauri na maelekezo yaliyotolewa na Kamati hiyo yamezingatiwa katika Mpango wa 2008/2009. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (MB) na Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkullo kwa hotuba zao ambazo zimefafanua masuala mbalimbali yanayohusu kilimo. Wakati wa kujadili hotuba hizo, Waheshimiwa Wabunge wametoa michango yao kuhusu uendelezaji wa kilimo na kushauri jinsi ambavyo usimamizi na utekelezaji wa shughuli za kilimo unavyotakiwa uwe. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa ushauri na maelekezo yao yatazingatiwa katika utekelezaji. Aidha, nawapongeza Mawaziri wenzangu ambao hoja zao zimekwishajadiliwa na kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Hali ya Kilimo na Ushirika Nchini, Ukuaji wa Sekta ya Kilimo, kwa ujumla ukuaji katika sekta ya kilimo unapanda na kushuka kulingana na hali ya hewa na kiwango cha matumizi ya pembejeo na teknolojia nyingine muhimu katika uzalishaji wa mazao ya kilimo. Katika mwaka 2004, kilimo kilikua kwa asilimia 5.9, mwaka 2005 asilimia 4.3, mwaka 2006 asilimia 3.8 na mwaka 2007 asilimia 4.0. Ili kilimo kitoe mchango unaotakiwa katika vita dhidi ya umaskini kinapaswa kukua kwa zaidi ya asilimia 10 kwa mwaka.

Hata hivyo, pamoja na ukuaji huo mdogo, sekta ya kilimo imeendelea kuchangia zaidi ya asilimia 95 ya chakula kinachopatikana nchini na hivyo kuchangia kwa kiwango kikubwa katika kudhibiti mfumko wa bei. Aidha, kwa mujibu wa takwimu mpya za pato la Taifa zilizotolewa mwaka 2007, kwa kuzingatia vigezo vipya vilivyotolewa na Umoja

wa Mataifa mwaka 1993, mchango wa kilimo katika pato la Taifa kwa mwaka wa 2007 ulikuwa asilimia 26.5. Pamoja na kupungua kwa mchango wa sekta ya kilimo kwenye pato la Taifa, kilimo kina nafasi ya kipekee katika uchumi na maendeleo ya Taifa kutokana na ukweli kwamba zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania wanategemea kilimo. Aidha, uchambuzi uliofanywa katika nchi nyingi umethibitisha kuwa ukuaji wa pato la Taifa unaotokana na sekta ya kilimo una uwezo wa kupunguza umaskini zaidi ya mara mbili ya ule unaotokana na sekta nyingine.

Mheshimiwa Spika, Hali ya Chakula kwa Mwaka 2007/2008, nachukua fursa hii kuwapongeza wakulima ambao wamekuwa wakijitahidi kuzalisha chakula cha kutosheleza mahitaji ya nchi na kuwa na ziada katika baadhi ya miaka. Kwa mfano, kwa miaka mitano kuanzia 2004/2005 hadi 2008/2009, Taifa limekuwa likijitosheleza kwa chakula kwa wastani wa asilimia 102.4. Uzalishaji wa mazao ya chakula katika msimu wa 2006/2007 ulikuwa tani milioni 10.66 zikiwemo tani milioni 5.42 za nafaka na tani milioni 5.24 za mazao yasiyo ya nafaka. Mahitaji ya chakula kwa mwaka 2007/2008 yalikuwa tani milioni 10.03. Hivyo, Taifa lilijitosheleza kwa asilimia 106.

Mheshimiwa Spika, tathmini za kina zilizofanywa na Wizara ikishirikiana na wadau wa usalama wa chakula mwezi Septemba na Desemba, 2007 na zile za Januari na Februari, 2008, zilionyesha kuwepo maeneo yenye upungufu wa chakula katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Shinyanga. Watu 398,504 walikuwa na upungufu wa chakula na walihitaji chakula cha msaada kwa nyakati mbalimbali kati ya mwezi Novemba, 2007 na Aprili, 2008. Kuanzia mwezi Novemba, 2007 kulitokea mabadiliko ya ghafla ya hali ya chakula yaliyoashiriwa na kupanda kwa bei za vyakula kwa kasi, hali ambayo iliendelea hadi mwezi Mei 2008. Hali hiyo, ilitokea kufuatia kwa baadhi ya maeneo ya nchi kukabiliwa na upungufu wa vyakula vya aina ya nafaka, hususan mahindi.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa vyakula vya nafaka kwa kiasi kikubwa ulichangiwa na upungufu wa mavuno ya vuli uliosababishwa na mvua za vuli kunyesha chini ya kiwango cha kawaida au kutonyesha kabisa katika kipindi cha mwezi Oktoba hadi Desemba, 2007.

Aidha, kupanda kwa bei za vyakula, hususan nafaka kulisababishwa na kupanda kwa gharama za usafirishaji kulikochangiwa na kupanda kwa bei ya mafuta duniani na kupungua kwa akiba ya chakula kwenye nchi mbalimbali duniani. Kulingana na takwimu za Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *(Food and Agriculture Organization of the United Nations - FAO),* akiba ya chakula ya dunia mwaka 2005/2006 ilikuwa tani milioni 469.8 ikilinganishwa na tani milioni 425.6 mwaka 2006/2007 kiasi ambacho ni cha chini sana kutokea katika kipindi cha miaka 25. Kutokana na kuendelea kupanda kwa bei za mazao ya chakula ndani na nje ya nchi na upungufu wa chakula uliojitokeza nchini, Serikali ilichukua hatua zifuatazo:-

(i) Kutenga na kutoa chakula kutoka Wakala wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula *(National Food Reserve Agency - NFRA)* na kukisambaza kwa walengwa walioathirika na upungufu wa chakula ambao waliuziwa chakula hicho kwa bei nafuu ya Shilingi 50

kwa kilo. Jumla ya tani 1,083.75 za mahindi na tani 193.66 za mtama ziliuzwa kwa utaratibu huo.

(ii) Mwezi Januari, 2008, Serikali ilisitisha kuuza nje ya nchi zao la mahindi ambalo ni mojawapo ya mazao makuu ya chakula nchini. Aidha, mwezi Mei 2008, Serikali ilisitisha uuzaji wa mazao yote ya chakula hadi hapo hali ya chakula itakapokuwa nzuri.

(iii) Kutenga tani 36,660 za mahindi kutoka Wakala wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula kwa ajili ya kuuzwa kibiashara kwa wananchi wa mikoa iliyobainika kuwa na upungufu wa chakula. Utaratibu huo ulihusu kuuza chakula hicho kupitia wafanyabiashara walioteuliwa na Mikoa husika ili kupunguza kasi ya kupanda kwa bei katika maeneo hayo. Hadi tarehe 30 Juni 2008, jumla ya tani 33,365 zilikuwa zimeuzwa.

(iv) Kuondoa kodi kwa uingizaji wa mahindi kutoka nje ya nchi kwa kusudi la kuongeza upatikanaji wa chakula na kupunguza bei. Jumla ya tani 300,000 za nafaka zenye nafuu ya kodi zilitarajiwa kuingizwa nchini katika kipindi cha mwezi Januari hadi Mei, 2008. Hata hivyo, hatua hiyo haikuwa na mafanikio kwani hadi mwezi Juni, 2008, tani 8,070 tu ziliingizwa nchini. Hali hiyo ilitokana na bei za vyakula katika soko la dunia kupanda sana. Kwa mfano, hadi mwanzoni mwa mwezi Mei, 2008, bei ya mahindi ilikuwa Dola za Kimarekani 251.0 kwa tani ikilinganishwa na bei ya Dola za Kimarekani 203.1 kwa tani mwezi Januari, 2008 na Dola za Kimarekani 160.0 kwa tani mwezi Mei, 2007.

Matarajio ya Upatikanaji wa Chakula 2008/2009, matokeo ya tathmini ya awali ya uzalishaji wa mazao ya chakula nchini katika msimu wa kilimo wa 2007/2008 yanaonyesha kwamba uzalishaji wa mazao ya chakula utafikia tani milioni 10.78 zikiwemo tani milioni 5.62 za mazao ya nafaka na tani milioni 5.16 za mazao yasiyo ya nafaka. Mahitaji ya chakula kwa mwaka 2008/2009, yanakisiwa kufikia tani milioni 10.34. Hivyo, Taifa linategemewa kujitosheleza kwa chakula kwa takriban asilimia 104. Kiambatisho Na. 1.

Mheshimiwa Spika, pamoja na tathmini kuonyesha kuwa Taifa litajitosheleza kwa chakula kwa asilimia 104, yapo maeneo kadhaa nchini ambayo yatakabiliwa na upungufu wa chakula kutokana na sababu mbalimbali.

Maeneo hayo ni ya Wilaya za Meatu, Kishapu, Shinyanga Mjini na Bariadi katika Mkoa wa Shinyanga; Manyoni - Mkoa wa Singida; Nzega na Tabora Mjini - Mkoa wa Tabora; Lindi Vijijini - Mkoa wa Lindi; Nanyumbu - Mkoa wa Mtwara; Morogoro Vijijini - Mkoa wa Morogoro; Bagamoyo na Kibaha - Mkoa wa Pwani; Same, Mwanga na Rombo - Mkoa wa Kilimanjaro; Bahi na Chamwino - Mkoa wa Dodoma; Misungwi, Kwimba, Magu na Ukerewe - Mkoa wa Mwanza na Bunda, Rorya na Musoma -Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na upungufu wa chakula, Wizara inaendelea kufuatilia kwa karibu hali ya chakula katika maeneo yenye upungufu na itafanya tathmini

ya kina mwezi Agosti, 2008 na Februari, 2009 ili kubaini kaya zitakazoathirika na upungufu na kuchukua hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, hali ya chakula duniani na nchi jirani, uchambuzi wa kina uliofanywa na kundi la nchi zilizoendelea *(OECD)* na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *(Food and Agriculture Organization of the United Nations- FAO)* mwezi Mei 2008, umeonyesha kuwa pamoja na uzalishaji wa chakula kuongezeka, kwa wastani bei za vyakula zitaendelea kuwa juu kwa karibu miaka 10 ijayo ikilinganishwa na miaka kumi iliyopita. Hali hiyo inatokana na kuongezeka kwa mahitaji, kubadilika kwa tabia nchi, bei za mafuta na mbolea kuendelea kuwa juu pamoja na kuongezeka kwa matumizi ya nafaka katika kuzalisha nishati.

Taarifa ya Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *(FAO)* ya Aprili 2008 kuhusu matarajio ya uzalishaji wa mazao ya chakula duniani inaonyesha matarajio ya mavuno mazuri kwa ujumla katika nchi za Kusini mwa Afrika isipokuwa Zimbabwe na baadhi ya sehemu za Kusini mwa Msumbiji. Pamoja na mvua za kupandia kuchelewa, mvua kubwa zilizonyesha kati ya mwezi Desemba 2007 na Januari 2008 katika maeneo mengi ya kusini mwa Afrika zilisababisha mafuriko katika maeneo ya mabondeni katika nchi za Msumbiji, Zambia, Zimbabwe, Malawi na Madagascar.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa chakula katika nchi jirani unaweza kuathiri upatikanaji wa chakula nchini kutokana na biashara za mazao ya chakula kati ya Tanzania na nchi hizo. Biashara ya mazao hayo hufanyika katika mipaka ya Tanzania na Kenya, Malawi, Zambia, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Uganda. Hivyo, Wizara itashirikiana na Mikoa inayopakana na nchi hizo kuwahamasisha wananchi kuhifadhi mazao ya chakula kulingana na mahitaji ya kaya na kuuza ziada tu.

Mheshimiwa Spika, Hali ya Uzalishaji wa Mazao Makuu ya Biashara, kati ya mwaka 2006/2007 na 2007/2008 uzalishaji wa mazao makuu ya biashara uliongezeka kwa viwango malimbali. Zao la pamba liliongezeka kwa asilimia 53.7, tumbaku asilimia 13.1, sukari asilimia 38.2, pareto asilimia 12.4, korosho asilimia 7.1 na mkonge asilimia 7.0. Aidha, uzalishaji wa zao la chai ulishuka kwa asilimia 2.3 na kahawa kwa asilimia 8.3. Maelezo ya kina ya uzalishaji wa mazao hayo yako Sehemu ya IV ya hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mazao ya matunda, mboga, viungo na maua umeendelea kuongezeka. Kwa mfano, uzalishaji wa maua uliongezeka kutoka tani 6,898 mwaka 2006/2007 hadi tani 8,277 mwaka 2007/2008. Aidha, uzalishaji wa mbegu za mafuta uliongezeka kutoka tani 953,000 hadi tani milioni 1.0 na matunda kutoka tani milioni 1.62 hadi tani milioni 1.94 katika kipindi hicho. Wizara pia iliendelea kuzalisha vipando bora vya mazao ya matunda, mboga na viungo katika bustani za Serikali na kuvisambaza kwa wakulima. Vilevile, Wizara iliwezesha uanzishaji wa Baraza la Kuendeleza Mazao ya Bustani *(Horticultural Development Council of Tanzania-HODECT)* ambalo lilizinduliwa rasmi mwezi Aprili 2008.

Mheshimiwa Spika, Hali ya Ushirika Nchini, kupitia Programu ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika *(Cooperative Reform and Modernization Programme)* Vyama vya Ushirika viliendelea kuanzishwa na kuimarishwa ambapo huduma

zinazotolewa zimewafikia wananchi wengi zaidi vijijini na mijini, wakiwemo wakulima na wajasiriamali wadogo. Wanachama wa Vyama vya Ushirika pamoja na wananchi kwa ujumla walinufaika kwa huduma zilizotolewa zikiwemo huduma za masoko ya mazao, hususan korosho, kahawa na pamba pamoja na huduma za kifedha, ikiwemo mikopo iliyotolewa na *SACCOS*. Mafanikio hayo yametokana na usimamizi wa Serikali na uhamasishaji wananchi ili kuanzisha au kujiunga na Vyama vya Ushirika. Baadhi ya mafanikio ni kama ifuatavyo:-

(i) dadi ya Vyama vya Ushirika iliongezeka kutoka vyama 7,299 mwezi Mei mwaka 2007 hadi vyama 8,257 mwezi Juni mwaka 2008, sawa na ongezeko la asilimia 13; *SACCOS* pekee ziliongezeka kutoka 3,469 hadi 4,524, sawa na ongezeko la asilimia 30.4;

(ii) Idadi ya wanachama iliongezeka kutoka milioni 1.3 hadi milioni 1.6;

(iii) Mikopo iliyotolewa na *SACCOS* iliongezeka kutoka Shilingi bilioni 115.1 hadi Shilingi bilioni 202.7; na

(iv) Hisa, akiba na amana za *SACCOS* ziliongezeka kutoka Shilingi bilioni 77.9 hadi Shilingi bilioni 138.2.

Mheshimiwa Spika, mafanikio hayo yanaashiria kwamba hatua zinazochukuliwa za kuimarisha ushirika zimeanza kuzaa matunda na hivyo kuwavutia wanachama wengi. Aidha, wananchi wengi wameanza kutambua umuhimu wa kuunganisha nguvu zao pamoja kwa njia ya ushirika ili kupunguza umaskini na kufikia maisha bora yanayotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mpango wa mwaka 2007/2008 ilitekeleza Malengo ya Milenia, MKUKUTA na Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2005. Maeneo yafuatayo yalifanikiwa kutekelezwa: -

Mheshimiwa Spika, Mapato na Matumizi, katika mwaka 2007/2008, Wizara ilikadiriwa kukusanya jumla ya Shilingi milioni 752.61 kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato, hususan ushuru kwenye ukaguzi wa mazao. Kufikia mwezi Juni 2008, makusanyo yalikuwa Shilingi milioni 812.21 sawa na asilimia 107.9 ya makadirio.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika ilitengewa jumla ya Shilingi bilioni 131.91 ambapo Shilingi bilioni 71.85 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi bilioni 60.06 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo, Shilingi bilioni 6.756 zilikuwa fedha za ndani na Shilingi bilioni 53.30 zilikuwa fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Matumizi ya Kawaida, hadi tarehe 30 Juni 2008, Wizara ilikuwa imepokea kutoka Hazina jumla ya Shilingi bilioni 70.31 sawa na asilimia 98.23

ya kiasi kilichoidhinishwa. Aidha, hadi tarehe 30 Juni 2008, matumizi ya kawaida yalifikia Shilingi bilioni 70.31 sawa na asilimia 100 ya kiasi kilichotolewa.

Mheshimiwa Spika, hadi tarehe 30 Juni, 2008 Shilingi bilioni 6.756 ya fedha za ndani zilikuwa zimetumika, sawa na asilimia 100 ya fedha zilizoidhinishwa. Aidha, Shilingi bilioni 48.45 ya fedha za nje sawa na asilimia 99.25 ya fedha zilizoidhinishwa zilikuwa zimetumika kugharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Program*-ASDP) mwaka jana nililifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa mwaka 2007/2008, ulikuwa ni mwaka wa pili wa kutekeleza *ASDP*. Katika ngazi ya wilaya ASDP iliendelea kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(District Agricultural Development Plans* – DADPs). Miradi mbalimbali ya DADPs iliibuliwa na wakulima na wafugaji. Miradi hiyo ni pamoja na: ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji 32, malambo 86, majosho 33, masoko 8, minada ya mifugo 12, maghala 13, kilometa 120.8 za barabara, machinjio ya mifugo 55, vituo vitano vya kilimo vya kata (*Ward Resource Centres*) na vituo vitano vya mafunzo ya wanyamakazi. Majosho 102 yalikarabatiwa.

Aidha, pampu 43 za umwagiliaji, mabomba 302 ya kupulizia madawa ya korosho, mashine 99 za kusindika mazao, matrekta madogo ya mkono (*power tillers*) 16 na majembe ya kukokotwa na wanyamakazi 172 yalinunuliwa. Miradi mingine ni pamoja na uanzishaji wa vitalu 75 vya kuzalisha miche bora ya mazao na uanzishwaji wa mashamba darasa 361. Wakulima 43,044 walipatiwa mafunzo mbalimbali, watendaji wa halmashauri 103 walipata mafunzo katika ngazi ya Shahada 52, Shahada za uzamili 33 na Stashahada 18. Kupitia *DADPs* jumla ya magari 89, baiskeli 2,200, pikipiki 538 na kompyuta 122 zilinunuliwa na kupelekwa kwa maofisa ugani katika Halmashauri, Kata na vijiji kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, katika ngazi ya Taifa ya utekelezaji wa *ASDP*, Wizara za Sekta ya Kilimo ambazo ni Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika, Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Biashara Viwanda na Masoko, Maji na Umwagiliaji na Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika mwaka 2007/2008, kupitia timu ya Taifa ya Wawezeshaji (*National Facilitation Team*) ziliendelea kuzijengea uwezo Halmashauri na Sekretariati za Mikoa wa kusimamia, kufuatilia na kuandaa taarifa za utekelezaji wa miradi iliyoidhinishwa. Timu za wawezeshaji za wilaya 132 zenye jumla ya wawezeshaji 1,056 (*District Facilitation Teams-DFTs*) zilipata mafunzo ya kuibua, kuandaa na kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya. Tathmini iliyofanyika inaonyesha kuwa uwezo wa kuandaa *DADPs* umeongezeka. Kati ya Halmashauri za Wilaya 132 zilizofanyiwa tathmini ili kupata fedha za nyongeza (*Top up District Agriculture Development Grant*) mwaka 2008/2009, Halmashauri 110 zilifuzu ikilinganishwa na Halmashauri 62 mwaka 2007/2008 na Halmashauri 49 mwaka 2006/2007.

Aidha, Halmashauri 17 zilifuzu kwa masharti (*provisional*) ikilinganishwa na Halmashauri 45 mwaka 2007/2008. Halmashauri 5 hazikufuzu ikilinganishwa na

Halmashauri 14 mwaka 2007/2008. Vilevile, *DADPs* za Halmashauri 132 za mwaka 2008/2009 zilichambuliwa na matokeo yameonyesha kuwa asilimia 20 zina ubora wa juu, asilimia 50 ubora wa wastani na asilimia 30 hazina ubora unaotakiwa. Wilaya za Longido, Ngorongoro, Kinondoni, Ilala, Njombe, Siha, Moshi Mjini, Ruangwa, Nachingwea, Kilwa, Tarime, Kilosa, Morogoro (V), Ulanga, Mvomero, Morogoro Mjini, Kilombero, Mtwara /Mikindani, Masasi, Nyamagana, Ukerewe, Ilemela, Kibaha, Mafia, Kisarawe, Bagamoyo, Mpanda, Tunduru, Pangani, Kilindi, Tanga *MC*, na Mkinga ambazo *DADPs* zake zilionekana kuwa hazina ubora unaotakiwa zilipatiwa wataalam wa kusaidia kuboresha mipango yao.

Mheshimiwa Spika, Washauri wa sekta ya kilimo kutoka Sekretariati za Mikoa yote nchini walipewa mafunzo juu ya mbinu za kuandaa mipango bora ya *DADPs* kwa kutumia mbinu shirikishi ili waweze kusaidia halmashuri kuandaa *DADPs* bora, kusimamia, kufuatilia na kuratibu utekelezaji wa *DADPs*. Aidha, Wizara za Sekta ya Kilimo ziliendelea kufuatilia utekelezaji wa miradi ya DADPs iliyoibuliwa na walengwa na kutoa ushauri wa kuboresha utekelezaji pale ilipoonekana kuna udhaifu. Hata hivyo, suala la usimamizi limeonekana bado halijapewa umuhimu unaostahili katika ngazi ya halmashauri na vijiji.

Mheshimiwa Spika, ukiondoa mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa stakabadhi za mazao ghalani, kwa ujumla uendelezaji wa masoko na sekta binafsi ni maeneo ambayo hayakutekelezwa kwa viwango vya kuridhisha. Sababu za utekelezaji hafifu ni pamoja na kukosekana kwa vivutio vya uwekezaji katika kilimo, kukosekana kwa mfumo unaounganisha uzalishaji, usindikaji na masoko, bidhaa kutokukidhi viwango vya ubora kulingana na mahitaji ya soko na kukosekana kwa benki ya kilimo inayoweza kukopesha wawekezaji katika kilimo. Aidha, Wizara ilifanya maandalizi ya awali ya kuanzisha Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko.

Mheshimiwa Spika, kupitia *ASDP* huduma za utafiti na ugani zinaendelea kuboreshwa kama ifuatavyo:-

(i) Kuangalia upya vipaumbele vya utafiti katika kanda kwa utaratibu shirikishi ili viendane na mahitaji ya soko ikiwa ni pamoja na kuongeza fedha za kufanya utafiti.

(ii) Kukamilisha maandalizi ya kuanzisha Mifuko ya Utafiti ya Kanda (*Zonal Agricultural Research and Development Funds* – ZARDEF) ili kuiwezesha Mifuko hiyo kuanza kazi mwaka 2008/2009. Kamati Tendaji za kusimamia shughuli za utafiti katika kanda na kamati za kusimamia matumizi ya Mifuko ya Utafiti ya Kanda zimeundwa katika kanda 7 na kupatiwa semina elekezi.

(iii) Kukarabati ofisi, nyumba za kuishi watumishi na mifumo ya maji katika vituo 6 vya utafiti vya *HORTI* Tengeru, Selian, Ukiriguru, Naliendele, Tumbi na Makutopora; na

(iv) Kugharamia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu *(BSc, MSc* na *PhD)* kwa watafiti 148 ili kuwajengea uwezo wa kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, huduma za ugani, katika mwaka 2007/2008, Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika kwa kushirikiana na ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilianza kutekeleza Mpango wa Kuimarisha Huduma za Ugani nchini. Utekelezaji wa Mpango huo ulikuwa kama ifuatavyo:-

i. Wataalam wa ugani 309 waliajiriwa na kupelekwa katika Halamshauri na kupangiwa katika maeneo ya kata na vijiji. Idadi hiyo ni ndogo ikilinganishwa na lengo la kuajiri watalaam wa ugani 2,500 kila mwaka kutokana na uhaba mkubwa wa watalaam wa ugani wenye sifa zinazotakiwa hususan, Maafisa Kilimo Wasaidizi Daraja la Pili. Ili kukabiliana na upungufu huo, Wizara imeamua kurejesha ngazi ya Astashahada katika Muundo wake wa Utumishi.

ii. Kueneza mbinu ya Shamba Darasa inayoshirikisha jamii katika utoaji wa huduma za ugani kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya. Jumla ya mashamba darasa 2,500 yalianzishwa katika ngazi ya Halmashauri.

iii. Kuongeza uzalishaji na tija kutoka wastani wa tani 2 kwa hekta hadi kati ya tani 4.5 na tani 6 kwa hekta katika kilimo cha mpunga katika skimu sita za umwagiliaji za Mombo (Korogwe), Nduguti (Shinyanga Vijijini), Mwamapuli (Igunga), Mwega (Kilosa) Mbuyuni (Mbarali) na Nakahuga (Songea Vijijini). Jumla ya wakulima wakufunzi 1,920 kutoka katika skimu hizo walipatiwa mafunzo ya mbinu bora ya kilimo cha mpunga kwa njia ya umwagiliaji, matumizi bora ya maji na zana bora za kilimo.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mazao makuu ya biashara, zalishaji wa zao la pamba uliongezeka kutoka tani 130,565 mwaka 2006/2007 hadi tani 200,662 mwaka 2007/2008 sawa na ongezeko la asilimia 53.7. Ongezeko hilo lilitokana na wakulima kuhamasika kuongeza uwekezaji katika uzalishaji wa zao la pamba kwa kupanua maeneo ya mashamba, kununua madawa ya udhibiti wa visumbufu na kuongezeka kwa bei ya zao la pamba kutoka Shilingi 350 mwaka 2006/2007 kwa kilo hadi kati ya Shilingi 450 na 500 kwa kilo katika mwaka 2007/2008.

Aidha, ruzuku iliyotolewa na Serikali katika madawa ya kudhibiti visumbufu vya pamba iliwezesha bei ya viuatilifu kupungua kutoka wastani wa Shilingi 3,000 kwa '*acre-pack*' moja hadi Shilingi 2,100 kwa viuatilifu vinavyochanganywa na maji na kutoka Shilingi 5,500 hadi Shilingi 4,600 kwa viuatilifu vinavyochanganywa na mafuta. Hata hivyo, mvua kubwa iliyonyesha wakati wa kupanda zao la pamba iliathiri uzalishaji kwa kufanya baadhi ya mbegu za pamba kuoza kutokana na maji kutuama mashambani na hivyo kusababisha kutofikiwa lengo la uzalishaji wa tani 300,000 katika msimu wa 2007/2008.

Uzalishaji wa zao la tumbaku uliongezeka kutoka tani 50,784 mwaka 2006/2007 hadi tani 57,454 mwaka 2007/2008 sawa na ongezeko la asilimia 13.1. Ongezeko hilo limetokana na bei nzuri ya msimu uliopita iliyowahamasisha wakulima kuongeza

uzalishaji. Pembejeo za tumbaku, hususan mbolea zilipatikana kwa wakati katika maeneo mengi yanayozalisha tumbaku. Aidha, maeneo mengi yanayozalisha tumbaku yalipata mvua zenye mtawanyiko mzuri na hivyo kuwezesha kuwa na zao zuri la tumbaku. Wizara kupitia Bodi ya Tumbaku ilisimamia ubora katika uzalishaji na biashara ya tumbaku ambapo ukaguzi wa viwango vya ubora ulifanyika katika vituo vyote vya kununulia tumbaku na katika viwanda vya kusindika tumbaku kwa mujibu wa maelekezo ya Sheria na Kanuni za zao la tumbaku.

Uzalishaji wa sukari uliongezeka kutoka tani 192,095 mwaka 2006/2007 hadi tani 265,434 mwaka 2007/2008 sawa na ongezeko la asilimia 38.2. Ongezeko hilo limetokana na mvua nzuri zilizonyesha katika msimu wa 2006/2007 ambazo zilisababisha kuwa na zao zuri la miwa iliyotumika katika uzalishaji wa sukari katika msimu wa 2007/2008. Aidha, ukarabati wa mitambo katika viwanda vya Kilombero na *TPC* Kilimanjaro uliongeza ufanisi katika kusaga miwa na hivyo kuchangia katika ongezeko la sukari. Kwa mfano, Kiwanda cha *TPC* Kilimanjaro kimewekeza na kuongeza uwezo wake wa kuzalisha miwa kutoka tani 60,000 hadi tani 80,000 kwa mwaka ambapo jumla ya Shilingi bilioni 40 zilitumika kugharamia upanuzi huo. Hata hivyo, uzalishaji wa sukari haukufikia lengo la kuzalisha tani 302,000 katika msimu wa 2007/2008 kutokana kutuama kwa maji na baadhi ya mashamba ya Kilombero, TPC na Mtibwa kuungua moto. Vilevile, kituo cha utafiti wa miwa Kibaha kimeendelea kufanya utafiti wa miwa kwa lengo la kutoa mbegu bora zenye tija kubwa zaidi.

Uzalishaji wa zao la pareto uliongezeka kutoka tani 2,046 mwaka 2006/2007 hadi tani 2,300 mwaka 2007/2008 sawa na ongezeko la asilimia 12.4. Kuanzia mwaka 2005/2006, Bodi ya Pareto ikishirikiana na Kituo cha Utafiti wa Mazao cha Uyole, Mbeya pamoja na kiwanda cha *Tanzania Pyrethrum Processors and Marketing Company Limited (TPPMCL)* imekuwa ikitekeleza mpango wa kufufua zao la pareto kwa kubadilisha pareto ya zamani iliyokuwa na tija na sumu ndogo. Katika kipindi hicho, jumla ya miche milioni 420 inayotosha kupanda eneo la hekta 12,000 ilizalishwa na kusambazwa kwa wakulima. Ongezeko la uzalishaji wa pareto katika msimu huo ni sehemu ya mafanikio yanayotokana na mpango huo. Aidha, bei ya pareto iliongezeka kutoka wastani wa Shilingi 550 kwa kilo hadi wastani wa Shilingi 900 kwa kilo. Ongezeko hilo la bei limechangia katika kuwahamasisha wakulima kufufua mashamba yao ya zamani kwa kupanda miche bora yenye tija kubwa zaidi. Wizara kupitia Bodi ya Pareto imeendelea kuwahimiza wakulima wa pareto kujiunga na vikundi vya wakulima ambapo vimefikia 179 na vyama vya Ushirika vya Msingi 10.

Uzalishaji wa zao la korosho uliongezeka kutoka tani 92,573 mwaka 2006/2007 hadi tani 99,107 mwaka 2007/2008, sawa na ongezeko la asilimia 7.1. Ongezeko hilo limetokana na utaratibu wa kutoa ruzuku ya madawa ya korosho pamoja na kuimarika kwa vyama vya ushirika ambavyo vimewalipa wakulima bei nzuri. Bei ya korosho kwa mkulima iliongezeka kutoka wastani wa kati ya Shilingi 450 na 500 kwa kilo msimu wa 2006/2007 hadi kati ya Shilingi 610 na Shilingi 710 kwa kilo mwaka 2006/2007. Mafanikio hayo kwa sehemu kubwa yalichangiwa na ufufuaji wa huduma za ushirika katika zao la korosho na kuanzishwa kwa utaratibu wa matumizi ya Stakabadhi za Mazao

Ghalani katika ununuzi wa korosho katika Mkoa wa Mtwara unaozalisha takriban asilimia 60 ya korosho nchini.

Uzalishaji wa mkonge, katani uliongezeka kutoka tani 30,847 mwaka 2006/2007 hadi tani 33,000 mwaka 2007/2008 sawa na ongezeko la asilimia 7.0. Ongezeko hilo limetokana na kufufuliwa kwa baadhi ya mashamba ya mkonge yanayomilikiwa na wakulima wakubwa na yale yanayomilikiwa na wakulima wadogo. Aidha, mkonge uliopandwa mwaka 2003/2004 umeanza kuvunwa katika mwaka 2007/2008 ambapo mavuno ya kwanza ya mkonge huo yamepatikana. Vilevile, wakulima wameendelea kuhamasika kutokana na bei nzuri ya mkonge ambayo katika mwaka 2007/2008 imepanda na kufikia wastani wa Dola za Kimarekani kati ya 800 na 1,000 kwa tani ikilinganishwa na wastani wa kuanzia Dola 400 hadi 600 katika mwaka 2006/2007.

Wizara kwa kupitia Bodi ya Mkonge na Mfuko wa Pamoja wa Bidhaa za Kilimo wa Umoja wa Mataifa *(Common Fund for Commodities – CFC)* imekamilisha ujenzi wa mtambo wa umeme wa Kilowati 750 unaotumia *bio-gas* inayotokana na mabaki ya mkonge. Uunganishaji wa umeme utakaozalishwa katika mtambo huo na Gridi ya Taifa upo katika hatua za mwisho. Aidha, utafiti wa kuzalisha bidhaa nyingine zitokanazo na zao la mkonge zikiwemo *ethanol* na *inulin* umekamilika na ambapo imebainika kwamba kiasi kikubwa cha bidhaa hizo kinaweza kuzalishwa. Majaribio ya mitambo ya kuzalisha karatasi kutokana na mabaki ya mkonge yameanza na mitambo hiyo inatengenezwa kwa kushirikiana na *Tanzania Automotive Technology Centre*-Nyumbu.

Uzalishaji wa zao la chai ulishuka kutoka tani 34,969 mwaka 2006/2007 hadi 34,165 mwaka 2007/2008 sawa na upungufu wa asilimia 2.3. Upungufu huo umesababishwa na hali mbaya ya hewa katika maeneo yanayozalisha chai, hususan katika maeneo ya Kaskazini ambako hakukuwa na mtawanyiko mzuri wa mvua na hali ya baridi kali katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, hususan maeneo ya Mufindi. Aidha, matumizi madogo ya mbolea katika uzalishaji wa chai bado ni changamoto inayokwamisha kuongezeka kwa tija katika uzalishaji wa chai katika maeneo ya wakulima wadogo. Hata hivyo, uzalishaji na upatikanaji wa miche bora ya chai umeongezeka kutokana na ruzuku kwenye miche hiyo. Jumla ya miche bora milioni 6.3 ilizalishwa katika msimu wa 2007/2008 ikiwa ni ongezeko la asilimia 26 ya lengo la kuzalisha miche milioni tano.

Uzalishaji wa zao la kahawa ulipungua kutoka tani 45,534 mwaka 2006/2007 hadi tani 41,764 mwaka 2007/2008 sawa na upungufu wa asilimia 8.3. Upungufu huo umetokana na tabia ya zao la kahawa kupunguza tija katika msimu unaofuatia misimu ambayo uzalishaji ulikuwa mkubwa. Hata hivyo, uzalishaji na upatikanaji wa miche bora ya kahawa yenye ukinzani dhidi ya magonjwa umeongezeka kutokana na ruzuku kwenye miche hiyo. Jumla ya miche bora ya kahawa milioni 4.98 sawa na asilimia 99.7 ya lengo la kuzalisha miche bora milioni tano ilizalishwa katika msimu wa 2007/2008. Aidha, miundombinu kwa ajili ya uzalishaji wa miche bora iliyojengwa katika msimu huo itawezesha uwezo wa uzalishaji wa miche hiyo katika misimu ijayo kuongezeka na kufikia wastani wa miche milioni 10 kwa mwaka.

Katika mwaka 2007/2008, uendelezaji wa mazao ya maua, mboga mboga na mbegu za mafuta. Wizara iliendelea kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na sekta binafsi nchini katika kuendeleza uzalishaji na usindikaji wa mbegu za mafuta. Jumla ya tani milioni moja za mazao ya mbegu za mafuta, hususan alizeti, karanga, ufuta, katamu (*Sarfflower*), soya na michikichi zilizalishwa mwaka 2007/2008 ikilinganishwa na tani 953,000 msimu wa 2006/2007. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya kupitia miradi ya wakulima ilinunua jumla ya mashine ndogo 79 za kukamulia mbegu za mafuta na kuwapatia wakulima katika maeneo yanayozalisha mazao hayo. Wizara pia iliwahamasisha wawekezaji binafsi walioanza kuwekeza katika usindikaji wa mbegu za mafuta. Hatua hiyo imeanza kuchochea ongezeko la uzalishaji wa mazao ya mbegu za mafuta katika mikoa ya Singida, Arusha, Dodoma, Mbeya, Lindi, Mtwara, Rukwa, Ruvuma na Iringa. Aidha, sekta binafsi imeanza kuwekeza katika uzalishaji na usindikaji wa zao la soya linaloweza kuzalisha mafuta na mashudu yanayohitajika katika ufugaji wa kisasa.

Mheshimiwa Spika, bustani za Serikali ziliendelea kuzalisha na kusambaza teknolojia za ukuzaji wa mazao ya bustani, hususan matunda, mboga na viungo. Jumla ya vipando 100,000 vya mazao hayo vilizalishwa na kusambazwa kwa wakulima. Aidha, vikonyo (*scions*) 1,115 vya aina 19 za michungwa bora viliagizwa kutoka Afrika ya Kusini ili kuwa chanzo cha vikonyo bora vya michungwa hapa nchini. Wataalamu 45 katika ngazi ya wilaya kutoka mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam na Morogoro walipata mafunzo ya mbinu bora za uzalishaji wa mazao ya matunda, uyoga, paprika na vanilla.

Mheshimiwa Spika, Uendelezaji wa Mazao ya Nishati na Yanayostahimili Ukame katika mwaka 2007/2008, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya nishati ilishiriki katika maandalizi ya maeneo ya kuzingatiwa katika Mwongozo wa Kilimo cha Mazao ya Nishati nchini. Maandalizi hayo yalihusisha Wizara za Nishati na Madini, Kilimo Chakula na Ushirika, Fedha na Uchumi, Katiba na Sheria, Maliasili na Utalii, Maji na Umwagiliaji, Ofisi ya Makamu wa Rais, Baraza la Taifa la Mazingira *(NEMC)*, Kituo cha Uwekezaji *(TIC)*, Shirika la Taifa la Maendeleo ya Mafuta (*TPDC)* na sekta binafsi.

Aidha, kwa kuzingatia umuhimu wa kudhibiti kilimo cha mazao ya nishati, Serikali ilichukua hatua ya awali ya kuagiza Wakuu wa mikoa kuwa waangalifu katika kutoa ardhi kwa wawekezaji na kuhakikisha kuwa ardhi inayofaa kwa mazao ya chakula haitumiki kwa mazao ya nishati. Katika kuendeleza mazao yanayostahimili ukame, hususan mhogo, Wizara ilishirikiana na Idara ya Magereza kuzalisha takriban vipando milioni 17 vya mhogo vyenye ukinzani dhidi ya ugonjwa wa batobato kali na magonjwa mengine ya mhogo kwa ajili ya kuendeleza zao hilo nchini. Vipando hivyo vilizalishwa katika Halmashauri za Masasi, Mtwara, Nachingwea, Korogwe, Bagamoyo, Serengeti, Sengerema, Kibondo, Urambo, Bukombe na Bunda.

Mheshimiwa Spika, huduma za utafiti, katika mwaka 2007/2008, Wizara ilitoa aina mpya saba za mbegu bora za mazao zenye sifa za kuvumilia visumbufu, magonjwa, hali ya ukame na hivyo kuongeza tija na uzalishaji. Kati ya mbegu hizo, Kituo cha utafiti

cha Selian kilitoa aina mbili za mbegu bora za mahindi zijulikanazo kwa jina la *Vumilia H1* na *Vumilia K1* na aina mbili za maharage aina ya *Cheupe* na *Selian 06*. Kituo cha Utafiti cha Makutopora kilitoa aina mbili za mbegu za zabibu aina ya *Makutopora Red* na *Chenin Nyeupe*. Kituo cha Utafiti cha Tengeru kilitoa aina moja ya mbegu ya nyanya ijulikanayo kama *Meru*.

Mheshimiwa Spika, vituo vya utafiti vya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika viliendelea kutoa huduma kwa wadau wa sekta ya kilimo kutokana na fursa na rasilimali zilizopo katika vituo hivyo. Huduma hizo ni pamoja na kupima aina za udongo ili kutambua aina za mbolea na virutubisho vinavyohitajika, kupima na kutambua wadudu na magonjwa yanayoshambulia mazao ya wakulima, na kutoa mafunzo kwa wataalam na wakulima walio karibu na vituo vya utafiti kuhusu mbinu za kilimo bora. Taasisi ya *TPRI* iliendelea kutoa huduma za ushauri kuhusu viwango vya ubora vya madawa ya kudhibiti wadudu, magugu na magonjwa ya mimea.

Aidha, Kituo cha Taifa cha Nasaba za mimea *(National Plant Genetic Resource Centre – NPGRC)* kilichopo *TPRI* Arusha kimeendelea kutafiti na kukusanya mimea iliyopo nchini kwa lengo la kutunza nasaba hizo kwa ajili ya matumizi ya watafiti katika kuzalisha aina bora za mazao sasa na siku zijazo. Hadi sasa kituo hicho kimekusanya na kinatunza aina 4,808 za mazao na mimea mingine muhimu kwa kilimo.

Mheshimiwa Spika, Mafunzo katika vyuo vya Kilimo, katika mpango wa kuimarisha huduma za ugani, Wizara ililenga kufundisha vijana tarajali 3,000 kila mwaka ili kuwezesha kufikia lengo la kuajiri maofisa ugani 11,703 ifikapo mwaka 2010/2011. Ili kufikia lengo hilo Wizara katika mwaka 2007/2008 ilitekeleza yafuatayo:-

(i) Ilifundisha wanafunzi 1,460 kati yao 1,252 walikuwa wanafunzi tarajali na 208 walikuwa watumishi wanafunzi *(in-service).* Utekelezaji huo ni sawa na asilimia 42 ya lengo la kufundisha vijana tarajali 3,000 mwaka 2007/2008. Lengo halikufikiwa kutokana na kutokupatikana kwa wanafunzi wenye sifa za kujiunga na vyuo vya kilimo.

(ii) Ilishirikisha vyuo vya binafsi vya Igabilo (Muleba) na Kilacha (Moshi) katika kutoa mafunzo ya kilimo ambapo jumla ya wanafunzi tarajali 140 walihitimu.

(iii) Ilikarabati majengo ya vyuo vya kilimo vya Uyole, Ilonga na *KATRIN*-Ifakara. Aidha, ilinunua vifaa na samani kwa vyuo vya Ilonga, *KATRIN*, Chuo cha Sukari Kidatu, Naliendele, Mlingano, *KATC,* Tumbi, Ukiriguru na Igabilo na kuvifanya vyuo hivyo viwe na uwezo wa kupokea wanafunzi 1,840 ikilinganishwa na uwezo wa kupokea wanafunzi 1,320 kabla ya ukarabati.

(iv) Iliajiri wakufunzi 72 kati ya lengo la kuajiri wakufunzi 116 katika mwaka 2007/2008 na ifikapo mwaka 2010/2011 kuajiri wakufunzi 258.

Mheshimiwa Spika, Mapinduzi ya Kijani *(Green Revolution)* kama nilivyolifahamisha Bunge lako Tukufu mwaka 2007/2008 kuhusu Maandalizi ya utekelezaji wa mpango wa kuleta Mapinduzi ya Kijani nchini, Wizara kwa kushirikiana

na *Alliance for Green Revolution in Africa (AGRA)* katika kipindi cha mwaka 2007/2008 ilitekeleza yafuatayo:-

(i) Ilitoa mafunzo kwa mawakala wa pembejeo za kilimo '*rural agro-dealers*' 319 kutoka katika Halmashauri 14 za Wilaya za Songea Mjini, Songea vijijini, Mufindi, Arusha, Kilombero, Mbeya Jiji, Mbeya vijijini, Mbozi, Rungwe, Mbarali, Namtumbo, Kyela, Chunya na Tunduru. Ili kuongeza kasi ya ufundishaji wa mawakala, wakufunzi 17 kutoka sekta binafsi na wakufunzi 14 kutoka Halmashauri za Wilaya za Mpanda, Nkasi, Sumbawanga, Chunya, Mbozi, Mbarali, Songea, Namtumbo, Njombe, Mufindi na Kilolo walifundishwa.

(ii) Ilihamasisha wakulima kuzalisha mbegu za aina mbalimbali za daraja la kuazimiwa (*Quality Declared Seeds - QDS*). Wizara pia ilishirikiana na makampuni binafsi ili kuzalisha mbegu bora za mazao kwa matumizi ya wakulima badala ya kuendelea kuagiza kutoka nje ya nchi. Jitihada nyingine ambazo zimefanyika ni kufundisha maafisa ugani wa kilimo 239 (kutoka Halmashauri za Wilaya/Miji na Majiji) zilizohusisha wilaya 122 kuhusu uzalishaji wa mbegu za nafaka na bustani. Aidha,Wizara ilitoa mafunzo kwa maafisa ugani 126 kuhusu usimamizi na ukaguzi wa uzalishaji wa mbegu bora.

(iii) Ilifanya majaribio ya matumizi ya utaratibu wa vocha katika utoaji wa ruzuku ya pembejeo za kilimo. Majaribio hayo yamefanyika kwa mafanikio katika wilaya za Kilombero (Mkoa wa Morogoro) na Mbarali (mkoa wa Mbeya). Walengwa katika maeneo hayo, waliukubali utaratibu huo kwa kuwa pembejeo, hususan mbolea na mbegu bora zinawafikia moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa mbolea, makadirio ya mahitaji ya mbolea kwa mwaka 2007/2008 yalikuwa ni tani 385,000. Hadi mwezi Aprili 2008 upatikanaji wa mbolea nchini ulikuwa tani 211,013, kati ya hizo, tani 99,483 zilikuwa ni albaki ya mwaka 2006/2007 na tani 111,530 ndizo zilizoingizwa nchini kuanzia Julai 2007.

Hadi mwezi Juni 2008, kiasi cha tani 81,979.95 za aina mbalimbali za mbolea zenye ruzuku ya Shilingi bilioni 14.3 zilisambazwa kwa wakulima. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 91.3 ya lengo la tani 89,820 za mbolea zilizopangwa kusambazwa. Lengo la usambazaji wa mbolea yenye ruzuku halikufikiwa kutokana na kushindwa kwa kampuni ya Minjingu kuzalisha tani 16,000 za mbolea ya chengachenga aina ya Minjingu ambayo ilikuwa itumike badala ya *DAP*. Aidha, kupanda sana kwa bei ya mbolea ya *DAP* kulichangia katika kufanya lengo hilo lisifikiwe. Bei ya mbolea aina ya *DAP* ilipanda kutoka Shilingi 41,000 mwaka 2007 hadi Shilingi 95,000 mwaka 2008 kwa mfuko wa kilo 50. Tazama Kiambatisho Na. 2.

Mheshimiwa Spika, wakati wa utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbolea zilijitokeza changamoto ambazo zilisababisha malalamiko kutoka kwa wakulima na hivyo kuashiria ruzuku inayotolewa na Serikali haiwafikii wakulima kama ilivyokusudiwa. Changamoto hizo ni pamoja na usimamizi hafifu wa Waraka wa Serikali wa Kusimamia Usambazaji wa Pembejeo za Ruzuku, hususan katika ngazi ya

Halmashauri; mbolea yenye ruzuku kutofika wilayani kwa wakati kutokana na uwezo mdogo wa kifedha wa mawakala; vituo vikuu vya kununulia mbolea mikoani kuwa mbali na wakulima; kuwepo kwa bei mbili za mbolea yaani bei ya soko na bei ya ruzuku; kutokuwepo kwa takwimu sahihi za mahitaji halisi ya pembejeo na makampuni ya pembejeo za kilimo kushindwa kufikisha pembejeo kwa wakati kwa mujibu wa Mbegu.

Mheshimiwa Spika, Upatikanaji wa mbegu, mahitaji halisi ya mbegu bora katika mwaka 2007/2008 yalikuwa tani 30,000 ambapo upatikanaji ulikuwa tani 16,621.12 za mbegu za mazao ya nafaka, mikunde na mbegu za mafuta ambayo ni sawa na asilimia 54.6 ya mahitaji halisi. Kati ya kiasi hicho, tani 447 zilizalishwa na Wakala wa Mbegu za Kilimo (*Agricultural Seed Agency*-ASA) na tani 159.76 zilitokana na wakulima wadogo wanaozalisha mbegu za daraja la kuazimiwa (*Quality Declared Seeds* – QDS). Makampuni binafsi ya mbegu nchini yalichangia jumla ya tani 16,014.36 zikiwemo tani 6,664.3 za mbegu kutoka nje ya nchi. Aidha, katika mwaka 2007/2008, Wizara iliidhinisha matumizi ya aina 10 za mbegu mpya za mazao ya mahindi, maharage, nyanya na zabibu. Mbegu hizo zina sifa za kutoa mavuno mengi, kustahimili ukame, ukinzani dhidi ya magonjwa na kukomaa haraka.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha pembejeo za kilimo zinapatikana kwa uhakika na kwa ubora unaotakiwa, Wizara imeendelea kuzijengea uwezo Mikoa na Halmashauri kwa kuwapatia mafunzo wataalam na wakulima kuhusu mbinu sahihi za matumizi ya pembejeo za kilimo na ukaguzi wa ubora wa mbegu na pembejeo nyingine za kilimo. Jumla ya maafisa ugani 234 kutoka mikoa ya Mwanza, Mara, Iringa, Dodoma, Morogoro, Kagera, Kigoma, Ruvuma, Tabora, Rukwa, Mbeya, Singida, Shinyanga, Tanga, Pwani, Lindi na Mtwara walipatiwa mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, ruzuku ya pembejeo za kilimo, katika msimu wa 2007/2008, Serikali iliendelea na utaratibu wa kutoa ruzuku kwenye pembejeo za kilimo ili kuongeza uzalishaji na tija ya mazao. Pembejeo hizo ni pamoja na mbolea, mbegu bora za mazao ya mahindi, mtama na alizeti, madawa ya kudhibiti visumbufu vya korosho na pamba, na miche bora ya mazao ya kahawa na chai. Aidha, ili kufanikisha na kurahisisha usambazaji wa mbolea ya ruzuku, vituo vikuu 23 vya usambazaji wa mbolea yenye ruzuku viliteuliwa. Vituo hivyo vipo Makambako, Njombe, Iringa Mjini, Mpanda, Sumbawanga Mjini, Mbinga, Songea Mjini, Tunduru, Karatu, Arusha Mjini na Moshi Mjini. Vingine ni Tabora Mjini, Urambo, Manyoni, Kahama, Mbozi, Rujewa, Mbeya Mjini, Kigoma Mjini, Babati Mjini, Tarime, Morogoro mjini na Ifakara. Kazi hiyo ilifanikishwa kwa ushirikiano kati ya Kamati za Pembejeo za Taifa, Mikoa, Wilaya na Kata ambazo zilisimamia usambazaji na matumizi ya mbolea yenye ruzuku.

Mheshimiwa Spika, madawa ya korosho, katika mwaka 2007/2008, Wizara kupitia Bodi za Korosho na Pamba ilitoa ruzuku ya jumla ya Shilingi bilioni 2.50 kwa ajili ya kugharamia ruzuku ya madawa ya udhibiti wa visumbufu vya mazao yanayosimamiwa na bodi hizo. Bodi ya Korosho iliratibu ununuzi na usambazaji wa tani 3,222.2 na lita 133,462.5 za madawa hayo. Kati ya hizo, tani 1,100 na lita 50,000 za madawa hayo zilitokana na ruzuku ya Serikali ya kiasi cha Shilingi bilioni 1.10. Kiasi kilichobakia cha tani 2,122.2 na lita 83,462.5 ziligharamiwa na fedha zilizotokana na

sehemu ya ushuru wa kuuza korosho ghafi nje ya nchi (*Export Levy*) ambapo jumla ya Shilingi bilioni 2.2 zilitumika.

Kwa upande wa zao la pamba, Serikali ilichangia Shilingi bilioni 1.4 ambayo iliwezesha bei ya *acrepacks* kushuka kutoka Shilingi 3,000 hadi 2,100. Hadi mwezi Aprili 2008, jumla ya *acrepacks* 500,000 zilipokelewa na kusambazwa kwa wakulima. Bodi ya Pamba kupitia Mfuko wa Pamba ilitoa ruzuku ya *acrepack* 1,337,655 na kufanya jumla ya dawa kuwa *acrepack* 1,837,655 zilizogharimu Shilingi bilioni 2.1.

Mheshimwa Spika, utaratibu wa ruzuku katika madawa ya kudhibiti visumbufu vya zao la pamba ulikabiliwa na matatizo na hivyo kusababisha malalamiko kutoka kwa wakulima. Baadhi ya matatizo hayo ni pamoja na usimamizi dhaifu wa kumbukumbu za viwango vya michango ya wakulima kupitia vitabu vya kumbukumbu *(pass-books)* ikiwa ni pamoja na wakulima kupewa pembejeo chini ya thamani ya kiasi cha fedha zilizoingizwa katika *pass-book* za wadau, baadhi ya mawakala kuwauzia wakulima madawa yenye ruzuku kwa bei kubwa kuliko iliyoainishwa chini ya utaratibu wa ruzuku na baadhi ya wakulima kubadilisha kumbukumbu kwenye *pass-book* zao.

Mheshimiwa Spika, mbegu na miche bora, mwaka 2007/2008 jumla ya makampuni 12 yaliingia mikataba na Serikali ya kusambaza jumla ya tani 1,769.70 za mbegu za mahindi, mtama na alizeti chini ya utaratibu wa ruzuku kupitia vituo vikuu 21 vya kusambazia mbegu hizo vilivyopo katika mikoa 15 nchini. Hadi kufikia mwezi Juni 2008, jumla ya tani 1,070.71 za mbegu bora sawa na asilimia 60.5 ya kiasi kilichopangwa ziliuzwa kwa wakulima. Lengo halikufikiwa kutokana na uwezo mdogo wa mawakala wa kununua na kusambaza mbegu bora kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara ilitumia Shilingi bilioni 1.0 kwa ajili ya kuzalisha miche bora ya chai na kahawa. Miche hiyo ilizalishwa kupitia Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai na *TACRI*. Hadi mwezi Juni 2008, miche bora ya kahawa milioni 4.98 na miche bora ya chai milioni 6.3 ilikuwa imezalishwa kwa ajili ya kusambazwa kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, zana za kilimo, katika mwaka 2007/2008, Wizara iliendelea kuhamasisha sekta binafsi kuingiza nchini zana bora za kilimo, hususan matrekta ambapo matrekta 464 yaliingizwa nchini. Kati ya hayo, matrekta 98 yaliuzwa kwa mkopo kupitia Mfuko wa Pembejeo na yaliyobaki yanauzwa kupitia utaratibu wa kawaida wa soko. Aidha, Wizara ilifanya tathmini ya matumizi na mahitaji ya zana nchini ambapo takwimu za awali zinaonyesha kuwa kuna idadi ya majembe ya mkono milioni 14, majembe yanayokokotwa na wanyamakazi 585,000, maksai milioni 1.3 na matrekta yanayofanya kazi 7,200.

Tathmini hiyo ilionyesha kuwa katika kipindi cha miaka mitatu ijayo, jumla ya matrekta 4,500 na majembe ya kukokotwa na wanyamakazi 120,000 yatahitajika ili kukidhi mahitaji ya kilimo katika kuongeza uzalishaji wa mazao. Pamoja na kuongeza tija katika mazao italazimu kupanua maeneo yanayolimwa ili kukidhi ongezeko la mahitaji ya chakula. Vilevile, tathmini ya ubora wa zana za kilimo zinazoingizwa nchini

inaendelea kufanyika kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda Biashara na Masoko, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine. Mwongozo wa matumizi bora ya punda na zana zake pia uliandaliwa ili kuwezesha wakulima walioko kwenye maeneo yenye punda wengi kuwatumia wanyamakazi hao kwa ufanisi zaidi na hivyo kuongeza tija katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, ili kueneza matumizi sahihi ya zana za kilimo hifadhi, mwaka 2007/2008 Wizara ilitoa mafunzo kwa maafisa ugani 38 kuhusu mbinu za matumizi sahihi ya zana za kilimo hifadhi katika wilaya za Arumeru, Karatu, Babati na Hanang. Kilimo hifadhi ni mojawapo ya mbinu za kisasa zinazotumika kudhibiti mmomonyoko wa udongo, kuongeza rutuba kwa kutumia masalia ya mazao, na kuhifadhi maji ya mvua, hususan wakati wa upungufu wa mvua. Wataalamu waliopatiwa mafunzo wamefungua mashamba darasa katika wilaya hizo ambapo jumla ya mashamba darasa 48 yenye wakulima 1,200 yalianzishwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilifanya mafunzo kwa vitendo kuhusu zana bora za kilimo kwenye skimu za umwagiliaji za Madibira, Kimani na Mbuyuni kwa lengo la kuwahamasisha wakulima kuongeza matumizi ya zana hizo katika uzalishaji, usafirishaji na usindikaji wa mazao ya kilimo. Mafunzo yaliyotolewa yalihusu matumizi ya matrekta madogo ya mkono, mashine za kupandikiza mpunga na zana za kuchavanga zinazokokotwa na wanyamakazi. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo hayo kwa wakulima wakufunzi 40 katika mikoa ya Mbeya, Pwani, Arusha, Manyara, Kigoma, Morogoro, Mwanza, Tabora na Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, mfuko wa pembejeo, katika mwaka 2007/2008, Mfuko wa Taifa wa Pembejeo ulitengewa jumla ya Shilingi bilioni 3.5. Aidha, Mfuko ulikusanya marejesho ya mikopo iliyotolewa misimu iliyopita yenye thamani ya Shilingi bilioni 2.7. Hadi Juni 2008, Shilingi bilioni 4.4 zilikuwa zimetumika kwa ajili ya mikopo ya pembejeo za kilimo, mifugo na zana za kilimo. Mikopo hiyo ilitolewa kupitia Muungano wa Vyama Vya Ushirika wa Akiba na Mikopo- *SCCULT, SACCOS*, Benki ya Uchumi ya Mkoa wa Kilimanjaro, Benki ya Ushirika Kilimanjaro, Benki ya Wananchi Mbinga na Benki ya Ushirika wa Wakulima Kagera.

Mheshimiwa Spika, Mikopo ya Pembejeo za Kilimo na Mifugo iliyotolewa ilikuwa ni ununuzi wa matrekta makubwa mapya 98 yenye thamani ya Shilingi bilioni 2.9 ikilinganishwa na lengo la matrekta 100; ununuzi wa matrekta madogo mapya (*power tillers*) saba yenye thamani ya Shilingi milioni 38.8 ikilinganishwa na lengo la matrekta 50; ununuzi wa pembejeo za kilimo na mifugo zenye thamani ya Shilingi bilioni 1.5 ambazo ni; mbolea tani 1,159 ikilinganishwa na lengo la tani 2,000, mbegu bora tani 32.4 ikilinganishwa na lengo la tani 50, madawa ya mifugo na mazao lita 13,171 ikilinganishwa na lengo la lita 10,000.

Mheshimiwa Spika, hifadhi ya udongo na matumizi bora ya ardhi, katika mwaka 2007/2008, Wizara iliendelea kuhimiza matumizi endelevu ya ardhi ya kilimo ili kuchangia katika juhudi za Taifa za kuzuia uharibifu wa mazingira. Ili kutimiza azma ya Serikali ya kuendeleza kilimo kinachozingatia hifadhi ya udongo na matumizi bora ya ardhi, katika mwaka 2007/2008, Wizara ilikamilisha maandalizi ya maeneo ya

kuzingatiwa katika Muswada wa Sheria ya Kutambua, Kuweka Mipaka na Kulinda Ardhi ya Kilimo. Aidha, ilifanya uchambuzi wa kutambua maeneo mapya yanayofaa kwa ajili ya kuendelezwa kwa kilimo cha kibiashara katika mikoa ya Lindi,Mtwara na Ruvuma. Wizara pia ilikusanya maoni na mapendekezo ya wadau kuhusu maeneo ya kuzingatia wakati wa kuandaa Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi ya Kilimo (*Agricultual Land Use Master Plan*).

Mheshimiwa Spika, usalama wa chakula, Wizara kwa kushirikiana na wadau imekuwa inafuatilia hali ya chakula nchini. Aidha, ilifanya tathmini za kina katika maeneo yaliyobainika kuwa na upungufu wa chakula ili kutambua kaya zenye upungufu, mahitaji yao ya chakula na hatua za kukabiliana na upungufu huo. Kazi ya kutoa mafunzo kuhusu teknolojia za kukadiria maeneo yaliyolimwa *(Geographical Information System - GIS na Geographical Positioning System - GPS)* haikufanyika kutokana na mtaalam aliyepatikana kutokidhi vigezo vya zabuni, na hivyo, kazi hiyo inategemewa kufanyika mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara ilitoa mafunzo ya teknolojia za usindikaji na matumizi ya mazao ya mtama, muhogo, matunda na mboga ili kuongeza uzalishaji, thamani na kupanua wigo wa matumizi. Mafunzo hayo yalitolewa kwa wataalamu 520 kutoka Halmashauri za wilaya 104 katika mikoa ya Dodoma, Shinyanga, Singida, Tabora, Kagera, Kigoma, Mtwara, Kilimanjaro, Mwanza, Mara, Tanga, Manyara, Morogoro, Pwani, Iringa na Mbeya. Aidha, Wizara ilikusanya maoni ya wadau wa teknolojia za uchanganyaji wa mazao ya chakula wakiwemo wasindikaji wakubwa kwa lengo la kukusanya mapendekezo yatakayotumika kuandaa mwongozo wa uchanganyaji wa vyakula nchini. Maandalizi ya mwongozo yameanza na utakamilika mwaka 2008/2009

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine na Taasisi ya Chakula na Lishe imeandaa mwongozo wa ufuatiliaji wa hali ya chakula ngazi ya kaya ambao unafanyiwa majaribio katika Halmashauri za wilaya za Njombe, Babati, Masasi na Ulanga. Kwa kutumia mwongozo huo, wananchi wataweza kukadiria kiasi cha mazao ya kuhifadhi kulingana na idadi ya watu katika kaya na ziada itakayobaki kuamua itumike kwa matumizi mengine ikiwa ni pamoja na kuuza.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara iliendelea kuzijengea uwezo Halmashauri wa kuibua miradi inayolenga kutatua matatizo ya upungufu wa chakula katika ngazi ya kaya, hususan miradi ya usindikaji wa mazao. Jumla ya miradi 99 ya usindikaji wa mazao na 13 ya hifadhi na ujenzi wa vihenge iliibuliwa kupitia DADPs.

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hali ya Hewa Nchini ilitoa mafunzo kwa wataalam wa ugani na wakusanyaji wa takwimu za mvua katika mikoa yote kuhusu mfumo wa kisasa wa ukusanyaji takwimu (Automation). Vifaa kwa ajili ya kuunganisha vituo vya kupima mvua katika mfumo huo vilinunuliwa. Mfumo huo utaliwezesha Taifa kuwa na utaratibu wa uhakika zaidi wa kukusanya taarifa za mvua na kukadiria kwa usahihi uzalishaji wa mazao na mwenendo wa hali ya chakula nchini.

Mheshimwa Spika, kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa duniani yanayosababisha athari katika maeneo mbalimbali, hususan kwenye uzalishaji wa kilimo, Wizara kwa kushirikiana na Idara ya Mazingira ya Ofisi ya Makamu wa Rais na wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ilifanya savei katika mikoa ya Iringa, Kagera, Kilimanjaro, Mbeya, Shinyanga na Singida kutafiti na kubaini sababu za baadhi ya maeneo, hususan katika mikoa ya kati kuwa na upungufu wa mara kwa mara wa chakula. Utatifi huo ulibaini kuwa mabadiliko ya tabia nchi yana athari kwenye kilimo. Athari hizo ni pamoja na:-

(i) Vipindi vya mvua kubadilika na kuwa tofauti na hali ya kawaida ya mvua iliyozoeleka. Kwa mfano, mvua kuanza mapema au kuchelewa kwa takriban kipindi cha mwezi mmoja;.

(ii) Mvua kunyesha chini ya viwango vinavyohitajika kuzalisha mazao katika kanda za uzalishaji, hali inayosababisha mabadiliko ya mifumo ya uzalishaji katika kanda hizo. Kwa mfano, maeneo ambayo awali zao la mahindi lilistawi kutokana na kuwepo kwa kiwango cha mvua za kutosha, sasa zao hilo halistawi tena, zikiwemo sehemu za Dodoma na Singida;

(iii) Mvua kunyesha kwa mtawanyiko usiotabirika;

(iv) Kuongezeka kwa joto; na

(v) Mabadiliko katika upepo ambapo upepo uliokuwa unasababisha mvua, sasa huvuma bila ya kuambatana na mvua.

Mheshimwa Spika, hatua zinazotakiwa kuchukuliwa kukabiliana na hali hiyo ni pamoja na kuwaelimisha wakulima kuhusu mabadiliko ya tabianchi na kuwajengea uwezo wa kuzalisha mazao kwa kupatiwa mafunzo na tekinolojia zinazofaa kwa kilimo kulingana na mabadiliko yanayotokea. Aidha, Halmashauri zitatakiwa kujengewa uwezo kimuundo ili ziweze kuratibu na kufuatilia athari za mabadiliko ya tabianchi katika maeneo husika na kushauri juu ya hatua za kuchukua. Mapendekezo hayo yatazingatiwa katika kuandaa mkakati na ufumbuzi wa kudumu wa kukabiliana na hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, akiba ya Taifa ya chakula, katika mwaka 2007/2008,Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(National Food Reserve Agency-NFRA)* ulianzishwa na kuchukua majukumu ya iliyokuwa Hifadhi ya Taifa ya Chakula (*Strategic Grain Reserve - SGR*). Katika mwaka 2007/2008, *NFRA* ilipanga kununua tani 27,500 za mazao ya nafaka. Hadi mwezi Mei 2008, *NFRA* ilikuwa imenunua tani 23,762 za nafaka, sawa na asilimia 86.4 ya lengo.

Kati ya hizo, tani 19,415 zenye thamani ya Shilingi bilioni 3.7 zilikuwa za mahindi na tani 4,347 zenye thamani ya Shilingi milioni 835.79 zilikuwa za mtama. Kiasi hicho cha ununuzi wa nafaka kikijumuishwa na akiba ya tani 124,331 za mahindi na tani 2,868 za mtama ghalani mwanzoni mwa mwaka 2006/2007 kilifanya NFRA kuwa na akiba ya chakula yenye jumla ya tani 143,747 za mahindi na tani 7,021 za mtama kabla ya kuuzwa. Hata hivyo, hadi tarehe 30 Juni 2008, NFRA ilikuwa imeuza tani 74,152 za

mahindi zenye thamani ya Shilingi bilioni 17.8 na tani 324 za mtama zenye thamani ya Shilingi milioni 77.76 na hivyo kubakiwa na jumla ya tani 76,291 zikiwemo tani 69,594 za mahindi na tani 6,697 za mtama.

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao ya kilimo, katika mwaka 2007/2008, Wizara kwa kushirikiana na Serikali za mitaa na wakulima iliendelea kudhibiti milipuko ya visumbufu vya mimea na mazao. Visumbufu hivyo ni pamoja na kwelea kwelea, nzige, viwavijeshi, panya na magonjwa ya mimea na mazao. Milipuko ya viwavijeshi ilidhibitiwa katika wilaya za Siha, Hai, Moshi vijijini, Rombo, Mwanga na Same mkoani Kilimanjaro, na wilaya ya Arumeru mkoa wa Arusha. Jumla ya lita 6,931 za viuatilifu zilitumika kuokoa hekta 11,768 zilizoshambuliwa na viwavijeshi katika maeneo hayo. Aidha, jumla ya maafisa ugani 341 na wakulima 275 kutoka mikoa ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro na Dodoma walipatiwa mafunzo juu ya matumizi ya mitego kwa ajili ya utabiri wa milipuko ya viwavijeshi.

Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kudhibiti Nzige wa Jangwani (*Desert Locust Control Organization- East Africa - DLCO-EA*) ilidhibiti ndege aina ya kwelea kwelea milioni 90.55 katika mikoa ya Morogoro, Tabora, Kilimanjaro, Singida, Shinyanga na Dodoma. Katika udhibiti huo jumla ya lita 2,985 za viuatilifu zilitumika. Ndege hao kama wasingedhibitiwa wangeweza kuleta uharibifu wa tani 905.5 za nafaka kwa siku. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kudhibiti Nzige Wekundu (*International Red Locust Control Organisation for Central and Southern Africa - IRLCO-CSA*), ilidhibiti nzige wekundu kwenye mazalio yao ya asili katika mbuga za Bahi, Malagarasi, Ziwa Rukwa, Iku na Wembere.

Katika udhibiti huo jumla ya lita 4,265 za viuatilifu zilitumika kudhibiti nzige hao kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 6,560. Aidha, uchunguzi uliofanyika mwezi Machi, 2008 umebaini kuwa kiwango cha nzige kimeongezeka katika mbuga za Iku na bonde la Ziwa Rukwa, na hivyo kuhitaji kudhibitiwa. Maandalizi ya kudhibiti nzige hao yamekamilika na kazi ya kuwadhibiti itafanyika kabla ya mwezi wa Agosti 2008.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007/2008 milipuko ya panya ilitokea katika vijiji 209 katika wilaya za Hanang, Kilosa, Mvomero, Kilombero, Misungwi, Magu, Maswa, Kahama, Ulanga, Bunda, Dodoma vijijini, Manispaa ya Dodoma, Chunya, Ulanga, Mbarali, Karatu, Hai na Moshi vijijini. Panya hao walidhibitiwa kwa kutumia kilo 7,873 za chambo chenye sumu. Aidha, jumla ya wakulima 374,686 walipatiwa mafunzo kuhusu kudhibiti panya katika wilaya hizo.

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya udhibiti husishi katika mazao ya mbogamboga, kilimo hai cha pamba na matumizi ya dawa asilia yalitolewa katika mikoa ya Kigoma, Kagera, Mwanza, Mara, Shinyanga, Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Singida. Aidha, udhibiti wa gugumaji uliendelea kwa kuzalisha na kusambaza mbawakavu katika ziwa Viktoria, mito na katika mabwawa yenye gugumaji katika mikoa ya Kanda ya Ziwa. Aidha, utafiti unaendelea kufanyika kwenye mto Kagera na Mara kubaini sababu za mbawakavu kushindwa kudhibiti gugumaji katika mito hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara iliendelea kutoa mafunzo kwa wakulima jinsi ya kutambua na kumdhibiti inzi wa embe ambaye amethibitika kuenea mikoa yote ya Tanzania bara na visiwani. Mitego 1,500 yenye kiuatilifu cha kudhibiti inzi hao ilisambazwa katika mikoa ya Tanga, Morogoro na Pwani. Aidha,

utafiti wa kutafuta wadudu wa kudhibiti nzi huyo wa matunda kwa njia ya kibaiolojia unaendelea kwa kushirikiana na kituo cha kimataifa cha utafiti *(ICIPE)* kilichopo nchini Kenya.

katika mwaka 2007/2008 kazi za kukagua mazao yanayoingia nchini na yanayosafirishwa nchi za nje ili kudhibiti ueneaji wa visumbufu vya mimea ziliendelea kutekelezwa katika vituo vya mpakani. Jumla ya tani milioni 1.03 za mazao mbalimbali zilikaguliwa kabla ya kusafirishwa nchi za nje. Aidha, tani 654,658.57 zilikaguliwa kabla ya kuingizwa nchini ambapo vyeti 7,220 vya usafi wa mazao na vibali 253 vya kuingiza mazao nchini vilitolewa. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (*FAO*) iliendesha mafunzo kwa wakaguzi 15 kuhusu kanuni na sheria za kimataifa juu ya kudhibiti uingiaji wa visumbufu vya mimea na mazao nchini. Aidha, majaribio ya viuatilifu na usajili ili kupata viuatilifu vyenye ubora unaokubalika yalifanyika na aina 72 ya viuatilifu vilifanyiwa majaribio na kusajiliwa.

Mheshimiwa Spika, miradi ya maendeleo, ipo miradi mitatu ambayo inatekelezwa kwa misingi ya ASDP. Maelezo ya utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Mradi wa Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo Wilayani (*District Agricultural Sector Investment Project* – DASIP) unaotekelezwa katika Halmashauri za Wilaya 28 za mikoa ya Kagera, Kigoma, Mara, Mwanza na Shinyanga ulizijengea uwezo wa kupanga na kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (DADPs) wilaya zote 28 za mradi. Aidha, mradi uliwezesha uibuaji na utekelezaji wa miradi midogo 516 yenye thamani ya Shilingi bilioni 7.056 ya sekta ya kilimo katika wilaya hizo. Kati ya fedha hizo DASIP ilichangia Shilingi bilioni 5.478 na walengwa walichangia Shilingi bilioni 1.577.

Mheshimiwa Spika, mradi pia ulitoa mafunzo ya mbinu bora za kilimo kwa njia ya shamba darasa kwa vikundi vya wakulima 1,484 vyenye jumla ya wanachama 38,082. Kati ya hivyo, vikundi 1,223 ni vya kilimo na vikundi 261 ni vya mifugo. Pia mafunzo yanayohusu mbinu za kubaini mahitaji ya wakulima, shamba darasa na ujasiriamali, teknolojia za hifadhi na usindikaji wa mazao na mafunzo ya udhibiti husishi wa visumbufu vya mimea yalitolewa kwa Waratibu wa Mafunzo 56 wa wilaya. Aidha, kamati za maendeleo za vijiji 780 zilipatiwa mafunzo ya kupanga, kusimamia utekelezaji, kufuatilia na kufanya tathmini ya miradi ya maendeleo. Vilevile, mradi uliwezesha ujenzi wa malambo saba, majosho 27, skimu za umwagiliaji saba, masoko ya mazao manne na maghala mawili. Mradi pia uliwezesha halmashauri 28 kununua baiskeli 2,000 kwa ajili ya wataalam wa kata na vijiji.

Mheshimiwa Spika, mradi shirikishi wa maendeleo ya kilimo na uwezeshaji, Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji (*Participatory Agricultural Development and Empowerment Project - PADEP*) uliendelea kutumia mbinu shirikishi jamii katika kujenga uwezo wa jamii na vikundi vya wakulima kutambua matatizo yao ya kilimo, fursa zilizopo, kubuni na kuandaa mikakati ya kuyatatua. Katika mwaka 2007/2008, mradi ulitekelezwa katika wilaya 32 za Tanzania Bara ambazo ni Masasi, Nanyumbu, Nachingwea, Morogoro, Mvomero, Iringa, Kilolo, Singida, Arumeru, Hai, Hanang, Kiteto, Mbulu, Babati, Iramba, Karatu, Sikonge, Urambo, Uyui, Handeni,

Kilindi, Kilombero, Korogwe, Monduli, Moshi, Rombo, Lushoto, Same na Ulanga. Kwa upande wa Zanzibar mradi unatekelezwa katika wilaya za Chake Chake, Wete, Kati, Kaskazini A na Magharibi.

Katika mwaka 2007/2008, mradi uliendelea kuwezesha jamii kuibua na kutekeleza miradi 978, vikundi vya wakulima na wafugaji kuibua na kutekeleza miradi 4,708, kutoa mafunzo rejea kuhusu utayarishaji na utekelezaji wa DADPs kwa timu za wawezeshaji wa wilaya na kata katika wilaya 32 zinazotekeleza mradi. Aidha, mradi uligharamia ununuzi wa magari 15 na pikipiki saba kwa ajili ya watumishi wa ugani wa wilaya. Vilevile, mradi uligharamia ukarabati wa maabara za utafiti wa udongo katika vyuo vya utafiti.

Mheshimiwa Spika, mwezi Desemba 2008 ni mwisho wa kutekeleza mradi wa *PADEP* ulioanza kutekelezwa mwaka 2003/2004. Mradi huo ulitekelezwa kwa mafanikio katika maeneo yote ya mradi ambayo yalihusisha mikoa 10 na wilaya 32. Mradi uliwezesha utekelezaji wa miradi 4,574 katika vijiji 768 ambayo imenufaisha kaya 694,610 kwa kupatiwa teknolojia bora za kilimo na ufugaji. Aidha, mradi uliwezesha utekelezaji wa programu za kuimarisha uwezo wa Halmashauri za Wilaya na taasisi zingine ili kusimamia maendeleo ya sekta ya kilimo. Kupitia mradi huo jumla ya kaya 827,593 katika vijiji 768 wamenufaika na mradi. Uzoefu uliopatikana katika utekelezaji wa mradi wa *PADEP* ulitumika katika kuboresha utekelezaji wa *ASDP*, hususan katika uandaaji na utekelezaji wa *DADPs*. Vilevile, mradi huo umefanikiwa katika kubuni utaratibu wa ushirikishwaji wa wakulima kuchangia katika ugharimiaji wa sehemu ya gharama za miradi yao ya maendeleo. Ubunifu huo umewezesha miradi iliyoibuliwa na kutekelezwa kuwa endelevu.

Aidha, mradi wa PADEP uliwezesha kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika kutoa huduma za kuboresha sekta ya kilimo. Maeneo yaliyowezeshwa ni pamoja na kufanya mapitio ya Sheria ya Nasaba za Mimea (*Plant Breeders Rights Act)* na uanzishwaji wa ofisi yake wizarani; Sheria ya Mbegu (*Seed Act*); Sheria ya Hifadhi ya Mimea (*Plant Protection Act)* na Sheria ya Afya na Magojwa ya Mifugo (*Veterinary and Animal Diseases Act*). Vilevile, mradi uliwezesha kuanzishwa kwa utaratibu wa kilimo cha mkataba (*contract farming*) kwenye mazao ya mahindi machanga (*baby corn*), maua, njegere, maharage machanga (*green beans*) na artemisia kwa vikundi 100 vya wakulima katika Wilaya ya Arumeru na kuunganishwa na masoko na kuwezesha uanzishwaji wa chama cha wazalishaji wa mifugo na usindikaji katika kijiji cha Kambala, wilaya ya Mvomero.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa *PADEP* pia uligharamia mchakato wa uanzishaji na uzinduzi wa Baraza la Maendeleo ya Kilimo cha Mboga na Maua Tanzania (*Horticultural Development Council of Tanzania - HODECT*) na Baraza la Nyama Tanzania *(Meat Council of Tanzania*). Maeneo mengine ambayo Mradi ulichangia ni pamoja na kuwezesha kikundi cha wajasiriamali kushiriki maonesho ya biashara ya kilimo (*Agribusiness Exhibition*) yaliyofanyika nchini Afrika Kusini mwaka 2007 na wakulima kushiriki maonesho ya kilimo ya Nanenane.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Kusaidia Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Programme Support- ASPS*) katika mwaka 2007/2008, ASPS iliendeleza mipango ya maendeleo ya kilimo ya wilaya *(DADPs)* katika Mikoa ya Iringa na Mbeya, kutoa mafunzo kwa maafisa ugani wa wilaya za mikoa ya Dodoma, Iringa, Morogoro, Lindi na Mtwara juu ya uzalishaji wa Mbegu za Daraja la Kuazimiwa *(QDS),* kutoa mafunzo ya ukaguzi wa mbegu hizo, kugharamia ukarabati wa maabara ya mbegu *TOSCI*- Morogoro na pia iliwezesha wakulima 577 wa Mikoa ya Dodoma, Iringa, Morogoro, Lindi na Mtwara kuzalisha tani 200 za mbegu za daraja la kuazimiwa za nafaka, mikunde, mbegu za mafuta na mbogamboga. Aidha, Programu ilifanikisha tafiti mbalimbali zenye lengo la kuboresha sera na sheria katika sekta ya kilimo na kuisadia sekta binafsi kuandaa maandiko ya kibiashara 125 ambapo kati ya hayo maandiko 105 yalipatiwa mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 6.5 kutoka benki za *CRDB, ACB, FBME* na *Exim*.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007/2008 ulikuwa mwaka wa mwisho wa utekelezaji wa ASPS ulioanza mwaka 2003. Programu imefanikiwa kugharamia uanzishaji wa utaratibu wa kuzalisha mbegu za daraja la kuazimiwa *(QDS)* katika wilaya 18 za mikoa ya Dodoma, Iringa, Morogoro, Lindi na Mtwara. Mafanikio mengine ni pamoja na ujenzi wa skimu za umwagiliaji maji za Naming'ong'o, Utengule, Usongwe, Nyanza na Irindi. Vilevile, Programu iliwezesha tafiti mbalimbali na maandalizi ya miswada ya sheria na uanzishwaji wa Baraza la Taifa la Kilimo (*Agricultural Council of Tanzania- ACT*).

Mheshimiwa Spika, uratibu wa utekelezaji wa sera na sheria za kilimo, katika mwaka 2007/2008, Wizara iliratibu mchakato wa kukusanya maoni na mapendekezo ya wadau kuhusu maeneo ya kuzingatiwa katika Sera mpya ya Kilimo. Mchakato huo uliwezesha kupata mapendekezo ya wadau kuhusu masuala muhimu yakuzingatiwa katika rasimu ya sera hiyo. Baadhi ya maeneo hayo ni pamoja na kuweka mkazo zaidi kwenye kilimo cha kibiashara, ushiriki wa sekta binafsi katika maendeleo ya sekta ya kilimo, huduma za ugani, utafiti, mafunzo kwa wataalam, wakulima na watoa huduma za pembejeo na zana za kilimo.

Aidha, sera izingatie matumizi ya bioteknolojia, uzalishaji wa mazao nishati (*biofuels*), kilimo hai *(organic farming),* mazao ya mbogamboga *horticulture* na mbinu za kujikinga na majanga *(risk management).* Wadau pia walipendekeza sera mpya izingatie kuwepo kwa utaratibu utakaosaidia upatikanaji wa soko la mazao ya wakulima kabla ya uzalishaji, kilimo cha mkataba na uanzishaji wa Benki ya Kilimo pamoja na matumizi ya Stakabadhi za Mazao Ghalani. Eneo jingine lililopewa msisitizo ni kuimarisha usimamizi wa sheria, kanuni na taratibu za uzalishaji, usindikaji na biashara ya mazao, usimamizi wa rasilimali za uzalishaji, hususan ardhi, maji, bio-nuai ya kilimo, rasilimali watu na huduma katika sekta ya kilimo. Maandalizi ya sera hiyo mpya yatakamilishwa mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara ilishirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kukamilisha maandalizi ya Muswada wa sheria itakayoweka utaratibu wa kusimamia utengenezaji, uingizaji, usambazaji na matumizi ya mbolea nchini. Wizara pia ilikamilisha ukusanyaji wa taarifa muhimu zitakazowezesha

kutungwa kwa sheria itakayotambua, kulinda na kuendeleza rasilimali za uzalishaji wa kilimo nchini ikiwa ni pamoja na ugani na kilimo cha mkataba. Kazi zingine zilizofanyika ni pamoja na kukamilisha uainishaji wa maeneo muhimu ya kuzingatiwa kwenye sheria ya kulinda na kuendeleza nasaba za mimea kwa ajili ya kilimo na chakula na kuandaa rasimu ya awali ya Muswada wa sheria hiyo. Rasimu ya awali ya Muswada wa marekebisho ya sheria za mazao ya kahawa, pamba, chai, tumbaku, pareto, mkonge, sukari na korosho nayo pia iliandaliwa.

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo Mifugo na Mazingira ya Zanzibar ilifanya uchambuzi wa maeneo ya kurekebishwa kwenye Sheria ya kulinda afya ya mimea (*The Plant Protection Act, 1997*) kwa lengo la kuwezesha Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuwa na mfumo unaofanana kwenye masuala ya afya ya mimea kama inavyotakiwa chini ya mikataba ya afya ya mimea ya kimataifa ambayo Tanzania ni mwanachama. Maoni ya wadau na wataalam kuhusu marekebisho ya sheria ya TPRI yalikusanywa.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya ushirika nchini, katika mwaka 2007/2008, Wizara iliendelea kutekeleza Programu ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika nchini kwa kushirikiana na wadau wengine. Chini ya Programu hiyo, Wizara ilitekeleza Mkakati Maalum wa kuimarisha Vyama vya Ushirika wa mazao ili viweze kufanya biashara na kuwalinda wakulima dhidi ya wanunuzi binafsi waliokuwa wanawapunja wakulima kwa kuwalipa bei ndogo kuliko ilivyostahili. Katika kuviwezesha Vyama kufanya biashara, Wizara ilitoa mafunzo ya ujasiriamali kwa viongozi na watendaji wa Vyama Vikuu vya *MAMCU* na *TANECU* (Mtwara), *TAMCU* (Ruvuma), *ILULU* (Lindi) *DARECU (DSM*) na *CORECU* (Pwani). Aidha, Serikali ilitoa watumishi 14 kusaidia kuimarisha uendeshaji wa Vyama hivyo na ilitoa udhamini wa mikopo ya benki ulioviwezesha kupata mikopo ya jumla ya Shilingi bilioni 26.1 ambazo zilitumika kukusanya na kuuza zao la korosho. Serikali pia ilidhamini mikopo ya benki iliyotolewa kwa vyama vya Ushirika vya *KNCU* na *SHIRECU* kwa ajili ya kununulia mazao ya kahawa na pamba.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2005 Bunge lako tukufu lilipitisha Sheria iitwayo *'the Warehouse Receipt System Act' Na. 10* ya mwaka 2005. Sheria hiyo kwa Kiswahili inajulikana kwa jina la "Sheria ya Stakabadhi za Mazao Ghalani" au "Sheria ya Benki Mazao". Sheria hiyo inatoa fursa kwa wakulima wa mazao na wazalishaji wa bidhaa nyingine nchini kukusanya na kuhifadhi mazao au bidhaa zao na kupata stakabadhi ambazo zinawawezesha kufanya shughuli za kibiashara ikiwa ni pamoja na kuchukua mikopo Benki wakati mazao au bidhaa zao ghalani zikiendelea kushindaniwa na wanunuzi au zikisubiri soko kuwa na bei nzuri. Kuanzia mwaka 2006, Serikali imekuwa ikihimiza wakulima na wazalishaji wengine nchini kuanza kuutumia utaratibu huo katika biashara ya mazao. Katika sekta ya mazao, mfumo huo unaweza kutumiwa kwa manufaa makubwa katika biashara ya mazao makuu ya biashara na ya chakula hata baada ya kuongezwa thamani.

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2007/2008, ili kukabiliana na changamoto za biashara ya zao la korosho nchini, Serikali ilielekeza utaratibu wa Stakabadhi za

Mazao utumiwe katika biashara ya zao hilo kwa kuanzia katika mkoa wa Mtwara ambao huzalisha takriban asilimia 60 ya korosho inayozalishwa nchini. Utaratibu wa Stakabadhi za Mazao Ghalani ulitekelezwa kwa mafanikio. Kwa mfano, kwa mara ya kwanza karibu wakulima wote walipata malipo kamili ya bei ya korosho zao. Wastani wa bei ya kilo moja kwa mkulima iliongezeka na kufikia Shilingi 610 hadi 780 kwa kilo ya korosho daraja la kwanza na Shilingi 480 kwa kilo ya daraja la pili. Malipo hayo ni ya juu kuliko yaliyokuwa yanatolewa na makampuni binafsi katika misimu iliyotangulia. Aidha, vyama vya Ushirika vimeweza kulipa mikopo yote ya benki, ushuru wa Halmashauri na kubakiwa na ziada ambayo itatumika kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya Vyama husika.

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2007/2008, Serikali pia ilianza kutekeleza mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani katika zao la pamba katika maeneo ya mikoa ya Manyara na Shinyanga. Uzoefu uliopatikana unaonyesha kwamba ili utaratibu huo ufanikiwe kwenye zao la pamba kuna haja ya kutenganisha huduma za ununuzi wa pamba mbegu na huduma ya uchambuzi wa pamba. Hatua hiyo ya kutenganisha itawezesha pamba iliyochambuliwa iendelee kumilikiwa na mkulima bila kulazimika kuwauzia wanunuzi ambao wengi ni wamiliki wa vinu vya kuchambua pamba.

Utaratibu huo utawapa wakulima fursa ya kuhifadhi pamba yao katika utaratibu wa Stakabadhi za Mazao Ghalani na kuuza pamba waliyozalisha katika soko kwa ushindani na hivyo kuongeza fursa ya kupata bei nzuri zaidi kama ilivyokuwa kwenye zao la korosho. Kwa mfano, mkulima aliyeshiriki katika utaratibu huo katika Mkoa wa Shinyanga alilipwa wastani wa kuanzia Shilingi 500 kwa kilo kama malipo ya kwanza na kulipwa malipo ya pili baadaye. Wastani wa bei ya pamba kwa wakulima ambao hawakushiriki katika utaratibu huo ulikuwa Shilingi 400 hadi 500 kwa kilo na hapakuwepo na malipo ya pili.

Mheshimiwa Spika; katika mwaka 2007/2008, Wizara ilitoa mafunzo ya uhasibu na utunzaji kumbukumbu kwa makarani 165 wa Vyama vya Ushirika wa mazao wa Mikoa ya Mtwara na Tabora ili kuboresha uandishi na utunzaji wa kumbukumbu pamoja na utayarishaji wa hesabu za mwisho wa mwaka kwa ajili ya kufanyiwa ukaguzi na kutoa taarifa kwa wanachama. Vilevile, Wizara ilitoa mafunzo kwa viongozi wa Vyama Vikuu vya Ushirika vinavyohusika na zao la tumbaku. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo kwa Maafisa Ushirika 51 kutoka katika mikoa inayozalisha pamba ili kuwajengea uwezo wa kusimamia biashara ya pamba katika msimu wa 2008/2009 na ilidhamini mafunzo ya kuwajengea uwezo watendaji wa *SACCOS* nchini katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Biashara cha Moshi.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha Vyama vya Ushirika vinatunza mahesabu yao kwa mujibu wa sheria, mwaka 2007/2008, Wizara ilifanya ukaguzi maalum katika Vyama vya Msingi viwili na Vyama Vikuu saba. Aidha, Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika *(COASCO)* lilifanya ukaguzi wa mwisho kwa Vyama vya Ushirika 1,654 sawa na asilimia 40 ya lengo la kukagua Vyama 4,116. Utekelezaji huo wa chini ulisababishwa na Shirika la *COASCO* kuwa na idadi ndogo ya wakaguzi, ikilinganishwa na idadi ya Vyama vya Ushirika na matatizo ya upatikanaji wa

fedha za kutosha kwa ajili ya kugharamia shughuli za ukaguzi wa vyama. Tatizo jingine ni baadhi ya Vyama vya Ushirika, hususan Vyama vya Ushirika vya Msingi kushindwa kufunga mahesabu yao kwa wakati na hivyo kutomwezesha mkaguzi kutekeleza kazi zake za ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008 Wizara iliandaa miongozo mbalimbali ya uendeshaji na usimamizi wa Vyama vya Ushirika, ikiwemo miongozo ya ujasiriamali na uendeshaji wa Vyama vya Ushirika kibiashara. Miongozo hiyo ilitolewa kwa viongozi wa Vyama vya mazao ya korosho na pamba na itaendelea kutolewa kwa vyama vingine vya Ushirika katika mwaka ujao wa fedha.

Wizara pia iliandaa miongozo ya uhasibu, ukaguzi na ya mifumo ya uendeshaji wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo ambayo iko tayari kwa ajili ya kusambazwa kwa Vyama vya Ushirika. Aidha, kwa kushirikiana na wadau Wizara iliendelea kuhamasisha wananchi kuanzisha au kujiunga na Vyama vya Ushirika. Vyama vipya vilivyoanzishwa ni pamoja na: Sekta ya fedha - SACCOS 1,055; Sekta ya Kilimo - AMCOS 11; Umwagiliaji - Vyama 10; Uvuvi Vyama 7; Viwanda - Vyama 20; Walaji - Vyama 59 na Huduma mbalimbali - Vyama 152.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya utekelezaji wa CRMP nafurahi kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba juhudi za Wizara za utekelezaji wa CRMP zinazolenga katika kuwa na vyama vya ushirika imara vinavyoweza kustahimili ushindani zilizoanza mwaka 2006/2007 zimeanza kuzaa matunda. Katika mwaka 2007/2008 pamoja na mafanikio yaliyoonekana kwenye Vyama vya Ushirika vya zao la korosho, Vyama vya Ushirika vya mazao ya kahawa vya *ACU, KCU, KDCU, KNCU* na *KANYOVU* navyo pia vimefanikiwa kujiendesha kiuchumi. Aidha, Chama Kikuu cha Maziwa cha Tanga (*Tanga Diary Cooperative Union- TDCU*) nacho pia kilifanikiwa kujiendesha kiuchumi.

Arusha Cooperative Union (ACU) kina vyama vya ushirika wanachama 29 na kinajishughulisha na kukusanya kahawa ya wakulima, kuisafirisha mpaka kiwandani na kuiuza mnadani. Kwa misimu mitatu mfululizo (2003/2004 – 2005/2006) chama hicho kimeweza kuwalipa wakulima malipo ya pili kwa wanachama waliouza kahawa yao kupitia chama hicho.

Kagera Cooperative Union (*KCU) Kagera Cooperative Union (1990) Ltd.* kinaundwa na vyama vya ushirika vya msingi 126 vya wilaya za Bukoba Vijijini, Misenyi, Bukoba Manispaa na Muleba. *KCU* ni miongoni mwa Vyama Vikuu vya Ushirika vichache nchini vyenye mafanikio kutokana na usimamizi mzuri unaowezesha kupata ziada ya kuwalipa wanachama malipo ya pili na ya tatu. Kwa mujibu wa hesabu zilizokaguliwa KCU ilipata ziada ya shilingi milioni 61.296 mwaka 2004 na shilingi milioni 212.209 mwaka 2005.

Msimu 2006/2007, chama kilipata fedha kutoka soko la kahawa ya ubora maalum *(Fair Trade)* ya Shilingi bilioni 2.22. Kutokana na mafanikio hayo, *KCU* imewekeza katika miradi inayowanufaisha wanachama moja kwa moja. Kwa mfano, kununua mashine za kukoboa kahawa kwa vyama vyote vya msingi na vifaa vya kupima ili

kuthibiti ubora. Aidha, *KCU* imeajiri maafisa ugani 46 wa kuhudumia wanachama wake. Habari zaidi kuhusu maendeleo ya *KCU* zinapatikana kwenye tovuti *(website)* yao www.kcu-tz.com.

Ubia wa Vyama vya Ushirika vya Msingi KANYOVU – Kigoma, Mradi wa pamoja wa *Kanyovu Coffee Curing Cooperative Joint Enterprise* unajumuisha Vyama vya Ushirika vya msingi vya Rumako, Kalinzi, Kibanda, Mkigo, Ntaruboza, Mbanga, Mahwenyi na Manyovu mkoani Kigoma ambavyo mwaka 2005 vilianzisha kiwanda cha kukoboa kahawa. Ubia huo umewezesha wanachama wa Vyama vya Msingi vinavyohusika kupata malipo ya pili. Aidha, kupitia ubia wa vyama hivyo kiwanda cha kukoboa kahawa kimekarabatiwa, ubia umeshiriki katika ujenzi wa sekondari maeneo ya vyama wanachama, umeyakarabati maghala ya vyama, umenunua na kusambaza pembejeo za kilimo kwa wanachama, umenunua lori aina ya Scania kwa ajili ya kusombea kahawa na kusambaza pembejeo, na gari kwa ajili ya matumizi ya ofisi.

Katika msimu wa 2007/2008, *Shinyanga Region Cooperative Union SHIRECU* ilishiriki katika biashara ya Pamba baada ya Serikali kukilipia deni la benki la Shilingi bilioni 1.5 na hivyo kuwa na sifa ya kukopesheka ambapo *SHIRECU* ilipata mkopo wa benki ya CRDB wa Shilingi bilioni 2.5 uliowawezesha kukusanya kilo milioni 2.7 za pamba mbegu ikiwa ni asilimia 15 ya makisio. Hali hiyo, ilitokana na uzalishaji mdogo wa pamba uliochangiwa na mvua kuwa nyingi na kusababisha mafuriko. Hata hivyo chama kilitoa changamoto kwa wanunuzi binafsi na kupelekea wakulima kunufaika na ongezeko la bei ambayo ilifikia shilingi 500 kwa kilo ya pamba daraja la kwanza. Katika msimu wa 2008/2009 chama kimepata mkopo wa benki na kinashiriki katika biashara ya pamba.

Nyanza Cooperative Union (NCU) haikununua pamba kwa msimu wa 2006/2007 na 2007/2008 kutokana na kuchelewa kupata mkopo na ushindani mkubwa uliokuwepo kutoka kwenye makampuni binafsi. Hata hivyo chama kilichukua hatua mbalimbali za kujipanga upya kuweza kufanya biashara. Hatua hizo ni pamoja na kuwatembelea wanachama wake na kuwafahamisha azma ya kukiimarisha ili kiweze kuwanufaisha, kuazimishwa watendaji wa Serikali akiwemo Meneja Mkuu na Mhasibu Mkuu na kuimarisha Bodi ya chama kwa kuteua wajumbe maalum ili kuimarisha uwezo wa kusimamia utendaji wa shughuli za chama. Chama hicho kinashiriki katika ununuzi wa pamba msimu wa 2008/2009. Chama kimeshapata mkopo kwa ajili ya utekelezaji wa jukumu hilo.

Mheshimiwa Spika, jitihada za kufufua ushirika nchini, mwaka 2007/2008 Wizara ilianzisha juhudi za kufufua na kuimarisha ushirika katika mikoa ambamo ushirika ulikuwa umekufa. Kwa mfano, katika Mkoa wa Mara Vyama vya Ushirika vingi vya mazao vilikuwa vimesinzia au vilikuwa mawakala wa makampuni binafsi kwa muda mrefu.

Kutokana na kutokuwepo kwa ushirika katika Mkoa huo wakulima hupunjwa bei na makampuni binafsi. Mwaka 2007/2008 Wizara iliwahamasisha wanaushirika wa Vyama vya Msingi katika Mkoa wa Mara kukubaliana kuanzisha Chama Kikuu cha

Ushirika ambacho kitaunganisha nguvu za wakulima mkoani. Vyama vya Ushirika vya Msingi 69 vilifanya mikutano mikuu na wanachama wake walikubaliana kuunda Chama Kikuu. Matarajio yao ni kukamilisha ukusanyaji wa hisa mwezi Julai, 2008 na kuwasilisha maombi ya kuandikishwa kwa chama kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, madeni ya wakulima, mwaka 2007/2008 nililiarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inakusudia kulipa madeni ya wakulima ambao walikopwa mazao yao miaka ya 1990 katika maeneo mbalimbali nchini. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali ilitenga Shilingi bilioni 2.5 kutokana na Bajeti yake ya 2007/2008 na hatua za kuwalipa wakulima zimeanza kuchukuliwa. Wakulima watakaolipwa ni wale ambao hesabu zao zilifungwa Desemba 2004 na iliyokuwa Wizara ya Ushirika na Masoko.

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya Rasilimali Watu. Katika mwaka 2007/2008, Wizara iliendelea kuwapandisha watumishi vyeo na kuandaa mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia mahitaji ya Wizara. Katika mwaka huo watumishi 124 walipandishwa vyeo na watumishi 131 walithibitishwa kazini. Aidha, Wizara iliajiri watumishi wapya 330 kwa utaratibu ulioainishwa katika Sera ya Menejimenti na Ajira katika utumishi wa umma. Kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na kutoa mafunzo ya kujikinga na maambukizi ya *UKIMWI* pamoja na kupima virusi vya *UKIMWI* ambapo watumishi 722 walipima, kati yao 20 walibainika kuwa na virusi vya *UKIMWI*.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Mwaka 2008/2009. Ilani ya Uchaguzi ya *CCM* kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2005 inatambua kuwa “kilimo cha kisasa ndio msingi wa uchumi wa kisasa.” Aidha, ili kubadili kilimo chetu kiwe cha kisasa, Ilani ya Uchaguzi imeelekeza zichukuliwe hatua zifuatazo:-

(i) Kufikisha kwa wakulima vijijini maarifa ya kanuni za kilimo bora kwa kutumia mbinu shirikishi na kuwaandaa wataalam wa ugani;

(ii) Kueneza matumizi ya plau za kuvutwa na wanyama na matreka;

(iii) Kuweka utaratibu wa uhakika wa upatikanaji na usafirishaji wa mbegu bora na mbolea na kuzifikisha kwa wakulima;

(iv) Kueneza matumizi ya mikokoteni ya kuvutwa na wanyama na vinu vya kisasa vya kukobolea na kusaga nafaka;

(v) Kuweka utaratibu mzuri wa mashindano ya kilimo kuanzia ngazi ya kijiji hadi tarafa;

(vi) Kuimarisha na kuboresha utaratibu wa kutoa ruzuku ya pembejeo;

(vii) Kuweka vivutio kwa wawekezaji wa mashamba makubwa;

(viii) Kuimarisha uzalishaji na tija katika skimu za umwagiliaji;

(ix) Kupunguza upotevu wa mazao, *pre and post harvest losses,* kwa kudhibiti visumbufu na kuimarisha uanzishaji wa viwanda vya usindikaji; na

(x) Kuhimiza uzalishaji wa mazao kwa kuzingatia uwezo wa ardhi na hali ya hewa, *Agro-ecological zones*.

Mheshimiwa Spika, aidha, kuhusu maendeleo ya Ushirika, Ilani ya Uchaguzi ya *CCM* kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2005 inasisitiza kuendelea na utekelezaji wa programu ya ushirika na kuhamasisha wananchi wengi kujiunga na kuanzisha vyama vya akiba na mikopo, *SACCOS*, na hivyo kuwapunguzia wananchi umaskini.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa mwaka 2008/2009 utatekeleza maelekezo ya Ilani ya *CCM* ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2005 kupitia *ASDP* na *CRMP*. Katika kutekeleza mpango huo, suala la usalama wa chakula limepewa kipaumbele maalum kutokana na tishio la upungufu wa chakula duniani.

Mheshimiwa Spika, kutokana na tishio hilo la upungufu wa chakula duniani mikakati mbalimbali imeanza kuchukuliwa kupitia vikao vya kimataifa. Kwa mfano, kikao cha Nne cha *Tokyo International Conference, TICAD IV,* kilichofanyika mjini Yokohama, Japan tarehe 28 hadi 30 Mei 2008, Mkutano wa Kufufua Kilimo uliofanyika tarehe 25 hadi 27 Juni 2008 mjini Tunis, Tunisia na kikao cha Wakuu wa nchi kilichofanyika Roma, Italia tarehe 3 hadi 5 Juni 2008, vilitoa tamko kuhusu usalama wa chakula na namna ya kukabiliana na kupanda kwa bei za vyakula. Vikao vyote hivyo, vilizungumzia hatua zinazotakiwa zichukuliwe kukabiliana na upungufu wa chakula duniani. Hatua hizo ni pamoja na kuwawezesha wakulima kupata mbegu bora, mbolea na masoko ya uhakika.

Kupanda kwa bei za mazao ya chakula ndani na nje ya nchi na upungufu wa chakula uliojitokeza duniani ni fursa nzuri kwa Taifa letu kuongeza maradufu uzalishaji wa chakula kwa ajili ya matumizi ya nchi na kuuza ziada nje ya nchi. Ili kuweza kutumia fursa hiyo, Wizara kupitia Mpango wa mwaka 2008/2009, inakusudia kutekeleza mkakati wa muda mfupi wenye kuleta matokeo ya haraka na mikakati ya muda wa kati na mrefu kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Mkakati wa Muda Mfupi wa Kuleta Mapinduzi ya Kijani. Kama nilivyolifahamisha Bunge lako Tukufu mwaka jana kwamba azma ya Serikali ni kuhakikisha kwamba pembejeo za kilimo zinapatikana kwa wakulima wakati wote ikiwa ni njia moja wapo ya kuleta Mapinduzi ya Kijani hapa nchini. Katika kipindi cha 2008/2009, Wizara inakusudia kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kutoa ruzuku kwa tani 130,000 za mbolea, tani 3,000 za mbegu bora, tani 2,000 za madawa ya mimea. Lengo ni kuongeza matumizi ya mbolea kutoka kilo 9 za virutubisho mwaka 2007/2008 hadi kilo 11 mwaka 2008/2009.

(ii) Kuhakikisha uzalishaji wa mbegu bora za aina mbalimbali unaboreshwa kwa kuhamasisha wakulima kuzalisha mbegu za daraja la kuazimiwa na makampuni binafsi kuzalisha mbegu. Wakala wa Mbegu za Kilimo, *Agricultural Seed Agency - ASA*, unatarajiwa kuzalisha jumla ya tani 1,000 za mbegu za msingi za mahindi, ngano, mtama, mpunga, soya, alizeti, ufuta, karanga, nyanya na bilinganya ambazo zitasambazwa kwa makampuni na wakulima.

(iii) Kutoa mafunzo kwa mawakala wa pembejeo katika wilaya 38 kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Aidha, mafunzo yataendelea kutolewa katika wilaya ambazo mafunzo yalianza kutolewa katika mwaka 2007/2008 ili kufikia lengo la kuwa na takriban mawakala 50 waliopatiwa mafunzo katika kila Wilaya.

(iv) Kuweka malengo ya uzalishaji yanayopimika kwa kila mkoa na Halmashauri za Wilaya.

(v) Kuwashirikisha viongozi, wanasiasa na watendaji wa ngazi zote katika halmashauri na Taifa kuhamasisha na kusimamia kilimo.

(vi) Kusimamia na kutathimini utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya pembejeo za kilimo.

(vii) Kusimamia utekelezaji wa sheria na kanuni za ubora wa mbolea.

(viii) Kuimarisha huduma za utafiti, ugani na ushirika.

(ix) Kujenga uwezo wa kuyahifadhi mazao ya chakula katika ngazi ya kaya na Taifa.

(x) Kuendeleza matumizi ya utaratibu wa stakabadhi za mazao ghalani katika mazao ya chakula.

(xi) Kuhimiza matumizi ya vyakula visivyotokana na nafaka, hususan mihogo, viazi, magimbi na ndizi ikiwa ni pamoja na kueneza teknolojia za usindikaji wa vyakula unaozingatia uchanganyaji wa vyakula hivyo.

(xii) Kuongeza uzalishaji na tija kutoka wastani wa tani mbili kwa hekta hadi kati ya tani 4.5 na tani sita kwa hekta katika skimu 10 za umwagiliaji zitakazo chaguliwa. Wakulima katika skimu hizo watapatiwa mafunzo kuhusu mbinu bora za kilimo cha mpunga, matumizi bora ya maji, zana bora za kilimo, pembejeo za ruzuku na huduma za ugani.

(xiii) Kuainisha fursa zilizopo za uzalishaji wa mazao ya chakula kwa kila Wilaya kutegemea hali ya hewa, *agro-ecological zones.* Kwa mfano, mikoa ya Dodoma,

Singida, Tabora, Shinyanga, baadhi ya wilaya za Mkoa wa Mwanza hususan Magu, Kwimba na Misungwi, Mkoa wa Mara hususan wilaya za Bunda, Msoma Vijijini na Rorya, Mkoa wa Kilimanjaro husuan maeneo ya Tambarare za katika Wilaya za Same na Mwanga zinafaa kwa kilimo cha mtama na uwele. Maeneo hayo kuendelea kulima mahindi ni kuendelea kupoteza nguvu za wakulima na kuathiri usalama wa chakula. Wizara itatilia mkazo kilimo cha mahindi katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Morogoro, Manyara, Arusha na Kilimanjaro na Mara katika Wilaya ya Tarime kwa kuzingatia uwezo wa uzalishaji kikanda kama inavyonyeshwa katika Kiambatisho Na.3. Natoa wito kwa Viongozi wa Mikoa na Wilaya washirikiane na Wizara yangu katika kuwahamasisha wakulima wa maeneo hayo kuzingatia maelekezo hayo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hatua za muda mfupi zitakazo chukuliwa matarajio ya uzalishaji wa chakula yanatarajiwa kufikia tani milioni 11.579 mwaka 2008/2009 ikilinganishwa na tani milioni 10.782 mwaka 2007/2008 kama ilivyooneshwa kwenye Kiambatisho Na. 4.

Mheshimiwa Spika, ili kutatua matatizo ya kutoa ruzuku ya pembejeo, kuanzia msimu wa 2008/2009, Wizara itapanua matumizi ya vocha kwa ajili ya kutoa ruzuku ya pembejeo, hususan mbolea. Utaratibu wa kutumia vocha utaanza kwa awamu katika mikoa 8 yenye uwezo mkubwa wa kuzalisha mazao ya chakula, hususan mahindi.

Vocha ni hati punguzo yenye thamani ya kiasi cha fedha inayotolewa kwa ajili ya kugharimia sehemu ya bei ya pembejeo za kilimo ili kumfanya mkulima apate pembejeo kwa bei nafuu. Tofauti na utaratibu ambao umekuwa ukitumika hadi sasa, vocha itawezesha ruzuku kutolewa moja kwa moja kwa wakulima na hivyo kuondoa nafasi ya mawakala kuwadanganya wakulima.

Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imetoa utaratibu unaoainisha majukumu ya wizara, mikoa, wilaya, kamati za vijiji, mawakala wa pembejeo za kilimo, makampuni ya pembejeo na ya benki. Aidha, maandalizi ya vocha na mawakala yanaendelea. Wizara pia itatoa mafunzo kwa watendaji wa mikoa, wilaya na vijiji kuhusu majukumu yao wakati wa utekelezaji wa utaratibu wa vocha. Vilevile, Wizara itaingia mkataba na Benki ya *NMB* kwa ajili ya kuwawezesha mawakala wa pembejeo kununua na kusambaza pembejeo kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa vocha utaweka vigezo vitakavyotumika kuchagua wakulima kama ifuatavyo: mkulima awe ni mkazi na mwenye shamba linalolimwa; awe tayari kupokea na kuzingatia ushauri wa kitaalam, na kuchangia sehemu ya gharama za pembejeo. Baada ya majina kuteuliwa yatapitiwa na Serikali ya kijiji na yatahakikiwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji. Wakulima watakaotambuliwa watapewa vocha na uongozi wa kijiji kwa ajili ya kununua pembejeo zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, Mikakati ya Muda wa Kati na Mrefu. Katika muda wa kati na mrefu , msisitizo utawekwa katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kuongeza uzalishaji na matumizi ya pembejeo, hususan mbolea na mbegu bora, upatikanaji wa matrekta na zana zinazokokotwa na wanyamakazi na ujenzi wa viwanda vya mbolea, zana na madawa.

(ii) Usindikaji wa mazao ya kilimo katika viwanda vya kati na vikubwa utatiliwa mkazo kwa nia ya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo. Wizara itahamasisha uwekezaji wa ndani na nje katika kilimo cha kibiashara na kuimarisha vyama vya ushirika.

(iii) Kuongeza uzalishaji kwenye skimu za umwagiliaji 40 kwa kutoa mafunzo kwa wakulima kuhusu mbinu bora za kilimo cha mpunga, matumizi bora ya maji na kupatiwa pembejeo zenye ruzuku, huduma za ugani na zana za kilimo.

(iv) Kuhimiza utafiti unaozingatia uzalishaji wa mazao ya chakula yanayostahimili ukame au kukomaa haraka na mbinu za kukabiliana na tabianchi na uharibifu wa mazingira kwa ujumla.

(v) Kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo Kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo, *Agricultural Sector Development Programme.* Mwaka 2008/2009, utakuwa ni mwaka wa tatu wa kutekeleza Programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo, *Agricultural Sector Development Programme – ASDP*, unaotekelezwa katika Wilaya zote za Tanzania Bara. Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji, *Participatory Agricultural Development and Empowerment Project – PADEP*, na Mradi wa Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo Wilayani, *District Agricultural Investment Project – DASIP*, ni sehemu ya utekelezaji wa *ASDP*.

Mheshimiwa Spika, *ASDP* ni programu inayotekeleza sera ya kupeleka madaraka kwa wananchi, *Decentralization by Devolution - D by D,* kwa kupeleka karibu asilimia 75 ya rasilimali za sekta ya kilimo wilayani na vijijini. Utekelezaji wa *ASDP* katika ngazi ya wilaya unafanyika kwa kupitia *DADPs*. Ili kutekeleza sera hiyo, mwaka 2008/2009, halmashauri zilipatiwa maelekezo ya kiasi cha fedha ambazo zitatengwa kwa kila halmashauri ili zitumie maelekezo hayo katika matayarisho ya mipango na bajeti zao kwa mwaka 2008/2009 na kujadiliwa na kamati ya fedha ya halmashauri husika na hatimaye kupitishwa na Baraza la Madiwani.

Hivyo, bajeti za mikoa zimetengewa jumla ya Shilingi bilioni 58.887 zitakazopelekwa kwenye halmashauri kutokana na fedha za Mfuko wa Pamoja wa *ASDP*. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 53.892 zikiwa ni fedha za nje na Shilingi bilioni 4.998 zikiwa ni fedha za ndani. Kupitia *PADEP* zitapelekwa Shilingi bilioni 5.885 na kupitia *DASIP* zitapelekwa Shilingi bilioni 16.514. Aidha, Sekretariati za mikoa nazo zimetengewa jumla ya Shilingi milioni 148.665 kwa ajili ya kusimamia na kuratibu utekelezaji wa *DADPs*.

Mheshimiwa Spika, Wizara za Sekta ya Kilimo zimetengewa Shilingi bilioni 18.278 na kati ya fedha hizo, Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika imetengewa Shilingi bilioni 10.31 kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma za utafiti, ugani na zana za kilimo, ukarabati wa vyuo vya kilimo, usalama wa chakula, sensa ya kilimo na mifugo, sheria na uratibu. Aidha, ili kuzijengea halmashuri za wilaya uwezo wa kusimamia na kuratibu utekelezaji wa *DADPs*, Wizara za Sekta ya Kilimo zitatekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuimarisha timu ya Taifa ya wawezeshaji, *National Facilitation Team,* kwa kuongeza idadi yao, kuifanya iwe ya kudumu na kuwajengea uwezo zaidi wa uwezeshaji, *Facilitation Skills.*

ii. Kuimarisha timu za wawezeshaji za wilaya na kata, *District and Ward Facilitation Teams,* kwa kuzifundisha namna ya kuandaa michanganuo ya miradi ya uwekezaji, *investment proposals,* iliyoibuliwa kupitia *DADPs*. Aidha, uimarishaji wa timu hizo utazingatia pia uibuaji na utekelezaji wa miradi ya kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula ili kuongeza uwezo wa kukabiliana na changamoto au fursa za upatikanaji wa mazao hayo.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Uwekezaji Katika Sekta ya Kilimo Wiloayani. Katika mwaka 2008/2009, Wizara kupitia mradi wa *DASIP* itaendelea kuzijengea uwezo Halmashauri za Wilaya 28 zinazotekeleza mradi na kuwezesha jamii kuibua, kupanga na kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya, *DADPs*.

Aidha, mafunzo mbalimbali yatatolewa kwa wakulima na wataalamu wa kilimo na mifugo kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kuwasaidia kutumia fursa walizonazo kuendeleza kilimo na ufugaji bora. Mafunzo kuhusu uimarishaji wa Vyama vya Akiba na Mikopo pamoja na kuendeleza masoko ya mazao ya kilimo na mifugo pia yatatolewa.

Mheshimiwa Spika, Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji. Kazi muhimu zitakazotekelezwa mwaka 2008/2009 ni pamoja na kuendelea kuwezesha utekelezaji wa miradi iliyoibuliwa ya jamii na vikundi vya wakulima katika wilaya za awamu ya tatu; kugharamia ukamilishaji wa utayarishaji wa rasimu ya muswada wa sheria ya mbolea na kanuni zake; kuandaa machapisho na kumbukumbu mbalimbali, *documentation*, kuhusu mchakato, uzoefu na changamoto katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya kilimo na mifugo; kuwezesha vituo vya utafiti katika kanda saba za utafiti kufikisha teknolojia zilizotolewa kwa wakulima na wafugaji; kuandaa taarifa ya kukamilisha utekelezaji wa mradi, *Project implementation completion report*; kufanya tathmini ya mwisho ya mradi, *Terminal evaluation*; na kufanya tathmini ya athari ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, Zana za Kilimo. Katika mwaka 2008/2009, Wizara itahimiza matumizi ya zana bora zikiwemo zana zinazokokotwa na wanyamakazi, matrekta madogo ya mkono *(power tillers)* na matrekta makubwa. Mafunzo kuhusu matumizi ya zana bora za kilimo yatafanywa kwa wataalamu wakufunzi 200 kutoka katika mikoa 14 ya Shinyanga, Mwanza, Mara, Tabora, Singida, Dodoma, Morogoro, Iringa, Mbeya, Rukwa, Mtwara, Arusha, Manyara na Kilimanjaro ili waweze kutoa mafunzo hayo kwa wakulima vijijini. Zana zitakazohusika ni pamoja na majembe ya palizi yanayokokotwa na wanyamakazi, "*Magoye ripper*", mashine za kupanda, matrekta madogo ya mkono na mashine za kupandikiza mpunga.

Aidha, Wizara itatoa mafunzo kuhusu matumizi ya mashine ndogo za usindikaji wa muhogo, korosho, mtama na ukamuaji wa mafuta kwa wataalam wakufunzi katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Morogoro, Singida, Manyara na Pwani.

Mheshimiwa Spika, Wizara itafanya tathmini ya kina kuhusu mahitaji ya mashine na zana za kilimo kulingana na uwezo na mahitaji katika kanda saba nchini na kuanzisha mfumo wa ukusanyaji, utunzaji na usambazaji wa takwimu za zana za kilimo ili kurahisisha uandaaji wa mipango ya maendeleo.

Aidha, Wizara itaandaa mwongozo wa kutumia zana za kilimo kibiashara pamoja na kutoa ushauri na utaalam katika Halmashauri za Wilaya ikiwa ni pamoja na kuhamasisha ulimaji wa mashamba katika eneo moja, *block farming*, ili kuongeza ufanisi wa matumizi ya zana za kilimo, huduma za ugani, matumizi bora ya ardhi, udhibiti wa

visumbufu, matumizi mazuri ya vyama vya Akiba na Mikopo, *SACCOS* na hivyo kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Pembejeo na Zana za Kilimo. Katika mwaka 2008/2009, Mfuko umetengewa jumla ya Shilingi bilioni 3 kwa ajili ya kutoa mikopo ya kununulia na kusambaza pembejeo na zana bora za kilimo. Aidha, Mfuko unategemea kukusanya kiasi cha Shilingi bilioni 4.7, hivyo kuwa na jumla ya Shilingi bilioni 7.7 ambazo zitatumika kutolea mikopo. Mikopo itakayotolewa ni ya matrekta madogo 107, matrekta makubwa mapya 124, zana za kukokotwa na wanyamakazi na zana ndogondogo za kilimo 104, tani 1,750 za mbolea, tani 40 za mbegu bora na lita 15,500 za madawa ya mimea na mifugo. Vilevile, mfuko utaendelea kukusanya madeni pamoja na kuuza dhamana za wadaiwa sugu.

Mheshimiwa Spika, Huduma za Ugani. Katika mwaka 2008/2009, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imepanga kuimarisha huduma za ugani kwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuboresha uenezaji wa teknolojia katika kilimo kwa kutumia mbinu shirikishi jamii.

(ii) Kutambua na kusajili watoa huduma binafsi za ugani katika halmashuri kwa lengo la kuwatumia na kuwasimamia katika kupanua wigo wa kutoa huduma za ugani kwa wakulima.

(iii) Kuandaa na kusambaza teknolojia bora za kilimo kwa njia ya redio, runinga, mabango, vijitabu na magazeti kwa lengo la kufikisha habari na maarifa kwa wakulima.

(iv) Kuratibu na kusimamia maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima Nanenane, Siku ya Chakula Duniani na Mashindano ya Kilimo kama mkakati wa kuhamasisha wakulima matumizi ya kueneza teknolojia za kilimo.

(v) Kufuatilia na kutoa ushauri wa kitaalam wa kuendesha huduma za ugani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kama njia ya kudumisha viwango vya utoaji wa huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara kwa kushirikiana na *TAMISEMI* itatoa mafunzo kwa vijana tarajali na kutoa ajira kwa wahitimu hao ili kukabiliana na upungufu wa wataalam wa ugani. Lengo ni kuajiri wataalam 11,703 ifikapo mwaka 2010/2011 kwa wastani wa watumishi 2,500 kila mwaka. Wizara itaongeza uwezo wa vyuo vya mafunzo kwa wataalam wa kilimo nchini kwa kukamilisha ujenzi na ukarabati wa vyuo hivyo ili kuwawezesha wanafunzi wa bweni 3,000 kujiunga na vyuo vya kilimo, kuajiri wakufunzi 100 pamoja na kununua vifaa vya maabara na karakana muhimu kwa ajili ya mafunzo ya kilimo kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, Utafiti wa Kilimo na Mafunzo. Katika mwaka 2008/2009, Wizara itaendelea kufanya utafiti ili kupata teknolojia sahihi zinazokidhi mahitaji ya kilimo na kuhakikisha kwamba matokeo ya utafiti yanawafikia wakulima kwa kufanya kazi zifuatazo:-

(i) Kutathmini aina za mbegu mpya za mazao zenye tija kubwa, kustahimili ukame, ukinzani dhidi ya magonjwa na visumbufu vya mimea na zinazokidhi viwango vya ubora na matakwa ya walaji.

(ii) Kuimarisha mahusiano kati ya watafiti na wadau wakiwemo wagani na wakulima kwa kuanzisha kitengo kipya cha kiungo, *Zonal Information and Education Liason Unit –ZIELU,* katika makao makuu ya kanda za kilimo.

(iii) Kuanzisha na kuendesha mifuko ya utafiti ya kanda itakayosimamiwa na wadau.

(iv) Kubuni na kutathmini mbinu shirikishi za udhibiti visumbufu na magonjwa ya mimea na mazao na kutathmini madawa asilia na ya viwandani yanayofaa kutumika bila kuathiri mazingira.

(v) Kuhifadhi na kuzalisha mbegu mama za mazao ya jamii za nafaka, mikunde, mbegu za mafuta na mazao ya mizizi.

(vi) Kutathmini viwango vya matumizi ya mbolea kwa madhumuni ya kutoa mapendekezo ya viwango kulingana na hali ya udongo, hewa na aina ya zao linalozalishwa katika eneo husika.

Mheshimiwa Spika, Usindikaji wa Mazao ya Kilimo. Wizara itawajengea uwezo wataalam wa kilimo wa halmashauri za wilaya kwa kuwapatia mafunzo ya teknolojia za usindikaji wa mazao ya chakula, hususan yale ya nafaka, mikunde, muhogo, mboga na matunda. Aidha, mafunzo ya utayarishaji na matumizi ya mazao ya mtama, muhogo, mboga na matunda yatatolewa kwa lengo la kupanua matumizi ya mazao hayo katika kuongeza uhakika wa chakula. Ili kuongeza soko na kupanua matumizi ya zao la muhogo, Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi itawahamasisha wasindikaji wa mazao ya nafaka kuchanganya muhogo na nafaka kama vile mahindi na mtama.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Udongo na Matumizi Bora ya Ardhi. katika mwaka 2008/2009, Wizara itakamilisha Mpango Kabambe wa Taifa wa Matumizi Bora ya Ardhi ya Kilimo na Hifadhi ambao utakuwa msingi wa upangaji na usimamizi wa matumizi ya ardhi ya kilimo. Aidha, Wizara itandaa utaratibu na sheria zitakazowezesha kutenga na kulinda ardhi kwa ajili ya kilimo, mifugo na makazi na kutoa miongozo ya teknolojia sahihi za utunzaji wa ardhi katika maeneo ya mabonde ya kilimo cha umwagiliaji. Kazi zingine zitakazofanyika ni kuweka mipaka na kupata hati miliki za ardhi katika maeneo yanayomilikiwa na Serikali yaliyo chini ya usimamizi wa Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika kwa mfano mashamba ya mbegu mama, maeneo ya vyuo vya Utafiti na Mafunzo ya Kilimo, maeneo ya kutunza nasaba za mboga, maua na matunda ili kudhibiti uvamizi unaofanywa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Udhibiti wa Visumbufu vya Mimea na Mazao. Katika mwaka 2008/2009, Wizara itaimarisha uwezo wake wa kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Afya ya Mimea kwa kutoa mafunzo kwa wakaguzi ili wasimamie ipasavyo utekelezaji wa sheria hiyo kwa ufanisi zaidi. Aidha, itatoa huduma ya karantini ya mimea na mazao ili kulinda mazao dhidi ya visumbufu kutoka maeneo mengine duniani. Itasimamia ubora wa afya ya mimea na mazao yanayosafirishwa nchini ili kukidhi viwango vya ubora unaotakiwa na masoko ya nje. Wizara pia itadhibiti milipuko ya visumbufu vya mimea na mazao kama itakavyojitokeza. Vilevile, Wizara itahamasisha wakulima kuanzisha au kuendeleza matumizi ya mbinu ya udhibiti husishi wa visumbufu vya mimea kama njia endelevu na salama.

Mheshimiwa Spika, Uzalishaji wa Mazao Makuu ya Biashara. Wizara kupitia Bodi za Mazao makuu ya biashara ambayo ni Pamba, Chai, Tumbaku, Sukari, Pareto, Korosho, Kahawa na Mkonge itasimamia utekelezaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo inayosimamia uzalishaji na biashara ya mazao hayo makuu nchini. Ili kuhakikisha tija na uzalishaji wa mazao hayo inaongezeka kwa mujibu wa malengo ya kitaifa, kimkoa na kiwilaya, Wizara itahakikisha kila mkoa na Halmashauri zinazozalisha mazao hayo, zinawahamasisha wadau wa mazao kuibua miradi ya kuzalisha miche na mbegu bora na usindikaji kwa ajili ya kuongeza uzalishaji, tija na ubora wa mazao hayo. Malengo hayo ni kama yanavyoonyeshwa kwenye Kiambatisho Na.5. Aidha, Wizara itakamilisha uanzishwaji wa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara itaratibu uzalishaji wa mazao makuu ya biashara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Pamba. Uzalishaji wa pamba katika msimu wa 2008/2009 unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 200,662 mwaka 2007/2008 hadi tani 432,000. Ongezeko hilo litatokana na wakulima kuongeza maeneo ya kilimo cha pamba, kuzingatia kanuni za kilimo bora, upatikanaji wa uhakika wa pembejeo za uzalishaji, hususan viuatilifu na mbegu bora za pamba.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha wakulima wanapata bei nzuri na soko la uhakika la pamba wanayozalisha, Wizara itawahimiza wakulima wa pamba kuuza pamba yao kupitia utaratibu wa Stakabadhi za Mazao Ghalani. Uzoefu uliopatikana katika

utekelezaji wa utaratibu huo uliofanyika kwa majaribio na kwa mafanikio katika Mkoa wa Manyara na katika Vyama vya Msingi 16 vya mkoa wa Shinyanga utatumika katika kuuneza utaratibu huo katika Vyama vyote vya Msingi vya zao la pamba katika mikoa ya Shinyanga, Mwanza, Mara na Manyara.

Lengo ni kuhakikisha pamba yote inayozalishwa nchini inanunuliwa chini ya utaratibu huo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani hivyo kumpatia mkulima fursa ya kupata bei nzuri na ya uhakika zaidi. Aidha, pamoja na kuanza utaratibu wa vocha katika ununuzi wa pamba, Wizara bado inasisitiza kwamba Halmashauri za wilaya zisitoze ushuru wa zaidi ya asilimia tano ya bei ya mkulima na kuruhusu ushindani katika ununuzi ili kumuongezea mkulima kipato.

Mheshimiwa Spika, Tumbaku. Uzalishaji wa tumbaku katika msimu wa 2008/2009 unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 57,454 mwaka 2007/2008 hadi tani 88,000. Ongezeko hilo litatokana na wakulima kuongeza tija na uzalishaji kwa kupanua maeneo ya kilimo, kuzingatia kanuni bora za kilimo cha tumbaku kutokana na bei nzuri ya zao iliyopatikana katika msimu wa 2007/2008, hususan baada ya wakulima kupata malipo ya pili. Aidha, itahakikisha wakulima wote wanaozalisha tumbaku na vituo vyote vya ununuzi vinasajiliwa na ununuzi unafanyika na wakulima wanapata malipo ya haki kulingana na madaraja na ubora wa tumbaku.

Mheshimiwa Spika, Sukari. Uzalishaji wa sukari katika mwaka 2008/2009 unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 265,434 mwaka 2007/2008 hadi tani 316,000. Ongezeko la uzalishaji litatokana na kuongezeka kwa tija na uzalishaji kutokana na ongezeko la matumizi ya mbegu bora, kuwajengea uwezo wakulima wadogo kudhibiti visumbufu vya zao la miwa, mafunzo ya kilimo bora cha miwa na kupanuliwa kwa uwezo wa uzalishaji katika viwanda vya sukari. Aidha, utaratibu wa kilimo cha *block farming* ulioanza kutekelezwa katika maeneo ya Kilombero na Kagera unategemewa kuongeza ufanisi katika uzalishaji wa miwa katika maeneo hayo. Wizara kupitia Bodi ya Sukari itatekeleza mradi wa kuendeleza zao la Sukari nchini wenye lengo la kuongeza ufanisi katika uzalishaji ili sukari ya Tanzania ifikie viwango vya ubora unaotakiwa katika soko la Ulaya. Mradi mwingine unaotekelezwa na Bodi ya Sukari kupitia ufadhili wa *CFC* unalenga kutoa aina bora za miwa yenye tija zaidi.

Mheshimiwa Spika, Pareto. Uzalishaji wa pareto katika msimu wa 2008/2009 unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 2,300 mwaka 2007/2008 hadi tani 3,000. Kiwango hicho cha uzalishaji kitafikiwa kutokana na kuongezeka kwa tija katika pareto iliyopandwa katika misimu ya 2005/2006 na 2006/2007 ambapo tija kwa hekta inategemewa kuongezeka hadi kilo 500 za maua ya pareto. Ili kufanikisha hilo, Wizara kupitia Bodi ya Pareto, sekta binafsi na vyama vya wakulima itaendelea kuratibu uzalishaji na usambazaji wa miche bora ya pareto kwa wakulima. Aidha, Wizara itawahimiza wakulima wa pareto kujiunga katika vikundi vya uzalishaji na vyama vya ushirika ili kuongeza ufanisi katika kuwafikishia wakulima teknolojia bora za uzalishaji wa pareto, uhakika wa upatikanaji wa masoko na bei nzuri.

Mheshimiwa Spika, Korosho. Uzalishaji wa korosho katika msimu wa 2008/2009 unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 99,107 mwaka 2007/2008 hadi tani 120,000. Ongezeko hilo litafikiwa kutokana na wakulima kuzingatia kanuni bora za kilimo cha korosho, hususan udhibiti wa visumbufu vya korosho ukiwemo ugonjwa wa ubwiri unga na utunzaji wa mashamba kutokana na bei nzuri na soko la uhakika walilopata wakulima wa korosho katika msimu wa 2007/2008. Aidha, ruzuku ya pembejeo inayotolewa kwenye viuatilifu vya korosho inatoa mchango mkubwa katika kuwahamasisha na kuwawezesha wakulima kununua viuatilifu vya kudhibiti visumbufu vya korosho.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Korosho itaratibu uzalishaji na usimamizi wa Sheria na Kanuni za zao la korosho. Ili kutekeleza jukumu hilo kwa ufanisi zaidi Bodi imepanga kuajiri wataalam 29 na kuwaweka katika maeneo ya uzalishaji wa korosho katika mikoa ya Mtwara, Ruvuma, Lindi, Tanga na Pwani. Utaratibu wa kutumia madaraja katika ununuzi wa korosho, *cutting test,* utatumika katika maeneo yote yanayozalisha korosho. Bodi itaratibu usambazaji wa kilo 20,000 za mbegu bora za korosho na miche 500,000 iliyozalishwa kwa kushirikiana na sekta binafsi. Aidha, itaratibu usindikaji wa tani 50,000 za korosho. Bodi itaendelea na utangazaji wa korosho ya Tanzania nje ya nchi kama vile Afrika ya Kusini, Misri na Namibia.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mkonge katika msimu wa 2008/2009 unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 33,000 mwaka 2007/2008 hadi tani 40,000. Ongezeko hilo litatokana na kuanza kuvunwa kwa mkonge uliopandwa mwaka 2004/2005 katika mashamba yaliyofufuliwa na katika maeneo ya Mikoa ya Kanda ya Ziwa. Bodi ya Mkonge itahamasisha kilimo cha mkonge, hususan kwa wakulima wadogo. Aidha, Bodi itaratibu ukamilishaji wa kazi za kuunganisha umeme unaozalishwa kwa kutumia mtambo wa *bio-gas* katika gridi ya Taifa. Vilevile, itakamilisha uandaaji wa mitambo ya kuzalisha bidhaa nyingine zinazotokana na zao la mkonge, hususan karatasi, *bio-ethanol* , *inulin* na kemikali za viwandani.

Mheshimiwa Spika, Chai. Uzalishaji wa zao la chai katika mwaka 2008/2009 unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 34,165 mwaka 2007/2008 hadi tani 37,000. Kiwango hicho cha uzalishaji kitatokana na kuanza uzalishaji kutoka mashamba yaliyofanyiwa ukarabati na kuzibwa mapengo kuanzia mwaka 2003/2004 hadi 2005/2006, hususan katika Wilaya za Njombe, Mufindi, Korogwe, Lushoto, Kagera na Tukuyu. Pia ukarabati wa barabara katika baadhi ya maeneo ya chai utasaidia kuokoa chai ambayo inaharibika bila kufikishwa viwandani.

Aidha, wakulima wataendelea kuhamasishwa kutumia pembejeo katika uzalishaji wa chai na kuzingatia kanuni za kilimo bora. Wizara kupitia Bodi ya Chai na Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai itaratibu uzalishaji wa miche bora milioni 10 ya chai na kuisambaza kwa wakulima. Vilevile Bodi itawasajili wakulima wa chai, itakagua viwanda vya kukaushia chai na viwanda vya kutengeneza majani ya chai. Lengo ni kuhakikisha, chai ya Tanzania inakuwa na ubora wa kuiwezesha kushindana kwa ufanisi katika soko la ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Kahawa. Uzalishaji wa zao la kahawa katika mwaka 2008/2009 unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 41,764 mwaka 2007/2008 hadi tani 50,000. Kiwango hicho cha uzalishaji kitafikiwa kutokana na kuingia mzunguko wa juu wa uzalishaji wa mmea wa kahawa. Aidha, Wizara kupitia Bodi ya Kahawa na *TaCRI* itaratibu uzalishaji wa miche bora milioni 10 ya kahawa na kuisambaza kwa wakulima. Sehemu kubwa ya miche hiyo itazalishwa chini ya utaratibu wa ruzuku. Wizara itawahamasisha wakulima kujiunga katika vikundi na vyama vya Ushirika ili iwe rahisi kuwapelekea teknolojia za kilimo bora na taarifa za masoko ya kahawa kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mchango wa mazao ya bustani katika kuongeza pato la ndani na nje ya nchi, katika mwaka 2008/2009, Wizara itatoa mafunzo kwa wataalam kuhusu uzalishaji bora wa mazao ya bustani hususan matunda, vikolezo, mboga na maua kulingana na mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi. Bustani za serikali zitaendelea kutunza nasaba na kuzalisha vipando bora vya mazao ya bustani kwa ajili ya wakulima. Wizara itahimiza uwekaji kipaumbele katika Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya, *Districts Agricultural Development Plans-DADPs,* uzalishaji wa mazao ya bustani kulingana na uwezo wa kiekolojia, *agro-ecological potentiality*, katika maeneo husika. Aidha, sekta binafsi itahamasishwa kuwekeza katika viwanda vya kusindika mazao ya bustani ili kuyaongezea thamani na kuwa na uhakika wa soko.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara itaendelea na uandaaji wa mwongozo wa kilimo cha mazao nishati. Aidha, Wizara itafanya uchambuzi na kuainisha maeneo yanayofaa kwa ajili ya kilimo cha mazao nishati kwa ajili ya wawekezaji wanaotaka kulima mazao hayo. Maeneo yote yanayofaa kwa kilimo cha mazao ya chakula hayatatumika kuzalisha mazao nishati.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara itaendelea kuhimiza utaratibu wa kilimo cha mkataba kwa mazao yanayozalishwa nchini kwa lengo la kumhakikishia mkulima soko la mazao yake na pia kukidhi mahitaji ya ubora wa mazao katika soko. Aidha, Wizara itatoa mafunzo kwa wataalamu juu ya manufaa ya kilimo cha mkataba katika maeneo yanayofuata utaratibu wa kilimo hicho.

Mheshimiwa Spika, Usalama wa Chakula na Hifadhi ya Mazao. Katika mwaka 2008/2009, Wizara itaendeleza mpango wa kuzijengea uwezo Halmashauri za Wilaya wa kuibua miradi inayolenga kutatua matatizo ya upungufu wa chakula kupitia *DADPs* kwa kutoa mafunzo kwa timu za wawezeshaji wa Halmashauri za Wilaya. Mafunzo hayo yatahusu masuala mchanganyiko ya Usalama wa Chakula, matumizi ya teknolojia za *Geographical Information System, GIS, Geographical Positioning System, GPS*, ukusanyaji wa takwimu na taarifa za mvua na hali ya mazao mashambani, teknolojia za usindikaji wa mazao ya nafaka, mikunde, mizizi na matumizi ya teknolojia za kuhifadhia mazao ya chakula.

Mheshimiwa Spika, Wizara itafanya tafiti maalum zitakazochangia kuongeza uwezo wa kubuni mikakati ya kuboresha usalama wa chakula, hususan mikakati wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwenye usalama wa chakula. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha uwezo wake katika kuratibu hali ya uzalishaji wa mazao

ya chakula nchini. Wizara pia itaendelea kufanya savei mbalimbali za utabiri wa uzalishaji wa mazao ya chakula ili kubaini hali ya chakula nchini na hatua za kuchukuliwa. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na wadau itafanya tathmini za kina katika maeneo yatakayobainika kuwa na upungufu wa chakula na kuishauri serikali kuchukua hatua zinazostahili kwa kuzingatia maslahi ya wazalishaji na walaji.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Chakula. Katika mwaka 2008/2009, *NFRA* imepanga kununua tani 100,000 za mahindi na tani 5,000 za mtama zenye thamani ya Shilingi bilioni 31.0. Kiasi hicho cha nafaka kinakusudiwa kununuliwa kutoka hapa nchini. Kazi zingine zitakazotekelezwa na *NFRA* ni pamoja na ununuzi wa magunia, maturubai, dawa za kuhifadhia nafaka na ukarabati wa maghala. *NFRA* pia itahamisha nafaka kutoka kanda zake zenye ziada na kuzipeleka kwenye kanda zenye upungufu.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kuratibu utekelezaji wa Programu ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika. Katika mwaka 2008/2009, Wizara itaratibu uimarishaji wa vyama vya ushirika wa pamba, korosho na tumbaku kwa kuvijengea uwezo kiutawala na kuwahudumia wanachama katika kuwapatia masoko ya uhakika ya mazao, hususan kupitia utaratibu wa stakabadhi za mazao ghalani na kuwawezesha kupata pembejeo za uzalishaji. Aidha, Wizara itasambaza miongozo ya uendeshaji wa Vyama vya Ushirika ili itumike kuweka mifumo na taratibu makini za uongozi na uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, Wizara itasimamia utekelezaji wa sheria ya ushirika ili kulinda maslahi na haki ya wanaushirika nchini. Ili kutekeleza hilo, itaimarisha uwezo wake wa ukaguzi wa Vyama vya Ushirika kuanzia ngazi ya kitaifa yaani Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania na *SCCULT* na muungano wa vyama vikuu na vyama vya ushirika vya msingi. Aidha, Wizara itatoa mafunzo kwa viongozi na watendaji ili kuimarisha uendeshaji wa Vyama husika na uwajibikaji; kutoa mafunzo na vitendea kazi kwa maafisa ushirika wa mikoa na wilaya; kuunganisha Vyama vya Ushirika vilivyodhaifu kiuchumi kwa lengo la kupata Vyama imara kiuchumi vinavyoweza kutoa huduma bora kwa wanachama wake na kuviwezesha Vyama vya Ushirika kupata mikopo ya benki ili kuboresha na kuimarisha utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara itakamilisha maandalizi ya Sera ya Kilimo na itaendelea kuandaa na kufanya mapitio ya sheria na kanuni za sekta ya kilimo ili kuhakikisha zinakidhi mahitaji ya sasa au malengo ya kutungwa kwa sheria na kanuni hizo. Aidha, Wizara itaandaa mwongozo wa utekelezaji wa sera ya kilimo ambao utajumuisha majukumu ya kila mtekelezaji. Vilevile, Wizara itakamilisha mchakato wa kuandaa muswada wa sheria ya kutambua, kuweka mipaka na kulinda ardhi ya kilimo kwa kuzingatia mahitaji ya sasa na ya baadaye. Sheria hiyo itahusisha pia kuratibu na kusimamia kilimo cha mkataba, *contract farming*, huduma za Ugani, *extension services*, na kilimo cha umwagiliaji. Aidha, Wizara itafanya marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo, *Agricultural Inputs Trust Fund*, ya mwaka 1994 kwa madhumuni ya kuimarisha utendaji wa Mfuko katika kusimamia utaratibu wa utoaji wa mikopo kwa ajili ya pembejeo na Hati ya Makubaliano Rasmi, *Memorandum of*

Undersatnding – MoU, kati ya Serikali na Vituo binafsi vya utafiti kwa lengo la kulinda maslahi ya taifa katika shughuli za utafiti na matumizi ya matokeo ya utafiti.

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya Rasilimali Watu. Katika mwaka 2008/2009, Wizara itaajiri watumishi 105 ili kuongeza nguvu kazi katika utoaji wa huduma na kupandisha vyeo watumishi 313 katika madaraja mbalimbali. Aidha, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa watumishi kuhusu mbinu za kujikinga na maambukizi ya *UKIMWI*, kupima virusi vya *UKIMWI* na kutathmini hali ya *UKIMWI* katika Wizara na Taasisi zake ili kutoa elimu juu ya utayarishaji na usindikaji wa vyakula vyenye virutubisho kwa wanaoishi na virusi vya *UKIMWI*. Vilevile, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa wataalam wa Halmashauri na wakulima kuhusu utayarishaji na matumizi ya mazao ambayo yana virutubisho muhimu katika kusaidia kuongeza kinga ya mwili katika kupambana na *UKIMWI*. Mafunzo kuhusu namna ya kuzingatia sera ya jinsia katika upangaji na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kilimo pia yatatolewa kwa watumishi 50. Wizara itaendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti Rushwa pamoja na Mpango Mahsusi wa kisekta, *National Anti-Corruption Strategy and Action Plan – NACSAP,* wa 2006 – 2010.

Mheshimiwa Spika, Wizara itatekeleza Programu ya Kuboresha Utumishi wa Umma, Awamu ya Pili, *Public Sector Reform Program* II *-PSRP II,* ambayo inalenga kuboresha utendaji kazi wa wizara kwa kuanzisha mfumo wa Serikali Mtandao, *e-Government,* ili kuimarisha na kurahisisha utoaji wa huduma na uwazi kwa wadau mbalimbali wa wizara. Aidha, wizara itapanua mtandao, *Local Area Network-LAN*, kwa kuunganisha kanda tatu za utafiti kwenye mtandao wa Wizara, *LAN/WAN,* ili kuwasiliana na watumishi walio nje ya makao makuu ya wizara kwa lengo la kuboresha mawasiliano na utendaji. Vilevile, mtandao utakaowaunganisha watumishi ndani, *intranet*, ya Wizara bila kuingiliwa na watumiaji wa nje utawekwa. Mtandao huo utasaidia kuboresha utawala na ubadilishanaji wa habari ndani ya Wizara ili kuongeza utoaji wa maamuzi ya haraka, hivyo kuongeza ufanisi; kuboresha mfumo wa kumbukumbu za kiutumishi na kiutendaji ambazo zitasaidia upatikanaji haraka wa taarifa ili kupunguza malalamiko kutoka kwa wateja.

Aidha, Wizara itatoa mafunzo ya Mfumo wa Wazi wa Kupima Utendaji kazi, *Open Performance Review and Appraisal System – OPRAS,* kwa watumishi wa wizara ambao hawakupata mafunzo hayo katika kipindi kilichopita. Wizara pia itahimiza watumishi kuzingatia maadili ya utumishi katika utoaji huduma kwa umma na itapitia upya na kuzindua Mkataba wa Huduma kwa Mteja ili kwenda na mabadiliko yaliyotokea ya muundo wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, Shukrani. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, hususan Kamati ya Bunge ya Kilimo Mifugo na Maji ikiongozwa na Mheshimiwa Gideon A. Cheyo, Mbunge wa Ileje iliyochambua makadirio ya matumizi ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika kwa kina na kutoa mapendekezo ambayo yamesaidia katika kuboresha mapendekezo ya Mpango wa mwaka 2008/2009. Mchango wao utaendelea kuwa sehemu muhimu katika kuendeleza sekta ya kilimo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kuzishukuru Nchi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa ambayo yamesaidia sana Wizara katika juhudi za kuendeleza Kilimo. Kwanza napenda kuzishukuru nchi za China, Denmark, Finland, India, Ireland, Israel, Indonesia, Japan, Korea ya Kusini, Marekani, Misri, Ubelgiji, Uholanzi, Ujerumani, Uswisi, Norway na Sweden.

Nayashukuru pia Mashirika na Taasisi za Kimataifa zifuatazo: Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, *IFAD, DFID, UNDP, FAO, JICA, EU, UNICEF, WFP, CIMMTY, ICRISAT, ASARECA, USAID, ICRAF, IITA, CFC, WVRDC, AGRA,* R*ockefeller Foundation* na *Bill and Melinda Gates Foundation*. Ushirikiano na misaada ya Nchi na Mashirika hayo bado tunauhitaji ili tuweze kuendeleza kilimo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za pekee, kwa wakulima wa nchi hii kwa kazi kubwa wanayofanya katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara pamoja na mazingira magumu waliyo nayo.

Napenda kumshukuru Naibu Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi; Katibu Mkuu Bw. Peniel M. Lyimo; Naibu Katibu Mkuu Bibi Sophia Kaduma; Wakurugenzi, Taasisi na Asasi zilizo chini ya Wizara; watumishi wote na wadau mbalimbali wa sekta ya kilimo kwa juhudi, ushirikiano na ushauri uliowezesha kutekelezeka kwa majukumu ya Wizara bila kukwama. Mwisho natoa shukrani kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kufanikisha kuchapishwa kwa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, Hitimisho. Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo na Programu Kabambe ya Modenaizesheni na Mageuzi ya Ushirika zinatekeleza Ilani ya *CCM* kwa ajili ya Uchaguzi wa mwaka 2005 na Sera ya Serikali ya kupeleka madaraka kwa wananchi ili washiriki kikamilifu katika kuainisha matatizo yanayowakabili, kupanga mipango ya kukabiliana nayo, kushiriki katika utekelezaji wa mipango hiyo na kufanya tathmini ya utekelezaji wa mipango hiyo. Aidha, Wizara kupitia Mpango wa mwaka 2008/2009 itatekeleza malengo ya *MKUKUTA* yafuatayo:-

(i) Kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula kutoka tani milioni 9.0 mwaka 2003/2004 hadi kufikia tani milioni 12 mwaka 2010/2011.

(ii) Kudhibiti mmomonyoko wa udongo na upotevu wa bioanuwai ya kilimo.

(iii) Kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sekta ya kilimo ni mtambuka, ni matumani yangu kuwa wote tutashirikiana katika kuyapatia ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, Maombi ya fedha kwa Mwaka wa 2008/2009. Naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 113,737,050,400 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika kwa mwaka 2008/2009. Kati ya fedha hizo,

Shilingi 93,704,218,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi 20,032,832,400 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Katika fedha hizo, Shilingi 2,516,709,000 ni fedha za ndani na Shilingi 17,516,123,400 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Asante sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. Kwa kweli hotuba hii inavutia sana ina mambo meengi yanayoshiria matumaini makubwa kwa wakulima wa nchi yetu. Tunakushukuru sana. Sasa nimuite Mhehimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, kwa niaba yake, Mheshimiwa Saidi Nkumba. *(Makofi)*

MHE. SAID J. NKUMBA K. N. Y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 99 (7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, kwa niaba ya Mwenyekiti wa kamati, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilikutana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwenye Ofisi ndogo ya Bunge ya Dar es Salaam, tarehe 3 - 4 Juni, 2008. Katika Kikao hicho Kamati ilipata maelezo ya kina kutoka kwa Wizara kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2008/2009 ambayo yamezingatia Dira ya Taifa ya 2025, Ilani ya Uchaguzi ya *CCM* ya mwaka 2005, Mwelekeo na Majukumu ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa 2007/2008. Wakati wa kujadili bajeti ya mwaka wa 2007/2008, Kamati yangu ilitoa mapendekezo kadhaa na nafurahi kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba yote yalifanyiwa kazi kwa kiasi cha kuridhisha. Naipongeza Wizara kwa utekelezaji huo mzuri. Baadhi ya maeneo yaliyofanyiwa kazi ni pamoja na:-

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa Mradi wa Maji wa Kituo cha Utafiti na Chuo cha Kilimo cha Ukiliguru ulikuwa haujakamilika. Kamati yangu inaihimiza Wizara isimamie utekelezaji wa mradi huu kwa umakini zaidi kwa kutambua ukweli kwamba taasisi hizi muhimu zimekuwa bila maji kwa miaka 31 tangu mwaka wa 1977 jambo ambalo linaathiri sana maisha ya wakazi wa maeneo ya taasisi hizo na utendaji wao wa kazi. Tunashauri kwamba ujenzi wa mradi huo wa maji ukamilike kabla ya mwisho wa mwezi wa Agosti 2008 kama Waziri alivyoahidi.

Mheshimiwa Spika, kasi ndogo ya uibuaji wa miradi ya maendeleo inatokana na upungufu wa watumishi wenye sifa. Kamati ilishauri msukumo uongezwe katika suala la uibuaji wa miradi ya maendeleo kwa kuongeza watumishi. Wizara imelifanyia kazi kwa

kuendelea kutoa mafunzo kwa wawezeshaji ngazi ya wilaya juu ya kuibua na kupanga mipango bora yenye kuleta matokeo yatakayowezesha vijiji na vikundi vya wakulima kujitosheleza kwa chakula na kupunguza umaskini. Aidha, viongozi wa wilaya wanashauriwa wawahamasishe wananchi waone umuhimu wa kuibua mipango bora ya kilimo ili iwawezeshe kuinua uchumi na kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilishauri Wizara ihamasishe wananchi, hususan wakulima, kuhusu umuhimu wa kilimo hai. Wizara imetekeleza hilo kwa kushirikiana na Mashirika yasiyo ya kiserikali hasa katika kilimo cha mbogamboga na cha mazao ya chai na kahawa kwa lengo la kupata bei nzuri kutoka nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kituo cha Utafiti cha Naliendele ni kituo muhimu sana cha utafiti katika mikoa inayolima korosho, ufuta, mahindi na mazao mengine yanayolimwa katika ukanda huo, Kamati ilishauri kituo hicho kiendelezwe ili kukiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Aidha, Wizara iangalie uwezekano wa kuanzisha vituo vidogo karibu zaidi na wakulima. Wizara imeona umuhimu wa suala hilo na mpaka sasa Kituo hicho ni moja ya vituo vya Wizara vilivyoimarika kwa maana ya kuwa na watumishi wenye ujuzi na uzoefu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilishauri Wizara iendelee kufuatilia taarifa za hali ya chakula nchini ili nchi isikumbwe na uhaba wa chakula. Wizara ilitoa taarifa kwamba ina utaratibu wa kufanya tathmini ya hali ya chakula kila mwaka ili kubaini maeneo na kaya zenye upungufu wa chakula na kuchukua hatua za kuhakikisha chakula kinapatikana.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2007/2008, Wizara ilifanikiwa kutekeleza kazi ilizojipangia. Baadhi ya kazi zilizotekelezwa ni kama zifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2007/2008, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika iliendelea kutekeleza Malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya *CCM* ya mwaka 2005, Dira ya Taifa ya 2025, Malengo ya *MKUKUTA* na Malengo ya Milenia kwa kupitia utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(ASDP).* Jumla ya shilingi bilioni 58 zilitengwa kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo. Sehemu kubwa ya programu hiyo inatekelezwa katika ngazi za Wilaya na vijiji kupitia mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo, Mbolea. Mahitaji ya mbolea kwa mwaka wa 2007/2008 yalikuwa tani 385,000. Hadi Mei, 2008 tani 211.013 sawa na asilimia 54.8 zilikuwa zimepatikana. Bei za mbolea kwenye soko la dunia zimepanda sana na pia kuna upungufu mkubwa wa mbolea katika soko hilo. Jambo hilo linasababisha kukosa mbolea ya kutosha ndani ya nchi. Ili taifa lijihakikishie upatikanaji wa mbolea, itabidi Serikali iongeze juhudi za kuharakisha ujenzi wa viwanda vya mbolea nchini.

Mheshimiwa Spika, kumekuwapo malalamiko mengi kutoka kwa wakulima kwamba mbolea ya ruzuku haiwafikii. Ni dhahiri kwamba kuwapo kwa mbolea yenye

punguzo la bei kutokana na kupewa ruzuku sambamba na mbolea inayouzwa kwa bei ya soko kunawafanya wafanyabiashara wapate mwanya wa kuuza mbolea nyingi kwa bei ya soko ambayo ina maslahi makubwa kwao. Wizara ilieleza kwamba inatambua matatizo yaliyopo na imebuni mbinu za kuyashughulikia.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya Mbegu bora katika mwaka wa 2007/2008 yalikuwa tani 30,000. Hata hivyo, upatikanaji wa Mbegu bora katika mwaka huo ulifikia tani 16,390, sawa na asilimia 54.6 ya mahitaji. Ili kilimo kiwe cha ufanisi na cha kumsaidia mtanzania suala la upatikanaji wa mbegu bora ni lazima liwe moja ya vipaumbele vya Taifa. Hivyo, Serikali ni lazima ijipange vyema kufanikisha suala hilo.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Bodi za Korosho na Pamba ilitoa ruzuku ya madawa yanayohusika na mazao yanayosimamiwa na Bodi hizo. Jumla ya tani 3,222.2 na lita 133,462.5 zilisambazwa kwa mpango wa ruzuku. Kati ya kiasi hicho, lita 50,000 na tani 1,100 za madawa ya korosho zilitokana na shilingi bilioni 1.0 zilizotolewa na Serikali na kiasi kilichobakia fedha zake zilitokana na ushuru wa mazao. Vilevile, Serikali ilitoa jumla ya shilingi bilioni 1.4 kwa ajili ya kuagiza *acrepacks* 500,000 za viuatilifu vya zao la pamba. Hadi tarehe 21 Aprili, 2008 *acrepacks* 420,000 zilipokelewa kati ya kiasi kilichoagizwa chini ya utaratibu wa ruzuku. Kati ya hizo *acrepacks* 200,000 zimesambazwa kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2007/2008, Mfuko wa Taifa wa Pembejeo ulitengewa jumla ya shilingi bilioni 3.5 kwa ajili ya kutoa mikopo ya kununulia na kusambaza pembejeo na zana bora za kilimo. Aidha, Mfuko ulikusanya madeni ya miaka ya nyuma yenye thamani ya shilingi bilioni 2.058. Marejesho hayo ni sawa na asilimia 70 ya madeni ikilinganishwa na asilimia 64 ya msimu uliopita. Jumla ya fedha zote zilizotolewa mikopo kwa mwaka wa 2007/2008 ni shilingi bilioni 4.180. Mfuko uliendelea kutoa mikopo kutokana na kiasi kidogo cha fedha kilichokuwepo.

Mheshimiwa Spika, huduma za ugani ni muhimu sana katika jitihada za kuboresha kilimo. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI inatekeleza mpango wa kuboresha huduma za ugani ambapo jumla ya Wataalam wa ugani 2500 wataajiriwa kila mwaka kwa kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka wa 2007/2008. Hadi kufikia Machi 2008 Wataalam wa ugani walioajiriwa na Halmashauri walikuwa 309 tu. Lengo halikufikiwa kutokana na uhaba wa wataalam wenye sifa zinazotakiwa hasa maafisa kilimo wasaidizi na maafisa kilimo daraja la pili. Kamati inakubaliana na uamuzi wa Wizara wa kuwapeleka vyuoni vijana waliomaliza kidato cha nne ili kufikia lengo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2007/2008 upatikanaji wa chakula kutokana na uzalishaji wa 2006/2007 ulifikia tani milioni 10.6, tani milioni 5.4 za nafaka na tani milioni 5.2 za mazao mengine, zikilinganishwa na mahitaji ya chakula ya tani milioni 10.0. Taifa lilijitosheleza kwa asilimia 106. Hata hivyo kulikuwapo maeneo yaliyokuwa na upungufu wa chakula katika mikoa ya Arusha, Manyara, Shinyanga, Kilimanjaro, Singida, Morogoro na Mwanza. Serikali ilitenga tani 9,427 za chakula kwa

ajili ya kuuzwa kwa shilingi 50/= tu kwa kilo kwa wananchi waliokabiliwa na upungufu wa chakula.

Aidha, kutokana na kupanda ghafla kwa bei za vyakula kuanzia mwezi wa Novemba 2007 kulikotokana na mvua za vuli kunyesha kwa viwango vya chini na mtawanyiko mbaya katika baadhi ya maeneo, Serikali ilitenga tani 36,660 za mahindi kutoka kwenye *SGR* ili ziuzwe kibiashara kwa wananchi wa mikoa iliyokabiliwa na upungufu wa chakula ili kupunguza kasi ya kupanda kwa bei. Kamati yangu inaipongeza Serikali kwa hatua ilizochukua za kuhakikisha kwamba wananchi waliopata matatizo ya uzalishaji wa chakula walipata chakula kwa bei wanazozimudu.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilifanya utafiti katika Mikoa ya Iringa, Kagera, Kilimanjaro, Mbeya, Shinyanga na Singida kubaini sababu za baadhi ya maeneo kuwa na upungufu wa chakula mara kwa mara. Taarifa za tafiti hizo zitasaidia katika kuandaa mkakati wa kukabiliana na hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2007/2008, shughuli za utafiti wa mazao ya kilimo ziliendelea katika Kanda zote saba 7 za utafiti wa kilimo zenye jumla ya vituo 17 ambapo aina 7 za mbegu kutoka vituo hivyo zimeidhinishwa kitaifa kwa matumizi ya wakulima. Kamati imebaini kwamba chini ya Mpango wa Maboresho ya Sekta ya Kilimo, zilianzishwa taasisi tatu za kilimo: *Tanzania Tea Reseach Insitute, TRITI*, Tanzania *Coffee Research institute, TaCRI,* na *Tobacco Research Institute of Tanzania, TORITA.* Taasisi hizi zilianzishwa chini ya Sheria ya Makampuni, *Cap.212* ambayo haifafanui masuala muhimu yanayohusiana na utafiti, ugharamiaji wake, miliki na matumizi ya matokeo ya utafiti na uhusiano kati ya taasisi za utafiti na wadau wengine.

TRITI na *TaCRI* zimeendelea kufanya kazi nzuri kwa kuwa zilikuwa na utaratibu mzuri wa kuzigharamia. *TORITA* haikuwa na utaratibu kama huo na imekuwa ikisuasua kama vilivyo vituo vya utafiti wa kilimo. Hali ilivyo sasa, taasisi hizi zinaweza kuuza matokeo ya tafiti zake bila kizuizi chochote, ilimradi Bodi za Wakurugenzi ziruhusu. Haja ipo ya kuboresha usimamizi na uendeshaji wa Taasisi hizo za utafiti.

Mheshimiwa Spika, Udhibiti wa Visumbufu vya Mimea. katika kipindi cha 2007/2008, Wizara kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa na Wakulima, iliendelea kupambana na milipuko ya visumbufu mbalimbali vya mimea na mazao ikiwa ni pamoja na milipuko ya ndege waharibifu aina ya kwelea kwelea, nzige, viwavijeshi, panya na magonjwa mbalimbali ya mimea ambayo husababisha upotevu wa mazao kati ya asilimia 30 na 40. Aidha, Wizara iliendelea kuhamasisha wakulima kudhibiti visumbufu vya mimea kwa kutumia njia ya udhibiti husishi, *IPM* na kufanya ukaguzi wa mazao yanayoingia nchini na yanayotoka nje ya nchi, kudhibiti uingizaji holela wa madawa ya Kilimo na pia kuendelea na juhudi za kudhibiti magugu maji katika ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2007/2008 Serikali iliviondolea baadhi ya Vyama vya Ushirika madeni na kuanzisha utaratibu wa stakabadhi ghalani ambao umewezesha wakulima wa korosho kuuza korosho zao zote na kwa bei nzuri. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hizo. Kutokana na mafanikio yaliyopatikana,

tunapendekeza utaratibu huo wa kufuta madeni ya vyama vya ushirika uendelezwe sambamba na utaratibu wa stakabadhi ghalani kwa mazao mengine likiwamo zao la tumbaku. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua inazochukua za kuanzisha Benki ya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Bajeti ya 2007/2008, Kilimo kimeendelea kukabiliwa na changamoto zifuatazo ambazo zinathiri utekelezaji:-

(a) Ufinyu wa bajeti ya kilimo unazorotesha ukuaji wa kilimo kwa kiwango kinachotakiwa. Kwa mfano bajeti inayotengwa haifikii kiwango cha asilimia 10 kilichokubaliwa na nchi za *SADC* na malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005;

(b) Kutokuwepo kwa utaratibu maalum wa kuwapatia wakulima mikopo ya kuendeleza kilimo;

(c) Kutokupatikana kwa pembejeo za kutosha zikiwemo mbolea, mbegu bora, madawa na zana za kilimo;

(d) Miundombinu mibovu, hasa barabara za vijijini inaathiri usambazaji wa pembejeo, usafirishaji wa mazao kwenda kwenye masoko na kusababisha gharama za usafirishaji kuwa kubwa;

(e) Kutokuwepo kwa Maafisa Ugani wa kutosha katika ngazi za Wilaya, Kata na Vijiji kunasababisha wakulima kutopata ushauri wa mbinu bora za kilimo na kuwepo kwa uwezo mdogo wa kuibua miradi ya kilimo, jambo linalosababisha wananchi kutokuwa na ujuzi wa kutosha wa kilimo bora na kushindwa kutumia fursa zilizopo;

(f) Udogo wa maeneo yanayolimwa kwa kutumia zana duni;

(g) Viongozi .na watendaji wa ngazi zote kutohimiza kilimo kama ilivyokuwa enzi za Siasa ni Kilimo na Kilimo cha Kufa na Kupona;

(h) Serikali za Mitaa kutokutekeleza kikamilifu majukumu yao ya kisheria ya kuhimiza na kuendeleza kilimo;

(i) Mfumo hafifu wa uratibu na mawasiliano miongoni mwa ngazi mbalimbali zinazohusiana na usimamizi wa kilimo unasababisha matatizo katika utekelezaji; na

(j) Shuguli za Utafiti.

- Fedha kidogo zinazotengwa haziwezeshi shughuli za utafiti kufanywa kwa viwango vya kuridhisha;

- Watumishi wa utafiti kutopewa maslahi na motisha za kuridhisha jambo linalosababisha wengi kukimbilia nchi za nje ambako wanalipwa vizuri; na

- Matokeo ya utafiti kutowafikia walengwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009, Wizara imepanga kutekeleza mambo mengi, baadhi yake ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(ASDP)*. Wizara itaendelea kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha timu za uwezeshaji za Wilaya na Kata, kwa kuzifundisha mbinu za kuandaa michanganuo ya miradi ili kufanikisha utekelezaji wa programu hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2008/2009, Wizara inaomba jumla shilingi bilioni 31.8 kwa ajili ya ruzuku ya pembejeo, shilingi bilioni 23.8 kwa ajili ya mbolea na kiasi kilichobaki kwa ajili ya mbegu bora na madawa ya Korosho na Pamba.

Jumla ya tani 60,000 ya mbolea ya Minjingu ya punje itasambazwa kwa ruzuku. Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi wa kununua na kusambaza mbolea yote itakayozalishwa na Kiwanda cha Minjingu ili itumike kama mbolea ya kupandia badala ya *DAP* ambayo bei yake iko juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Taifa wa Pembejeo, kwa mwaka wa 2008/2009 umepanga kutumia jumla ya shilingi bilioni 7.16 zikijumuisha shilingi bilioni 2.16 zilizotengwa kwenye bajeti ya 2008/2009 na shilingi bilioni 5.0 zinazotegemewa kurejeshwa kutoka kwa waliokopeshwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2008/2009 Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kutekeleza mpango wa kuimarisha huduma za ugani kwa wakulima. Wizara inakusudia kuongeza jitihada za upatikanaji wa Wataalam wa kilimo ngazi ya Wilaya, Tarafa na vijiji. Aidha, wanafunzi waliomaliza kidato cha nne watapatiwa mafunzo kutokana na kukosekana kwa vijana waliomaliza kidato cha sita wa kutosha. Wizara itaendelea kueneza Mbinu Shirikishi jamii katika kilimo ikiwa ni pamoja na Matumizi ya vikundi vya wakulima na dhana ya Shamba Darasa ambayo imeonyesha mafanikio kwa wakulima.

Katika msimu wa 2008/2009 Wizara, kupitia Bodi za Mazao mbalimbali, itaendelea kusimamia uzalishaji na ubora wa mazao yanayozalishwa nchini ili yawe na sifa zitakazoyawezesha kuuzwa kwa bei nzuri katika soko la ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za ushirika nchini kwa kuwahamasisha wananchi kujiunga na vyama ya ushirika na kuviimarisha vyama vilivyopo kupitia utekelezaji wa programu kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika kwa kushirikisha wadau wote. Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI, itaendelea kutoa mafunzo na kuongeza ajira ya Maafisa Ushirika katika ngazi ya Wilaya na vyama vya ushirika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza kwa ufupi utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa 2007/2008 na Matarajio kwa mwaka wa 2008/2009, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kilimo kiweze kukua kwa kiwango kinachotakiwa, kukiwezesha kupunguza umaskini, kupata chakula cha kutosha na kuchangia katika ukuaji wa uchumi, Kamati inaishauri Serikali kuongeza bajeti ya Kilimo ili ifikie kiwango kilichokubaliwa na nchi za *SADC* sambamba na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005 ya asilimia kumi (10%) ya Bajeti ya Serikali. Aidha, bajeti hiyo isimamiwe vizuri katika ngazi zote kuanzia ngazi ya Taifa hadi ngazi ya kijiji ili itumike kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imezuia uuzaji au upelekaji chakula nje ya nchi kwa tahadhari ya njaa, basi iwajibike kununua chakula cha ziada kutoka kwa wakulima. Aidha, Serikali iwajibike kununua chakula hicho kwa bei ya soko ili mkulima afaidike na mazao yake na ikitokea kwamba Serikali imeagiza chakula toka nje ambacho kitasababisha kushuka kwa bei ya mazao ya mkulima wa ndani ya nchi Serikali iwajibike kufidia tofauti ya bei. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikishia upatikanaji wa chakula cha kutosha, Kamati inaishauri Serikali ichukue hatua ambazo zitahakikisha kwamba wananchi wanazalisha mazao yanayostawi kwenye maeneo yao kwa viwango vikubwa vya kuwawezesha kujitosheleza kwa chakula. Hasa tukiangalia kwamba katika ulimwengu kwa sasa kuna tatizo la upungufu wa uzalishaji wa chakula hasa nafaka kunakotokana na wakulima wakubwa kuzalisha mazao ya nafaka kwa ajili ya nishati.

Aidha, kutumia sehemu ya mashamba yao kwa kilimo cha kuzalisha mafuta kama Mibono na mengine. Serikali itoe mwongozo na kusimamia kilimo cha mazao ya kuzalisha mafuta ili kusiwe na athari kwa kilimo cha mazao ya chakula.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kazi nzuri inayofanywa na Mfuko wa Pembejeo kwa kutoa mikopo ya pembejeo na zana za kilimo. Aidha, Kamati inapendekeza Mfuko wa Pembejeo upatiwe fungu maalum kutoka Hazina na upatiwe fedha zinazolingana na mahitaji ya Mfuko ili uweze kutoa mikopo kwa Watanzania walio wengi. Serikali iangalie uwezekano wa kupitisha sehemu za fedha za Mfuko wa Uwezeshaji kwenye Mfuko wa pembejeo ili ziwafikie wakulima walio wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili taifa lijihakikishie upatikanaji wa mbolea, Serikali ni lazima iongeze juhudi za kuharakisha ujenzi wa viwanda vya mbolea nchini. Mungu

ameijalia nchii hii kuwa na *deposit* (amana) za *phosphate* zilizoko Minjingu, Mpanda na Mshewe, Mbeya na kadhalika. Aidha, tuna gesi asilia ambayo inaweza kutumika kuzalisha mbolea za *nitrogen*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo malalamiko mengi kutoka kwa wakulima kwamba mbolea ya ruzuku haiwafikii, Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Serikali ifanye tathmini ya kina kuona utoaji wa ruzuku ya mbolea na pembejeo nyingine za kilimo umekuwa na manufaa gani, hasa ikizingatiwa kwamba kwa miaka minne iliyopita kilimo kimekua kwa kasi ndogo ya asilimia nne (4) tu.

(ii) Serikali iangalie upya utaratibu wa kutoa ruzuku ya pembejeo na kuona kama taasisi za pembejeo na za fedha zilizopo zingeweza kuchukua jukumu hilo kwa kuwa Wizara haina muundo wala utaalamu wa kuiwezesha kufanya kazi hiyo kwa ufanisi. Kamati imeshuhudia uzinduzi wa utoaji ruzuku kwa njia ya vocha hivi majuzi, Wizara isimamie vizuri utaratibu huu na tathmini ifanyike baada ya kipindi muafaka kupima mafanikio.

(iii) Serikali iangalie uwezekano wa kupanua utaratibu wa kutoa ruzuku ili ujumuishe zana za kilimo, kama majembe ya kukokotwa na wanyama, matrekta ya ukubwa mbalimbali na kadhalika, kwa lengo la kuongeza kasi ya matumizi ya zana hizo katika kilimo na katika maeneo mengi.

(iv) Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa mbegu bora za mazao bado ni tatizo kwani asilimia 70 ya kiasi cha mbegu bora hasa za mahindi chotara zinaagizwa kutoka nje ya nchi. Kamati inashauri Wizara itilie mkazo uzalishaji wa mbegu bora hapa nchini na kuzisambaza kwa wakulima.

(v) Mheshimiwa Spika, huduma za ugani ni muhimu sana katika sekta ya Kilimo. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ambazo imeanza kuzichukua za kuajiri Wataalam wa ugani ambao watakidhi mahitaji ya wakulima hususan katika ngazi ya Wilaya, Tarafa na vijijini. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuongeza Idadi ya watalaam wa ugani, pamoja na vitendea kazi ili sekta ya Kilimo iweze kuzalisha mazao yatakayotosheleza kwa chakula na biashara.

(vi) Mheshimiwa Spika, ili kuendelea kupata tekinolojia sahihi zinazokidhi mahitaji ya kilimo na kuhakikisha kwamba matokeo ya utafiti yanawafikia wakulima, Kamati inaishauri Serikali iendelee kuongeza bajeti ya vituo vya utafiti ili kukidhi mahitaji ya kazi zao.

Aidha, vituo vipatiwe vifaa vya usafiri vya kutosha yakiwemo magari na pikipiki. Pia Serikali iandae utaratibu shirikishi na endelevu wa kufikisha matokeo ya utafiti mbalimbali kwa walengwa, na tathmini zifanyike kupima manufaa ya tafiti zinazofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kuna umuhimu wa kutungwa kwa sheria itakayosimamia shughuli zote za utafiti wa kilimo nchini na ambayo itafafanua masuala yote muhimu yanayohusika, ikiwa ni pamoja na kutambuliwa kwa Serikali kuwa ndiyo mmiliki wa vituo vyote vya utafiti na matokeo ya tafiti zinazofanywa kwenye vituo hivi. Wizara iangalie kama kuna haja ya kuwa na sheria maalum ya *TPRI* au itatosha kuwa na sheria moja ambayo itajumuisha *TPRI*.

(vii) Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za ushirika nchini kwa kuwahamasisha wananchi kujiunga na vyama vya ushirika na kuviimarisha vilivyopo. Kamati inaishauri Serikali iendelee kufuatilia shughuli za vyama vya ushirika ikiwa ni pamoja na:-

(a) Kuviwezesha vyama vya ushirika kupata mikopo ya Benki ili kuboresha na kuimarisha utekelezaji wa majukumu yao.

(b) Kuendelea kuajiri wataalam wa ushirika katika ngazi za Wilaya na vyama vikuu ili kuongeza ufanisi.

(c) Kamati inaipongeza Serikali kwa kuviondelea vyama vya ushirika vya Korosho na Pamba madeni. Aidha, Kamati inapendekeza kwamba Serikali iendelee kuviondolea madeni vyama vya ushirika vilivyobaki ikiwemo vyama vya ushirika vya tumbaku.

(viii) Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri ni vizuri tuzalishe mazao kama Mahindi, Mpunga, Muhogo, Ngano sio tu kwa kujitosheleza mahitaji yetu bali pia kuwa wauzaji wakubwa kwenye Soko la Duniani, kwani kuna kila dalili za mahitaji ya mazao haya kuongezeka na bei yake kupanda.

Mheshimiwa Spika, mazao kama Alizeti, Mawese, Ufuta, Nazi, Karanga na Pamba licha ya kwamba yanakwenda sambamba na mazao ya chakula lakini vilevile hutumika viwandani. Kamati inashauri nchi izalishe mazao ya aina hii kwani soko lake linapanuka haraka na ni rahisi kuyazalisha kwani mengi yanavumilia ukame.

Mheshimiwa Spika, Mazao ya Singa na bidhaa nyingine (Pamba, Mkonge). Singa asilia zinatumika kwa bidhaa nyingi na matumizi yake sasa yanakua haraka kwenye soko. Ndio maana hata Umoja wa Mataifa umetangaza rasmi kuwa mwaka 2009 ni mwaka wa Singa Asilia (*2009 United Nations International Year Of Natural Fibres*). Mazao haya yanatoa singa na bidhaa nyingine kama mafuta na mashudu kutoka kwenye pamba; nishati, mbolea na dawa kutoka kwenye mkonge ambao unavumilia sana ukame na hauna magonjwa. Mazao haya yanaweza kutoa ajira kwa watu wengi kwani uzoefu unaonekana wa miaka mingi, linalohitajika sasa ni kuongeza tija maradufu.

Mheshimiwa Spika, Matunda, mazao kama embe, ndizi, mananasi, karakara (*passion fruit*) na viungo kama hiliki yanaweza kuzalishwa na kuuzwa kwa wingi kwani masoko yake yanakua haraka ulimwenguni. Zao kama embe, tunayo nafasi kubwa ya kuziba pengo la soko la dunia kwani wakati wazalishaji wakubwa hawana embe, Tanzania ndio tuko kwenye msimu hivyo kutufungulia soko kubwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeeleza kwamba kupitia bodi mbalimbali za mazao itaendelea kusimamia ubora wa mazao yanayozalishwa nchini ili yawe na ubora wa hali ya juu na yatakayoweza kuuzwa kwa bei nzuri katika soko la ndani na nje ya nchi. Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada inazochukua. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuongeza uzalishaji wa mazao ya Biashara kwa kufanya mambo yafuatayo:-

- Kutoa elimu kwa wakulima waweze kujua umuhimu wa kutunza mazao vizuri Mashambani na kuyapanga katika madaraja wakati wa kuuza.

- Kuimarisha huduma za ukaguzi wa mazao.

- Kuhakikisha Mazao yanauzwa katika vituo vilivyoidhinishwa na kuhimiza usindikaji wa mazao ya biashara.

- Kupunguza au kuondoa ushuru wa mazao.

- Kuongeza ruzuku kwa Bodi za Mazao ili kuongeza nguvu na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake. Bodi za mazao ziimarishwe ili kuchochea uzalishaji zaidi.

Mheshimiwa Spika, kutokuwapo kwa vyombo vya fedha vya kumpatia mkulima mikopo ya kumuwezesha mkulima kumudu gharama za kilimo kunasababisha ashindwe kupata mazao ya kutosha kwa eneo analolima, Kamati inaishauri Serikali iwawezeshe wakulima kimtaji kwa kuanzisha Benki ya wakulima yenye masharti nafuu na itakayotoa mkopo wa muda mrefu. Aidha, Kamati inashauri *SACCOS* ziimarishwe ili zitoe mikopo kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mazao Mchanganyiko. Ni muda mrefu sasa umepita tangu mpango wa kuanzishwa Bodi ya Mazao Mchanganyiko utolewe. Kamati inashauri, Serikali iharakishe kutoa Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo ambayo itasaidia kuundwa kwa Bodi ya Mazao Mchanganyiko ambayo itakuwa mkombozi kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutoa elimu kwa watumishi kuhusu mbinu mbalimbali za kujikinga na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI**.** Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kupitia Tume ya Taifa ya kudhibiti UKIMWI *(TACAIDS)* kwa hatua mbalimbali inazochukua kukabiliana na janga hili. Hatua hizo ni pamoja na:-

- Kuwapatia huduma ya chakula na virutubisho walioathirika ili kuimarisha kinga za mwili.

- Kueneza utaalam na maarifa ya kumsaidia muathirika na wanao wahudumia wagonjwa.

- Kuimarisha utafiti wa Mbegu na mimea yenye kuongeza virutubisho kwa wagonjwa wa UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika inaomba jumla ya Sh. 113,737,050,400/= kati ya hizo Sh. 93,704,218,000/= ni kwa matumizi ya kawaida na shilingi 20,023,832,400/= ni kwa Mipango ya Maendeleo. Kiasi kinachoombwa ni pungufu kwa asilimia 14 kuliko kiasi cha Sh. 131,912,102,600/= kilichotengwa mwaka wa 2007/2008. Upungufu huu unatokana na shughuli za umwagiliaji kuhamishiwa Wizara ya Maji na Umwagiliaji na fedha za *DASIP* na *PADEP* kupelekwa moja kwa moja kwenye Serikali za Mitaa zinazotekeleza mipango hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuwatambua Waheshimiwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ambao wamechambua na kutoa maoni, ushauri na mapendekezo kuhusu Bajeti ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika.

Wajumbe hao ni Mhe Gideon A. Cheyo – Mwenyekiti, Mheshimiwa Kidawa H. Saleh - M/Mwenyekiti, Mheshimiwa Kheri K. Ameir, Mheshimiwa Teddy L. Kasella – Bantu, Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa Salim H. Khamis, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa Joyce N. Machimu, Mheshimiwa Fred T. Mpendazoe,

Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, Mheshimiwa Juma S. Omary, Mheshimiwa Shally J. Raymond, Mheshimiwa Mwanakhamis K. Said, Mheshimiwa Salum K. Salum, Mheshimiwa Abdulkarim E. Shah, Mheshimiwa Kaika S. Telele na Mheshimiwa Said J. Nkumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, napenda kutumia nafasi hii kuwapongeza Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Steven M. Wasira (Mb), Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Mathayo David Mathayo (Mb) kwa ushirikianao wao mzuri. Pia nawapongeza wataalamu wote wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu ndugu, Peniel Lyimo na Naibu Katibu Mkuu Sofia Kaduma kwa jinsi walivyoweza kufafanua hoja mbalimbali zilizotolewa na Kamati wakati wa kuchambua Bajeti hii. *(Makofi)*

Aidha, natoa shukrani kwa Wajumbe wote wa Kamati hii kwa michango yao na ushirikiano mkubwa walioutoa chini ya Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Gideon A. Cheyo, Mbunge wa Ileje na Makamu Mwenyekiti - MheshimiwaKidawa H. Saleh katika kufanikisha kazi hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi pamoja na Ofisi yako hasa Kaimu Katibu wa Bunge ndugu Thomas D. Kashililah na Makatibu wa Kamati hii Ndugu Frank K. Mbumi na Pamela E. Pallangyo kwa kuratibu taarifa hii. *(Makofi)*

Aidha, napenda niwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Sikonge kwa kuniunga mkono katika shughuli zangu za kutekeleza kazi zangu za Ubunge na ninawaahidi kwamba sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lao Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka wa 2008/2009, jumla ya Sh. 113,737,050,400/=.

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kutamka kuwa naunga mkono hoja ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Said Nkumba kwa kuwasilisha maoni ya Kamati, sasa ni zamu ya Msemaji wa Sekta hii ya Kilimo kutoka Kambi ya Upinzani, ni mwenyewe Waziri Kivuli Mheshimiwa Salim Hemed Khamis.

MHESHIMIWA SALIM HEME KHAMIS - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA KILIMO,CHAKULA NA USHIRIKA:

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama leo hii kwa ajili ya kuwasilisha mawazo ya Kambi ya Upinzani katika Wizara hii ya kilimo chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Spika, pili, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani napenda kukushukuru wewe binafsi na Naibu wako kwa kunipa fursa ya kuweza kuwasilisha mawazo ya

upinzani Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2008/09 Kwa mujibu wa la kanuni za Bunge, kanuni ya 99(7) toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru viongozi wangu wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mheshimiwa Dr. Wilbord Slaa kwa kunipa ushirikiano mkubwa mwanzo hadi mwisho wa maandalizi ya hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mkosefu wa fadhila ikiwa sitowashukuru wanachama wa chama changu cha Wananchi- *CUF* hasa wa jimbo langu la Chambani ambao kwa msaada wa Mwenyezi Mungu na kura zao ndio sababu ya mimi kuwepo hapa leo. Nawaahidi nitakuwa nao na nitasimama kidete katika kutetea haki zao. Pia na mwisho lakini si kwa umuhimu namshukuru Naibu Waziri Kivuli kwa wizara hii Mheshimiwa Juma Said Omar, mbunge wa Jimbo la Mtambwe kwa ushirikiano mkubwa alionipa katika maandalizi ya hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, wote tunafahamu kuwa kilimo ndio sekta mama nchini kwani ndiyo sekta inayotegemewa na watanzania zaidi ya asilimia 65% kwa kipato chao na karibu watanzania milioni 40 kwa kuendeleza maisha yao ya kila siku. Sekta hii ni miongoni mwa sekta muhimu zenye kutoa mchango mkubwa katika jitihada za kunyanyua uchumi wa nchi yetu na imeendelea kuwa sekta muhimu inayochangia kwa kiasi kikubwa katika pato la taifa. Hivyo kuwa na umuhimu mkubwa katika juhudi zetu za kuondoa umaskini, kukuza uchumi na kuongeza ajira.

Mheshimiwa Spika, licha ya umuhimu wa sekta hii kwa wananchi na taifa kwa ujumla, bado ukuaji wake haufanani na mahitaji yake kwa jamii. Kwa mujibu wa Ripoti ya Umasikini na Maendeleo ya Binadamu nchini ya 2007, takwimu zinaonyesha kuwa kati ya mwaka 2000 na 2006 kulikuwa na ukuaji wa sekta ya kilimo kwa asilimia 4.7%. Wakati ripoti ya Hali ya Uchumi wa Taifa katika mwaka 2007 inaonyesha kuwa katika mwaka 2000 sekta ya kilimo kwa maana ya mazao ilikuwa kwa asilimia 4.7%, mwaka 2004 asilimia 6.6% na mwaka 2007 ilikuwa kwa asilimia 4.5%. Hii inaonyesha ukuaji wa sekta hii nyeti umedumaa na pia kushuka kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Spika, katika hali ya ongezeko la idadi ya watu la zaidi ya asilimia 3%, ukuaji wa sekta ya kilimo kwa asilimia 4.7% ni hatari kubwa kwa taifa. Ukitilia maanani kuwa sekta hii ni muhimu kama chanzo cha kujitosheleza kwa chakula na wakati huohuo kusaidia ukuaji wa kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, takwimu za zamani zilionyesha kuwa mwaka 2004 Sekta ya Kilimo iliweza kuchangia Pato la Taifa kwa 46.2% wakati mwaka 2005 ilichangia kwa asilimia 46.1%. Hata hivyo, kwa mujibu wa Ripoti ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2007, takwimu zinaonyesha kuwa kwa kutumia kizio cha mwaka 2001**,** katika mwaka huo huo wa 2004 sekta ya kilimo kwa maana ya mazao imechangia asilimia 22.4% tu na huku mchango wa sekta hii kwa mwaka 2007 ni 19.0% tu.

Mheshimiwa Spika**,** katika nchi kama yetu ambayo Watanzania walio wengi bado wanategemea sekta ya kilimo katika kujiendeleza kimaisha, udumavu huu wa ukuwaji na uchangiaji wake katika pato la Taifa ni hatari kwa usalama wa nchi. Tukumbuke kuwa katika dunia yetu hii ya sasa, suala la kilimo na chakula sio suala la ustawi wa wananchi kijamii na kiuchumi tu, bali pia ni suala la kiusalama. Vilevile kwa hali kama hii ni wazi Tanzania haitaweza kufanikiwa kufikia malengo ya MKUKUTA ya kuwa na kilimo endelevu kinachokua asilimia 8 – 10 na kuwezesha kufikia ukuaji wa uchumi wa asilimi 6 - 8 ifikapo mwaka 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, udumavu huu wa ukuaji wa sekta ya kilimo unaonyesha wazi kuwa kamwe serikali ya awamu ya nne ambayo ilingia madarakani kwa Ilani ya uchaguzi iliyowaahidi Watanzania kuwa kilimo kitakuwa kwa asilimia 20, haitaweza kufikia lengo hilo ifikapo mwaka 2010. Ni wazi ilani hii ilikuwa ama ya kilaghai ama ya kusadikika kwani wachumi waliobobea wanadai ukuaji wa kasi ya aina hii haujawahi kutokea kwa nchi yeyote duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa linalodumaza kilimo chetu ni pamoja na bajeti ndogo ya Serikali katika kilimo. Leo hii, badala ya kuongeza fedha za bajeti katika Wizara ya Kilimo, Serikali imepunguza kutoka bajeti ya Sh.131,912,102,600/= 2007/2008 hadi Sh.113,737,050,400/= mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, japokuwa Serikali imetoa sababu za upungufu huo, lakini Kambi ya Upinzani haikubaliani na sababu hizo kwa msingi kuwa, bajeti ya umwagiliaji maji iliyopelekwa kwenye Wizara ya Maji na umwagiliaji kwa mwaka 2008/2009 ni Sh. 13,185,574,000/=, Fedha hizi zikijumlishwa na za bajeti ya Wizara ya Kilimo ya mwaka huu zinakuwa Sh. 126,922,624,400/=.

Hata hivyo bado bajeti ya mwaka huu ni pungufu kwa Sh. 4,989,478,200/= sawa na 3.78% kulinganisha na bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuwa wakati duniani kote wenzetu wanajipanga kupambana na tishio la upungufu wa chakula sisi ndio kwanza tunapunguza bajeti ya Wizara ya kilimo. Hii sio tu inatuingiza katika hatari ya janga kubwa la njaa lakini pia inatulazimu kuendelea na tabia ya kuombaomba chakula ambacho tulipaswa kukizalisha sisi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani kwa kuona umuhimu wa sekta hii katika kuongeza ajira, Pato la Taifa na kuweza kuyalinda maisha ya watu ambayo yanaweza kupotea wakati wowote kutokana na uhaba wa chakula, tulipendekeza kiasi cha shilingi bilioni *959.2* ikiwa ni mara saba na nusu (7.5) ya bajeti ya Wizara ya kilimo ya Serikali kwa mwaka huu wa 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, katika Ilani ya CCM Ibara ya 31(l) inatamka bayana kuwa, nanukuu: “CCM inazitaka Serikali kuhakikisha kuwa sekta ya kilimo inatengewa si chini ya asilimia 10 ya uwekezaji unaofanywa na Serikali, sambamba na lengo la Jumuiya ya maendeleo ya nchi za kusini mwa Afrika *(SADC)”*. Mwisho wa kunukuu. Kambi ya Upinzani inajiuliza hivi Serikali hii inafuata na kutekeleza sera na ilani za nani? Serikali hii ya CCM haijui kuwa ilani ya uchaguzi ni ahadi takatifu kwa wananchi na ni lazima kuheshimiwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilimo cha Watanzania kinafanywa na wakulima wadogo wadogo ambao mashamba yao ni madogo sana kati ya hekta 0.5 na 2.5 lakini hadi sasa suala la kuwasaidia kikamilifu wakulima hawa limekuwa ni la hadithi za Alfu Lela Ulela. Inashangaza kuwa Serikali ya nchi iliyomasikinishwa kama Tanzania, inadharau udogo wa mashamba ya Watanzania, wakati inajulikana wazi kuwa suala sio udogo au ukubwa wa eneo la kulima, bali ni tija inayopatikana kwa maeneo hayo *(production per area or productivity).*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inatambua na kuthamini mchango wa wakulima wadogo wadogo kuwa ndio injini ya kilimo hapa nchini na ndio wanaolisha Watanzania takriban millioni 40.

Mheshimiwa Spika, katika nchi za mashariki ya mbali, mfano; China, Taiwan,Vietnam na nyingize, wakulima wadogo wadogo wenye wastani wa mashamba chini ya hekta moja ndio wazalishaji na wasafirishaji wa chakula cha nafaka inayotumika duniani kote. Wakulima hawa wamejengewa mazingira mazuri na serikali zao kwa kuweza kupata mbolea, utaalamu wa kilimo, mbegu bora, miundombinu ya umwagiliaji maji na barabara bora za vijijini zinazosaidia kufikia masoko.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapaswa kutambua kuwa ukuwaji wa haraka wa idadi ya watu unaweza kuchochea uzalishaji kwa kutanua soko kwa ajili ya bidhaa na huduma, kutengeneza nafasi za uwekezaji wa uzalishaji na pia inachochea uwekaji wa akiba.

Mheshimiwa Spika, na sisi watanzania tukiwa makini katika mipango yetu inawezekana siku moja tukafika huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sekta ya kilimo ni moja ya sekta yenye miradi mingi sana ambayo inatokana ama kwa ufadhili ama mikopo kutoka kwa mataifa na asasi mbalimbali duniani. Hata hivyo, kama ilivyo katika miradi mingi ya nchi hii, suala la ushiriki ama ushirikishwaji wa wanajamii katika kupanga, kutekeleza na kusimamia miradi hii halijatiliwa mkazo ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali inapenda kudai kuwa inajenga utamaduni wa kuwashirikisha wananchi katika miradi kadhaa inayotekelezwa hivi sasa chini ya wizara ya kilimo kama vile mradi wa *ASDP* kwa njia ya *D by D (Decentralization By Devolution).* Tafiti mbalimbali za asasi za kiraia zinaonyesha kuwa utaratibu huu umeelelezwa hadi ngazi ya Halmashauri za Wilaya tu. Haujavuka kwenda katika ngazi ya

Kata, Vijiji, Vitongoji hadi kwenye Mitaa. Matokeo yake hali hii inatengeneza mazingira ya ufisadi miongoni mwa watendaji wanaokabidhiwa majukumu ya uratibu na usimamizi na vilevile kukosekana kwa mwamko wa kutosha miongoni kwa upande wa walengwa ili kujihusisha vyema katika miradi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika nchi ya Malawi, kwa mfano, wameweza kupata mafanikio makubwa ya kilimo yanayochangiwa kwa kiasi kikubwa na ushirikishwaji wa moja kwa moja wa jamii. Ni muhimu kwa Wizara kufahamu na kuheshimu falsafa ya kuwa hakuna maendeleo bila ya jamii kupewa kipaumbele *(Community Base).*

Mheshimiwa Spika**,** Mfuko wa Pembejeo *(Agricultural inputs trust fund - AGITF)* ulianzishwa rasmi kwa sheria ya Bunge mwaka 1994 na kuanza kazi rasmi mwaka 1995 ukiwa na jukumu kuagiza na kusambaza pembejeo za kilimo kwa wakulima.

Sambamba na hilo, mfuko unajishughulisha na kutoa mikopo ya kusambaza pembejeo kupitia kwa mawakala wa pembejeo, wakulima binafsi, vyama vya wakulima na kuanzisha vituo vya kukodisha matrekta.

Mheshimiwa Spika, toka kuanzishwa kwake mwaka 1995 hadi mwaka jana (2007), taarifa zinaonyesha kuwa Mfuko wa Pembejeo ulikuwa umetoa mikopo ya jumla shilingi billioni 18.5 na kukusanya asilimia 46 ya fedha hizo, ambazo ni sawa na shillingi bilioni 8.5 tu.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa shughuli za mfuko huu umekumbwa na majanga mbalimbali ya uzembe na ufisadi. Moja ya janga lililoukumba mfuko huu ni lile la kufaidisha watu wasio walengwa ambao kuna tetesi kuwa wengi wao ni watu wenye nafasi kubwa katika chama na Serikali. Taarifa zinaonyesha kuwa wengi wao waliweka dhamana hewa ya mikopo hiyo na kuilaghai Serikali.

Mheshimiwa Spika, janga lingine ni lile la mfuko huu kutowasaidia sana wakulima wadogo wadogo walio wengi na wenye uhitaji mkubwa wa mbolea za ruzuku. Kwa kiasi kikubwa wakulima waliofaidika na mfuko huu ni wale wakubwa na mawakala wa kilimo *(rural agro dealers/stockist)* wakiwaacha wakulima walio wengi kununua pembejeo hizo za ruzuku kwa bei ya soko au zaidi ya hapo. Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri kulieleza Bunge lako Tukufu:

(a) Ni hatua gani zimechukuliwa kwa wakopaji ambao hadi sasa wanadaiwa kiasi cha Shilingi billioni 10?

(b) Ni hatua zipi zimechukuliwa kwa wale waliotumia vifaa hivi kwa udanganyifu na wala trekta hazikununuliwa na/au hazikukarabatiwa.

(c) Kambi ya Upinzani inataka taarifa ya kina itolewe katika Bunge lako Tukufu ili Waheshimiwa Wabunge katika Majimbo yao waweze kuthibitisha kama kweli matrekta hayo yapo.

Mheshimiwa Spika, kila mwaka Serikali hutenga kasma kwa ajili ya mfuko wa pembejeo ili kutoa mikopo ya kununulia na kusambaza pembejeo na zana za kilimo. Pamoja na kwamba Serikali imejitoa katika kuhudumia mfuko wa pembejeo mwaka huu na kuiachia sekta binafsi lakini imetenga shilingi billioni 7.16 kwa bajeti hii ya 2008/2009. Kati ya fedha hizo shilingi billioni 5 ni zile zinazotegemewa kurejeshwa toka kwa waliokopeshwa miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo la kubahatisha, kwani wadeni hao wanaweza kushindwa kulipa madeni yao kama ambavyo imejitokeza katika miaka iliyopita. Ikiwa hilo litajitokeza tena, basi mfuko huo hautokuwepo. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza itatumia kasma gani kufidia fedha za mfuko wa pembejeo kwani dhana ya wakopaji wengi hapa nchini ni kuwa fedha za Serikali ni fedha za bure. Kama wanavyoamini katika fedha za mfuko wa JK. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matumizi ya mawakala wa kilimo *(rural agro-dealers)* ambao wengi inasemekana wengi wao ni watu wenye maslahi Serikalini na pia katika sekta ya kilimo imesababisha tatizo kubwa la ulanguzi wa mbolea ya ruzuku na kuifanya kuuzwa kwa bei kubwa sana. Taarifa zinaonyesha kuwa katika mkoa wa Iringa, kwa mfano, mbolea ya ruzuku inauzwa kati ya Sh. 70,000/= hadi Sh. 90,000/= kwa mfuko wa kilo hamsini (50) badala ya bei halali ya Serikali ya Sh. 23,000/=. Kambi ya Upinzani inaitaka Waziri itueleze ni kwanini Serikali inashindwa kuthibiti bei ya mbolea ya ruzuku na kuwafanya wakulima washindwe kuinunua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imebahatika kuwa na eneo kubwa na la kutosha kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji la zaidi ya hekta milioni 29.4, kati ya hizo hekta milioni 2.3 zinauwezo mkubwa wa kuendelezwa na hekta milioni 4.8 zina uwezo wa wastani na hekta milioni 22.3 zina uwezo mdogo wa kuendelezwa. Hadi sasa eneo lililoendelezwa kwa umwagiliaji ni hekta milioni 0.29 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania haina uhaba wa maji. Kati ya eneo lote la Tanzania lenye ukubwa wa hekta millioni 94.5, hekta milioni 5.5 zimefunikwa na maji ya mito na maziwa. Tanzania ina ziwa la pili kwa ukubwa duniani la Victoria, ziwa lenye kina kirefu kuliko yote duniani la Tanganyika na vilevile mito mikubwa kama Malagalasi, Rufiji, Ruvu, Kilombero, Kagera, Ruvuma, Pangani, Wami na kadhalika inayofaa kabisa kwa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, tunapenda kumkumbusha Mheshimiwa Waziri kuwa alitoa ahadi hapa Bungeni katika bajeti ya mwaka 2006/2007 kuendeleza hekta milioni moja kwa kipindi cha miaka mitano (2006/2007 - 2009/2010). Lakini kwa masikitiko makubwa, mpaka sasa eneo la umwagiliaji ni hekta 275,388 tu, ambalo ni kiasi cha asilimia 27.5 tu ya lengo hilo na imebakia miaka miwili tu kufikia 2010. Je, itawezekana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Morogoro peke yake una mito ipatayo 176 isiyokauka mwaka mzima, kama vile Mto Kilombero, Ruaha Kuu, Kihansi, Mpanga, Mgeta na kadhalika. Mkoa wa Mbeya umebahatika pia kuwa na jumla ya hekta 82,000 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji lakini cha kushangaza ni kwamba kiasi cha hekta 17,000 tu ambazo ni sawa na asilimia 20.7 ndizo zinazotumika kwa kilimo hicho.

Vile vile jumla ya eneo lote la Mkoa huu linaloweza kutumika kwa kilimo ni hekta milioni 5.7 lakini eneo linalolimwa ni hekta 712,558 tu ambalo ni sawa na asilimia 12.5. Hii yote inatokea wakati Mikoa hii yenye vyanzo vingi vya maji vinavyoweza kutumika kwa kilimo cha umwagiliaji havitumiki.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya yote hayo, Mikoa hii miwili iliyobarikiwa na raslimali zote hizo, ni miongoni mwa Mikoa iliyokuwemo katika orodha ya Mikoa iliyokumbwa na njaa katika mwaka 2007/2008**.** Kambi ya Upinzani inaiuliza Serikali kuwa itawezaje kuleta mapinduzi ya kijani ikiwa kilimo cha umwagiliaji hakipewi nafasi inayostahili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Mpango Shirikishi wa Kilimo cha Umwagiliaji (*PIDP*), Serikali ilishauriwa na kukubali ushauri wa kuvuna maji ya mvua katika Mikoa yenye matatizo ya ukame ya Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga, Mwanza na Arusha. Hadi sasa bado utekelezaji wake haujaonekana na maji ya mvua yanaendelea kuachwa yapotee baharini.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo ni muhimu sana kwa ukuaji wa sekta hii ni upatikanaji wa Benki ya kilimo. Katika bajeti iliyopita ya Wizara hii Serikali iliahidi kubadilisha Benki ya Rasilimali *(TIB)* kuwa Benki ya Kilimo. Lakini hadi sasa maamuzi hayo bado hayajatekelezwa kwa madai kuwa Serikali haina mtaji wa kuanzisha benki hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapingana kabisa na dhana ya kubadilisha *TIB* kuwa Benki ya Kilimo na pia sababu ya kwamba Serikali haina fedha za mtaji wa kuanzisha Benki ya Kilimo. Tunaamini kuwa endapo Serikali ingetumia fedha

ilizotoa kwa Benki ya *Exim* na *CRDB* kwa ajili ya kuwakopesha wakulima kama mtaji wa kuanzisha Benki ya Kilimo ingewezekana, badala ya kuendelea kuzinufaisha benki hizo kibiashara ambazo kiukweli zinaendelea kukwepa jukumu la kuwasaidia wakulima wadogo.

Mheshimiwa Spika, pia tunashauri Serikali kutumia kiasi fulani cha ushuru wa mazao mbalimbali kama vile Pamba, Kahawa, Korosho, Miwa na kadhalika kuwa kama nyongeza ya mtaji kwa ajili ya uanzishwaji wa Benki ya Kilimo. Vilevile Serikali ingetumia kiasi cha shilingi bilioni 2.8 ilizozitoa mnamo Julai, 2003 kukopesha wakulima binafsi na kupitia Vyama vya Msingi vya Ushirika pamoja na *SACCOS* kuanzisha benki hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaamini ili kupiga hatua ya maendeleo ya kweli tunahitaji kufanya maamuzi magumu na kama kweli Serikali iko makini na tayari kuachana na utamaduni wa maneno tu, Tanzania inaweza kuwa miongoni mwa nchi bora katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo cha mazao mbalimbali. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ya mwaka 2007/2008 alisema kuwa, nanukuu "Hakuna njia ya mkato ya kuinua kipato cha wananchi walio wengi na kufikia azma ya maisha bora kwa kila Mtanzania bila ya kuleta mapinduzi katika kilimo". Suala la mapinduzi ya kilimo limekuwa kama kauli mbiu ya kudumu kwa Serikali tangu enzi za *TANU* hadi sasa. Lakini suala hili limebaki kuwa nadharia ya kuwapa Watanzania matumaini yanayoendelea kupotea bila ya utekelezaji wake kuonekana. Maana ya mapinduzi ni mabadiliko ya haraka yenye kuonyesha mafanikio yake kwa muda mfupi. Sasa sijui ndugu zetu hawa wanaongelea mapinduzi gani yasiyoonekana hata baada ya miaka 46 ya Uhuru na miaka 44 ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na uzalishaji usioridhisha kwa mazao ya kilimo mwaka hadi mwaka. Mfano, kwa mujibu wa ripoti ya Hali ya Uchumi wa Taifa katika Mwaka 2007, uzalishaji wa mazao mengi makuu umeshuka kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano sukari imeshuka kwa asilimia nne sawa na tani milioni 11.3; kahawa imeshuka kwa asilimia 25.08 sawa na tani milioni 11.82; pareto imeshuka kwa asilimia 51.6 sawa na tani milioni 1.046; mahindi yameshuka kwa asilimia 3.53 sawa na tani 121,000; ngano imeshuka kwa asilimia 24.2 sawa na tani 26,500; muhogo umeshuka kwa asilimia 15.57 sawa na tani 316,800 na ndizi zimeshuka kwa asilimia 12.16 sawa na tani 142,200.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kushuka huko kwa uzalishaji kwa zao moja moja, lakini kuna tatizo la msingi la kushuka kwa uzalishaji kwa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Kwa nini basi Serikali haitumii ipasavyo Vyuo vyetu vya Tafiti kama vile Mlingano-Tanga, Serian-Arusha na *SUA*-Morogoro kubaini aina na ukubwa wa tatizo kwa maeneo husika ili kuwanusuru wakulima na hasara wanayoipata mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumesema kuwa uzalishaji ni ule wenye tija na tija inatokana na huduma makini na sahihi ya utaalam wa kilimo. Katika kijitabu cha

mwelekeo wa utekezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa kipindi cha mwaka 2005-2010 kinasema uzalishaji wa pamba utapanda toka kilogram 100 kwa hekta hadi kilogram 1000.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Mikoa inayolima pamba inazalisha kilogram 250 kwa hekta, huu ni uzalishaji mdogo sana kwa kulinganisha na lengo la ilani ya CCM. Lakini licha ya uzalishaji huu mdogo bado wakulima hivi sasa wanakosa soko na bei ya uhakika. Kambi ya Upinzani inataka Serikali ilieleze Bunge lako Tukufu, ikiwa kwa uzalishaji huu mdogo wa pamba haina soko wala bei nzuri: Je, hali itakuwaje pale uzalishaji utakapofikia kilogram 1000 kwa hekta? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri Serikali kuacha mtindo wa kutenganisha mazao ya biashara na chakula kama ilivyoainishwa katika Sera ya Kilimo ya 1997. Tafiti zinaonyesha kuwa jambo hili ndilo linalowazidishia wakulima wetu kuzama kwenye lindi la umaskini. Kambi ya Upinzani inaamini kuwa kila zao ambalo linaweza kuingizwa sokoni na kuuzwa ni zao la biashara na linapaswa kupewa umuhimu ulio sawa na mazao mengine.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inakemea vikali tabia ya Viongozi wa Serikali kuingilia uhuru wa wakulima kuuza mazao yao yaitwayo ya chakula. Hili linapelekea wakulima hao kuuza mazao yao kwa bei ya chini ambayo inawaletea umaskini badala ya kuwakomboa kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vyombo vya habari vimetangaza hivi karibuni kuwa, Serikali inataka kuiuzia mahindi Kenya na kuna tetesi kuwa Wakenya hao hao wanauza mahindi yao sehemu nyingine. Kwa nini basi wafanyabiashara binafsi wakitaka kusafirisha mahindi yao Kenya wakamatwe na kushtakiwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaitaka Serikali iache mara moja mtindo huu wa kuwapangia wakulima jinsi ya kuuza mazao yao vinginevyo iwe tayari kuwalipa fidia kwa kiasi kile wanachoingia hasara kutokana na utekelezaji maamuzi hayo ya kisiasa.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua upungufu na kuongezeka kwa bei ya wa chakula duniani, Serikali inadai inaandaa mikakati ya kuongeza uzalishaji wa chakula. Mikakati hiyo ni ya muda mfupi na muda mrefu. Mfano, mikakati ya muda mfupi ni kama ifuatayo:-

(1) Kusitisha uuzaji wa mazao makuu ya chakula nje ya nchi;

(2) Kutoa msamaha wa kodi wa uingizaji mahindi kutoka nje ya nchi *(tax waiver*); na

(3) Kuhamasisha na kuhimiza matumizi mazuri ya chakula katika ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kuwa mikakati ya aina hii haikufanyiwa utafiti wa kutosha na kamwe haitoweza kuongeza uzalishaji wa chakula nchini. Inashangaza kuwa

wakati wenzetu wanajipanga kutumia vyema rasilimali walizonazo kuzalisha chakula, sisi tunajipanga kusamehe kodi za uagizaji wa mazao toka nje na kumzuia mkulima asiuze mazao yake nje kwa faida. Kinachotakiwa ni Serikali kujipanga Kimkoa na Kiwilaya kuzalisha chakula kwa wingi na kuwapunguzia wakulima mzigo wa kodi unaowaelemea wakulima wetu ambao wanalipa mara 17 (5% Vs 0.3%) zaidi ya kodi anayolipa mwenye kiwanda.

Mheshimiwa Spika, taarifa zinaonyesha kuwa kumekuwa na ongezeko la wawekezaji binafsi katika sekta ya kilimo kutoka 77 mwaka 2001 hadi 219 mwaka 2007, sawa na ongezeko la wastani la asilimia 7.9%. Kwa mwaka 2007 kilimo kilikuwa na miradi 27 yenye thamani ya dola za kimarekani milioni 142.45.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa Tanzania haina sera makini zenye vishawishi vya kuwavutia wawekezaji wakubwa kwenye kilimo, wala aina sera makini za matumizi bora ya ardhi. Huu ni udhaifu mkubwa kwa Serikali. Serikali inaandaa Sera wakati huu ambapo wawekezaji tayari wanaendela kuhodhi maeneo yenye rutuba kwa kilimo cha mazao ya chakula ili wazalishe mazao ya nishati mbadala.

Mheshimiwa Spika, katika suala la wawekezaji Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ihakikishe kunakuwepo na uhusiano wa moja kwa moja kati ya viwanda na kilimo *(foward and backward linkage)* ili wawekezaji wakubwa waweze kuvipatia viwanda vyetu vya ndani malighafi ili pasiwepo na haja kwa viwanda hivyo kuagiza malighafi toka nje ya nchi. Bidhaa za viwanda hivyo zitosheleze soko la ndani kwanza na ziada iuzwe nje.

Mheshimiwa Spika, mpango huu wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(ASDP)* ambao unapaswa kutekelezwa kwa miaka saba kuanzia mwaka 2006 hadi mwaka 2014 kwa kutumia jumla ya shilingi trilioni 2.5, una fedha nyingi sana ambazo kama tungekuwa makini zingeweza kabisa kuinua sekta ya kilimo kwa kiasi kikubwa kabisa.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Wizara inaonyesha kuwa kazi zitakazofanyika chini ya programu hii katika mwaka huu wa fedha ni pamoja na kuimarisha timu za wawezeshaji katika ngazi ya Taifa, Wilaya hadi Kata, kuendelea kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa *DADPS* katika ngazi za Wilaya na Vijiji, kuboresha utangazaji na uenezi wa matokeo ya kazi na *ASDP* na kuendelea kujenga uwezo wa watendaji katika ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inajiuliza kama kweli Serikali iko makini na kilimo badala ya kutumia programu hii kwa kuingiza nchini matrekta ya kutosha, mbolea na madawa, kuwapa maofisa ugani wachache tulionao vitendea kazi na motisha mbali mbali, tunatumia fedha nyingi za programu kwa watendaji katika semina, makongamano na warsha mambo ambayo hayaongezi tija ya moja kwa moja katika uzalishaji kwa mkulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inahoji pia ni kwa nini kiasi fulani cha fedha hizi kisitumike katika uanzishwaji wa Benki ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ilikuwa ni nchi ya mfano katika Vyama vya Ushirika. Wasomi wengi wamesomeshwa na Vyama vya Ushirika vya Mikoa yao. Swali la kujiuliza, kwa kiwango hicho kilichofikiwa ni kwa nini Ushirika ulikufa?

Mheshimiwa Spika, ushirika wa wakati huo haukuwa ni wa kununua mazao tu kama ilivyo hivi sasa, bali ulikuwa ni wa kumsaidia mkulima katika hatua zote za kuzalisha hadi kumtafutia soko kwa bei stahili.

Mheshimiwa Spika, ushirika uliopo sasa ni wa kibiashara mno badala ya kutoa huduma kwa mkulima, kwa sababu *SACCOS* ndizo zinazochukua nafasi ya Vyama vya Ushirika. *SACCOS* zimeanzishwa kwa misingi isiyo thabiti yenye utashi wa kutengeneza faida zaidi kuliko kutoa huduma. *SACCOS* zina mapungufu makubwa ya uongozi na utaalam katika kuziendesha. Misingi ya ushirika sio mikopo kama zinavyofanya *SACCOS* za leo kwa kuziendea taasisi kama *PRIDE, SELF* na BENKI bali msingi mkuu wa ushirika ni michango ya wanachama wake. Kambi ya Upinzani inaona kwa kuwa *SACCOS* msingi wao ni mikopo na kupata faida, mwisho wake utakuwa ni kuiingiza Serikali kwenye mtego wa kulipa madeni, kwani *SACCOS* hizo zitakufa kifo cha mende kutokana na kukosa misingi imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Maafisa Ushirika Wilayani ndio wasimamizi waelekezi wa *SACCOS*, lakini nao wanakumbwa na matatizo makubwa ya kutokuwa na fani ya ushirika pamoja na vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, jambo la kusikitisha ni kuwa hata vile Vyama vya Ushirika vilivyobaki kwa kusuasua bado vinakabiliwa na matatizo makubwa ya uongozi na ubadhirifu wa mali za ushirika.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu lilipitisha sheria ya kuundwa kwa chombo ambacho kitakuwa na mamlaka ya kukagua mahesabu ya Vyama vya Ushirika nacho ni *COASCO*. Jambo la kusikitisha ni kuwa Vyama vingi vya Ushirika havijakaguliwa kwa muda mrefu na *COASCO* ipo. Jambo la ajabu zaidi ni kuwa Vyama vya Ushirika vinapeleka vitabu vyao vya mahesabu *COASCO* badala ya *COASCO* kwenda vilipo Vyama vya Ushirika na kuona hali halisi na ikibidi kukutana na wanaushirika. Kambi ya Upinzani inauliza kwa utaratibu huu, ni kweli tutaweza kushinda ubadhirifu ndani ya Vyama vya Ushirika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitahadharisha Serikali kutorudia makosa yaliyosababisha Vyama imara vya Ushirika kufa kwa kuchanganya siasa na ushirika. Hivyo basi, ushirika uongozwe na katiba zilizounda ushirika huo na ziwe huru katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya mara kwa mara ya muundo wa Wizara inayohusika na Kilimo, Chakula na Ushirika yamekuwa yakileta mkanganyiko mkubwa wa kiutekelezaji na kifedha kwa watendaji wa sekta hii.

Mheshimiwa Spika, mkanganyiko huu wa mara kwa mara kwa sekta nyeti kama hii unatoa taswira mbaya. Serikali inashindwa kufanya maamuzi ya kitaalam kama vile muundo wa Serikali bila ya kutumia na kuthamini ushauri wa wataalam wetu, hali ambayo inapelekea kulingiza Taifa letu katika matumizi ya ziada ya kodi za Watanzania pasipo na ulazima na kusababisha mkanganyiko mkubwa wa kisera na kiutekelezaji miongoni mwa watendaji wetu, kiasi cha kuathiri utekelezaji wa mipango mingi ya kuendeleza sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukubwa wa nchi yetu na wingi wa asasi na miradi iliyo chini ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, tunashauri Serikali ichukue hatua za haraka za kuanzisha Mamlaka ya Maendeleo ya Kilimo nchini *(National Agriculture Development Authority-NADO)* ambayo itakuwa na majukumu ya kusimamia Bodi zote za Mazao mbalimbali, miradi yote ya kilimo na kuhakikisha utekelezaji wa mikakati na mipango yote ya kilimo nchini. Mamlaka hii ambayo inapaswa kuwa chini ya Wizara husika itakuwa ndio kiungo muhimu cha usimamizi wa utekelezaji wa mikakati, mipango na miradi yote ya kilimo nchini inayotekelezwa na ama ndani ya Wizara husika ama asasi na Bodi mbalimbali za mazao ya kilimo nchini.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sana kuanzisha mamlaka hii ili kuhakikisha nafasi ya wataalam wetu katika kuendeleza sekta hii nyeti na vilevile kupunguza mzigo mzito wa majukumu uliopo katika Wizara. Tukifanya hivi ni wazi tutakuwa tunatengeneza mazingira bora ya kuendesha kilimo chetu kitaalam zaidi na kupunguza athari za maamuzi ya kisiasa yanayoendelea kuidumaza sekta hii siku hadi siku.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kambi ya Upinzani inaamini wakati umefika wa kuwa na sheria maalum ya kilimo nchini ambayo itaweka wazi haki na wajibu wa wakulima kwa upande mmoja na Serikali na asasi nyingine kwa upande mwengine. Kama ilivyo katika sheria ya madini, ni muhimu kuwa na sheria hii ya kilimo ambayo itaonyesha wazi masuala ya kodi za shughuli za kilimo, masuala ya umiliki na mamlaka ya maamuzi ya uuzaji na matumizi ya mazao ya kilimo na vilevile kuonyesha wazi ni vipi Serikali inapaswa kuwezesha sekta hii kama ambavyo inafanya katika sekta za madini na ujasiriamali.

Mheshimiwa Spika, uwepo wa sheria ya kilimo utawezesha kuondoa matatizo mbalimbali yanayowakumba wakulima na sekta ya kilimo kwa ujumla. Vilevile sheria hii itaweza kubainisha nafasi ya mazao ya kilimo hasa yale ya chakula katika muktadha mzima wa maendeleo na usalama wa Taifa letu. Ni muhimu sana kuanzisha sheria hii ambayo itaondoa ukiritimba wa maamuzi na kuweka bayana mipaka ya mamlaka mbalimbali zinazohusika katika utekelezaji wa masuala mbalimbali ya kilimo. Sheria hii inapaswa kuweka wazi ushiriki wa Wizara mtambuka katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Msemaji wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Salim Hemed Khamis. Waheshimiwa Wabunge kwa hali ya kawaida sasa tungeeendelea na

mjadala kwa Wizara hii ya Kilimo lakini kama mnavyofahamu, asubuhi tumetengua Kanuni ya 69(1) ili kuahirisha huu mjadala na pia tumetengua kanuni ya 140(f) ili kuruhusu mgeni aingie ndani ya ukumbi. Kwa hiyo, kwa heshima na taadhima namwomba *Sergeant-at-arms* amlete mgeni wetu Dr. Asha-Rose Migiro, Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Nitawaomba anapoingia tumpe heshima kwa kusimama. *(Makofi)*

(Hapa Mheshimiwa Dr. Asha Rose Migiro aliingia Ukumbini)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hakutakuwa na maana yoyote kwangu kujaribu kuelezea mgeni tuliye naye ni nani. Ni Mtanzania maarufu, ameleta heshima kubwa kwa nchi yetu, tunajivunia na tumefurahi zaidi kwamba baada ya kufika huko kwenye kazi nzito aliyopewa amemudu vizuri sana na sasa umaarufu wake ni katika dunia nzima. Tunashukuru sana. *(Makofi)*

Kabla sijamwomba kuhutubia nilikuwa napenda kutambua uwepo wa watu mashuhuri katika maisha yake kama ifuatavyo, kwanza Profesa Cleofas Migiro ambaye ni mumewe, naomba asimame, ahsante sana Profesa, sina hakika kama Profesa amehamia *New York* lakini kama bado yupo hapa basi, loh! Ndiyo kazi tena hiyo. Yupo Bwana Oscar Fernandes, Mwakilishi Mkazi wa Umoja wa Mataifa hapa Tanzania *(UNDP). Welcome Mr. Fernandes, we are very happy to receive you in the House, of course is not your first time*. Wapo dada zake Dr. Migiro nao ni Amina na Farida Mtengeti, wale pale, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Yupo Msaidizi wa Dr. Asha-Rose Migiro ambaye ni Balozi Tuvalo Manongi, karibu sana Mheshimiwa Balozi, kazi yako ngumu, tulivyokutana *Cape Town* tuliona jinsi ambavyo unashughulika kupanga ratiba na kadhalika. Yupo Bi Enot Zabron, Mlinzi wake na Mlinzi wa pili au sijui wa kwanza lakini kwa sababu tunawatanguliza akinamama basi huyu wa pili, ni Bwana Mohammed Aidar. *(Makofi)*

Wengine ambao wamo katika msafara ambao wamejiunga kutoka hapa nchini ni Bi Shufaa Mahmoud, dada yake Dr. Asha Rose na huyu sijui ni Bi au Bibi Nimar Sitta, hana uhusiano wowote na Spika. Unajua hizi koo za kichifu ni pana, kwa hiyo, Bi Sitta yeye ni Mkuu wa Ofisi ya Kanda ya *World Food Programme* hapa Dodoma. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hayo, kwa heshima na taadhima, naomba sasa nimkaribishe Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro - Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa aweze kulihutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Karibu sana Mheshimiwa.

MHE. DR. ASHA-ROSE M. MIGIRO – NAIBU KATIBU MKUU WA UMOJA WA MATAIFA: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge wote, ninayo furaha kubwa na ya pekee kuwepo tena katika Bunge hili Tukufu. Nasimama mbele yenu kwa unyenyekevu mkubwa nikiwa nimevaa kofia mpya, kofia ya Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa lakini bado nikijivunia sana nchi yangu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitovu changu kimezikwa hapa, mizizi yangu imejikita katika nchi hii nzuri ambayo ndiyo imenifikisha hapa nilipo. Aidha, nadiriki kusema chimbuko la heshima hii, wadhifa huu nilioupata wa sasa ni Bunge hili Tukufu. Hivyo, naongea nanyi kama Mtanzania mwenzenu hata kama nitakuwa nikifanya hivyo kwa kutumia jicho la Umoja wa Mataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali kabisa napenda nitambue vilevile na nishukuru sana kwa mapokezi makubwa na mazuri ambayo sikuyatarajia lakini nimeyafurahia, nashukuru sana yanaonyesha udugu na mapenzi, nimepata makaribisho makubwa toka nimekuja kwa likizo fupi ya kikazi Dar es Salaam, leo hii hapa Dodoma na nilipoingia katika viwanja vya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa dhati kabisa, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa dhati kwa kunipa heshima ya pekee, kwa kunipa fursa hii adhimu ya

kulihutubia Bunge hili Tukufu kuhusu uhusiano wa karibu baina ya nchi yetu Tanzania na Umoja wa Mataifa pamoja na kuzungumzia mchango muhimu unaotolewa nanyi Waheshimiwa Wabunge kama wawakilishi wa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, heshima hii hivi sasa ni yangu binafsi lakini ni heshima pia kwa Umoja wa Mataifa. Ninaposimama hapa, naomba pia nilete salaam za Mheshimiwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa - Mheshimiwa Banki Mun. Kama yeye asingekubali kuwa *New York* katika kipindi hiki isingekuwa rahisi kwangu kuchukua likizo. Kwa hiyo, namshukuru yeye pia lakini naleta salaam zake kwenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tangu uhuru Umoja wa Mataifa umekuwa mshiriki mkubwa katika maendeleo ya Tanzania. Historia ya Tanzania inahusiana kwa karibu na misingi na maadili ya Umoja wa Mataifa. Msimamo wa Tanzania katika mshikamano, amani na usalama, haki za binadamu na maendeleo ni thabiti kabisa, haya ni maeneo makuu ya kazi za Umoja wa Mataifa. Naweza pia kuthibitisha kwa niaba ya familia ya Umoja wa Mataifa kuwa Tanzania imepiga hatua kubwa katika kuleta maendeleo kwa wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mazingira haya yaliyojengwa yanatoa fursa nzuri sana ya kuimarisha uhusiano baina ya Tanzania na Umoja wa Mataifa. Hivi sasa Umoja wa Mataifa umo katika mchakato muhimu wa kujitathmini ili kubaini namna ya kuhuisha jitihada zake za kuhamasisha maendeleo. Kwa upande wangu mbali na kupewa dhamana ya kuratibu shughuli za maendeleo mojawapo ya majukumu yangu kama Naibu Katibu Mkuu ni kusimamia jitihada za kuimarisha shughuli za Umoja wa Mataifa na kufuatilia utekelezaji wake katika nchi mbalimbali ikiwemo Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kwamba Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo zimepiga hatua kubwa kati ya nchi nane ambazo zinafanyiwa majaribio ya kuimarisha shughuli za Umoja wa Mataifa chini ya mpango maalum unaojulikana kama Program ya Umoja wa Mataifa ya kutoa huduma zake kama taasisi moja, yaani *delivering as one*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lengo la mchakato huu ni kuufanya Umoja wa Mataifa uimarishe huduma zake ili kusaidia juhudi za nchi wanachama katika kuondoa umaskini na kuleta maendeleo stahimilivu ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Azma ya mpango huu ni kuhakikisha kwamba wawakilishi wa Umoja wa Mataifa hapa nchini wanashirikiana kutekeleza majukumu yao bila kugongana ama kukinzana. Mpango huu tayari umetuwezesha Oktoba, mwaka jana kuzindua *program* ya pamoja ambayo imejielekeza katika maeneo ambamo Umoja wa Mataifa una ustadi na nafasi ya pekee kuchangia maendeleo ya nchi wanachama.

Mheshimiwa Spika, program hii ya Umoja wa Mataifa ilizinduliwa baada ya mchakato shirikishi baina ya Serikali, wadau wa maendeleo na Vyama visivyo vya Kiserikali. Mpango huu kwa sasa ndiyo msingi wa ushirikiano madhubuti baina ya Tanzania na Asasi za Umoja wa Mataifa. Halikadhalika, mpango wa kufanya kazi kwa pamoja na kutoa huduma zake kama taasisi moja maana yake ni kuainisha shughuli zetu.

Mheshimiwa Spika, manufaa ya utaratibu huu ni kupunguza mlolongo wa usimamizi na kuelekeza nguvu na rasilimali zaidi katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo. Maana yake pia ni kubadili au kuimarisha aina za misaada. Tumebaini pia kwamba ili kuokoa rasilimali zaidi na kupunguza gharama za uendeshaji itakuwa vyema iwapo Mashirika ya Umoja ya Mataifa yaliyopo Tanzania yatahamia katika jengo moja.

Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kuliomba Bunge lako Tukufu liunge mkono jitihada za kupatikana kwa jengo moja kwa ajili ya Ofisi za Asasi za Umoja wa Mataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ambayo imetoa ghorofa mbili katika moja ya majengo yake muhimu ili kuyapatia Mashirika ya Umoja wa Mataifa yaliyowakilishwa kule Zanzibar kuwa na ofisi moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuleta mageuzi katika Shirika la Umoja wa Mataifa kama ilivyo katika taasisi nyingine si kazi rahisi, inachukua muda na inahitaji nguvu za pamoja kutoka kwa wadau wote. Katika muktadha huu nalitia shime Bunge lako Tukufu lishirikiane nasi katika kuimarisha mchakato huu wa *delivering as one* ili kuleta tija zaidi na mafanikio kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto zilizopo, familia ya Umoja wa Mataifa inayaona mageuzi haya kama fursa ya kuimarisha malengo yaliyoainishwa kwenye Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania yaani *Joint Assistance Strategy*. Mipango ya maendeleo inayopendekezwa na Asasi za Umoja wa Mataifa inawiana sawia na vipaumbele vya Kitaifa vilivyomo katika MKUKUTA na MKUZA. Kwa maneno mengine MKUKUTA na MKUZA ndiyo dira ya ushirikiano kati ya Tanzania na Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Spika, mageuzi ya mfumo wa Umoja wa Mataifa sio lelemama. Hata hivyo, tunafarijika kwamba kati yetu tumeshafikia makubaliano ya nini kifanyike. Umoja wa Mataifa unahitaji kuwa madhubuti zaidi na kuimarisha uwajibikaji wa kazi zake za kila siku katika kila nchi ikiwemo nchi yangu nzuri Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, washirika katika maendeleo ni sharti waendeleze na kuongeza misaada yao kadri mipango yetu ya maendeleo inavyopanuka. Natiwa moyo na jinsi Wahisani wa Kimataifa wanavyoungwa mkono mabadiliko tunayofanya. Hadi sasa wahisani wametoa dola milioni 39 kupitia Mfuko wa Fedha wa Pamoja wa Utekelezaji wa Program ya Mageuzi. Fedha zilizopatikana zitatusaidia kuleta mabadiliko yanayohitajika. Msaada huu pia utawezesha Umoja wa Mataifa kuweka mpango wa muda mrefu na kufanya upatikanaji wa fedha kuwa unaotabirika.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa upande wake imeonyesha utashi wa hali ya juu wa kuongoza na kushika hatamu katika kufanikisha mabadiliko haya. Naipongeza

Serikali na kutoa rai kwamba jitihada hizi ziendelezwe zaidi kwa maana ya utashi wa kisiasa na hali kadhalika kwa kutoa rasilimali zinazohitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutetereka kidogo tu kwa jitihada hizi kutarudisha nyuma hatua muhimu ambayo tumeshafikia hivi sasa. Ningependa kusema kwamba kuleta mageuzi siyo mwisho wa kuimarisha shughuli za Umoja wa Mataifa. Mabadiliko haya ni mojawapo tu ya nyenzo muhimu za kufikia malengo makuu ya kimaendeleo kama vile kupiga vita umaskini, kuongeza idadi ya wanafunzi wanaoingia shule za msingi, kuongeza upatikanaji wa dawa za kupunguza makali ya virusi vya *UKIMWI,* kukabili mfumko wa bei za vyakula na mafuta ya *petrol* na pia kukabiliana na majanga yanayotishia usalama wa nchi nyingi Barani Afrika na kwingineko duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia jitihada za kuleta mageuzi katika Umoja wa Mataifa. Ningependa sasa kugusia changamoto chache ambazo zinaukabili Umoja wa Mataifa katika kipindi tulichonacho. Mojawapo ya changamoto tulizonazo ndani ya Umoja wa Mataifa ni kukuza kasi ya utekelezaji wa malengo ya Milenia yaliyokubaliwa na viongozi Wakuu wa Nchi, mwaka 2000 kuwa Dira Kuu ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mpaka hivi sasa tumefikia nusu ya muda tuliojiwekea katika kuyatekeleza malengo ya Milenia ifikapo mwaka 2015. Nilipopata fursa ya kuzungumza na wana habari hivi karibuni kuhusu kazi za Umoja wa Mataifa, nilitanabaisha kwamba nchi nyingi za Kiafrika ziko nyuma katika utekelezaji wa malengo haya. Hususan nchi zilizoko Kusini mwa Jangwa la Sahara. Inakisiwa kwamba kama hakuna hatua madhubuti zitakazochukuliwa hivi sasa nchi nyingi za Kiafrika hazitaweza kufikia malengo yote.

Hata hivyo bado tunayo fursa ya kuongeza kasi ya utekelezaji wa malengo ya Milenia kwa kuzingatia mafanikio yaliyopatikana katika baadhi ya maeneo kwa kuwa na mipango madhubuti na kuongeza rasilimali.

Huu ndiyo wakati wa kuzidisha jitihada. Duniani kote mamilioni ya watu wamenaswa katika lindi la umaskini. Mamilioni wanakabiliwa na athari za mabadiliko ya hali ya hewa na hawa wote wanahitaji msaada wa haraka. Azma yetu ya dunia iliyo bora kama ambavyo imekusudiwa na malengo ya kimaendeleo ya milenia ina uwezekano mkubwa wa kutimia. Hilo litawezekana tu endapo nchi zote duniani zinazoendelea na zilizoendelea zitatimiza ahadi zao. Nchi zinazoendelea kuweka sera madhubuti, kuchochea uwekezaji na kuchukua hatua za kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, nchi zinazoendelea zitakuwa na jukumu la kuongeza ushirikiano na kuzidisha rasilimali. Umaskini hauna mipaka na suala la kutafuta ufumbuzi ni letu sote. Kupiga vita umaskini kunahitaji jitihada zetu za pamoja Kitaifa, Kikanda na katika ngazi ya Kimataifa. Mabadiliko katika Umoja wa Mataifa yanayolenga kutufanya tutoe huduma zetu kama Taasisi moja yaani, *delivering as one* kama nilivyosema hapo awali ni sehemu muhimu ya jitihada zetu katika kutafuta suluhisho la matatizo ya umaskini na kusaidia jitihada za nchi mbalimbali ikiwemo Tanzania.

Mheshimiwa Spika, maendeleo yatakayopatikana nchini Tanzania katika azma yetu hii yatakuwa chachu hapa nyumbani na kwa Jumuiya nzima ya Umoja wa Mataifa. Changamoto kubwa ni kuhakikisha kwamba Tanzania inafanikisha. Bunge laweza kuwa mshiriki muhimu katika jitihada hii. Kwa kutambua hilo, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa - Mheshimiwa Banki Mun amechukua hatua mbili kuu muhimu.

Kwanza, ameunda Kamati ya Afrika kuhusu malengo ya maendeleo ya milenia ambayo inajumuisha Taasisi mbalimbali za Kimataifa kama vile za Kamisheni ya Umoja wa Afrika, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Dunia, Shirika la Fedha Duniani na vyombo vingine vinavyojishughulisha na maendeleo ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Kamati hii ilizindua rasmi mapendekezo ambayo ni madhubuti yenye lengo la kuongeza kasi ya utekelezaji wa malengo ya Milenia ya maendeleo. Tunapenda kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Jakaya Mrisho Kikwete yeye akiwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika, alisimamia uzinduzi wa mapendekezo haya kule Sham AlSheh wakati wa Kikao cha Wakuu wa Nchi za Umoja wa Afrika kilichofanyika mwanzoni mwa mwaka huu. Aidha, nchi za Umoja wa Afrika kupitia viongozi wao zimeyaunga mkono mapendekezo hayo kama mpango wa kuhamasisha utekelezaji wa malengo hayo katika Bara la Afrika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pili, Katibu Mkuu Banki Mun akishirikiana na Rais wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa anaitisha Kikao cha Viongozi Wakuu wa Nchi tarehe 25 Septemba, kule *New York* chenye lengo la kuongeza uelewa wa Kimataifa na kuhamasisha kasi ya kuyatekeleza malengo hayo. Kikao hiki kitafanyika mara tu baada ya kikao kingine maalum cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kitakachohusu mahitaji ya maendeleo ya Afrika ambacho nacho kitafanyika Septemba, 22, mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Mheshimiwa Banki Mun kwamba Bunge lako Tukufu litakuwa tayari kuchangia jitihada hizi. Tunatumaini kwamba katika kuchangia bajeti ya Serikali mwaka huu na katika majadiliano ya Bunge siku zijazo Waheshimiwa Wabunge mtayachukulia malengo ya Milenia kuwa dira kuu ya kuishauri Serikali. Tuna imani kwamba mchango wenu Waheshimiwa Wabunge, utajidhihirisha katika sera na sheria za kuimarisha utekelezaji wa malengo hayo vile vile kama yalivyoainishwa katika MKUKUTA na MKUZA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni kupanda kwa bei za vyakula. Zipo sababu nyingi zilizoleteleza kupanda kwa bei za vyakula. Nisingependa kutumia jukwaa hili kuzizungumzia sababu hizo zote. Itoshe tu kusema kwamba kupanda kwa bei za vyakula na kupanda kwa bei ya mafuta ya petroli ambako kumechangia pia kupanda kwa bei za chakula ni sawa na kengele ya kutuzindua usingizini kwamba wakati umefika kwa nchi kama Tanzania kujizatiti na kupania kuwekeza zaidi katika sekta ya kilimo ili kuongeza uzalishaji wa chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kupongeza jitihada zenu Waheshimiwa Wabunge, katika kuhimiza Serikali kukuza uwekezaji katika sekta ya kilimo. Tanzania

kama zilivyo nchi nyingine nyingi Barani Afrika, inakabiliwa na changamoto kubwa katika kufikia lengo la kwanza la malengo ya maendeleo ya milenia la kupunguza njaa na umaskini ifikapo mwaka 2015.

Mojawapo ya mbinu muhimu ya kukuza sekta hii ni kupanua maeneo ya kilimo, kutumia mbolea, mbegu bora na kupanda mazao yanayostahimili ukame. Jitihada hizi Waheshimiwa Wabunge, ni muhimu ziende sambamba na ujenzi wa miundombinu itakayoimarisha kilimo kama vile ujenzi wa barabara vijijini, upatikanaji wa nishati ya uhakika, upatikanaji wa teknolojia nyepesi na rahisi na vile vile kuweka mipango ya kudumu ya umwagiliaji na kujenga maghala ya vyakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe hata hivyo kwamba ukuzaji wa sekta ya kilimo hauwezi kuwa jukumu la Serikali peke yake. Katika nchi nyingi ambazo zimeshuhudia ukuaji wa kilimo, sekta binafsi imekuwa na mchango wa pekee. Wakati ni huu wa kuhamasisha jitihada za wawekezaji binafsi wa ndani na nje katika kilimo. Hilo lisipofanyika sasa wakati ambapo ishara za uhaba wa chakula katika siku zijazo zipo wazi hatudhani kama kutakuwa na fursa nyingine ya kutuzindua. Kupitia kwenu Waheshimiwa Wabunge, msisite kuchukua hatua za makusudi kuweka sera na sheria za kukuza ushiriki wa sekta binafsi katika kilimo. Umoja wa Mataifa upo tayari kusaidiana nanyi Waheshimiwa Wabunge, kusaidiana na Serikali na wadau wengine wa maendeleo katika kufikia azma hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine la changamoto ni amani, usalama na haki za binadamu. Nchi nyingi Barani Afrika zipo katika kuondokana na migogoro ya kivita. Hatua muhimu zimepigwa katika kukuza demokrasia, kuleta ustawi na kulinda haki za binadamu na hivyo kupunguza migogoro. Umoja wa Mataifa umekuwa tayari wakati wowote kushirikiana na nchi mbalimbali katika kuimarisha maeneo haya kwani migogoro hiyo imechukua muda mwingi na rasilimali muhimu za Umoja wa Mataifa ambazo zingeweza kutumika katika kukuza maendeleo.

Mheshimiwa Spika, napenda kupongeza mchango wa Tanzania katika kushirikiana na Umoja wa Mataifa katika kulinda amani sehemu mbalimbali duniani. Hivi sasa vipo vikosi vya kulinda amani vya Tanzania kule *Lebanon*, waangalizi wa Kijeshi *Sierra Leone* na tunafahamu zipo jitihada za kusaidia nyanja mbalimbali katika maeneo mengine yenye migogoro.

Ni matumaini yetu kwamba Bunge hili Tukufu litaendelea kuunga mkono jitihada za kukuza ushiriki wa Tanzania katika kulinda amani duniani na kuendelea kuwatia ari, vijana wa Kitanzania waliopo mstari wa mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia amani na usalama niruhusu niseme machache kuhusu umuhimu wa kuimarisha demokrasia kama sehemu ya kustawisha amani. Nafurahi kwamba Bunge lako Tukufu limetambua hili na hivi sasa linashirikiana na Umoja wa Mataifa kupitia mpango wa uimarishaji demokrasia Tanzania. Mpango huu unakusudia kusaidia maeneo manne makubwa. Programu ya nchi za Afrika ya

kujitathimini yaani *African Peer Review mechanism*, uchaguzi, elimu ya uraia na utawala bora na uwajibikaji wa Serikali.

Kumekuwa na shughuli nyingi mahsusi zilizolenga kuimarisha Waheshimiwa Wabunge katika kazi zao, wafanyakazi wa Bunge na Kamati zake ili kuziwezesha kufanya kazi vizuri ikiwa ni pamoja na kuchambua bajeti, Miswada, kusikiliza wananchi na kuweka vizuri vipaumbele. Umoja wa Mataifa utakuwa tayari kuendelea kushirikiana na Serikali, kushirikiana na Bunge lako Tukufu na wadau wengine katika kupanua mipaka ya demokrasia nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania inaendelea kupigiwa mfano kama nchi yenye kuheshimu haki za binadamu. Ninapenda kuchukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa kuwasilisha ripoti ya nne, ya tano na ya sita mbele ya Kamati ya Kuondoa Ubaguzi wa aina zote Dhidi ya Wanawake. Ni matumaini yetu kwamba Serikali itaendelea kutoa taarifa zake kwa wakati na kufanyia kazi mapendekezo ya kuimarisha maeneo mbalimbali yanayohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunategemea pia kwamba kwa ile mikataba ambayo Tanzania imekwishatia saini, Bunge lako Tukufu litahimiza kuridhiwa kwa mikataba hiyo kwa mfano Mkataba wa watu Wenye Ulemavu, Mkataba wa Kulinda Haki za Wafanyakazi Wahamiaji Pamoja na Familia zao na Mikataba mingine. Aidha, kwa mikataba ambayo tayari imesharidhiwa kama vile Mkataba wa Haki za Watoto wa mwaka 1999 na Mkataba wake wa nyongeza au Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Watoto bado Tanzania haijatunga Sheria ya kuipa nguvu mikataba hiyo. Ningependa kutoa rai kwa Bunge lako Tukufu likishirikiana na Serikali kuchukua hatua muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, licha ya kutoa mwito huu Umoja wa Mataifa unaipongeza Serikali pamoja na Bunge lako Tukufu kwa kupitisha Sheria ya Kuzuia na Kudhibiti Virusi vya *UKIMWI* na *UKIMWI* ya mwaka 2007. Sheria hii itatoa mchango mkubwa katika kukabiliana na ugonjwa huu na kushughulikia matatizo yanayowakabili waathirika. Umoja wa Mataifa utakuwa tayari kushirikiana na Kamati husika za Bunge na wadau wote katika kuzuia maambukizi na kupiga vita UKIMWI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miaka 63 iliyopita viongozi wa dunia waliunda Umoja wa Mataifa kama chombo cha kuyakabili matatizo ya wakati huo ambayo kimsingi yalihusu Amani na Usalama. Leo dunia yetu inapambana na matatizo makubwa zaidi yasiyojua mipaka kama vile umaskini uliokithiri, ukosefu wa chakula, mabadiliko ya hali ya hewa na milipuko ya maradhi. Changamoto hizi ni za kidunia na zitahitaji suluhisho la kidunia. Ni wajibu wa viongozi wa Kitaifa na Kimataifa kubuni mbinu mpya za kuyakabili matatizo haya.

Mheshimiwa Spika, hatuna shaka viongozi wote wa Tanzania likiwemo Bunge hili Tukufu mtakuwa sehemu ya kutafuta suluhisho hilo la kidunia. Umoja wa Mataifa utakuwa wima kushirikiana nanyi Watanzania wenzangu kutimiza azma hiyo.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru tena kwa heshima na taadhima kwa nafasi hii adhimu uliyonipa. Pia niwashukuru ninyi Waheshimiwa Wabunge kwa kuridhia Utenguzi wa Kanuni mbalimbali ili kuniwezesha mimi kuingia tena katika Bunge hili. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge, kwa kunisikiliza niko tayari kwa niaba ya Katibu Mkuu kuendeleza urafiki, kuendeleza udugu ili tujenge dunia iliyo bora zaidi. Mungu ibariki Tanzania, Mungu bariki Umoja wa Mataifa. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mtu unasema nini zaidi ya hapo, unakuwa na ile faraja ya kujivuna kama Mtanzania. Kweli tuna mwakilishi ambaye tunaweza kutembea kifua mbele popote duniani. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa niaba yetu nilikuwa namwoma Mheshimiwa wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambaye ndiye anamwakilisha humu ndani kwa leo Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Masuala ya Sera, Uratibu na Bunge ili aweze kusema maneno mafupi ya shukrani kwa niaba yetu sisi sote. Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. *(Makofi)*

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, kwa niaba ya sisi Waheshimiwa Wabunge wote, kwa niaba ya Serikali na kwa kweli kwa niaba ya Watanzania najua wengi sasa hivi wanatusikiliza na wanatuona tunapenda kwanza kabisa tuendelee kukupongeza, usichoke kupokea pongezi zetu ambazo hazina ukomo kwa uteuzi wako kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Umeweka historia kubwa kabisa kama ni mwanamke wa kwanza kushika nafasi hiyo, Mtanzania wa kwanza kushika nafasi hiyo na Mwafrika wa kwanza kushika nafasi hiyo. Umetujengea heshima kubwa sana sisi Watanzania na Afrika kwa ujumla bado tunakupongeza. Mungu akubariki sana. Unapofanya kazi zako uwe na uhakika kabisa kwamba sisi sote Watanzania karibu milioni 40 tupo nyuma yako, tunakuunga mkono, utembee kifua wazi ukijua kwamba tupo pamoja na wewe wakati wote. *(Makofi)*

Pili, tunapenda tukushukuru kwa uamuzi wako wa kuja Dodoma kutusalimia. Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro upo likizo ungeweza kabisa sasa hivi ungekuwa labda Ngorongoro kule unatazama wanyama, ungeweza kuwa Zanzibar kwenye fukwe nzuri kule unapumzika. Lakini umeamua kuja Dodoma kutusalimia, ahsante sana, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa taarifa yako kwa kweli tunaku-*miss* sana ndani ya Bunge hili. Nadhani unamkumbuka jirani yako Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu ulivyokuwa unamsaidia kufafanua maswali yake alipokuwa anajibu yale maswali hasa ya nyongeza ulikuwa ndiyo upo hodari kumfafanulia, maana yake yalikuwa babu kubwa! Wewe peke yake uliweza kuyafafanua vizuri. Kwa kweli tunajisikia vizuri sana kuwa na wewe tena ndani ya Bunge letu. Waswahili wanasema kwamba “aliye juu hamjui wala hamthamini aliye chini.” Mheshimiwa Dr. Asha- Rose Migiro wewe upo juu, tena upo juu kweli kweli, lakini umeshuka toka juu mpaka umefika hapa Dodoma tulipo sisi chini kabisa

huku. Tunashukuru sana kwa hekima na busara hiyo kutufikia sisi Watanzania huku chini kabisa na kuja kuwasalimia Watanzania kupitia Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro tunataka kukuhakikishia kwamba tunafuatilia kwa makini sana tangu umekwenda Umoja wa Mataifa kazi unazozifanya, tunaridhika sana, unatuwakilisha vizuri, na unatangaza vizuri sana jina la Tanzania popote unapokwenda duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro tunakushukuru vilevile kwa nasaha nzito kabisa ambazo umetupatia mchana huu wa leo, umetueleza programu ya Mageuzi ya Umoja wa Mataifa kufanya kazi kama Taasisi moja, umetueleza juhudi zinazofanyika katika kutatua migogoro duniani, umetuonya kuhusu kupanda kwa bei ya mafuta na chakula, umetueleza habari za kupambana na *UKIMWI*, na umeomba Bunge hili liunge mkono hayo yote.

Tunataka tukuhakikishie kwamba Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro tutaunga mkono juhudi zote hizi Tanzania kama sehemu ya dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Asha Rose – Migiro amesema vilevile kwamba angependa Serikali yetu itafute namna ya kuwezesha Taasisi za Umoja wa Mataifa ziwe katika jengo moja, hili nalo tumelipokea kwa mikono miwili kama ni kutafuta jengo, nafikiri Waziri wa Miundombinu amesikia tutatafuta haraka iwezekanavyo, kama ni ardhi ya kujenga Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ndiyo mimi, uliniacha nikiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, magazeti yakawa yanatoa utani tulipoteuliwa, mimi, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na wewe Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro - Waziri aa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, magazeti yakawa yanaandika Mheshimiwa John Chiligati *in* na Mheshimiwa Dr. Asha - Rose Migiro *out.* *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Asha - Rose Migiro alipoteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa wakasema Dr. Asha - Rose Migiro *out* kabisa. Sasa mimi nipo Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kwa hiyo, rafiki yangu kama unahitaji ardhi ya kujenga jengo kubwa la Umoja wa Mataifa kama ni Dar es Salaam ama Dodoma hapa, basi tupo tayari kukusaidia hiyo ardhi ipatikane ili Taasisi zote za Umoja wa Mataifa ziwe katika Jengo moja kama lilivyo Azimio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jukumu langu lilikuwa ni kumshukuru Dr. Asha-Rose Migiro, nisiseme maneno mengi mwisho nikaharibu utamu wa maneno aliyotwambia mchana wa leo. Kwa hiyo, naomba niishie hapo kwa kukukaribisha sana tena sana Dodoma wakati mwingine ukipata likizo njoo Dodoma utusalimie na tupo tayari kukukaribisha tena. Mungu akubariki sana wewe mwenyewe na familia yako. Mungu aibariki Tanzania, Mungu aibariki Afrika, Mungu aubariki Umoja wa Mataifa. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

SPIKA: Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi nakushukuru sana. Haishangazi kwamba wewe ulichaguliwa kuwa Katibu wa Uenezi wa Chama cha Mapinduzi. Kwa kweli unamudu kujieleza. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tutakuwa na fursa nzuri sana saa 9.00 kamili kuwa na mgeni wetu katika Ukumbi wa Pius Msekwa hapo ndipo itakuwa Wazungu wanasema *interactive session*, tutaongea naye atakuwa katika hali siyo kama hii ya sasa iliyo rasmi mno.

Kwa hiyo, baada ya kufika hapo tukio hili la kupokea hotuba ya Mheshimiwa Dr. Asha –Rose Migiro Naibu Katibu Mkuu Umoja wa Mataifa ndiyo imefikia hatma yake. Nitaomba tusimame ili aweze kutoka nje ya Ukumbi kabla hatujaendela na hatua nyingine za Bunge. Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro ahsante sana.

Naomba wale waliomsindikiza waendelea kama ilivyokuwa. Naona anakwenda kuonana na Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye *Lounge* hapo. Ahsante sana. *(Makofi)*

(Hapa Mheshimiwa Dr. Asha -Rose Migiro Aliondoka Ukumbini)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, baada ya tukio hilo na kwa kuzingatia kwamba hakuna muda wa kuanza tena kuwasikiliza wachangiaji. Ninao wachangiaji 41 na tutaanza saa 11.00 jioni. Lakini tutatoa muda wa kutosha msiwe na wasiwasi kuhusu Wizara hii na baada ya hotuba ya Mheshimiwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa na msisitizo aliouweka kwa kilimo. Nadhani tutajitahidi kuwapa nafasi wachangiaji wengi kadri inavyowezekana waweze kuchangia.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sasa naomba niwataje wale wachangiaji watano watakaoanza saa 11.00 Jioni. Hawa ni wale ambao hawajachangia hata mara moja. Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Yusuf Makamba, Mheshimiwa Richard Nyaulawa, Mheshimiwa William Shellukindo na Mheshimiwa Danie Nsanzugwanko. Hawa watano.

WAHESHIMIWA WABUNGE: Wengine wamekwishachangia.

SPIKA: Wamo waliokwishachangia!

WAHESIMIWA WABUNGE: Ndiyo!

SPIKA: Sasa rekodi yangu Katibu hapo muwe mnaangalia vizuri. Nadhani Mheshimiwa Yusuf Makamba ndiyo kweli hajachangia.

WAHESHIMIWA WABUNGE: Ndiyo!

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, labda tuanze na Mheshimiwa Yusuf Makamba. Lakini Waheshimiwa Wabunge, huwa mnajivuta vuta, sana sana saa 11.00 jioni kunakuwa hakuna hamasa, na kwa hiyo, Yusuf Makamba ni mzungumzaji mzuri. Mimi ninadhani lazima Waheshimiwa Wabunge, wengine wapashe moto kwanza. Kwa hiyo, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Nyaulawa, itakuwa hiyo ni saa 11.30. Tunaweza kumweka na Mheshimiwa William Shellukindo hata Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko ili kwenye saa 12.00 hivi ndiyo Mheshimiwa Yusuf Makamba aweze kuongea. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kutoa maelezo hayo, ni kusisitiza tu kuhusu saa 9.00 katika Ukumbi wa Pius Msekwa ambako kutakuwa na matukio mawili. Moja, ni kuelezea Ulimwengu pale kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa jitihada za Bunge hili katika kuhamasisha Mapambano Dhidi ya Ukatili wa Wanawake na kama nilivyosema, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge pamoja na Makamishna wa Tume ya Huduma za Bunge watatakiwa wakae mbele kwa kile kitendo cha kuweka saini kwa niaba ya wenzetu wote. Ile kadi inayohusu tamko hilo la Mapambano Dhidi ya Ukatili wa Wanawake. Halafu baada ya hapo au sambamba na hilo basi tutaendelea na kuongea na mgeni wetu na saa 10.00, basi tutamaliza ili tujiweke tayari kwa ajili ya Bunge litakaloendelea hapo saa 11.00 jioni.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo, sasa nasitisha Shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni.

(Saa 06.58 Mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Zubeir Ali Maulid) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyotangaziwa pale asubuhi sasa tutaanza kuichangia hii hoja ambayo imewasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika na mchangiaji wangu wa mwanzo atakuwa Mheshimiwa Gaudence Kayombo atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Nyaulawa na Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko ajiandae.

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, lakini kwanza ni budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na kutupa afya sisi sote kuweza kufika siku hii ya leo. Ninazungumza hivi kwa sababu kipindi kama hiki sikuwepo, nilikuwa kwenye matibabu nchini India. Kwa hiyo, leo kuwa na afya kamili hapa ni jambo la kumshukuru Mungu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni kwa vile Mheshimiwa Spika hayupo, lakini pengine ningekutana naye angeweza akafafanua wakati anasitisha Bunge alisema kwamba kutakuwa na Wabunge ambao wanapasha moto. Mimi nimemwelewa nia yake, lakini naona *message* zinazokuja hazina nia ambayo alikuwa nayo yeye. Lakini ningependa kuwathibitishia wananchi wa Mbinga na wa Tanzania mimi kama Mbunge kazi yangu ni kutoa hoja na kuisaidia Serikali na kuwakilisha wananchi wa Jimbo langu kwa kikamilifu na sio kupasha kiti cha mtu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sana nitoe rambirambi kwa wananchi wa Mbinga katika wiki mbili zilizopita, tulifiwa na Mwenyekiti wetu wa Chama cha Mapinduzi wa Wilaya - Ndugu Osmund Komba. Napenda kuwashukuru sana viongozi wa Serikali Mheshimiwa *DC*, *DED*, Mwenyekiti wa Halmashauri, Waheshimiwa Madiwani na wananchi wote ambao walihakikisha kwamba tunamzika Marehemu kwa heshima kubwa anayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema nayo, naomba pia niishukuru Serikali kwa mambo mazito na mazuri sana ambayo wananchi wa Mbinga wamefanyiwa hususan Jimbo la Mbinga Mashariki. Kwanza kwa kuonekana kutimizwa kwa ahadi ya kujenga barabara kutoka Songea mpaka Mbinga kwa fedha za *MCC*. Lakini pia Halmashauri nayo inajitahidi sana kujenga barabara ambazo ziko katika himaya za Wilaya. La pili, ni umeme ambao umekuwa kilio kikubwa kwa wananchi wa Mbinga toka Wilaya hiyo imezaliwa, lakini toka tarehe 6 Septemba, 2007 wananchi wa Mbinga wameanza kupata umeme na majenereta mawili yaliyoahidiwa na Serikali yamekwishawasili na shughuli ya kuanza kuyaweka pamoja ili kuweza kupata umeme na hizo jenereta zimekwishaanza. Tunaishukuru sana Serikali, bila shaka Serikali hii itatimiza ahadi yake ya kuleta umeme wa gridi itakapofika mwaka 2010.

Tatu, napenda kuipongeza Serikali pia na kuishukuru kwa kusogeza kituo cha usambazaji kuwa Mbinga. Msimu uliopita ule ilikuwa Songea sasa kimesogea mpaka Mbinga, lakini sasa kuna utaratibu mpya ambao unaanza katika awamu hii ya fedha

ambayo nafikiri ni mzuri zaidi. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali. Nne, naishukuru pia Serikali, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa kukubali sasa na kuanza kulipa malipo ya fedha ambazo wakulima walikuwa wanadai Vyama vya Ushirika na Serikali ya Awamu ya Tatu ilikubali kubeba huo mzigo na Serikali ya Awamu ya Nne inaanza kutekeleza makubaliano hayo. Nawashukuru sana Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. *(Makofi)*

Mimi mchango wangu utalenga hasa katika upande wa kilimo kwa ujumla, lakini kwa namna ya maswali. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 11 amesema naomba kunukuu: "Uchambuzi wa kina ulifanywa na kundi la nchi zilizoendelea *(OECD)* na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *(Food and Agriculture Organization of the United Nations – FAO)* mwezi Mei, 2008, umeonyesha kuwa pamoja na uzalishaji wa chakula kuongezeka, kwa wastani bei za vyakula zitaendelea kuwa juu kwa karibu miaka 10 ijayo ikilinganishwa na miaka 10 iliyopita."

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui wenzetu Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika wamelionaje jambo hili. Mimi naona hii ni nafasi (*opportunity)* ya kuwafanya wakulima wetu wakatengeneza fedha. Nchi nyingine hazina ardhi, hazina mvua za kutosha, lakini sisi katika nchi yetu na mimi nazungumzia hasa zile *(Big Four)* Mikoa minne ile Ruvuma ikiwepo mvua tunazo za uhakika, ardhi tunayo ya kutosha, kuna ardhi nyingine haijalimwa toka Adam na Eva. Sasa hapa tunaambiwa kwamba dunia hii inakabiliwa na njaa, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika inayo mikakati gani ya kuhakikisha kwamba wakulima wanapata faida ya matatizo haya ambayo yanayotokea duniani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika kama ingekuwa mambo ya viwanda, Serikali ingekuja na mpango maalum kwamba kiwanda fulani zalisha kwa sababu mahali fulani kuna uhaba. Lakini kwa upande wa mkulima huyu tunafanyaje sasa? Mipango gani thabiti ambayo inakuja? Nasoma hiki kitabu sioni ikijitokeza vizuri kama ambavyo natarajia kumsaidia huyu mkulima. Ndiyo naelewa tumeacha sekta binafsi ifanye hiyo shughuli, lakini kuna mambo mengine ambayo Serikali lazima ifanye ili sekta binafsi iweze kudaka na kuweza kuendelea, ningependa kuona Mheshimiwa Waziri anapohitimisha hoja yake ananieleza au anatueleza hiyo mipango kamili ambayo anayo.

Pili, pamoja na sera nzuri tulizonazo juu ya kilimo toka miaka ile ya 1970, "Siasa ni Kilimo", Mheshimiwa Njwayo leo aliuliza swali kule Mkoa wa Mtwara, kulikuwa na *UNJAMA*, Mkoa wa Ruvuma kuliwa na Operesheni ya Kuondoa Njaa kupitia agizo la Mlale na Mikoa mingine walikuwa na maagizo kama hayo. Tunavyo vyuo vizuri vya utafiti na vyuo vya kilimo, tunazo mvua, tunayo mito mingi sana, bado tukisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri tunakuta bado njaa inatuelemea na inatunyemelea, tatizo liko wapi? Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ni Wizara ambayo imepata wafadhili kwa muda mrefu na hata bajeti yake ya mwaka jana inaonekana walipata karibu yote, kwa nini bado nchi yetu inanyemelewa na njaa pamoja na maji tuliyonayo, pamoja mvua nzuri tulizonazo pamoja na wataalamu wazuri tulionao? Haya mimi nafikiri ni majibu ambayo Serikali inapaswa ijielekeze na itueleze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, kilimo kinataka *incentives* na *incentive* mojawapo ni kuona watu waliofanikiwa. Tunao watu wetu katika Mikoa ambao wamefanikiwa katika kilimo ambako wakulima wengine wanaweza wakajifunza, ingefaa pengine hata katika hotuba wangetajwa hao wakulima maarufu na wazuri ambao wamelelewa wakakua na wakawa mfano kwa wakulima wengine ili wakulima wengine pia waweze kuiga. Kama nitakuwa na muda nitaomba pia ninukuu kitabu kimoja ambacho nilikipata *South Korea* juu ya mkulima mmoja juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inachukua hatua gani kusaidia hawa wakulima na imefanya tathmini gani kuona nani anayelima na kwa nini anafanya kazi hiyo ya kulima pamoja na kwamba kilimo kinaonekana hakina tija hakiwezi kumwendeleza mtu na hizo zana, lakini Serikali inafanya nini na kimekuwepo kilio cha Wabunge cha muda mrefu cha kuanzisha Benki ya Wakulima. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri linaonekana ni jambo ambalo linasema iko mikakati mbioni na haya ni mambo ambayo yako kila mwaka. Benki ya Wakulima haionekani kama ni jambo la dharura, tumepata uzoefu katika mikopo ya mabilioni ya JK. Benki ya *NMB* haikuanza mapema kuwakopesha wakulima kwa sababu haikuwepo katika sera yao kuwakopesha wakulima kwa hiyo unaona kabisa taasisi za fedha zinamkimbia mkulima. Kwa hiyo, hitaji la kuwa na Benki kwa ajili ya mkulima ili kilimo kiweze kuendelea, ili aweze kupata zana ambazo anazihitaji kwa mfano kwenye maonyesho ya Saba Saba kulikuwa na trekta pale linauzwa shilingi milioni 50, mkulima wa kawaida atapata wapi fedha ya kununua trekta kama hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa labda nielekee kwenye kilimo cha kahawa ambacho robo tatu ya wananchi wa jimbo langu ndicho wanachokilima na ndicho kinachowategemea. Kwanza, nawashukuru Serikali ilitoa ruzuku kwenye miche ile ya kahawa kupitia kile kituo cha *TACRI* pale, lakini pia katika Sheria ya Kahawa ya mwaka 2001 Bodi ya Kahawa inatakiwa iwaandikishe wakulima, wakulima wawe *registered.* Mpaka leo toka hiyo Sheria ya mwaka 2001 hadi leo hakuna hatua zozote na wala hakuna mkulima ambaye yuko *registered* na mbaya zaidi sheria hiyo inawataka wanunuzi wa kahawa, waende wakanunue kahawa kwa wakulima ambao wameandikishwa na usipofanya hivyo ni kosa la jinai, sheria inatamka. Kwa hivi kahawa inanunuliwa kila siku na hawa watu wanafanya makosa ya jinai kila siku na Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ipo na Bodi ya Kahawa ipo kwa nini mpaka leo Bodi ya Kahawa haijaandikisha wakulima. Faida za kuwaandikisha wakulima ziko wazi kabisa kwanza huyu mkulima atafahamika yuko wapi na hivyo anaweza akakopesheka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifanya mazungumzo ya kupitia tu pamoja na Benki ya Wananchi ya Mbinga kama hili jambo likifanyika inawezekana hawa wakulima wakakopesheka inawezekana kabisa kuwakopesha kwa urahisi zaidi. Kumbe adui wa mkulima wa kahawa ya Mbinga sasa ni *Tanzania Coffee Board* na mzigo huo hawawezi kukwepa na mimi ningependa Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha hoja anieleze ni kwa nini Bodi ya Kahawa hawajafanya *registration* ya wakulima. La pili, Wakaguzi wa Kahawa. Bodi inatakiwa ichague Wakaguzi wa Kahawa haijafanya mpaka leo *unless* niambiwe kwamba hii sheria ilishafutwa.

La tatu, kuna huu ushuru wa asillimia tano, ushuru huu mimi ningependa nipate tafsiri ya *farm get prices*. Sababu pale Mbinga mkulima anayeuza kwa mnunuzi moja kwa moja shambani anakatwa ushuru wa asilimia tano. Lakini yule ambaye anauza kupitia Chama cha Ushirika na Chama cha Ushirika kinapeleka Moshi wanakatwa fedha zao kupitia lile soko la kahawa la Moshi wanakatwa asilimia tano lakini wao wanakatwa kwa fedha za kigeni maana yake analipa fedha nyingi zaidi kuliko yule mkulima aliyeuzia pale shambani. Sasa tofauti hii inaleta matatizo kule Mbinga. Ningeomba Waziri hapa atusaidie juu ya tatizo hili. Nne, *Coffee Board* pia inatakiwa ifanye madaraja ya kahawa, jambo hili pia halijafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni Ushirika. Nimekwishazungumza na Mheshimiwa Waziri na nashukuru Mungu kwamba Mheshimiwa Waziri amenikubalia kwamba ushirika wamekaa kule Mbinga utarudi, lakini nafikiri watendaji wanamwangusha kwa sababu sijaona juhudi zozote za kiutendaji zinaendelea. Huko nyuma *Co-operative* zote hazikufilisiwa *co-operatives* zilizoko chini ya mufilisi ni *MBICU* na Chama cha Ushirika cha kule Musoma kwa Mheshimiwa Waziri sielewi ni kwa nini, kwa sababu zote zilikuwa katika hali iliyo sawa. Sasa haya matatizo yaliyotokea ni ya kiutendaji ndani ya Serikali, mimi naomba yarekebishwe hawa wananchi wapatiwe haki yao na ushirika huu uanze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kengele ya kwanza imeshalia na mimi nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kayombo kwa kututunzia vizuri pamoja na kuokoa muda. Sasa namwita Mheshimiwa Richard Nyaulawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela ajiandae.

MHE. RICHARD S. NYAULAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kushiriki katika kujadili hoja hii na hasa kwa sababu sikuwepo kwa muda mrefu kutokana na matibabu ambayo yalikuwa ya saratani ya tumbo, lakini nawashukuru sana Wabunge wote pamoja na Watanzania kwa ujumla kwa sala zao na upendo wao ambao wameuonyesha ambao Mwenyezi Mungu ameweza kunibariki na nimeweza kurudi salama. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Nawashukuru sana wananchi wa Mbeya Vijijini kwa mapokezi mazuri ambayo walikuwa wameyafanya pamoja na sala zao na upendo ambao walikuwa wameonyesha kwa muda wote ambao nilikuwa sipo, kwa hakika nipo hapa sasa tayari katika kushughulikia shughuli zetu za maendeleo na kushirikiana katika mambo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningetaka kuanza kwa kueleza tu kwamba maisha ya wananchi wa Tanzania wanaokaa mijini pamoja na vijijini ni magumu sana kwa wakati huu kutokana na mfumko mkubwa wa bei ambao unakwenda kwenye asilimia 7.2 kutoka kwenye asilimia 5.5 kama miaka mitatu au minne iliyopita. Mfumko huu unatokana kwa kiasi fulani na matatizo ya mafuta ambayo yanachangia tu katika mfumko huo kwa asilimia tisa tu. Lakini matatizo makubwa yanatokana na uhaba wa chakula nchini ambao unachangia kwa asilimia 47 ya mfumko wa bei. Sasa hiyo asilimia ni kubwa sana,

maana yake tusipofanya juhudi katika kutatua tatizo la chakula, basi bado tutaendelea kuwa na matatizo ya mfumko wa bei na maisha ya Watanzania yatakuwa ni magumu kadri siku zinavyokwenda. Uhaba unajitokeza kwa sababu uzalishaji ni duni kwa sababu hatuna zana za kutosha, zana za kilimo, mbolea ni ndogo na haipatikani kwa wakati unaofaa, madawa ni machache na ni ghali kwa wakulima, mbegu ni chache na hazipatikani kwa urahisi na wataalamu ugani nao ni wachache na wengi wao hawakai vijijini kama ambavyo wanastahili kukaa kwa sababu ya matatizo mbalimbali waliyokuwa nayo.

Kwa hiyo, uzalishaji unakuwa ni duni sana, lakini kinachosikitisha ni kwamba uzalishaji huu unakuwa ni duni kwa sababu Serikali haijawekeza sawa sawa katika shughuli za kilimo na ushirika. Leo hii tunataka kutumia shilingi bilioni 23 kwa ajili ya kununua mbolea kuagiza kutoka nchi za nje, lakini kiwanda kimoja cha mbolea kinagharimu shilingi bilioni 13, 14 au 15, kiwanda ambacho kingeweza kuzalisha mbolea kwa muda mrefu zaidi lakini sisi tunatumia fedha hizo kwa kununua mbolea ya mwaka mmoja ambayo bado haitoshelezi kwa wananchi walio wengi. Serikali yetu bado haijawekeza vya kutosha katika shughuli mbalimbali za kilimo na kama tukiendelea na hali hiyo hatutapiga hatua ya aina yoyote, tutaendelea kutwanga maji kwenye kinu kwamba tuna njaa, tuna njaa mwaka hadi mwaka.

Kwa upande wa ushirika, ni kweli kabisa kwamba uwekezaji katika ushirika haujafanikiwa sana ingawaje Serikali imefanya kazi kubwa sana na hapa lazima nitoe pongezi kwa upande wa ushirika wa *SACCOS*. Lakini ushirika wa uzalishaji na wa masoko wa mazao ya aina mbalimbali bado hatujaanza kuona matokeo yake. Serikali inatoa ruzuku ya mbolea tunashukuru katika hilo.

Lakini mbolea hii imekuwa ni kero kubwa sana kwa wananchi waliokuwa wengi kwa sababu mara nyingi ni chache sana na wala haitoshelezi kwa kiwango chochote kinachohitajika na wananchi. Haipatikani kwa muda muafaka kwa muda mrefu na mara nyingi inahusishwa na mambo ya ulanguzi kwa sababu mbolea ambayo hugawiwa wakati mwingine unaweza kuiona katika maduka ya wafanyabiashara wa kawaida. Kwa kiwango kikubwa kazi hii ya kuagiza mbolea inawanufaisha zaidi wasafirishaji kuliko walengwa ambao ni wakulima.

Kwa hiyo, tuna uzoefu wa muda mrefu wa zaidi ya miaka mitano ambako tumekuwa tukitoa mbolea, lakini mbolea hii imekuwa haitoshi kwa njia ya aina yoyote ile. Kwa kiwango kikubwa tunaweza kusema kwamba mbolea ambayo inatolewa haijawahi kuongeza tija au uzalishaji wa kutosha ndiyo maana tunakuwa na njaa pamoja na kwamba tunatumia fedha nyingi sana, lakini ndiyo maana tunakuwa na matatizo ya njaa katika nchi yetu. Gharama za kusambaza mbolea hiyo kwa wakati huu kama Mheshimiwa Waziri alipokuwa akitoa kuhusu mambo ya vocha leo asubuhi gharama yake itakuwa ni kubwa zaidi kuliko mbolea anayopata mwananchi. Unachukua Serikali nzima inakwenda kufanya usambazaji wa mbolea ambayo mwananchi anapata robo kilo au kilo moja gharama hizo ni kubwa zaidi kuliko hata thamani ya mbolea ambayo anapata mwananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuwa na utaratibu tofauti, hiyo mbolea chache ambayo haileti tija chakula chake kikiweza kupatikana basi kinauzwa kwa bei ya chini sana. Kinauzwa kwa bei ya chini kwa sababu mfumo mzima wa kuuza chakula kwa kupitia wafanyabiashara wa kati sio sahihi na mara nyingi haupitii katika Vyama vya Ushirika kwa sababu nguvu ya mkulima ambaye ni mnyonge ni kuungana katika Vyama vya Ushirika. Mkulima mmoja mmoja hawezi kuwa na mazao ya kutosha ya kuweza kukidhi soko kwa hiyo inakuwa ni vigumu kwake kuweza kupata soko lililokuwa zuri. Lakini kama wangekuwa wameungana kwa pamoja na kufanya kazi katika ushirika nina imani kabisa kwamba wakulima wangeweza kufaidika na mazao yao ambayo wanayapata, kwa hiyo, mazao hayo machache ambayo wanayapata hayapati soko zuri. Kwa msingi wakulima wanavutiwa na bei nzuri na kama bei ni nzuri kuzalisha kwa wingi. Kipato cha mkulima kinatokana na bei nzuri ya mazao yake.

Kwa hiyo ambacho ningeshauri hapa ni kwamba badala ya kutumia fedha nyingi kununua mbolea fedha hizo ambazo zingetumika katika ruzuku ya mbolea zitumike katika kuboresha bei ya mazao ya mkulima, kwa maana kwamba mkulima apate bei nzuri badala ya kumpa ruzuku ya mbolea. Mkulima kama atakuwa amejua bei ya mazao ambayo ni nzuri atalazimika na atahamasika katika kulima mazao ya aina mbalimbali. Kwa mfano, kwa wakati huu kilo moja ya mahindi Mbeya wakati wa msimu huwa inanunuliwa kwa Sh. 200/= ambayo maana yake ni kwamba labda gunia moja linaweza kuuzwa kwa shilingi 24,000/= lakini kama Serikali ingekuwa inatoa ruzuku tungesema kwamba hizi shilingi bilioni 23 zitatumika kwa ajili ya kutoa ruzuku Serikali ikatangaza kabla ya msimu ikatangaza bei ya mazao mapema nina uhakika kwamba wakulima wangeanza kulima zaidi kwa sababu wangekuwa na uhakika kwamba watakapokuwa wanauza mazao yao hizo shilingi bilioni 23 zitatumika. Hizo shilingi bilioni 23 zitatumika katika kuboresha bei ambayo itamfikia yule ambaye amelima.

Kwa hiyo, haitakwenda kwa mtu mwingine yoyote kasoro mkulima ambaye amefanya kazi hiyo ya kulima, kwa hiyo, itafika kwa mlengwa. Lakini kwa kufanya namna hiyo wakulima wengi wangeweza kulima mazao na sisi tusingekuwa na njaa ambayo inatupata sasa hivi. Kwa hiyo, kazi kubwa ya Serikali ingekuwa ni kutangaza bei mapema ili kuweza kuwavutia wakulima zaidi, lakini kingine ambacho kingekuwa ni cha msingi ni kuweza kuwahamasisha wawekezaji mbalimbali ili waweze kuwekeza katika shughuli mbalimbali za kilimo. Vyote hivi vikifanyika kwa pamoja nina uhakika

kwamba mazao ya chakula yatapatikana kwa urahisi yatakuwa ni mengi na sisi hatutakuwa na sababu yoyote ya kuweza kuagiza chakula kutoka nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri vile vile kwamba Serikali ijenge maghala ya kutosha aidha, yenyewe au kwa kushirikiana na watu binafsi. Ni aibu kwa leo hii kwamba Serikali yetu inaweza kuwa na chakula cha *SGR* cha tani 150 ambapo mahitaji ya wananchi wa kawaida kwa nchi nzima inakwenda kwenye tani milioni 11. Sisi tunakuwa na ghala la tani 150 na ndiyo maana kila mara tunapokuwa na matatizo ya chakula tunaagiza tani nyingi za chakula kutoka nje na hatuwezi kukidhi mahitaji yetu sisi wenyewe.

Kwa hiyo, ningeshauri kwamba tuanze kujenga maghala kama Serikali au kwa kushirikiana na watu binafsi ili angalau tuweze kuwa na tani milioni moja za chakula. Hoja yangu hii ni ya msingi kwa sababu kadri siku zinavyokwenda huko mbele chakula duniani kinazidi kuwa haba hakipatikani kwa urahisi, haitakuwa rahisi kuweza kupata chakula kama ambavyo tunapata sasa hivi. Bei itazidi kuwa ngumu kubwa kwa maana hiyo upatikanaji wa chakula hata kama tutakuwa na fedha za kutosha za kuweza kununua lakini chakula hicho duniani itazidi kuwa kidogo kadri siku zinavyokwenda.

Kwa hiyo, ni muhimu kwamba sisi wenyewe tunaweza kutumia fedha zetu, rasilimali yetu katika kuzalisha chakula cha kutosha badala ya sisi kununua chakula kutoka nchi za nje, basi sisi tuweze kuuza chakula katika nchi za nje. Kwa hiyo, ningeshauri tena kwamba Serikali itumie fedha ambazo zinatumia kwenye ruzuku ya mbolea katika kuboresha bei ya mazao ya mkulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nilitaka kuchangia kwenye upande wa Bodi za Mazao hazitendewi haki kwa kupatiwa fedha kidogo sana za kuweza kuendesha shughuli yake. Bodi za Mazao zina majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na uhamasishaji wa uzalishaji, utafutaji masoko pamoja na shughuli mbalimbali za udhibiti. Lakini kufuatana na bajeti ambazo zinajitokeza ni kwamba fedha hizo ambazo zinapatikana kwa ajili ya Bodi za Mazao ni kidogo sana na inaonyesha jinsi ambavyo Serikali haiwekezi katika shughuli mbalimbali za kilimo ambazo zinaweza kusaidia kuongeza uzalishaji wa mazao na chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ni Maafisa Ugani kwa ngazi ya kata na kijiji ambao wamekuwa ni wachache hawatoshi na kazi zao ni ngumu, lakini vile vile hazionekani kwa urahisi. Kwa ushauri wangu ni kwamba kama tunataka kuwa na matumaini makubwa katika kilimo na tukaepukana na matatizo ya njaa, basi ingekuwa ni vizuri kama Serikali ingewekeza zaidi katika kuongeza wafanyakazi wa ugani vijijini na kwenye ngazi ya Kata, lakini vile vile walioko huko vijijini ukiwaona unaweza kusikitika kuhusu hali zao wanakuwa wamechakaa kweli kweli. Wana hali mbaya wakati mwingine ukiwaangalia wanakuwa huwezi kutofautisha kwamba kuna mtaalamu hapa katika kijiji, huwezi kutofautisha kama kuna mtaalamu yoyote wa kilimo ambaye kazi yake ni kuwasaidia wakulima katika kuongeza utaalamu wa kilimo katika kijiji.

Ningeshauri kwamba hawa wangekuwa wanapewa mafunzo ya aina mbalimbali ya muda mfupi *(refresher courses)*, kwa sababu natumaini wakishapelekwa huko vijijini

kwa muda mrefu huwa hawapati mafunzo ya aina yoyote na inafika mahali ambapo mkulima anakuwa na elimu kubwa zaidi kuhusu mazao anayozalisha kuliko Afisa Ugani, sasa hiyo inakuwa ni hatari katika shughuli zote za kilimo.

Lakini vile vile labda tungejaribu kuwajengea nyumba kwa sababu kwa wakati huu mara nyingi hawakai katika maeneo yao ya kazi. Ukimtafuta Afisa Kilimo kwenye ngazi ya kata hata kwenye ngazi ya kijiji huwezi kumpata kwa urahisi. Wengi wanakaa sehemu nyingine mbali kabisa na vijiji ambako labda zinakuwa ni sehemu za mjini na kazi zao huwa inakuwa ni kusafiri mara moja moja kwenda kijijini kwa ajili ya kuweza kufanya kazi za wananchi. Lakini vile vile wapewe vitendea kazi kama ikiwezekana wapewe baiskeli kwenye ngazi ya kijiji ili kurahisisha kazi zao za kuweza kutembelea wakulima kutoka mahali hadi mahali lakini kwenye upande wa Kata ningeshauri vile vile wapewe labda usafiri wa pikipiki kwa sababu Kata kwa wakati huu ni kubwa sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Jimbo la Kasulu Mashariki, naomba kwa heshima nitoe mchango wangu kwa sekta hii ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwenye Jimbo langu, Mkoa wa Kigoma takriban asilimia hadi 98 ni wakulima. Sisi kwetu hii ni Wizara mama hasa kwa sababu ni Wizara inayogusa maslahi ya wananchi wetu na wapiga kura wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kukupongeza wewe Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wako na timu yote kwa kazi mnayoendelea kuifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yako ya bajeti, nina mambo machache ambayo ninapenda na kushauri au kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla sijaendelea, ninaomba nimrejeshe Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 97 wa kitabu hiki. Ukurasa wa 97 kuna kiambatanisho ambacho ni muhimu kweli kinasema Kanda za Kilimo kulingana na hali ya hewa. Takwimu hizi zimenivutia sana lakini kwa maoni yangu na kwa heshima zote Mheshimiwa Waziri, kile kiambatanisho hakipo sawasawa hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kimechukua mambo ya jumla jumla tu. Kwa mfano kwenye ukurasa wa 99 pale E(3), takwimu hazikukamilika, mwisho, inaandikwa *not found*. Maana yake kitu hakikufanyiwa kazi na tumeletewa tu ukurasa wa 99. Lakini hoja yangu ya msingi nataka niipeleke ukurasa wa ule wa 104 kwenye *profiling* ile ya kilimo na udongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile *Western highlands* W-*2, Sub zone* 13.427, kuna Wilaya ya Kasulu, Nyakanazi na Simbo. Ninataka kumkumbusha Mheshimiwa Waziri nadhani pengine haijui vizuri lakini Kigoma pia tunalima kahawa, Kasulu tunalima kahawa na kwa taarifa za *TACRI* za mwaka jana, kahawa ya Mkoa wa Kigoma ilikuwa ni kahawa bora katika nchi yetu na katika soko la kahawa. Sasa ukiangalia takwimu zile hazionyeshi kwa kina hii *profiling* inawezaje kutusaidia kuelewa maeneo ambayo kwa kweli tunaita kuwekeza katika kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Wilaya ya Kasulu, Kasulu ni kubwa sana ina *zone* tatu za kilimo. Ina uwanda wa juu wa kahawa na inauwanda wa chini ambao tunaweza tukalima pamba na mazao mengine. Lakini kwa *profiling* ile, Mheshimiwa Waziri haionyeshi hata kidogo takwimu zile zinakuwa za ku-*cut* na ku-*paste*, hazionyeshi chochote juu ya maeneo haya ambayo mlikuwa mmeya-*cluster* kulingana na hali ya hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu zaidi ya hayo, nikumbushe tu kwamba Waheshimiwa Wabunge, nadhani mtakubaliana na mimi kwamba katika *volcanic soils*, haziwezi kuwa na *low fertility*, haziwezekani. Nadhani wasomi mko wengi mnajua, maeneo yenye udongo wa volkano kwa uasilia wake huwa ni maeneo tajiri kwa ardhi. Sasa ukiangalia *profiling*, hii ni kama mtu ame-*cut* na ku-*paste* pale na huoni kama kulikuwa na *seriousness* yoyote na Mheshimiwa Waziri hata *source* haionekani, nani katengeneza hii? Huku mwanzo kote umeonyesha, angalia kwenye ukurasa wa 96 umetupa mpaka *website*, ukurasa wa 95 kuna *source* pale lakini *profiling* ya maeneo ya kilimo na hali ya hewa, hukutueleza hasa *source* ni nani? Ni watu wa Ardhi Mlingano Tanga au nani katayarisha hii? Iko *so incorrect*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kuangalia, The Ufipa Highland, ziko *very rich in soil*. Ni maeneo tajiri sana kwa kilimo yale lakini *profile* hii kwa maoni yangu na kwa heshima zote naomba irudiwe ili tupate *a proper profile* ya maeneo ya kilimo kulingana na hali ya hewa, itatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona nianze na hilo dogo ambalo niliona limekaa kushoto sana. Maeneo ya Kigoma, Kagera Rukwa, ni *very rich* kwa udongo kwa sababu yana uasili wa *volcanic soils* ambazo ni tajiri kwa kilimo. Nilifikiri nianze na hilo dogo tu ili niweze kuweka mambo sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nimevutiwa sana na ukurasa wa 66, Mapinduzi ya Kijani (*The Green Revolution).* Mimi nimefurahishwa sana katika ukurasa wa 66, 67 mpaka 70. Umetupeleka na kutuongoza vizuri kuhusu mkakati wa muda mfupi wa kuleta mapinduzi ya kijani lakini eneo hili lina mambo mengi ya jumla. Tunajipangaje na uhaba wa chakula, tunajipangaje na kupanda kwa bei za chakula?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Wizara katika ukurasa 66 mpaka 70 kwamba kwa taarifa hizi zilizomo humu ndani wangeweza wakaja na kampango hivi ka kuonyesha tunavyotoka hapa na kujihami katika tatizo hili la ongezeko la bei ya chakula na zahama hii ambayo inaikumba dunia ambapo ni chakula na mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimevutiwa sana kwa mfano na lengo la nne ukurasa wa 67, kuweka malengo ya kuzalisha yanayopimika kwa kila Mkoa na Halmashauri. Hilo lengo limenivutia sana Waheshimiwa Wabunge kwa sababu hatuwezi kuzungumza kilimo kwa ujumla wake tu. Lazima tuwe na vitu *specific* vinavyopimika kwamba kesho unaweza ukapima Halmashauri kwa Halmashauri, ukapima Mkoa kwa Mkoa na hili ungesaidia hata kuelekeza rasilimali zetu vizuri zaidi katika maeneo ambayo kuna vitu ambavyo kwa kweli viko *specific*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango ule mimi nauafiki kabisa mia kwa mia lakini ninaomba sana Mheshimiwa Waziri hebu basi mjiandae kuja na *action plan* ya kutuongoza kwamba kwa mwaka huu 2008, tunatoka hapa tulipo mpaka masika inayokuja kwa mfano ambayo kwa maeneo mengi ni mwezi wa pili au wa tatu, kuwe na kitu ambacho unaweza ukakiona ambacho kitatusaidia katika kutuongoza katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 68, Mheshimiwa Waziri amezungumzia kwamba Wizara itatilia mkazo kilimo cha mahindi katika Mikoa za Nyada za Juu Kusini na Mikoa inayozalisha mahindi, ukautaja Mkoa wa Kigoma na ni kweli. Wewe umeutaja lakini kwenye hotuba yako huu Mkoa wa Kigoma haukuandikwa, nadhani ile ni *error* tu. Sasa isije ikawa katika mipango yako unaendelea kuisahau Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni wazalishaji wakubwa sana, tunalisha Congo, Burundi na tunalisha migodi. Hii migodi yote unayoiona yote inalishwa na Mkoa wa Kigoma. Uliutamka Mkoa wa Kigoma lakini kwenye Kitabu Mkoa wa Kigoma hauonekani. Niongezee kusema kwamba kama kuna *the big four* basi Kigoma iongezeke iwe *the big five* na kama kuna *the big five* basi Kigoma iongezeke iwe *the big six.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kigoma ina hali ya hewa nzuri kwa mujibu wa takwimu za hali ya hewa. Mkoa wa Kigoma ndiyo Mkoa wa pekee ambao haujawahi kupelekewa chakula cha msaada tangu uhuru. Lakini ni ajabu hakuna mradi wowote wa maana wa kilimo umewekezwa katika hali ya hewa ya Kigoma na ardhi tajiri ya Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti nimkumbushe Mheshimiwa Waziri tu kwamba wakati umefika, wekezeni Kigoma kuna ardhi tajiri na ardhi mama iliyolala na inahitaji tu uwekezaji wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya muda haujaniishia nizungumzie huu mradi wa *DASP*. Napenda kwa masikitiko makubwa sana, nizungumzie mradi huu wa DASP. Mradi huu ni mradi ambao unahusisha Mikoa mitano ya Kigoma, Kagera, Mara, Shinyanga na Mwanza. Lakini mpango huu kwa kweli unaendeshwa kizamani sana na Mheshimiwa Wassira tumezungumza hapo nje kwa kirefu sana juu ya mradi huu, mradi huu unaendeshwa kizamani kweli kweli. Mradi uibuliwe Kasulu lakini *authority* ya kuutekeleza itoke Mwanza kilomita 800, mambo ya kizamani haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu mbuni mambo mapya ili hii *DASP* iweze kuwa na *impact* kwa wakulima na nashauri kwamba kwa mujibu wa hii ripoti ya *DASP* ambayo ni ya mpaka tarehe 14 Julai, 2008, hii project mngeitizama upya yote na mkai-*review* yote. Nina hakika na ndugu zangu wa Mikoa ya Kagera, Shinyanga na Mwanza, hii *DASP* bado inasuasua. *Impact* yake ni *negligable* kwa sababu mradi unaendeshwa kizamani, maamuzi bado ni ya kizamani, utendaji kazi wake ni wa kizamani, kwa nini msichukue *mode* ya *TASAF*, mradi kunakoibuliwa basi kunakuwa na maamuzi ya utekelezaji yanakuwa yako karibu. Sina haja ya kwenda kwenye takwimu maana mpaka sasa Mkoa wa Kigoma umepokea fedha kidogo sana chini ya mpango huu. Mradi wa bilioni 24 lakini mpaka sasa Mkoa wa Kigoma umepokea shilingi milioni 908. Mpango huu unasikitisha sana na ndiyo mradi pekee wa kitaifa ambao umewekezwa katika Mkoa wa Kigoma lakini ni mradi ambao unasuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *DASP*, ushauri wangu kwa Wizara na Serikali ni kwamba huu mradi upitiwe upya, uangaliwe ili uweze kuwa na *impact*. Lakini zaidi ya hayo, huu mradi unatumia fedha nyingi sana kwa utawala. Maana kuna *training*, *sensitization, visiting*, yote ni vitu vinavyofanana tu. Naomba sana huu mpango uweze kuwa re-*visited* ili hatimaye fedha nyingi zijielekeze kwenye maeneo yanayohitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ni huduma za ugani. Mheshimiwa Waziri, katika hotuba yako umezungumzia juu ya nia ya kuongeza Mabawana Shamba na Mabibi Shamba, ni jambo jema sana. Lakini kama ulivyosema kwenye mkakati wako wa muda mfupi basi tuwe na vigezo vya kuwapima Mabwana Shamba hawa. Tusiwe na watu ambao wamekaa tu hawana *impact* yoyote ya kuongeza tija ya kilimo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshauri Mheshimiwa Waziri, hawa Mabwana Shamba tuwe na vigezo vya kuwapima hata ikibidi waajiriwe kwa mikataba kama wanavyofanya Misri. Nchi ya Misri na Ghana, Maafisa Ugani wanaajiriwa kwa mikataba

na wanapimwa kwa vigezo vilivyowekwa na sisi tunaweza tukaanza utaratibu huo kuliko kuwa na Mabwana Shamba ambao hawana tija na unawaongeza lakini bila kuwa na mkakati sawasawa hata wakiongezeka wasiwe na faida yoyote iliyokubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, ni wataalamu wa kilimo wamejaa katika Mawizara yetu. Jamani wataalam hawa waende vijijini. Wataalam wa kilimo waliosoma hawavai suti, sasa wanavaa suti wako maofisini na wamejaa tele humo wanagombania safari na *imprest* tu humo. Waende Mawilayani wakazalishe, waende kwenye maeneo ya kilimo wakatusaidie kwenye Halmashauri zetu. Wako wengi Mawizarani na wengine kwa kusikitisha wako kwenye Sekratarieti, naona akinamama wale wananisikiliza vizuri, kuna watu wamekaa hawana hata tija wako kwenye Sekretarieti Mawizarani ndiyo usiseme, wanavaa suti kila asubuhi. Mtu umesoma Kilimo, una digrii mbili tatu unakuwa umevaa suti asubuhi? Ushauri wangu wataalam wa kilimo wapelekwe vijijini wakaongeze uzalishaji huko na hili jambo linakuwa ni la kufa na kupona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana nilikuwa na mengi lakini mengine nitachangia kwa maandishi. (*Makofi*)

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia hotuba ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika lakini nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, ni hotuba nzuri sana na Waheshimiwa Wabunge, kama kweli yote ambayo Mheshimiwa Waziri ametupa leo kwenye kitabu hiki tutayaweka kimatendo, Serikali pamoja na sisi Wabunge nina uhakika tutaweza kupiga hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuzungumze ukweli kwamba nchi yetu ni nchi ya wakulima na ili tuwakomboe Watanzania, hakuna njia nyingine yoyote zaidi ya kuboresha kilimo cha Tanzania. Nakumbuka ukisoma vitabu katika miaka ya sitini, nchi kama Indonesia, Thailand, India, Ufilipino katika uzalishaji wa mazao ya kilimo zilikuwa chini ya Afrika au zilikuwa zipo sawa na Afrika ikiwepo pamoja na Tanzania lakini leo hii ukiangalia wenzetu wa Thailand, Wafilipino, India wamekwenda juu zaidi, wako mbali *actually* wana-*export* chakula sana. Sisi Tanzania bado tuko pale pale lakini lazima tujiulize ni kwa sababu gain? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia sababu za msingi, sababu ya kwanza unaweza ukagundua ni labda mbegu bora katika ardhi ile ambayo inatumiwa. Utagundua ni matumizi ya mbolea, je, tunatumia mbolea inayofaa? Utagundua sababu nyingine ni

teknolojia lakini kubwa ambalo nitaliongelea leo ni kwamba kilimo ni vyema tukakiunganisha na viwanda kwa maana ya usindikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitaongelea kilimo lakini kilichounganishwa na usindikaji kwamba kinaleta faida kiasi gain. Lakini naomba nizungumzie hilo nikiwa ndani ya Jimbo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa siko Bungeni kwa takribani siku mbili. Nilikwenda Jimboni kwangu kwa sababu ya matatizo ya kilimo. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri, ninayoyazungumza leo, nimetumwa na wananchi wa Same Mashariki kwako na ninakusihi unisikilize vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Same ina maumbile mawili, ina tambarare na milima. Lakini milima ni zaidi ya asilimia 60 na tambarare ni chini ya asilimia 40. Wananchi wanaoishi milimani Same kote Mashariki na Magharibi, naomba nizungumze ukweli ndiyo wanaolima tangawizi nyingi mnayoiona Tanzania. Tangawizi mnayoiona Tanzania, naomba niseme kwamba kwa sababu utafiti umefanywa na *AMSDP* wakahakikisha kwamba Milima ya Wilaya ya Same ndiyo inayotoa Tangawizi nyingi iliyopo Tanzania. Ni kitu ambacho kimefanyiwa utafiti wa ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo sasa kwenye tangawizi, wananchi wa Same Mashariki na Magharibi wote kwa ujumla, wanalima tangawizi lakini kwa taabu sana. Tangawizi ni zao ambalo linahitaji maji kwa wingi. Kwa hiyo, ni lazima wafanye kazi masaa kumi na sita ili wanyweshee tangawizi. Inapokuwa kwenye bei, kilo Sh.50/- au imezidi sana kilo Sh.200/-.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimelia kwenye Bunge hili, nimepiga makelele, nimekwenda kwenye Halmashauri kwa sababu wananchi hawana mahali pa kulilia lazima walilie kwa Wabunge. Tumezungumza kwenye Halmashauri, ila naomba leo nizungumze ukweli nikiwa kidogo nimepata faraja, niishukuru sana Halmashuri ya Wilaya ya Same, *AMSDP,* naomba nirudie tena, niishukuru sana *AMSDP*. Nimshukuru Mkuu wa Wilaya yangu ya Same, Ibrahim Marwa na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro ambao wamesikia kilio cha wananchi wa Same Mashariki milimani na Same Magharibi milimani na kutupa mawazo ya kwamba ni lazima sasa tujenge kiwanda cha kusindika tangawizi ile ambayo ni *organic* jinja. Sio hizi tangawizi ambazo zimemea kwa mbolea zenye kemikali hapana! Ni ile tangawizi ambayo ni ya kilimo hai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa, naomba Serikali isikie kwamba tumeanza ujenzi wa kiwanda cha kusindika tangawizi yetu. Tumeanza kwa nguvu za wananchi na Tarafa inayoongoza inaitwa ni Tarafa ya Mamba Vunju. Inalima tangawizi miezi kumi na mbili katika mwaka, inavuna tangawizi kuanzia mwezi Januari mpaka Disemba. Kwa hiyo, pale sasa ikabidi tupaweke *centre*. *AMSDP* baada ya kufanya *research* kupitia Akilimali, wakaona kwamba tujenge kiwanda pale, wakatupa michoro na tutaanza ujenzi

wa kiwanda hicho. Mheshimiwa Waziri nimekuletea picha ya hatua gani tumefikia mpaka sasa hivi wa ujenzi wa kiwanda hicho. Naomba kupitia kwako Mwenyekiti picha hizi zimwendee Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

(Hapa Michoro ya Kiwanda Husika Ilitolewa)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini imebidi tuunde ushirika ambao una vikundi 21. Wakulima wa tangawizi 2000, tumeweka mikakati kila mwanaushirika mmoja alipe Sh.15,500/-, Mheshimiwa Mbunge nikachangia shilingi milioni 2/-, maana sina Mfuko wa Jimbo. Nikachangia hiyo milioni 2/-, mifuko 200 ya *cement*, mabati 300 na kofia 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikwambie na niiambie Serikali, upande wa jengo la kiwanda hiki wananchi pamoja na mimi Mbunge, ikifika Desemba tutakuwa tumemaliza hili jengo. Litakuwa limekamilika tunangoja kuweka mitambo na kuanza *production*. Lakini wananchi tunahitaji pia na msaada kutoka Serikalini, kiwanda kile kwa mzunguko mmoja wa miezi mitatu kinahitaji bilioni 1.3/-. Lile jengo tumenunua kiwanja wenyewe, tukimaliza jengo tutakuwa tumemaliza milioni 40 ambao utakuwa mchango wa wananchi pamoja na Mbunge wao lakini sasa lazima Serikali ikubali kwamba nitaomba kiasi kidogo hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye Ilani ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 ukurasa wa 28 kifungu kidogo cha (n) kinasema hivi:-

"CCM itazitaka Serikali kuhamasisha na kusaidia uanzishwaji wa viwanda vya usindikaji na ufungashaji wa mazao ya kilimo kwa lengo la kuyaongezea thamani, kuvutia soko na kupunguza uharibikaji na upotevu." Tunatekeleza Ilani ya uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hawa watakuwa wamechangia milioni 40. Sasa vyanzo vya mtaji; Halmashauri ya Wilaya ya Same imetuchangia milioni 50 na naishukuru sana. Tunaomba kutoka Wizara ya Kilimo, kwa unyenyekevu mkubwa kwa heshima na taadhima, mtuchangie milioni 300/-. Naiomba Wizara ya Viwanda na Biashara kwa unyenyekevu mkubwa, ituchangie milioni 200/-. Narudi TAMISEMI, tunaomba mchango wa milioni 100/- kwa sababu hata mtoto anayebebwa ambaye anamshikilia mama yake mgongoni ndiye anayebebwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wananchi wamejitahidi. *SIDO* Kilimanjaro kwa sababu ndiyo watakao *supply* mitambo, hatununui mitambo nje tunashirikiana na *SIDO*; wao wanatuchangia milioni 20/-. Faida Mali, wanatuchangia milioni 30/-, Fomu ambao ndiyo walikuja kuangalia ubora wa ile tangawizi wakagundua kwamba ni *organic*, wamekubali kutuchangia milioni 20/- *Board of External Trade* ambao nao wamechangia kututafutia masoko, wametuchangia milioni 20/- yote haya yapo kimaandishi pamoja na kwamba tutaingia Benki kukopa shilingi milioni 250/-. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshapata soko la tangawizi yetu ambalo tayari wanangoja tuanze *production* wanunue kutoka kwetu. Soko hili ni la uhakika kwa sababu limefanyiwa na wenyewe *AMSDP*. Tuna soko la Ufaransa kampuni inayoitwa *Unifine Co. Ltd*. ambao wao wamesema watakuwa wanachukua tani 25 kwa mwezi lakini watachukua katika *chips.* Nimeleta mfano *chips* hizi na nitaomba vyote hivi vimfikie Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda cha kutengeneza *Biscuit* cha Jambo cha Nairobi, watachukua tani 1.5 ya unga kwa mwezi ambao tulishaanza kutengeneza (*local*) kienyeji kule Miamba na nitaomba Mheshimiwa Waziri aone. Kampuni ya *TATEPA* tani 156 ya unga kwa mwezi. Hizi ni *order* ambazo zina uhakika. *Super Market* za Moshi, Arusha na Dar es Salaam, tani 13 za unga kwa mwezi. Kwa Zanzibar, kuna *Tanzania Zanzibar Organic Product (TAZOP*), nao wamesema watakuwa wanahitaji tani 40 za *chips* kwa mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kuwanyanyua hawa wananchi kutoka pale walipo, tumeona hakuna njia nyingine ni lazima tujenge kiwanda cha usindikaji. Bei ambayo ipo sokoni sasa hivi ya tangawazi ya unga ni Sh.5,000/- mpaka Sh.6,000/- kwa kilo. Ndiyo bei ambayo tumepata lakini mwananchi anapewa kilo moja Sh.150 na mfanyabiashara mkubwa wakati kilo mbili za tangawizi mbichi ndiyo unapata kilo moja ya tangawizi ya unga. Kwa hiyo ni Sh.300/- kwa Sh.5,000/-, ndiyo maana tumeona hakuna njia ya kuwakomboa wale wananchi ni lazima tujenge kiwanda hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali katika hili hebu jamani tuwakomboe wale wananchi wa Same milimani kilio chao ni kikubwa. Wanalima kwa masaa kumi na sita lakini wanaishia kuwa maskini kuzidi kiasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nimepata faraja kumsikia Mheshimiwa Rais akiwa Tanga kwamba ameona ni muhimu kujenga pia kiwanda cha usindikaji machungwa yanayooza Tanga lakini ukienda Geita tena, tatizo ni hilo hilo, mananasi na maembe yanaoza Geita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naomba tuzungumze kwa ujumla kwamba kilimo kitakachowakomboa Watanzania hebu tukiunganishe na usindikaji, tukiunganishe na viwanda. Mheshimiwa Waziri iwapo utasimama imara katika kuunganisha kilimo na usindikaji, tutakuwa tumewakomboa Watanzania kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili la kiwanda, naomba Serikali inisaidie sana. Mimi sina zaidi ya kuchanga milioni 2/-, nimechanga mifuko 200 ya *cement*, mabati 300 na kofia 100, sina Mfuko wa Jimbo, ndiyo Wabunge sasa muone umuhimu wa Wabunge kuwa na Mfuko wa Jimbo. Ningekuwa na Mfuko wa Jimbo, ningeelekeza nguvu zangu zote, pesa zote kwenye ujenzi wa kiwanga hiki. Kwa sababu kitakuwa si kiwanda cha pale Same Mashariki tu, kitakuwa kiwanda cha nchi nzima kwa sababu sehemu zote

ambazo zina tangawizi ya unga ni watu wanatengeneza kienyeji lakini hakuna mahali penye kiwanda cha kimataifa cha kutengeneza tangawizi ya unga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niihakikishie Serikali kwamba tumejizatiti kutengeneza *packaging* nzuri ambayo itafanana sawa na hii ambayo tuna-*import* kutoka *South Africa*. Tutapenya kwenye soko la nje kama ambavyo tumepata *order* na kwa jinsi ambavyo tangawizi yetu ina hadhi ya juu, tutakuwa tuna uwezo wa kupata soko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. YUSUF R. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekaa muda mrefu sana bila kuzungumza, nilikuwa shuleni, maana sisi tuliozoea kuzungumza kwenye mikutano ya hadhara inayotawaliwa na maneno ya "pasua baba", ukiingia hapa unaweza kuharibikiwa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kuzungumza katika Bunge hili Tukufu, naomba nichukue nafasi hii, kwanza, kumshukuru Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuniteua kuwa Mbunge. Deni la fadhila hulipwa kwa fadhila. Nina deni kubwa sana kwake, natafuta namna ya kulilipa, sijui nitalilipaje lakini nafikiri namna nzuri ya kulipa deni hili ni kujitahidi kwa uwezo wangu wote kuitumikia nchi yetu na Chama changu kwa bidii zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma Maandiko Matakatifu ndani ya Biblia yanasema:-

"*Anayetamani Uaskofu, anatamani kazi njema*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo nazungumza Spika hayupo, lakini nafikiri yatamfikia. Kama anayetamani Uaskofu anatamani kazi njema, basi anayetamani Uspika, naye anatamani kazi njema, lakini ni ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nichukue nafasi hii kumpongeza Spika na mimi naridhika na namna anavyotuongoza. Nafurahi hasa kwa kuzingatia kwamba ni Spika anayetoka Chama changu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vile vile nichukue nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda, kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu. Siku njema, huonekana mapema, ameanza vizuri! Labda niseme tu kwamba pengo la jino la dhahabu limezibwa kwa jino la dhahabu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Nabii Yeremia anapewa unabii, aliogopa sana, lakini Mwenyezi Mungu akamwambia usiogope, nitatia maneno yangu katika kinywa chako na wewe utazungumza kwa niaba yangu, ndipo Yeremia akapewa Utume. Kwa hiyo, Waziri Mkuu hayupo lakini nataka nimwambie kwamba asiogope, huyo anayemteua kwa kawaida huweka maneno katika kinywa chake ambaye ni Rais na Chama chake. Kwa hiyo, mimi nafikiri atafanya vizuri, tumtie moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uniruhusu vile vile na mimi niwashukuru Wabunge wa Chama changu. Ninapotembelea Jimbo langu la Uchaguzi, ninawakuta huko, wanajitahidi sana katika kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Mimi nataka niwaondoe hofu, tukienda namna hii, mwaka 2010 kazi ni rahisi. Tukiendelea namna tunavyokwenda hivi sasa, kazi yetu mwaka mwaka 2010, ni rahisi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naomba na mimi niseme mambo machache na wala sitasema mambo makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, mtaniwia radhi, Mzee Ngombale alipokuwa anachangia hapa Bungeni, alisema anaipongeza Serikali ya Awamu ya Nne, kwa kazi nzuri inayoifanya na hasa Mheshimiwa Rais kwa kusimamia utekelezaji wa Ulani ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku mbili baada ya hotuba ya Mzee Ngombale, alisimama Mbunge mwingine (kwa staili ile ya waandishi wa habari, jina ninalo), akasema sisi wenzenu wa Kambi ya Upinzani, masikio tunayo, macho tunayo na midomo tunayo. Haya tunayoyasema, tunayaona, haya tunayoyasema tunayasikia, akamaliza, asubuhi yake gazeti liliandika, “Mzee Ngombale awekwa kitanzini”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa na mimi nataka niseme, unaweza ukawa na macho, unaweza ukawa na masikio, lakini unapoona mambo mazuri yanayofanywa na Serikali ya CCM, unaweza ukayafumbia macho tu usione. Unaweza ukawa na masikio, lakini ukayaziba, ukayatia hata na pamba ili usisikie mambo mazuri yanayozungumzwa juu ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Hata ukaambiwa kwamba pale Dodoma kinajengwa Chuo Kikuu, unaweza lile jengo ukalipa kisogo usilione. Unaweza hata kitabu kizuri hiki cha bajeti tuliyosomewa leo, mipango mizuri hii ya kilimo usiione, ukaona Ibara moja ndogo tu ambayo kwako unaona ina upungufu, ukakazana na hiyo, ukashindwa kujua kwamba hotuba yote hii imetengenezwa kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndugu zangu kuwa na masikio si hoja, kuwa na macho si hoja. Sasa ninachotaka kusema ni kwamba ukijua kulaumu, ujue kusifu, vinginevyo wenzako watakwambia una kilema. Maana yale unayoyasema hayafanyiki?

Yanafanyika hata kwenye Jimbo lako, watu wako wanaona, wewe huoni! Nafikiri mmenielewa! Nasema ukijua kulaumu, ujue kusifu, vinginevyo utaambiwa una kilema!

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, nataka sasa nimpongeze Mheshimiwa Rafiki yangu Wasira kwa hotuba nzuri na ili nisije nikasahau, basi naunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, humu ndani tunaye bingwa wa kuandika maandiko mbalimbali ya Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Ngombale-Mwiru. Tulianza mwaka 1972 na Siasa ni Kilimo, kitabu ninacho hapa lakini kabla ya mwaka 1972 kulikuwa na Mwongozo wa 1971 umezungumza kilimo. Azimio la Iringa limezungumza kilimo, Sera za CCM katika miaka ya 1990, zinazungumza kilimo, Ilani ya Uchaguzi ya Chama chetu, inazungumzia kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniruhusu nilitazame lile Azimio la Iringa la Mwaka 1972, Ibara ya 36, inasema hivi:-

"*Watumishi wa kilimo hawawezi kuwepo katika kila kijiji wakati ule ule wanapohitajika, lakini maarifa ya kilimo lazima yaenezwe kila mahali hivi sasa, 1972"*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio hilo hilo la Iringa katika Ibara ya 36, linasema:-

"Kazi za viongozi ni nne. Ya kwanza, wajifunze wao wenyewe kanuni za kilimo".

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi humu ndani tunatakiwa tujifunze sisi wenyewe kanuni za kilimo. Sina hakika Wasira unazijua kwa kiasi gain, nimemtaja ni rafiki yangu, hatanipeleka kokote!

"*Pili, wawaeleze wananchi kwa nini kilimo cha kizamani hakifai tena na kuwafanya wakulima wawe na hamu ya kujifunza na kutumia maarifa mapya. Tatu, kuhakikisha pembejeo na zana nyingine zinawafikia wakulima kwa wakati unaofaa"*.

Hivyo ndivyo tunavyoelekezwa kwamba sisi wenyewe tujifunze kanuni za kilimo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma hotuba iliyotolewa hapa, ukurasa wa 20, Ibara ya 31, Waziri anatuambia mwaka 2007/2008 wataalam wa ugani 309 waliajiriwa, lakini lengo ni 2500, hawatoshi. Nafikiri hata ukifikisha lengo hili la 2500, nafikiri namna nzuri ambayo tunaweza tukafanya ni viongozi kujua kanuni za kilimo. Nchi hii ina viongozi

wengi sana, viongozi wa CCM wanaanzia kwenye Shina, Kata, Wilaya, Mkoa. Kwa maelekezo ya kitabu hiki ni kwamba sisi wenyewe lazima tuongoze kwa mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ukilitazama shamba la rafiki yangu Siraju, ni mfano, watu wako wanaweza wakaja wakajifunza kwenye shamba lako? Usikasirike, wewe ni mtani wangu! Shamba la rafiki yangu Lowassa, ng'ombe nakubali, maana ng'ombe wako nimewaona lakini shamba lako je? Shamba la rafiki yangu Kapuya, ni mfano? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichukue nafasi hii, Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwasihi, tunaandika sana, tunasema sana, lakini tatizo ni kwenda kutekeleza yale ambayo tunayasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kitabu cha Mathayo 23 kinasema:-

"Maneno ya Makuhani hawa na Mafarisayo, yasikilizeni kwa sababu wamekaa katika kiti cha Musa, lakini kwa mfano wa matendo yao msifuate. Wananena, hawatendi, wanawatwika watu mizigo mikubwa, wenyewe hawagusi hata kwa vidole".

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya *Quran* maneno hayo yamo. Kwa wale wenzangu waliobobea, akina Siraju, wanajua, yanasema:-

"Yaa-ayyuha Illadhiina aamanuu limaatakuluu na maalata f-aluuna. Enyi mlioamini mbona mnasema maneno ambayo ninyi wenyewe hamtendi?".

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi tunazungumzia kilimo, mashamba yetu mabaya na wananchi wanatusikiliza hapa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya CCM katika miaka ya 1990 inasema hivi:-

"Kwanza, Serikali inatakiwa kutambua na kuwaenzi wakulima wa mfano. Pili, kuanzisha mashindano ya kilimo. Tatu, kuwatumia wakulima bora kuwafundisha wakulima wengine".

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata wale wakulima bora ambao tulionao wanaweza kuwa Maafisa Ugani kwa kuwafundisha wakulima wengine, wapo? Kwenye mashindano ya Nane Nane, *TASO* inaendesha mashindano, wanapatikana wakulima bora kutoka kila vijiji na kata, lakini je, wanaporudi kule, tunawaenzi? Je, tunawatumia kuwafundisha wengine? Hatufanyi hivyo! Lakini maandiko yako pale, kila mtu akiandika, anaya-*quote*, kuyatekeleza hamna! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Uchaguzi ya 2005, Kifungu cha 31(e), kinazungumzia zawadi, tuzo kwa Mikoa na Wilaya. Inasema hivi:-

"Serikali itatakiwa kuhimiza kutoa vivutio, zawadi na tuzo kwa Mikoa na Wilaya ambazo wakulima wake wataweza kuongeza maradufu tija na mazao yanayovunwa katika heka katika kipindi cha Ilani hii. Msisitizo utawekwa kwenye mazao ya mahindi, mpunga, migomba, kunde, tumbaku, chai".

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaendelea sura ya 9 ya Ibara ya 132, inasema:-

"Viongozi waongoze mapinduzi ya kilimo kwa kutenda wao wenyewe".

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo Mikoa ambayo tayari imekwishaonyesha mfano katika uzalishaji wa mahindi; Rukwa, Mbeya, Iringa na Ruvuma, sikumbuki, labda Wiziri atakapohitimisha atuambie, mmewatia moyo kwa tuzo gani?

(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Makamba, hiyo ni kengele ya pili, mchango wako ni mzuri sana, lakini muda tu.

MHE. YUSUFU R. MAKAMBA: Nilikwisha unga mkono hoja!

MWENYEKITI: Tunashukuru sana kwa hilo!

MHE. YUSUFU R. MAKAMBA: Ahsante sana! *(Makofi)*

MHE. BUJIKU P. SAKILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi nichangie katika hoja hii ya Wizara ya Kilimo. Kwanza, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea mambo mawili tu nayo ni kilimo cha pamba na upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuendelea, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri sana. Naamini kwamba haya aliyoyasema yakitekelezwa vizuri, tutasogea mbele kidogo. Nampongeza yeye, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hii walioshiriki katika uandaaji wa hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha pamba. Pamba inalimwa kila mwaka. Pamba kilimo chake chote kina shughuli tisa na gharama yake ni kama shilingi 240,000/=. Kinachosikitisha sana ni bei ya pamba. Mwaka huu pamba inanunuliwa kwa Sh.400/500, kwa kilo. Kwa wastani, ekari moja inatoa kama kilo Sh.300/400. Tufanye hesabu, utaona kwamba fedha hiyo hairudishi gharama ya mkulima kwa ekari moja. Ili mkulima aweze kupata faida kidogo, apate angalau kilo 600 - 1000 kwa ekari. Lakini, mazingira ya kilimo hiki cha pamba hasa katika Kanda ya Ziwa, bado hatujafika katika

kiwango hicho cha kilogramu 600 – 1000, kwa hiyo, mkulima analima kwa hasara. Sababu zinazochangia, ni mbegu na dawa zinachelewa kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha pamba ni cha mwezi mmoja au miwili. Tarehe 15 mwezi wa kumi na moja mpaka tarehe 15, ukichelewa sana, mwezi wa kwanza, ukicheleweshe mbegu kipindi kile, kilimo kitakuwa cha bahati nasibu, mapato yatakuwa duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa wale watu wote wanaohusika, wajaribu kufuata majira ya kilimo cha pamba, mbegu zifike mapema, dawa zinapohitajika ziweze kufika mapema ili angalau kuweza kuongeza kidogo pato la pamba kwa ekari kwa wakulima ili waweze kufidia gharama wanayotumia katika kilimo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu nilipokuwa mtoto mdogo, nimeona watu wanalima pamba mpaka leo watu bado wanalima. Sijaona mabadiliko makubwa sana, sijaona kama kilimo kimekuwa bora au kipato kimeongezeka sana! Inafika wakati mtu unajiuliza, hivi kweli kuna sababu yoyote ya kuendelea kulima pamba? Kwa nini Serikali isikubali kuwahamasisha watu walime dengu badala ya pamba? Kwa nini wananchi wasilime mazao mengine badala ya pamba? Kwa sababu kwa jinsi utaratibu wa kilimo cha pamba unavyoendelea sasa hivi, sioni uwezekano wa wananchi kuondokana na umaskini katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejiondoa katika biashara, mtu unajiuliza, hivi ni kwa ridhaa ya nani? Serikali ina wajibu wa kulinda haki za wananchi pamoja na wakulima. Hivi sasa kwa jinsi tunavyojionea katika biashara maana hata biashara ya pamba na yenyewe haiko Serikalini, maana yake nini? Maana yake ni kwamba wakulima pamoja na pamba yao, wameachwa mikononi mwa walanguzi. Walanguzi ni wajanja sana kuliko wakulima, mizani zinapunja, hakuna mtu ambaye anaangalia. Nafikiri ni vema Serikali ikaangalia kwa ukaribu zaidi, siyo kusema kwamba imeishajiondoa, huku wakulima wanaanza kuhangaika na walanguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naangalia utaratibu wa kilimo cha pamba. Katika kipindi cha kilimo, mwanchi anahangaika peke yake, labda wale ambao wanapata ruzuku ya mbolea lakini, kwa mkulima wa pamba ambaye hapati ruzuku kwa kweli, ni kama anajitegemea, gharama yote ya kilimo iko juu yake. Lakini, inapofika wakati wa kuuza, hana uwezo wa kupanga bei ya pamba yake, hapa mkulima anahitaji msaada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukombozi wa mkulima ni ushirika. Kwa bahati nzuri sana, Kanda ya Ziwa hasa Mkoa wa Mwanza tuna Nyanza. Nyanza ndiye tulitegemea kwamba angetukomboa, kwa utaratibu jinsi ulivyokuwa, hakuwa ameandaliwa kushiriki katika ushindani na wenzake, alikuwa peke yake. Ushindani umekuja, soko huria limekuja, limemkuta bado hajajiandaa kushindana, likamzidi nguvu. Madeni yakawa makubwa sana kwa Chama cha Nyanza. Nashukuru sana Serikali imejaribu kusaidia kidogo lakini bado msaada huo haujasaidia sana Nyanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu katika msimu huu wa kilimo, Nyanza iliomba shilingi bilioni sita ili iweze kununua pamba kwa wakulima. Kwa bahati mbaya sana, kiasi kile hakikukubaliwa. Nyanza ilikubaliwa kwamba inaweza kukopeshwa kiasi cha shilingi bilioni tatu. Bilioni tatu nazo hazikupatikana. Kiasi kilichopatikana kati ya bilioni sita zilizoombwa na Nyanza ni bilioni moja tu na ikapewa masharti kwamba utakaponunua pamba ya kutosha kwa hiyo bilioni moja, tunaweza kukutafutia pesa zingine kama asilimia 60 ya bilioni moja. Hapa mtu anafikiria kwamba wanunuzi wengine watasimama? Kwa sababu katika ushindani unaweza kununua ile pamba ya bilioni moja, ukakuta pamba imeisha!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri, kwa sababu tunasema kwamba watu wajiunge katika *SACCOS*, wajiunge katika Ushirika, vyama hivyo vya ushirika vinavyopatikana, basi tujitahidi sana kuviunga mkono. Wakiomba bilioni sita, wapewe bilioni sita, wakiidhinishiwa bilioni tatu, wapewe bilioni tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye upungufu wa chakula. Wizara hii ili iwe imefanya kazi, haina budi kuhakikisha kwamba wananachi wanapata chakula cha kutosha. Mimi ninapenda kuuliza, hivi wakulima wakubwa wako wapi? Kiko wapi kilimo cha kisasa? Naomba kufahamu, Maafisa Ugani wako wapi? Hatuwezi kubadilisha kilimo bila Maafisa hawa kuwa katika vijiji vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Wizara ijipange upya ihakikishe kwamba wataalamu hawa wanafika vijijini wakawasaidie, kwa sababu kama nilivyosema kilimo cha pamba mimi nimekiona tangu nilipokuwa mtoto mpaka leo hii, lakini hakijabadilika sana na sana hata mapato yake bado ni yale yale. Mimi naamini kwamba kama wataalam watafika vijijini, wakawa karibu sana na wananchi, inawezekana kabisa wananchi wanaweza kunufaika na utalaam huo, wakaongeza mazao na wakapata kipato kikubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwa upungufu wa chakula, inawezekana labda, mimi naamini kwamba Wilaya ya Kwimba tayari imeishasema kwamba ina upungufu wa chakula. Naomba sana sana Mheshimiwa Waziri, maombi haya kama yameishafika mezani kwako, uyasimamie haraka. Watu wana shida ya chakula, naomba sana hilo jambo lisichelewe sana. Kuna maeneo mengi sana ya wakulima ambayo hayakupata chakula cha kutosha na si vyema tukasubiri mpaka dakika ya mwisho ndiyo tuanze kukimbizana, chonde chonde Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Asante sana! *(Makofi)*

MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu.

Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kalambo, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, kwa jinsi alivyowasilisha hotuba yake ya bajeti

leo hii. Niwapongeze Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu na wataalamu wote wa kilimo kwa jinsi wanavyosimamia suala hili la kilimo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kina wakulima wadogo wadogo ambao ni karibu asilimia 85 katika nchi yetu hii ya Tanzania. Lakini, jambo la kusikitisha ni kwamba kwa muda wote huu toka tupate uhuru, tumekuwa tukizungumza habari ya kuboresha kilimo katika nchi hii na kuboresha zana za kilimo lakini asilimia yote hiyo 85 wanatumia zana duni. Ni jambo la kusikitisha bado wanatumia jembe la mkono na bado wanatumia zana zile za kuvunia ambazo ni duni. Kwa kweli kilimo chetu bado ni cha kijungu jiko, ni kile cha kuvuna na kula tu lakini, hatuna uwezo wa kuweka akiba kubwa. Hili ni tatizo, ni lazima Wizara hii iangalie ni jinsi gani ya kuboresha kilimo chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Rukwa, wananchi wamejitahidi sana kwa asilimia 78 wanatumia maksai, wanatumia ng'ombe wanaokokota majembe kwa ajili ya kilimo. Hii ni hatua nzuri na Mikoa mingine tayari nayo pia inaendelea kuiga kilimo hiki, Mbeya, Iringa hata Kigoma wanaanza kuiga, wanafanya hivyo. Inabidi sasa Wizara ya kilimo ihimize kilimo cha majembe ya kukokotwa na wanyamakazi kwa sababu hii ni njia mojawapo itakayotukomboa katika kilimo chetu ambacho tunakiendesha katika nchi yetu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi cha chakula tunachokihitaji ili tuweze kulisha watanzania waliopo katika nchi hii na hasa wanaoongezeka kila mwaka aslimia 3 kwa nchi nzima, ni jambo ambalo linahitaji kilimo kiwe endelevu na kiwe ni kile kinachozalisha chakula cha kutosha. Bila kuendelea kutoa ruzuku katika mbolea, tutaendelea kupata matatizo kwa sababu hata akiba ya chakula kinachowekwa na Serikali hakitoshi hata kidogo ni sawa sawa na familia tu ambayo wanajitunzia chakula ambacho kitwasaidia wakati wa njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoweka akiba ya chakula tani laki moja na hamsini elfu kwa nchi nzima hiyo si chochote kwa sababu nchi hii tungeweza kuwa tunazungumzia kuweka tani milioni moja, milioni mbili za chakula cha akiba, hapo tutakuwa tumefikia hatua nzuri lakini tutafikia hapo tutakapotekeleza kama Mheshimiwa Waziri alivyozungumza juu ya suala la kutekeleza Mapinduzi ya Kijani *(Green Revolution).* Katika nchi hii, tukiweza kutekeleza *Green Revolution* kama alivyozungumza Mheshimiwa Waziri, ndiyo tutafika wakati tutakapoweka chakula cha kutosha kwa ajili ya kusaidia nchi hii, tunapopatwa na matatizo ya njaa, lakini kila mwaka tunazungumza habari ya njaa angalia kiasi cha mazao yanayozalishwa na yanayotunzwa, bado tupo mbali na ni lazima tujitahidi kuweza kuzalisha zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mbolea tumekuwa tukilizungumza kila mwaka. Mheshimiwa Waziri hapa amezungumza hatua mbalimbali zitakazochukuliwa na mbinu mbalimbali atakazozitumia ili tuweze kusambaza mbolea, lakini inasikitisha nchi hii tunayo madini ya *phosphate* pale Minjingu, Mbeya, Mpanda hasa katika eneo la Karema karibu na kijiji cha Kaparamsenga, kwa bahati mbaya Serikali wala haijajishughulisha kwa namna yoyote ile si Wizara ya Viwanda wala si Wizara ya Kilimo wala Wizara yoyote, madini haya hatujayatumia kiasi kinachohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutafute jinsi ya kuweza kutumia madini ya *phosphate* yaliyopo Mpanda na Mbeya kwa ajili ya Nyanda za Juu Kusini ili watu waweze kuzalisha mazao mengi zaidi, hatuwezi tukaendelea kuagiza mbolea kutoka nje wakati sisi wenyewe tuna mbolea na hawa wenzetu tunaoomba watupatie misaada ili tutafute mbolea wanatucheka. Kila mwaka mbolea katika Mkoa wa Rukwa haitoshi, mbolea katika Jimbo langu la Kalambo ambalo wanalima sana mahindi haitoshi siku zote, kwa nini wakati tunayo madini ya *phosphate* ambayo yanaweza kusaidia kuzalisha mazao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali iamue kutumia madini ya *phosphate* yaliyopo humu ndani, kutumia gesi iliyopo Songosongo, iliyoko *Mnazi bay* ili tuweze kupata mbolea yetu sisi hapa hapa, ili kumsaidia mkulima wa Tanzania na hasa katika Mikoa ya Magharibi ambayo haijafikiwa na miundombinu kiurahisi.

Mhehsimiwa Mwenyekiti, ni vizuri kabisa Wizara hii ya Kilimo ifikirie kuwa na Benki ya Mkulima badala ya kuwa na mifuko. Tukiwa na Benki ya Mkulima ikasambaa nchi nzima, tutaondokana na suala la Mfuko wa Pembejeo ambao uko Dar es Salaam, wananchi wote nchi nzima waende wakasongamane pale Dar es Salaam kuomba mikopo hiyo kutoka kwenye mifuko.

Mhehsimiwa Mwenyekiti, kama benki zimesambaa Mikoani, haya yote yanaweza kufanyika katika Mikoa hiyo na kupata fedha na mikopo midogo midogo ili waendeleze kilimo lakini hii ya kufuata Mifuko Dar es Salaam, tutaendelea kupata kiasi kidogo.

Mhehsimiwa Mwenyekiti, mbolea ya ruzuku wanaofaidi, ni wafanyabiashara wa kati ambao wanachukua mbolea hii wanaifanyia wanavyotaka. Wengine si waaminifu wanachukua mbolea badala ya kuifikisha katika Mikoa waliyopangiwa, wanaipeleka nje ya nchi wanakwenda kupata fedha nyingi zaidi. Hili ni tatizo, ni lazima tujidhatiti kuweza kuondokana na tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo matatizo ya wadudu wanaoharibu mazao kama mahindi lakini madawa nayo hayapatikani mara nyingi kwa wakati ili kuweza kutunusuru wakulima ili wapate dawa hizo. Mwaka huu katika Jimbo langu la Kalambo, tumepata matatizo ya wadudu wanaoshambulia maharagwe ambao yananyauka na kubadilika rangi na yanadumaa lakini Maafisa Ugani hawakuwepo kuwashauri wananchi watumie aina gani ya dawa zile ambazo zinafaa kwa mazao haya. Tumepata hasara kubwa sana, wananchi wamelima sana lakini mazao mengi yameharibika kwa sababu hatukupata ushauri wa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia lipo tatizo la madawa tunayopewa, madawa mengine tunayoletewa siyo mazuri ndiyo maana tunashauri wakati mwingine hata dawa za *DDT* nazo zianze kuletwa. Kama zikitumika katika kiwango kinachoshauriwa, tunaweza tukaua wadudu ambao wamesambaa. Hivi sasa wapo watu wanavuna mazao shambani wanakuta tayari yameshatobolewa yakiwa shambani, hii si hali nzuri tunakwenda mahali pabaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la umwagiliaji ingawa najua suala la umwagiliaji liko katika Wizara nyingine lakini Wizara ya Kilimo maeneo ya umwagiliaji yakishaongezeka wazalishaji wataongezeka na mazao yataongezeka.

Mhehsimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Kalambo, wakulima wanalima kilimo cha kiangazi, wanalima katika mabonde, nimeomba fedha kutoka Wizara ya Maji, ili niweze kufufua mradi ule wa Katuka ambao ulikuwa umeachwa kwa kipindi kama cha miaka mitatu, ninawashukuru sana pamoja na kwamba Wizara haijafika lakini nimeona dalili kwamba fedha zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

Mhehsimiwa Mwenyekiti, lakini upo mradi mwingine pia katika Wilaya ya Mpanda ambao nao pia ulikuwa umetelekezwa, kwa hiyo, tunaomba miradi hii ikamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mradi wa Msanzi naomba pia upatiwe fedha pamoja na mradi wa Singiwe na Kasanga. Miradi hii ikiweza kupatiwa fedha, nina uhakika kabisa, wananchi katika Jimbo langu watazalisha zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamegundua kilimo cha kiangazi ambapo wanavuruga ile ardhi mara kwa mara baada ya kuvuna, unyevunyevu unaanza kupanda, wanaita kilimo cha Fuga Unyevu. Kilimo hiki kinasaidia wakulima katika Mkoa wa Rukwa kuweza kupata mazao mara mbili na mazao haya yanayopatikana wakati wa kiangazi hayana wadudu wa kutoboa mahindi wala kuharibu mahindi. Hivyo, wanapata mazao mazuri ambapo wanapouza wakati njaa imeongezeka, wanapata fedha nyingi sana na wengi wanajenga nyumba bora na kujipatia vifaa vya nyumbani. Nawapongeza sana wananchi wangu katika Jimbo la Kalambo, naomba waendelee na kilimo hicho lakini tunaomba na wataalamu wajifunze ili waweze kuona kama kilimo hiki kingeweza pia kuendelezwa katika maeneo mengine kwani ni kilimo kinachosaidia sana kupata mazao mengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la zana za kisasa, katika Mapinduzi ya Kilimo ya Kijani *(Green Revolution)* bila kuwa na zana bora za kilimo, tuwe na matrekta ya kutosha lakini si suala la kulima mashamba makubwa bila ya kuwa na uwezo wa kuyavuna inakuwa ni matatizo pia. Tunaomba pia Wizara hii iangalie jinsi ya kuweza kuwakopesha wakulima, wale ambao wana uwezo wa kulima zaidi wawe na mashine zile ambazo zitasaidia katika kuvuna mahindi, maharagwe, ngano ili waweze kupata mazao mengi zaidi. Hivyo suala la mapinduzi ya kilimo ni lazima yaambatane pia na uzalishaji pamoja na kuwa na zana za kisasa za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara ni lazima ijaribu kuwashawishi wakulima watumie mbinu ipi kutunza mazao yao, kwa sababu siku hizi kuna mifuko ya kutunzia mahindi, haya ni *synthetic fibres* ambazo zimetengenezwa na magunia ya kamba ambazo zinaharibika baada ya muda mfupi. Lakini yapo magunia ya katani ambayo yamezoeleka na wakulima lakini haya hatuyaoni tena na ndiyo magunia mazuri kwa sababu yanatunza mazao vizuri na hewa inaingia vizuri. Haya magunia yanayoletwa ya kamba hizi ambazo

ni *synthetic* hayasaidii sana, mazao yanapata joto sana yanapotunzwa na yanaharibika haraka sana. Tunaomba tuweze kuletewa magunia yale katika Mkoa wa Rukwa na hasa katika Jimbo langu ili yaweze kutunza mazao hasa tunapoyaweka katika maghala yetu.

Mheshimiwa Spika, suala la upotevu wa chakula tunapokusanya chakula mashambani, tunapotunza katika ghala zetu na kusafirisha, kwa kweli mazao mengi yanapotea. Wataalamu wanasema asilimia 30 ya chakula kinachovunwa kama mahindi mpaka yafike sokoni na kuweza kutumika na mlaji inakuwa imeshapotea, inapotea shambani, inapotea katika ghala, magari yanayosomba mahindi katika magunia haya, magunia yanatoboka halafu mahindi yanamwagika njia nzima unakuta ni mahindi hivyo tunapoteza chakula kingi. Tutafute jinsi ya kuzuia hii asilimia 30 isiendelee kupotea kwa sababu nayo ni hasara kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya mazao yetu, tunaomba masoko ya mahindi, masoko ya alizeti kwa sababu wakulima wanalima lakini unakuta wanapata bei ambayo hairidhishi. Katika Jimbo langu, tunalima alizeti, karanga tena tunalima kwa kilimo hai ambayo ni *organic farming.* Katika Kata ya Mtai, *organic farming* imeanza. Tunaomba *organic farming* ienezwe katika Kata nyingine ili tuweze kupata bei nzuri kwa alizeti, karanga na mazao mengine ya mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia suala la kuhitaji umeme katika Jimbo la Kalambo, ni ili tuweze kusindika mazao yetu tunayozalisha, bila umeme, hatuwezi kusindika. Wengine wanazungumzia habari ya kujenga viwanda lakini mimi siwezi nikazungumza habari ya kujenga kiwanda katika Jimbo langu la Kalambo kwa sababu sina umeme wa kuaminika na ule unaotoka Zambia tunajua matatizo yake. Tunaomba tupate umeme huo ili tuweze kusindika mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru sana *Energy Milling* pale Sumbawanga, wameanza suala la usindikaji wa mahindi, tunapata unga safi katika *grade* mbalimbali na unauzwa sehemu mbalimbali, hii itaongeza bei ya mahindi lakini tunaomba na hawa watu wa *Energy Milling* pamoja na wengine wanaojiingiza katika suala hili, waweze kuwapatia wakulima bei nzuri ya mahindi ili na wao waweze kufaidika na bei hizi kwa sababu wasipopata bei nzuri wakati gharama za ukulima zimeongezeka na mafuta yamepanda bei na kila kitu kimepanda bei wakulima wanaumia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimkumbushe Mheshimiwa Waziri aweze kuona jinsi ya kuweza kuchukua hatua juu ya suala la kuanzisha Benki ya Wakulima itakayosambaa mpaka kwa wakulima kulikokuwa na mifuko ambayo wakulima wa kawaida hawawezi wakapata mikopo kutoka kwenye mifuko hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ahsante sana.

MHE. LEDIANA M. MG'ONG'O: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Kilimo, kwa kazi nzuri na maandalizi mazuri ya hotuba hii yenye mchanganuo mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nichukue nafasi hii kuwapongeza wataalamu wa kilimo wote popote walipo, kwa kazi nzuri wanayofanya kumwendeleza Mtanzania katika suala la kilimo ili kuhakikisha kwamba Watanzania tunakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuchangia kuhusiana na suala la mbolea. Nikiangalia Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ambayo ni Iringa, Mbeya, Rukwa na Ruvuma, Mkoa wa Iringa katika Wilaya nyingi sasa hivi tunavyozungumza hasa Wilaya ya Makete, wananchi tayari wameshaanza maandalizi ya kilimo cha msimu unaofuata lakini mbolea haipo, wanalima bila mbolea. Wakati mbolea inapokuja kutolewa wanakuwa wamechelewa na matokeo yake wanapata mazao pungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa kwamba mbolea sehemu nyingine imeshapelekwa kama Makambako, naomba Wizara iangalie mapema kuhakikisha kwamba mbolea inasambazwa katika vituo mbalimbali na ninapongeza kabisa suala la vocha ambayo itatumika kama ruzuku ya wananchi kwa ajili ya kununulia pembejeo na Mkoa wa Iringa ukiwa ni mmojawapo wa kufaidika. Kama wengine wameshaanza kulima sasa hivi wakati hizo vocha hazajaanza kutolewa, nina wasiwasi kwamba utakapofika wakati wa kutoa, wananchi hao watalima bila kuwa na pembejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza Serikali kwa hili la kuhakikisha kwamba kunakuwa na vocha ambayo itawezesha wakulima kuweza kupata pembejeo na kupunguza ulanguzi uliokuwa unafanywa na walanguzi kwa kupandisha bei ya mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa angalizo kwa Serikali kwamba wakumbuke kuwa kuna wakulima ambao wanahitaji kulima lakini hawana uwezo na hawa ni pamoja na wanawake, wazee au wanawake na familia zinazotunza wagonjwa na yatima na kuna watoto ambao ni wakuu wa kaya, sielewi utaratibu huu utawalenga vipi. Nafikiria Serikali iweke utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba hili kundi pia linaangaliwa vizuri na ikiwezekana wapewe hiyo vocha na ile itakayobaki ambayo watatakiwa walipie, Serikali iwalipie ili kuhakikisha kwamba na wenyewe wanajitosheleza kwa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyepita, Mheshimiwa Edward Lowassa, aliweka utaratibu mzuri, alitoa mbolea kwa watoto wakuu wa kaya katika Wilaya ya Makete. Watoto na walezi hawa waliweza kupata chakula cha kujitosheleza. Naomba tuangalie utaratibu uliotumika na ikiwezekana utaratibu huo pia uendelezwe ili tuhakikishe kwamba kila mwananchi Serikali yake inamjali na kuhakikisha kwamba anapata chakula cha kutosha. Nina uhakika kabisa, Waziri wa Kilimo ni mtu mwenye huruma sana atalifanyia kazi ili kuhakikisha kwamba hawa walezi hawahangaiki na hao watoto wakuu wa kaya kutafuta chakula kinachowapelekea hatimaye kwenda kutafuta ajira mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, naomba nizungumzie wataalamu wa kilimo na nipongeze Serikali kwa mpango mzuri walionao wa kuhakikisha kwamba kila kijiji kinapata mtaalamu wa kilimo na kwamba kuna lengo la kuhakikisha kwamba kila mwaka wanaajiri wataalamu wa kilimo wapatao 2500, lakini kwa mwaka uliopita walioajiriwa hata robo ya hawa haifiki. Nashauri kwamba ili tuweze kupata wataalamu wengi wa kilimo, napongeza kwamba tumeamua kurudisha Astashahada au Cheti cha Kilimo katika mafunzo na kwamba tuchukue wanaomaliza Kidato cha Nne, wasiwasi wangu ni kwamba yawezekana tusifikie hilo lengo kama hatutaboresha mazingira ya kufanyia kazi. Hatuwezi kuchukua mtaalamu wa kilimo, tukampeleka kijijini hatujafanya maandalizi ya nyumba, hivi kweli huyu atafanya kazi vizuri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuelewe kwamba pia kuna Wilaya zenye mazingira magumu na yawezekana ndani ya Wilaya ikawa Wilaya isiyokuwa na mazingira magumu lakini Kata au Kijiji kikawa cha mazingira magumu. Sisi tunategemea kwamba mtaalamu wa kilimo atakwenda kufanya kazi pale, ni lazima tuandae mazingira mazuri na maslahi mazuri, tuwape motisha, wale tunaotegemea kwamba watakwenda kufanya kazi katika vijiji ambavyo ni vigumu au kata ngumu isiyofikika na pia tuhakikishe kwamba tunawapa usafiri, usafiri huu ni pamoja na kuwawezesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kwamba wanafanya kazi mbali sana na Makao Makuu ya Wilaya, kila mwezi wanatakiwa wafauate mishahara yao lakini hawapati posho. Ule ule mshahara alioupata ndiyo huo anaoukata, atumie kwa ajili ya nauli, hivi unategemea huyu kweli atafanya kazi? Ndiyo maana utakuta wataalamu wengine wa ugani, ukimkuta kule utamwonea huruma yaani huwezi kujua mtaalamu ni yupi, amekuwa *frustrated* kwa sababu ya mazingira anayofanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwe na *package* nzuri itakayowahamasisha vijana wengi kuipenda fani ya kilimo la sivyo wataalamu wengi wa kilimo tutawapoteza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi niliuliza swali kuhusiana na vyuo vya kilimo ikiwemo Chuo cha Kilimo Uyole, kuweza pamoja na kutoa Cheti, Diploma itoe pia Shahada. Jibu nililopata halikuniridhisha na hii ndiyo inayofanya wataalamu wengi wa kilimo wanahamia fani nyingine, wanaacha kilimo kwa sababu hakuna vyuo vile vya kuweza kuwapandisha anapokuwa kule kijijini basi yeye ni kijijini tu. Tunasema wataalamu wa cheti ina maana yeye ataendelea kukaa na cheti tu wakati na yeye pia anapenda ajiendeleze ili aweze kuwa mtaalamu bora? Tumeona kabisa nchi nyingine ukienda utakuta Afisa Kilimo aliyeko katika ngazi ya chini ana digrii yake, kwa hiyo siyo kwamba ukishasoma cheti basi wewe ndiyo hapo hapo na cheti chako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tuna mazingira magumu nilikuwa napenda kutoa ushauri kwamba labda Serikali iangalie utaratibu wa kuvihamasisha vijiji kwa sababu kuna vijana waliomaliza Kidato cha Nne na Kidato cha Sita wako kule kule vijijini, wahamasishe vijiji viwapendekeze waende mafunzo na wakirudi, warudi kwenye vijiji vyao, kuliko hii ya kuchukua jumla tu na kuwapeleka mafunzo halafu katikati hapa wnapotea kwa sababu ya mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la Bodi ya Mazao. Ninaipongeza Serikali kwa jitihada kubwa wanazofanya na ninakumbuka bodi hii mimi nilizungumza mwaka jana katika bajeti ya Wizara ya Kilimo na baadaye katika hotuba hii inaonesha kwamba mchakato unaendelea, sielewi mchakato unaendelea mpaka lini! Nilifikiri labda Waziri baadaye mwaka huu angekuja na Muswada ambao ungewezesha kuanzisha bodi hii ambayo tumeona itakuwa ni ukombozi mkubwa wa mazao ikiwemo mazao ambayo yalikuwa yanazungumzwa kama zao la Iliki, Tangazwizi ambalo nalo haliko katika mazao yenye bodi zinazozungumzwa, mazao ya njegere, ambazo zinalimwa sana Mkoa wa Iringa na wananchi kupewa bei ndogo kwa sababu hakuna chombo ambacho kinawatetea, zao kama la Karanga, ufuta na mazao mengine ya mafuta kama alizeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara wanawapa wakulima pembejeo halafu baadaye wananunua alizeti zao lakini hatujui kama alizeti wanazonunua ndiyo bei iliyotakiwa itolewe. Nafikiri ni vema Serikali iharakishe kuleta Muswada wa Kuanzisha Bodi ya Mazao mchanganyiko mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza wazo la kuanzisha Baraza la Kilimo, ni muhimu sana na kwa kweli litasaidia kutatua matatizo mbalimbali ambayo yanajitokeza na mengine ambayo yanajitokeza kwenye bodi zilizopo. Muswada wa Kuanzishwa Baraza la Kilimo, ninapenda uharakishwe kuletwa hapa Bungeni pamoja na sheria mbalimbali ambazo zipo lakini ni za muda mrefu sana zimeshapitwa na wakati tunatakiwa twende na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda liharakishwe, ni suala la ushirika. Wataalamu wa Ushirika ni wachache kwa hiyo elimu ya ushirika haiwafikii walengwa kama ilivyotakiwa ifikiwe. Hata wale wachache waliopo, idara hazina vitendea kazi wala fedha za kuweza kufanya ufuatiliaji wa kuweza kutoa mafunzo kwa Vyama vya Ushirika hasa *SACCOS* na hasa kufanya ukaguzi wa mahesabu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuwawezeshe watendaji wa Idara ya Ushirika ili waweze kutoa elimu kwa Vyama vya Kuweka na Kukopa na vyama hivi viwezeshwe, vikiwemo Vyama vya Kuweka na Kukopa vya Wanawake. Mfuko wa Pembejeo uangalie pia kuwezesha vyama hivi ili kuhakikisha kwamba pembejeo zinawafikia ili hawa waliopo kwenye vyama vya kuweka na kukopa waweze kupata pia pembejeo kununua matrekta ambayo yanaweza kuwasaidia kulima na kuongeza mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la kuanzisha Benki ya Kilimo, nafikiri kweli huo ndio utakuwa ukombozi wa mkulima. Nina hakika kabisa, benki hii ikianzishwa, itawafikia wakulima wengi. Lakini wakati tukiwa kwenye maandalizi ya kuanzisha benki hii, Mfuko wa Pembejeo uliopo, uongezewe fedha ili uweze kufanya kazi ya kuwafikia wakulima na hasa waliopo kwenye vikundi vya uzalishaji mali, *SACCOS* pamoja na wakulima wakubwa la sivyo watafaidika wakulima wakubwa na wakulima wadogo watabaki nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nizungumzie suala la umeme vijijini. Nakumbuka nililizungumza sana wakati tulipokuwa tunajadili Muswada wa Sheria ya Umeme Vijijini, bila ya kuwa na umeme vijijini maendeleo hayatafika, wakulima mazao yao yatakuwa yanachukuliwa na kwenda kusindikwa mijini kwa hiyo wataendelea kunyonywa jasho lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwe na vituo vya umeme ili wakulima vijijini kama wakulima waliokuwa wanazungumziwa wa Same wanaoanzisha kiwanda cha Tangawiza, basi na wakulima wa vijijini kama Iringa kuliko na alizeti na mazao chungu nzima ambayo yanalimwa kule lakini kwa sababu hakuna viwanda vya kusindika yanachukuliwa na kupelekwa mijini na wao kupewa bei ndogo, tuanzishe viwanda vidogo vidogo lakini umeme uwe ni kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumzia uzalishaji wa mazao ya chakula, lakini sijaona mahali popote…

(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mng'ong'o, ni kengele ya pili mchango wako mzuri, muda unakutupa mkono.

MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MHE. HASNAIN G. DEWJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kupata nafasi jioni hii ili kuchangia hotuba ya Waziri wa Kilimo na Ushirika. Nasema ahsante sana, hotuba yake ni nzuri na kazi nzuri aliyoifanya, nampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawashukuru wananchi wangu wa Kilwa walioniwezesha kusimama hapa na leo hii nawawakilisha na kwa kura walizonipa ili niweze kuwatetea, nasema ahsanteni sana wananchi wangu, nitazidi kuwatetea hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongelee kuhusu suala la mibono. Maeneo makubwa Kilwa yamegawiwa kwa makampuni makubwa hususani kampuni mmoja inayoitwa *Biyoshape* yenye makao makuu yake Uholanzi, wakulima wangu hawajatendewa haki kwa wale wawekezaji kupewa eneo kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mazuri yenye rutuba, yenye kuzalisha kwa wingi mpunga, mahindi na mazao mengine, yametolewa kwa wawekezaji hawa, ni maeneo makubwa kweli nikisema. Hatuwezi kugawa ardhi ovyo jamani, tutapata matatizo, *this is next* Zimbabwe, watu wameishi pale *fifty years*, maeneo kama Mavuji, Migeregere, Inokwe, Liwiti, Kiwawa, kilomita nyingi za mraba zimegawiwa sina takwimu lakini nina uchungu sana tunavyofanya hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, zao hili la mibono ni geni kwetu, hatujalilima hata mwaka mmoja ndiyo kwanza tunaanza kulilima, tunalilima tu. Mfano, tunatoa eneo kubwa sana la ardhi kwa ajili ya mibono, hii siyo haki, yale maeneo yarudishwe. Mheshimiwa Waziri, nakuomba tafadhali, wale jamaa wanasubiri hati ili waanze kukopa huko kwao, wanakuja, tunawaheshimu wawekezaji, wazalishe lakini siyo sawa kumpa jamaa mmoja au kampuni moja eneo kubwa kama lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijiji hakijahusishwa juu ya mgao au *payback* kwa kijiji, kipate *dividend,* hatuwezi kusema kwamba, *okay this is exclusive* kwa miaka 50 kwa kampuni ya kigeni, naomba Kijiji kipate *dividend* kila mwaka na wana kijiji waifanyie kazi kwa ajili ya maendeleo ya vijiji vyao husika. Hatuwezi kuwahusisha wawekezaji peke yao. Sasa hivi kinachotokea pale wenye mashamba madogo madogo wanakwenda kufanya kazi kutwa shilingi 2000 hela ya kujikimu, watazalisha lini wananchi hawa? Wakulima hawa watazalisha lini mazao yao au watajikimu vipi na njaa inayokuja keshokutwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuwa mkali kwa sababu naona huzuni kubwa sana wananchi wetu wa Kijiji ni *innocent,* hawaelewi, wakienda kwenye mikutano wakipewa vibahasha basi wanapitisha tu. Maeneo ni mazuri mno kwa kilimo cha chakula, yameshagawiwa. Sasa hivi mwanakijiji anakwenda pale kutafuta hela ya kujikimu ili ale na watoto wake, kesho hana kitu. Kibaya zaidi anaacha shamba lake akienda kule kutafuta hela ya kujikimu huku shamba lake anakuta limeshavamiwa na nyani, nguruwe, tembo, hiyo siyo haki. Tuione sera ya uwekezaji kwenye kilimo jamani. Mheshimiwa Waziri ndugu yangu, watakuja kuomba hati ya miaka 50 tusiwape, tuliangalie hili, nasema tunawaheshimu lakini tuliangalie tusije kugawa maeneo ovyo tukasema Kilwa mna eneo kubwa lakini tuligawe kwa kampuni moja *exclusive* pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hilo la mibono, nataka niingie moja kwa moja kusema kwamba Wilaya nzima ya Kilwa ina karibu matrekta matano tu. Matrekta mawili ya Mheshimiwa Mbunge mengine ya jamaa, tuna matrekta 3 peke yake. Tuna eneo kubwa katika Wilaya nyingi Tanzania, Wilaya kubwa kabisa ni Kilwa. Lakini mkulima maskini akienda kukopa pale kwenye mfuko wa pembejeo akaambiwa kalete hati ya nyumba, mkulima maskini ataipata wapi nyumba yenye hati, yeye anamiliki kibanda kibovu, akienda nacho kula hakina hati hapewi mkopo wa trekta. Tutafanya nini, mashamba yao madogo madogo hayaruhusiwa kuwa kama *collateral* au *security*. Huyu mkulima mdogo *security* ataipata wapi? Hali ni mbaya mno halafu tunasema wananchi tuzalishe zaidi, watazalisha kutokana na nini wakati hela ya kujikimu hawana maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hili la kilimo, Kilwa tuna eneo kubwa mno na la rutuba, unaweza kutupia tu zile mbegu zikaota zenyewe (*the virgin land),* ardhi ambayo haijaguswa lakini wakulima wangu wanashindwa kuitumia ile ardhi ili iweze kuzalisha zaidi kwa sababu hatuna matrekta, kwa sababu sisi ni maskini hatuna dhamana, dhamana zitatoka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu nakuomba Mheshimiwa Waziri, wakati unajumuisha, tupate kujua hawa wakulima wetu, dhamana tutaitoa wapi. Hatuwezi kuzalisha bila dhamana, bila wao kupata mikopo, matrekta matano kwa Wilaya kubwa kama ile haiwezekani, *security* iko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi wa Makangaja wa kumwagilia maji. Leo takribani miaka miwili na nusu, Serikali ya Japan imetoa milioni 151 ili ule mradi ukamilike, lakini mpaka sasa hivi mifereji hii ndiyo iliyotengenezwa kazi imefikia asilimia 50, fedha zimeisha. Tutawezaji kulima kwa kiangazi, maeneo tunayo, mradi unasuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye *zone* Mtwara, utaambiwa bado, ngoja hiki, ngoja hiki, ule mradi ni mkubwa mno lakini mpaka sasa haujatekelezwa. Leo hapa Bungeni nauliza swali ule mradi umefikia wapi Mheshimiwa Waziri wakati unajumuisha wananchi wangu wajue mradi wa Makangaja wa kumwagilia maji umefikia wapi, hatua gani uliofikia na hatma yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda moja kwa moja kwenye pembejeo, *voucher*, tunasema sisi watu wa Kusini tunahitaji hiyo voucher kwenye madawa ya korosho, tuitumie *voucher*. Nitatoa mfano mwaka jana zilikuja pembejeo Kilwa Masoko, Makao Makuu ya Wilaya, yale madawa ya korosho yaligawiwa pale pale Makao Makuu ya Wilaya, zile dawa hazikuwafikia wakulima. Tunasema hivi kama huo mpango wa *voucher* unafaa sehemu zingine uletwe kwenye madawa ya korosho, tutajua wakulima ni nani na nani analima na kiasi gani cha dawa apewe kwa punguzo maalum la pembejeo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dawa zinatolewa holela mno, wanapewa wasio wakulima halafu mkulima huyo huyo anakuja analanguliwa ananunua kwa bei kubwa. Pale Wilayani wanauziana wenyewe kwa wenyewe lakini mimi mkulima ananipigia simu Mheshimiwa Mbunge vipi *Sulphur*, vipi *Biofiden* haziwafikii wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongelee korosho. Korosho yetu ya Lindi na Mtwara, inakwenda nje kama malighafi kwa viwanda vya huko. Asilimia 80 ya korosho ya Lindi na Mtwara, inakwenda nje badala ya kuzalishwa humu ndani. Nilipata bahati ya kuongea na wenye viwanda, mwaka huu viwanda vinafungwa mwezi wa nane, hawana malighafi korosho nyingi zimepelekwa nje. Kuwe na udhibiti wa korosho kupelekwa nje tuzidi kuongeza viwanda hapa Tanzania ili malighafi isitoke nje ili tuzidishe ajira na vile vile soko. Leo korosho iliyobanguliwa mitaani, inauzwa shilingi 14,000 yaani dola 12 kwa kilo lakini mkulima huyo huyo kaiuza kwa dola mbili kwa kilo ikiwa ghafi, hatujaendelea bado, hatujaleta ajira bado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirika umefanya kazi nzuri sana, wenzetu wa Mtwara wamepata mgao wa pili, sisi Lindi tulichelewa, wakulima wameuza korosho yao mpaka shilingi 900, sisi wa Lindi mwaka huu tunaanza kuiga mfano wa Mtwara ili tuweze kuwa na ushirika ambao ni mtetezi wetu kati ya tajiri na sisi wakulima, awe mtetezi wetu, yuko katikati na tuweze kupata *dividend* mgao wa pili kama wenzetu wa Mtwara. Tuna matatizo na viongozi wetu, wengine baadhi walikuwa wanapingapinga sijui hivi ushirika

haufai na kadhalika, mimi nasema ushirika umefanya kazi nzuri, tuwape meno na tuwape mtaji mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, nasema naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitazungumzia mambo mawili, matatu ambayo labda yanaweza yakaisadia nchi yetu kuinua kiwango cha kilimo, kuongeza tija kwa chakula ambacho kitatumika katika nchi yetu na tukawa na ziada ya kusafirisha nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma tuliambiwa kwamba ili tuendelee tunahitaji mambo manne, watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora. Watu tunao wa kutosha na wanaendelea kuzaliwa. Ardhi ipo tena nzuri, kubwa na ina rutuba na maji ya kumwagilia yanaweza yakapatikana katika ardhi hii lakini nafikiri kuna ukosefu wa siasa safi na uongozi bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitabu hiki cha Siasa ni Kilimo ambacho kilikuwa kikiuzwa shilingi 10, kama utakipitia, ukaona maazimio yaliyokuwemo ndani mle ndani juu ya kilimo cha nchi hii, ni kitabu hiki hiki kilichoonyeshwa na Mheshimiwa Makamba na ndiyo ninacho kwa bahati nzuri na nafikiri ni mtu wa pili tu kwa Bunge hili kuwa nacho wengi hawana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mambo mengi mazuri yamo ndani ya kitabu hiki ambayo yanaweza kuifanya hii nchi isiwe tegemezi tena. Kwa nini mpaka leo tunaagiza chakula? Tuchukue mfano mmoja mdogo tu, matunda tunayoyazalisha nchi hii, *we produce what we do not eat and we eat what we do not produce, yes*! Leo sisi wenyewe Wabunge hapa tunapokwenda kwenye Kamati, tunapotembelea sehemu mbalimbali au tunapokuea kwenye semina, tunakaribishwa na *juice* kutoka Afrika Kusini, ni aibu kwa Tanzania kwamba mpaka leo sisi Wabunge wenyewe tunakunywa *juice* kutoka Kenya na kutoka Afrika Kusini! Muheza machungwa yanaoza, Morogoro machungwa yanaoza, maembe yapo tena mengi ya kutosha, kuna nanasi ambalo ukubwa wake sawa sawa na ukubwa wa kichwa cha tembo, nenda Mbeya, nenda Geita, tunayafanyia nini? Nanasi moja peke yake lanaweza likatoa lita tano au sita za *juice*. Kilichokosekana hapa ni *capital* ya kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya kusindika. *Capital* haiwezi kupatikana kwa kuwachukua wajasiriamali tukawaambia waende *CRDB* au benki yoyote wakapewa mkopo, haiwezekani katu abadani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tufanye nini? Tuwachukue Wabunge wa maeneo yanayozalisha matunda, wapewe *government guarantees.* wakapewa mikopo mabenki, wafungue viwanda vidogo vidogo ili wasindike na kutoa ajira kwa vijana wetu katika maeneo yale. *That is the only solution,* hakuna njia nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo matunda haya tunainua kiwango cha utalii lakini hayapelekwi katika mahoteli ya utalii kwa sababu hakuna *infrastructure*. Matokeo yake

kutoka Muheza mtu anabeba machungwa anapeleka Kenya na watu walivyokuwa wabaya duniani, binadamu hawa akijua kwamba ile *fruit* ni *perishable,* anamwambia mimi nataka kwa bei fulani, *whether* unauza niuzie hutaki rudi nayo, atarudi nayo vipi? Anajua *after three days* kutokana na *temperature* iliyokuwepo pale matunda yale yataoza, atauza kwa bei ambayo haitampa manufaa mkulima, mnunuzi wala mfanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna *Board of External Trade more than 30 years*, inafanya kazi gani kutafuta soko na na vitu kama hivyo, ni simply tu, viwanda vyenyewe ni vidogo vidogo kabisa *(small scales industries)* lakini *nobody cares,* hakuna Benki ya Wakulima ambayo itatoa mikopo ya muda mrefu na riba ndogo watu wakaweza kuweka viwanda vikawasaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye korosho hizi zilizozungumziwa sasa hivi. Kwa wale wanaosafiri na hasa wanaokwenda *London,* ukifika zile hoteli za maana, angalia korosho inauzwa kwa bei ya juu, *a very small candy cashnut,* wenyewe wanakuambia sijui *Masala Cashnut* au *soltape cashnut, more than five/six pounds*. Korosho tunazalisha sisi hapa katika Afrika, Tanzania na Msumbiji, kwa nini tusizi-*process* korosho hizi tukasafirisha katika nchi ambazo zinahitaji na nchi ambazo zinahitaji korosho nyingi *Europe* ni Ujerumani, Uingereza na *Poland* na ukienda kwa *Far East* ni Austrilia, *do you know the reason why?* Kwa sababu ndiyo wanywaji wakubwa wa bia na wanapokunywa bia huwa wanatumia na zile korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawezeshwe hawa Wabunge katika maeneo ambayo yanatoa korosho kwa wingi, wapewe tiketi, waende wenyewe wakatafute soko, wagawiwe makundi mawili, moja liende *Europe,* Ujerumani na *Poland* moja liende *Australia,* wao ndiyo watakaokuwa na uchungu wa Majimbo yao kwa sababu ya kulinda kura zao na kuheshimu wapiga kura wao na wao ndiyo watakaotafuta soko la uhakika kwa nchi hii. *Otherwise* mkumbuke sasa hivi nchi ya *Indonesia* na *Vietnam* wanajidhatiti kabisa kuzalisha zao la korosho. *Indonesia* ni hatari sana ndiyo hawa waliopiku zao la karafu la Zanzibar hata tukafikia sisi tumeshindwa kusafirisha na kuzalisha kuliko wanavyofanya wao. Sasa hivi *Vietnam* wanazalisha korosho, sasa *Indonesia* wanazalisha korosho, korosho katika miaka ya 1980 tulikuwa tunazalisha mpaka tani 145,000 tulitegemea kwamba kiwango kitapanda, matokeo yake kimeshuka tuko tani 99,000 *almost 100,000 tone 40 years back.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiondoka kwenye korosho twende kwenye hali ya *crisis* ya chakula duniani. Kama Tanzania tutakuwa *serious,* tukaachana na kasumba za kwamba tuzipe *priorities* Wizara nyingine na kuacha kilimo ambacho ni uti wa mgongo, tutafika mahali pabaya. *This is the golden chance* Tanzania tunaweza tukaitumia tukazalisha chakula kwa wingi, tukasafirisha na kingine kikabaki tukakitumia sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbukeni miaka ya 1980, tulikuwa na mashamba katika Wilaya ya Hanang Basuto ambayo yalidhaminiwa na Canada ambayo walikuwa tayari hata kujenga kiwanda cha ngano pale Manyoni, tulikuwa tukizalisha karibuni tani 45, 50% ya mahitaji ya nchi hii. Leo baada ya miaka 28 tunazalisha tani 84,0000 yaani ni ongezeko mara mbili tu lakini uki-*calculate* na *population wise* utaona tuko pale pale

kwenye *50% of the Tanzania production* na hata leo haikuonyeshwa kwenye kitabu kwamba sisi tunasafirisha chakula gani kwa sababu hatuna cha kukisafirisha, zaidi tunaagizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaingia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, kuna mikakati ya kuizua Kenya isinunue mchele wa basimati kutoka Pakistan ili Tanzania iiuzie Kenya mchele, ndiyo, lakini je, tuko *serious* na hilo? Tunakaribisha *investors* kutoka nje, ilipotokea *political crisis* Zimbabwe wale wakulima wa Zimbabwe walitafuta mahali pa kwenda ku-*invest* walikwenda Msumbiji, walikwenda Zambia, walikwenda mpaka Nigeria, hatukuonyesha *interest* ya kuwapa sura wale watu wakaja kwetu. Wale wana-*harvest in bumper* yaani *harvest* yao ilikuwa kubwa sana. Zimbabwe ilikuwa ni nchi ya mwanzo katika Afrika katika miaka ya 80 kuweza kusafirisha chakula kupeleka nchi nyingine za Kiafrika. Hata ikawa inaitwa *AFA (Africa Feed Africa).* Ilipoingia ukame Manika Msumbiji, Zimbabwe ndiyo aliyeuza *United Nation* kupeleka Manika, kupeleka Kenya, kupeleka Ethiopia na kukawa na treni inakwenda mara mbili kwa wiki ikawa inaitwa *Maize train* 1986, leo Zimbabwe ime-*drop,* sisi ilikuwa tuchukue nafasi ile, *are we serious for that?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanakuja watu wajanja wanaichukua ardhi yetu kwa kutaka eti kuzalisha jatropha, waje na viwanda, jatropha wawaachie wananchi wenyewe wazalishe wauze kwenye viwanda vyao. Siyo wao kuja kupewa ekari za mamilioni hapa kuzalisha wananchi wetu wakawa ni watumwa katika mashamba yale, hapana, *we must be serious on that. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *otherwise* kama sisi tunakuwa kweli tuko *serious*, tukayachukua mashamba yale ya Basuto tukarejesha tena kilimo cha ngano, sisi tunaweza tukapata chakula chetu cha ngano kila siku. Tukachukua maeneo ambayo yanazalisha mpunga, tukazalisha mpunga tutakuwa na mchele wa kula sisi na wa kusafirisha nchi za nje, lakini *we are not serious*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwa kutumia jembe la mkono kuna nchi zinaendesha kilimo kwa matrekta na kwa kutumia jembe la mkono. Sisi tume-*advance* kutoka jembe la mkono, tumeingia kwenye plau, tumeingia kwenye trekta na watu wapo wafanyabiashara ambao wataonyesha imani ya kutaka ku-*invest* kwenye *agricultural* lakini ukiritimba umekuwa mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kama utafungua kiwanda cha kutengeneza *juice* inayotokana na mananasi, machungwa au maembe utaona ile *juice* inakuwa ni aghali hata kuliko ile inayoagizwa kutoka *India, Pakistan, Saudi Arabia* au inayoagizwa kutoka Afrika Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dodoma hapa hapa, jana nilikwenda kwenye duka nikakuta kuna *juice* inayotoka Yemen. *Just imagine, desert country* Yemen wana-*produce juice* wanatuuzia sisi Watanzania! Lazima tukae na wafanyabiashara tuwaamshe vichwa vyao kwamba hizi ndizo *investment* ambazo zitaendelea *the coming hundred years* siyo kwenda kuchukua mali *Dubai, China* kuja kutuuzia sisi. Tuzalishe sasa na sisi

tusafirishe, tutafute soko na soko lipo, hatuoni aibu nchi kama Oman, *Saudi Arabia* zinatoa maziwa, tuna ng'ombe lakini maziwa hatuna, tuna ng'ombe lakini hatuna ngozi, tuna ngozi hatuna viatu, tuna pamba hatuna nguo, nguo za Jeshi na Polisi tuagize kutoka nchi za nje, *is shame for our country, definitely I am telling you*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamba yetu sisi tunaweza tukatengenezea nguo, leo Jeshi letu la Polisi nguo tuagize kutoka China, kutoka Uingereza, kutoka India, nenda *Egypt* mkaone wanazalisha pamba, Wanajeshi wao wote wanawavalisha nguo wanazotengeneza wao wenyewe. Nenda *South Africa*, mkaone nguo zao za Wanajeshi na Polisi zote zinatengenezwa *South Africa*. Sisi tuna pamba ya kutosha kabisa, tuna ngozi nyingi tu za kutengeneza viatu, matokeo tunanunua viatu kutoka *Italy*, unavivaa kutoka Ilala mpaka Kariakoo, soli unaiacha Kariakoo unarudi nyumbani na ngozi ya juu, *yes* ni plastiki. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema kwamba Tanzania kama tutakuwa tayari tutakuwa na uwezo wa kuweza kujenga maghala ya kisasa, *SGR* itafanya kazi vizuri ya chakula kwenye maghala. Ikifika wakati kama kuna pamba *harvest*, uzeni ile ya kwenye maghala wataondokana na gharama za *fumigation*, halafu mnaweka mali mpya ndani. Wakishaweka mali mpya ndani wanaangalia soko la nje liko namna gain, wanauza kwa nchi jirani. Tusiwazuie watu waliopo mipakani kuuza bidhaa zao ambazo wanazizalisha. Wanatumia nguvu zao, tunaichosha ardhi yetu kuzalisha halafu nafaka zile au matunda yale yanakuwa hayamsaidii mkulima, hayaleti tija kwa nchi, ardhi inakufa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka mchungwa unazaa, maembe yanazaliwa, Bukoba ndizi zipo, lakini nenda Dubai ndizi zinatoka *Brazil*, machungwa yanatoka India, mboga zinatoka *Iran*, sisi Watanzania kujivunia tu tuna ndege mbili *everyday* zinaingia Tanzania. Tuwachukue hawa wajasiriamali, tuwape mikopo midogo midogo isiyokuwa na riba waweze kuzalisha mboga mboga wazipeleke katika soko la Dubai, *we can manage to do that, why not*? Ndiyo hiyo siasa safi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunategemea ajira itoke kwa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, aitoe wapi? Akawaweke vijana kule Ikulu wakafanye kazi? *No!* Ajira inapaswa tuzitengeneze sisi Waheshimiwa Wabunge na ile kuzuia Mfuko wa *CDF* inatuumiza sisi Wabunge. *CDF* lazima iwepo, *CDF* kama itatolewa kama inavyotolewa Kenya, tukapata fedha kama za Kenya sisi wenyewe tunaweza tukaanzisha miradi midogo midogo na viwanda vidogo vidogo kwa kuunganisha nguvu za Waheshimiwa Wabunge katika maeneo ambayo yanazalisha matunda na yanayozalisha korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *a very good example* ni ya Mheshimiwa Anne Kilango Malecela hapa, yeye mwenyewe ni mmoja tu, kama kweli angekuwa amepata *CDF*, akachukua na yale Majimbo yaliyo karibu na yeye waka-*organize* kitu kizito ambacho kitaleta manufaa kwa nchi, angeweza kuzalisha zaidi na angeweza kutafuta soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Tanzania unakwenda kwenye *Supermarkets* zote zimejaa bidhaa za nje na maziwa yote yanatoka nje ya nchi, maziwa yanatoka Afrika Kusini, yanatoka Saudi Arabia, yanatoka Netherlands na yanatoka Australia. Unakuta Wachina wanakuja hapa nchini na mitumba yao wanauza, hawana viwanda ilikuwa waje na teknolojia, waje na viwanda, waje na *capital*, kwa nini hatuwapi *conditions*, wale leo ndiyo wakuuza karanga, wale ndiyo wa kusukuma malikwama Kariakoo, sisi tumelala!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba matunda yetu yasindikwe. Hata juzi Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, alipokwenda Tanga alilizungumzia suala hilo ili tuzidishe thamani ya fedha katika kile tunachokizalisha.

(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA: Hiyo kengele ya kwanza au ya pili?

MBUNGE FULANI: Unga mkono hoja.

MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA: Kuunga mkono si tatizo unaweza kuunga mkono na hali ikawa ile ile.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sanya, muda umekwisha usiendelee na kuchangia.

MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Sasa namwita Mheshimiwa Basil Mramba ili atufungie mjadala jioni ya leo.

MHE. BASIL P. MRAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunifanya niwe msemaji wa mwisho kwa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja hii kwa sababu ukisoma malengo katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, utaona wazi kwamba angalau anajua anakokwenda. Kinachotakiwa sasa ni utendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusikiliza sana wasemaji walionitangulia, lazima nikiri kwamba Mheshimiwa Waziri Stephen Wasira, ana kazi kubwa. Sasa sijui tuseme siasa ni kilimo ama kilimo ni siasa? Kama siasa ni kilimo na ndivyo ilivyo sera, basi anakotupeleka Mheshimiwa Waziri, ndiyo njia sawa. Lakini tukianza kusema kilimo ni siasa ndiyo tutaanza kuchanganyikiwa upya na ndiyo tutarudi nyuma. Hakuna siasa hapa kuna kazi ya kulima ili tuweze kulisha watu wetu na ili tuweze kuuza nje ya nchi ama moja kwa moja kama ilivyo sasa chakula hakitoshelezi au kwa utaratibu uliokuwa unaelezwa hapa kwa kusindika na kuuza bidhaa ambazo zimekwishasindikwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshauri Waziri, Mzee wangu wa siku nyingi, kama kweli tunataka *Green Revolution,* kilimo cha Tanzania lazima kiwe kilimo mchanganyiko, wakulima wadogo na wakulima wakubwa kwa kila zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tulipo ndiyo hivi tunaanza kufufuka. Nadhani mwaka juzi, Wakuu wetu wa Mikoa, waliitwa hapa na Mheshimiwa Waziri Lowassa alipokuwa Waziri Mkuu, wakakubaliana juu ya malengo ya kila zao, wenye tumbaku wakakubaliana, wenye kahawa wakakubaliana, wenye chai wakakubaliana. Natumaini kwamba kazi hiyo bado inaendelea na nafikiri inaendelea kwa sababu ukisoma hotuba ya Waziri, kuna takwimu hapa za ongezeko la uzalishaji kwa mazao mengi hasa ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa Kambi ya Upinzani kile kitabu walichotoa leo hapa asubuhi kinaonyesha mambo ambayo sasa sijui tumwamini Kambi ya Upinzani ama tumwamini Waziri! Nafikiri hapa lazima tumwamini Waziri. Waziri anaonyesha ongezeko la uzalishaji, pamba asilimia 53.7, tumbaku asilimia 13.1, sukari asilimia 38.2, pareto asilimia 12.4, korosho asilimia 7.1, mkonge asilimia 7 kamili na ongezeko pia katika matunda, maua na mboga. Kuna ongezeko la uzalishaji ndiyo maana nampongeza Mheshimiwa Waziri na kumwambia songa mbele kuelekea kwenye malengo yale ambayo yalikuwa yamewekwa na Wakuu wa Mikoa wakiongozwa na Waziri Mkuu wa wakati ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao mawili yameshuka, ambayo ni chai na kahawa. Mimi nataka niseme kwamba kama tunataka hii *Green Revolution* lazima tutimize masharti manne. Sharti la kwanza, ongezeko la uzalishaji. Sharti la pili, kuwepo usafirishaji wa mazao yaani barabara za vijijini ziwe zinapitika kwa masaa 24 hasa kwenye mazao husika. Tatu, lazima kuweko na uwezo wa kusindika mazao haya kule kule yanakozalishwa, korosho kwenye korosho, kahawa kwenye kahawa. Nne, lazima yawepo masoko ambayo kwa ndani yatakuwa ni walaji ambao wanaweza kuwa ni watu au viwanda na kuuza nje kama kuna ziada. Masharti manne, uzalishaji, usafirishaji, usindikaji na masoko ili kweli tuweze kufanikisha hiyo *Green Revolution. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uzalishaji, ni lazima tuzungumze juu ya *units yields* kwamba kama tuna mibuni, wataalamu wanasema mbuni mmoja lazima uzae kilo 5 za kahawa, tusipofikia kilo 5 kwa mbuni bado hatujafika. Kwa hiyo, lazima tuzungumzie siyo tu *production,* ni *productivity* na tungefanya hivyo, hapa tulipo, tungeweza tukaongeza sana uzalishaji. Tutafikiaje *productivity?* Ni kwa utaratibu wa *extension,* huduma kwa wakulima ambazo ni za kitaalamu kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano wa chai, nimekuwa nikisoma taarifa hapa, taarifa inayoitwa *Tea Research Institute of Tanzania, Annual Report 2006/2007* na nina *documents* zingine zinazozungumzia juu ya chai kwa sababu nataka kulinganisha chai na kahawa. Mimi siyo mkulima wa chai, mimi ni mkulima mdogo wa kahawa, *small holder.* Lakini kwenye chai tunajifunza kwamba kuna hii *research station* inaitwa *Tea Research Station,* nadhani iko kule Mufindi. Utafiti unaofanywa na Stesheni hii, unasogea njia yote mpaka Tukuyu na ndiyo maana leo watu wa Tukuyu ambao wamezingatia kwa dhati ushauri wa Kituo hiki, naweza nikasema kwamba wakulima

wadogo wa Tukuyu ni wakulima wa mfano na hakuna mkulima mwingine wa zao lingine lolote Tanzania anayefikia wakulima wa Tukuyu. Wakulima wa Tukuyu wanajilipa mishahara, wana *insurance,* wana pensheni na wana hisa kwenye Kiwanda cha Kusindika Chai katika Wilaya ya Rungwe. Hakuna wakulima wengine wowote waliofikia hatua hiyo ya kuwa na bima ya afya, pensheni, na kuwa na fedha nyingi mikononi mwao ambayo wanaitumia kwa maendeleo yao wao wenyewe, hakuna! Hawako kwenye kahawa, hawako kwenye tumbaku, hawako kwenye pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ilifanyika kwa sababu kuna muunganisho wa utafiti na *extension services.* Nasikia kwamba wataalamu wanane tu wanahudumia wakulima wadogo 16,000 kule Rungwe. Kwa hiyo, uwingi siyo hoja, hii ya kusema mtaalamu kila kijiji, wingi siyo hoja, hoja ni ubora na mbinu. Kutokana na kazi hizo, wataalamu wale wanalipwa vizuri na wanahudumiwa vizuri na wakulima wanafaidika. Wale wakulima tena ndiyo wanalipa hawa wataalam. Kwa hiyo, wakulima wadogo wa mazao ya biashara wanaweza wakalipa gharama zao au hata wakakopa na kurejesha na wakaendelea kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mtaniuliza mbona zao la chai lilishuka? Ndiyo lilishuka, lakini sababu ni mbili tu, hali ya hewa na bei ya mbolea kupanda. Hivi sasa nasikia wakulima wa chai Mkoa wa Tanga wanaiga wa Kusini Magharibi, wa Mufindi, wa Iringa, wa Rungwe na wale nao wataendelea. Mheshimiwa Shellukindo yuko hapa ananisikia, nasikia wameanza kupata huduma ya Kituo hiki cha Utafiti wa Chai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwenye kahawa, tuna *TACRI.* Kituo cha Kahawa cha *TACRI* kingefanya kazi inayofanana na Kituo hiki cha Chai cha Kusini Magharibi na wa pamba wakafanya hivyo na wa korosho wakafanya hivyo na wa pareto wakafanya hivyo na mazao yale mengine yote wakafanya hivyo, nchi hii tungeweza kuendelea bila ongezeko lolote ya maeneo ya kilimo isipokuwa kwenye mashamba makubwa, mkulima mdogo angeweza akaendelea kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwuliza Mheshimiwa Waziri kama tayari wana mfano mzuri kule kule Wizarani kwenye chai, tuletee basi kwenye mazao mengine kwa mtindo huo huo, sisi tuko tayari kuupokea ili kusudi angalau tuendelee bila hata kuongeza maeneo ya ziada ya kilimo. Mimi natoa ushauri huo kwamba jifunze kwenye chai na sambaza kwenye mazao mengine. Kwenye kahawa hatuwezi kuendelea mpaka hapo kutakapotokea mapinduzi ya kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la kahawa ndiyo la kwanza kwa kutuletea fedha za kigeni. *Number one foreign exchange earner,* ni kahawa na *number two foreign exchange earner* ni korosho lakini mazao haya hayapati huduma zinazotakiwa, yaani ni sawa sawa kuwa na ng'ombe ambaye halishwi ingawa ndiye anayetoa maziwa kuliko ng'ombe wengine. Ili zao la kahawa liweze kuendelea ni lazima tufanye wanachotushauri Kituo cha Utafiti wa Kahawa. Ng'oa mibuni yote ambayo imezeeka, lakini wakulima hawatang'oa mpaka wajue watakula nini pindi wakisubiri kahawa mpya iweze kuzaa na kutoa tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwamba Wizara ifikirie uwezekano wa kutafuta mfuko maalum wa kuhudumia wakulima wa kahawa wakati wanapong'oa kahawa na kahawa hiyo waing'oe kwa pamoja siyo hii wanang'oa mibuni 10 au 20 kwa nyakati tofauti, nashauri Ing'olewe kwa pamoja mara moja. Lakini wapatiwe namna ya kuishi mpaka hapo mibuni hiyo itakapozaa na wapatiwe mbegu mpya kwa mpigo na wapatiwe *extension service* na huduma nyingine zinazoendana na zao la kahawa, pembejeo kwa mfano, mashine za kupukuchua zile ndogo ndogo za vijijini, madawa ya aina mbalimbali, mikopo ya kuendeleza zao hilo na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivyo ndani ya miaka mitatu tu au minne ijayo na bila kuongeza kabisa eneo jipya la kahawa, tunaweza tukaongeza zao la kahawa maradufu, mara tatu ya uzalishaji wa hivi sasa. Bila kufanya hivyo, kila mwaka utaendelea kuona zao la kahawa likidumaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu walizotoa hapa, ni za kweli lakini siyo hizo tu, mkulima anaogopa kubadili mibuni ya zamani kwa sababu atakula nini na swali hili linawezekana kama Wizara itaunda mfuko maalum na kuzungumza na mkulima iweje, tufanyeje ili tuweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niko tayari kushiriki katika mazungumzo ya namna hiyo kama yataendeleza mkulima wa kahawa Tanzania nzima. Mimi sizungumzi habari za Kilimanjaro na Arusha tu, nazungumzia Tanzania nzima, *formula* iwe ni ile ile na huduma ziwe ni zile lakini kama ilivyo kwenye chai tutumie *TACRI* kama ndiyo msingi wa kupeleka *extension service* na huduma nyingine kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuzungumzia zao la matunda. Nafurahi sana hapa msamiati unaotumika ni mazao ya bustani. Ni kweli ni mazao ya maeneo ambayo hayana ardhi nyingi. Nakubaliana na mkakati mnaoweka, lakini naomba Mheshimiwa Waziri ufikirie ndizi, maembe, maparachichi, matunda haya yanastahi sana kwenye baadhi ya Mikoa yetu na Wilaya zetu. Mfano Tukuyu, *South West Kilimanjaro*, Arusha, Lushoto ambako hakuna maeneo makubwa lakini nayo yanahitaji *extension service* ya maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi, vituo viko tayari, Seliani wako tayari kutoa utaalam, Chuo Kikuu cha Sokoine, wako tayari kutoa utaalam lakini tunahitaji mkulima apewe mbegu mpya na msaada wa kuchukua mbegu hizo mpya kama ulivyosema hapa kwenye baadhi ya mazao, kama ni *subsidy* au kumpa kabisa mbegu ili aweze kulima *quality* matunda na aweze kutumia kama chakula na vile vile kama zao la biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Rombo, tuko tayari na tumekwishaanza, tunahitaji nguvu, ushauri na msaada zaidi kutoka Wizarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, namalizia kwa kutoa rai kwamba ni vizuri tujenge *private sector* kwenye kilimo, *private sector* ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naunga tena mkono hoja. Ahsante sana kwa nafasi ulionipa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Basil Mramba.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani tutakubaliana kwamba wachangiaji wetu walioomba kuchangia hoja hii leo walikuwa na michango mizito na mizuri sana. Kwa hiyo na mimi nashukuru kwa kukaa nikasikiliza michango mizito sana jioni ya leo.

Pamoja na hivyo, napenda niwatangaze wachangiaji wetu watano wa mwanzo kesho, atakuwa ni Mheshimiwa William Shellukindo, atafuatiwa na Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mheshimiwa Mgana Msindai, halafu mtu wa tano atakuwa Mheshimiwa Anthony Mwandu Diallo.

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo kwamba Wabunge wote walioalikwa kwenda kushiriki chakula cha jioni pamoja na Mheshimiwa Dr. Asha Rose Migiro, Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, *St. Gasper Hotel* kwamba kutakuwa na usafiri wa kuwapeleka huko mara baada ya kuahirisha Bunge.

Kwa hayo machache na kwa kuwa muda tulionao hautoshi kwa mchangiaji mwingine kutoa mchango wake, napenda niahirishe Kikao hiki cha Bunge mpaka kesho Jumatano, tarehe 23 Julai, 2008, saa tatu barabara, asubuhi.

(Saa 01.45 Usiku Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatano
Tarehe 23/7/2008 Saa Tatu Asubuhi)